Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Thelathini na Tatu - Tarehe 26 Julai, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla kikao hakijaanza, napenda kuwatambulisha Wageni wa Kimataifa walioko kwenye *gallery* ya Bunge asubuhi hii ni Mheshimiwa Balozi wa Afrika ya Kusini pamoja na mkewe wamekuja kututembelea. Tunawakaribisha. *(Makofi)*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:**

Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 305

**Ofisi za Kutunza Nyaraka za Wabunge Majimboni**

**MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali na Mahakama huweka nyaraka zao maofisini na kwa kuwa Bunge lina Ofisi Dodoma na Ofisi Ndogo za Dar es Salaam na Zanzibar tu wakati Waheshimiwa Wabunge hawana Ofisi Majimboni wala Wilayani:-

(a) Je, Bunge kama moja ya nguzo Kuu Tatu za Uongozi nchini, limeweka utaratibu gani wa mahali pa kutunza nyaraka wanazopewa Waheshimiwa Wabunge kila mara ili ziwasaidie pia wanaowawakilisha?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba Ofisi za Wabunge Majimboni/Wilayani zikijengwa mapema zitasaidia sana Wabunge kuwa na mahali pa kutunzia kumbukumbu zao kuliko hali ilivyo sasa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba Bunge ni moja ya nguzo tatu za uongozi hapa nchini. Ibara ya 63(3), ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1997, imeelezea vyema na kufafanua kazi zote na majukumu ya Bunge. Vilevile Serikali inatambua kwamba, Waheshimiwa Wabunge kwa kipindi kirefu wamekuwa wakikabiliwa na ukosefu wa Ofisi kwa ajili ya kuwahudumia Wananchi katika maeneo yao. Kwa kutambua tatizo hili na kama nilivyoeleza juzi tarehe 20 Julai, 2004, wakati najibu swali la Mheshimiwa Kassim Mbaruk Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, kama hatua ya muda mfupi Serikali imeamua kutafuta Ofisi katika majengo ya Serikali kote nchini kwa ajili ya Ofisi za Waheshimiwa Wabunge.

Aidha, Ofisi yangu itaendelea na juhudi za kukarabati majengo hayo na kuweka samani ili ziweze kukidhi mahitaji ya Waheshimiwa Wabunge angalau kwa kiasi fulani. Jukumu hili linaendelea kufanyika kwa ushirikiano wa karibu na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mikoa, Wilaya na Waheshimiwa Wabunge wenyewe.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba, Ofisi za muda za Waheshimiwa Wabunge ambazo Serikali imekwishazianzisha, hazikidhi matakwa ya Waheshimiwa Wabunge kutokana na kuwa na majengo yasiyotokana na ramani maalum za Ofisi za Wabunge. Kwa hiyo, kimsingi Serikali inakubaliana kabisa na hoja ya Mheshimiwa Mbunge ya kutaka Serikali kuona umuhimu wa kujenga Ofisi zenye hadhi na zinazozingatia majukumu ya Wabunge. Jambo hili litawezekana uwezo wa Serikali utakaporuhusu na kulingana na maandalizi yatakayokuwa yamefanyika.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walipewa fedha kwa ajili ya matengenezo ya Ofisi zao wanazozitumia, lakini wengine hawakupewa likiwemo pia Jimbo la Nkasi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba sasa fedha hizo zitolewe kwa Waheshimiwa Wabunge wote ikiwa ni pamoja na yale malimbikizo ambayo walipaswa kupata lakini hawakupewa? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa ni kweli kila tunapokuja hapa tunapata vitabu vingi na nyaraka mbalimbali ambazo zinatakiwa na Wapiga Kura wetu na Wananchi wengine waweze kuzisoma, lakini nyaraka hizo zimekuwa zikitunzwa majumbani na wengine kutokuona umuhimu wa kuzitunza na badala yake kuzichanachana. Je, Serikali itakubali kutoa fedha za dharura ili kuhakikisha kwamba makabati yanatengenezwa kwa ajili ya shughuli hiyo kama *Library* ndogo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, si sahihi sana kusema kwamba Waheshimiwa Wabunge walipewa fedha, hakuna Mheshimiwa Mbunge aliyepewa fedha kwa maana ya kukabidhiwa ili aweze kuzitumia kutengenezea Ofisi. Serikali ilichofanya katika Bajeti ya mwaka 2002/2003 na hata kabla ya hapo, walikuwa wameagiza Mikoa ijaribu kutenga fedha kwa ajili ya kutengeneza ya Ofisi za Waheshimiwa Wabunge ndani ya fedha zao za *OC*. Ndiyo maana mtaona kwa mwaka wa kwanza kilichofanyika kwa kweli kila Mkoa kulingana na *ceiling* waliyokuwa wamepewa, baadhi waliweza kutekeleza kiasi fulani cha majukumu hayo na wengine hawakuweza kutenga fedha zozote kabisa kwa sababu *ceiling* ilikuwa imewabana. Tulichofanya kwa mwaka 2003/2004, tukaitaka Mikoa sasa itenge fedha ndani ya *OC* ili ijulikane kabisa kila Wilaya na kila Ofisi ya Mbunge, imetengewa kiasi gani na ndiyo jedwali tulilolitoa juzi linajaribu kuonyesha jambo hilo.

Kwa hiyo, kwa kiasi fulani naweza kusema tu kwamba, ilikuwa ni utaratibu wa Kiserikali ndani ya Serikali yenyewe na hatukutoa fedha zozote kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge. Lakini tunakiri kwamba, zoezi hilo bado halikufanyika vizuri kwa sababu ya *ceiling* na uwezo mdogo wa Serikali. Kwa maana hiyo basi, uwezekano wa kusema kwamba kutakuwa na malipo ya malimbikizo, hayawezi kuwepo. Lakini tutakachofanya ni kuhakikisha kadri muda unavyokwenda na kadri fedha zinavyopatikana, tutazidi kuboresha hilo zoezi.

Kuhusu swali la pili, wapi waweke vitabu vyao na kwa nini Serikali isitoe fedha za dharura ili kuweza kukidhi kwa kiasi fulani mahali pa kuweka vitabu. Tutakachoweza kuwaambia tu Wakuu wa Mikoa ni kuona ndani ya fedha hizo walizotenga kutokana na *OC,* katika mambo watakayoyawekea kipaumbele, wajaribu kutumia utaratibu wa kutengeneza makabati kama hatua mojawapo ya dharura ili kukidhi jambo hilo kwa kiasi fulani.

Na. 306

**Kodi Zilizofutwa na Serikali**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED (k.n.y MHE. FRANK G. MAGHOBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imefuta kodi zote zilizokuwa zinawakera Watanzania na kwa kuwa baadhi ya kodi zilizofutwa ni pamoja na kodi za majengo, ng'ombe baiskeli na kadhalika:-

(a) Je, ni kitu gani kinachofanya baadhi ya Halmashauri kutotekeleza agizo la Serikali la kuondoa kero hizo hasa kodi ya majengo?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kutamka wazi kwamba Halmashauri zinazoendelea kutoza kodi za majengo ziache kufanya hivyo mara moja?

(c) Kama ikibainika kuwa hizo Halmashauri zilifanya kitendo hicho kwa makosa, je, Serikali itakuwa tayari kuwarudishia Wananchi hao fedha zao ambazo walilipa kodi za majengo wakati Serikali ilizifuta?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Frank Maghoba, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Serikali ilifuta baadhi ya kodi zenye kero kwa Wananchi zikiwemo zinazohusu baadhi ya nyumba za makazi ili kuhamasisha Wananchi kujihusisha zaidi na shughuli za uzalishaji na uwekezaji na Halmashauri zote zimetekeleza agizo hili. Agizo hili lilifuatiwa na marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na.9/1982 yaliyofanywa kupitia Sheria ya Fedha Na.15 ya 2003 *(Finance Act No. 15 of 2003)* iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (a) ya majibu yangu, siyo majengo yote ya makazi yaliyonufaika na uamuzi wa Serikali wa kufuta kodi ya majengo. Kwa mujibu wa Kifungu 4(b) cha Jedwali la Sheria ya Fedha Na.15 ya mwaka 2003, inayorekebisha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na. 9/1982, majengo ambayo hayatakiwi kulipia kodi ya majengo ni haya yafuatayo:-

(i) Muundo *(structure)* wowote ambao siyo jengo.

(ii) Jengo lolote ambalo halitumiki kwa madhumuni ya makazi.

(iii) Jengo lililosamehewa chini ya kifungu cha saba cha Sheria ya Kodi ya Majengo Na.2/1983 *(The Urban Authorities Rating Act No.2 of 1983).*

(iv) Jengo la makazi la tope *(Mud House).*

Kwa hiyo, endapo zipo Halmashauri zinazoendelea kutoza kodi ya majengo kwa majengo niliyoyaeleza, ninazitaka ziache mara moja. Kwa majengo mengine yote ambayo hayamo katika makundi haya niliyoyataja, Halmashauri zinaagizwa ziendelee kukusanya kodi hiyo ili fedha hizo ziweze kutumika katika kutoa huduma mbalimbali katika Halmashauri.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika sehemu (a) na (b), Serikali haioni kosa kwa Halmashauri kutoza kodi ya majengo, kwa majengo ambayo hayana msamaha wa kisheria nilioueleza. Hata hivyo, Ofisi yangu itafuatilia toka Halmashauri za Jiji la Dar es Saalam ili kuthibitisha iwapo utozaji wa kodi ya majengo unazingatia Sheria nilizozitaja na iwapo itabainika kukiukwa kwa Sheria husika, Halmashauri hizo zitatakiwa kurejesha fedha zilizokusanywa kinyume cha sheria kwa wahusika wote. *(Makofi)*

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali dogo na jepesi kama ifuatavyo:-

Baada ya kufutwa kwa kodi na ushuru wa aina mbalimbali kama mapato ya Halmashauri, je, ni vigezo vipi vinavyotumika katika kupata ile fedha kwa ajili ya kuwakopesha akinamama kama asilimia 10 ?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, baada ya uamuzi wa Serikali wa kufuta kodi pamoja na ushuru ambao ulionekana ni kero, Serikali ilichofanya ni kujaribu kufidia pengo linalotokana na vyanzo hivyo ambavyo Serikali ilikuwa imeamua kuvifuta. Vyanzo vingine vyote ambavyo havikufutwa kutokana na uamuzi wa Serikali, Halmashauri zinatakiwa kuendelea kukusanya kama ambavyo wamekuwa wakifanya zamani. Lakini Serikali inatazama namna pengine bora zaidi ambayo nadhani ndiyo itakidhi swali la Mheshimiwa Anatory Choya, la kuona kama tunaweza tukawa na misingi au vigezo ambavyo vinaweza pengine vikaonekana vinatenda haki zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Nasema hili kwa sababu baadhi ya maeneo walikuwa na vyanzo vyenye nguvu sana kwa maana kwamba, vilikuwa ni vyanzo vyenye mapato makubwa na wakati mwingine inawezekana hatufikii kiasi hicho na ndiyo maana unaona kunakuwa na hilo tatizo.

Na. 307

**Uhaba wa Walimu wa Sekondari Serengeti**

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wananchi wa Jimbo la Serengeti wamejitahidi kujenga shule za sekondari katika kata zote 18 lakini shule hizo zina matatizo ya uhaba wa walimu na vifaa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzipatia walimu na vifaa vya kutosha shule hizo?

(b) Je, Serikali imezipatia walimu wangapi na vifaa gani shule hizo tangu mwaka 1997 - 2004 kwa orodha katika kila shule?

(c) Je, ni wanafunzi wangapi kutoka shule hizo wamefaulu na kupata *Division One* tangu mwaka 1997 - 2005 na Serikali inaweza kukiri kuwa kufanya vibaya kwa wanafunzi katika shule hizo ni kwa sababu ya kutozipatia walimu na vifaa vya kutosha?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha, Mbunge wa Serengeti lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mpango wa Serikali wa kuzipatia shule hizo walimu na vifaa vya kutosha ni ule Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES 2004 - 2009). Katika mpango huo matatizo ya upungufu wa walimu na vifaa yamepewa kipaumbele. Serikali imeamua kuongeza nafasi katika Vyuo vya Ualimu vilivyopo na kukibadilisha Chuo cha Ualimu cha Dar es Salaam na shule ya Sekondari ya Mkwawa kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa lengo la kuwapata walimu bora wa Stashahada na Shahada wa kutosha. Aidha, Vyuo vingine ya Ualimu wa Stashahada kuanzia na kile cha Mtwara, baada ya marekebisho vitakuwa Vyuo Husishwa, yaani *Associated Colleges* ya hivyo Vyuo Vikuu Vikuu Vishiriki ili navyo vitoe Stashahada ile ile ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambayo itakuwa sawa na mwaka wa kwanza wa shahada ya Ualimu.

(b) Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 1997 na 2003, jumla ya walimu 67 walipangwa kufundisha katika Sekondari za Wilaya ya Serengeti. Aidha, kati ya walimu 20, walimu 12 wakiwa wa Sayansi na wanane wakiwa wa masomo ya *Arts,* wamepangwa Sekondari za Wilaya ya Serengeti mwezi Juni, 2004 tukiwa hapa Bungeni. Orodha ya Walimu kwa kila shule ya sekondari katika Wilaya hiyo imeonyeshwa kwenye Jedwali Namba 1 ambalo Mheshimiwa Mbunge, atapewa au amekwishapewa.

(c) Mheshimiwa Spika, Shule za Sekondari za Natta, Kisaka na Rigicha ni shule mpya zilizofunguliwa mwaka huu wa 2004 na sekondari za Ikoma na Ikorongo zilianza mwaka 2002. Kwa hiyo, hazijapata wanafunzi wa Kidato cha nne. Matokeo ya Shule za Sekondari za Dr. Omari Juma, Kambarage Kisangura, Machochwe, Ngoreme, Ring'wani na Serengeti kuanzia mwaka 1997 hadi 2003 ni kama ifuatavyo: Daraja la kwanza wanafunzi sita sawa na asilimia 3.2. Daraja la pili, watahiniwa 14 sawa

na asilimia 7.5, daraja la tatu, watahiniwa 39 sawa na asilimia 21. Jumla daraja la kwanza mpaka la tatu ni 59 sawa na asilimia 31.7 na daraja la nne ni 127 sawa na asilimia 68.3 kati ya jumla ya watahiniwa 186. Matokeo hayo kwa kila shule yamo katika Jedwali Namba 2 ambalo nalo atapewa Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kufanya vibaya kwa wanafunzi katika shule hizo, pamoja na ukosefu wa walimu na vifaa kunatokana pia na mazingira yasiyoridhisha ya kusomea na kufundishia, utayari mdogo wa wanafunzi wenyewe kujituma kusoma kwa bidii, msingi mdogo wa taaluma wa wanafunzi wanaoingia Kidato cha Kwanza na ukosefu katika baadhi ya shule wa huduma muhimu kama vile maji, umeme, nyumba za walimu, madarasa na maabara ya kutosha.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, shule hizi ni muda mrefu hazijatembelewa na *senior* yeyote kutoka Wizarani hasa Mheshimiwa Waziri ili aweze kujionea matatizo ya hizi shule. Je, yuko tayari kwenda Serengeti na kuzitembelea ili aweze kuona matatizo ya hizo shule?

**SPIKA:** Jibu fupi Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Dr. James Wanyancha kwamba, shule hizo mimi mwenyewe sijazitembelea. Nadhani kwa kweli amenilenga mimi kwa sababu wengine kama vile Wakaguzi wa kanda huwa wanafika kufanya ukaguzi. Kwa hiyo, napenda kumhakikisha kwamba, ninayo nia kubwa ya kufika katika maeneo na katika Mikoa na Wilaya kule ambako sijafika tangu nimeteuliwa kuwa Waziri. Kwa hiyo, katika mipango ya kipindi hiki kilichobaki, nitahakikisha nafika katika shule hizo na katika Jimbo lake Mheshimiwa Dr. James Wanyancha.

Na. 308

**Bajeti ya Wizara ya Elimu Kuhusu Walimu**

**MHE. ESHA H. STIMA** aliuliza:-

Kwa kwa kila mwaka katika bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni hutengwa fedha kwa ajili ya huduma mbalimbali za walimu nchini yakiwemo matibabu; na kwa kuwa walimu bado wanahangaika kujitibu kwa fedha zao wenyewe na kuwa kero kwa familia zao kutokana na mishahara yao kuwa midogo sana:-

(a) Je, Serikali inatuma kiasi gani cha fedha kwenye Halmashauri au Manispaa au Miji kwa matibabu ya walimu wote nchini?

(b) Je, Serikali inafuatilia kujua kama fedha hizo zinatosha kwa matibabu yao?

(c) Je, watumishi waliopo Wizarani wanatengewa kiasi gani na uwiano wa fedha hizo ukoje kwa Wilaya zote za Mkoa wa Shinyanga?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esha Hassan Stima, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, fedha zinazotengwa katika bajeti ya Wizara yangu kwa ajili ya huduma mbalimbali yakiwemo matibabu hazitumwi kwenye Halmashauri bali hutumwa moja kwa moja kwenye shule ya sekondari au Chuo cha Ualimu ama Ofisi ya Wakaguzi wa shule wa Kanda na Wilaya husika kwa njia ya *Warrant of Funds.* Matibabu ya watumishi wote wa Serikali wakiwemo walimu hutolewa na Mfuko wa Bima Afya. Aidha, magonjwa yasiyohudumiwa na Mfuko huo, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ilikwishatoa Waraka Na.C/AC/45/126/01/A/54 wa tarehe 6 Mei, 2003, unaofafanua kuwa itaendelea kutoa huduma zote ambazo hazitatolewa chini ya Sheria ya Bima ya Afya Na. 8 ya mwaka 1999.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya huduma mbalimbali yakiwemo matibabu kwa watumishi wake, zilikuwa hazitoshi, ndiyo maana Serikali ilichukua hatua za kuanzisha Mfuko wa Bima ya Afya kwa sheria iliyopitishwa na Bunge hili. Mfuko huu unaendelea kuimarika na kuboresha huduma kwa wanachama wake wote wakiwemo walimu. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, itaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuona kuwa Mfuko huu unaimarishwa ili uweze kutoa huduma bora na huduma iliyo endelevu.

(c) Mheshimiwa Spika, hakuna fedha za matibabu zinazotengwa kwa ajili ya watumishi walioko Wizarani peke yao. Wizara yangu inahudumia watumishi wote kwa ujumla wao bila kubagua kati ya wale wa Makao Makuu na wengine walio katika Vyuo vya Ualimu, Shule za Sekondari na Ofisi za Wakaguzi Wakuu wa Shule wa Kanda na Wilaya.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, nilikuwa naomba anipe jibu kuhusu matibabu ya walimu hao kupitia Bima ya Afya. Je, anaelewa kwamba Bima ya Afya haitoi fedha za kuweza kupata lishe wanapokuwa wanaugua na kwamba hiyo ndiyo sababu mojawapo ya walimu wanamalizika kwa vifo kila mwaka kutokana na matatizo ya lishe? *(Makofi)*

La pili, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba hatofautishi malipo ya matibabu kwenye Wizara yake kwa watumishi wa Wizara na walimu katika nchi nzima. Kwa nini mafungu yanatofautiana ya Wizara yanakuwa makubwa na ya Mikoani yanakuwa madogo kama hakuna ubaguzi wa matibabu kati ya watu wachache waliopo Wizarani na wale ambao wako wengi Mikoani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza kuhusu tiba inayotolewa chini ya Mfuko wa Bima ya Afya hailipi lishe, kwa hiyo, ndiyo maana tunapata vifo vingi vya walimu. Inawezekana hali hiyo ndivyo ilivyo, lakini hivyo ndivyo ilivyo pia sheria iliyotungwa na Bunge hili kwamba watalipiwa mahitaji ya madawa na siyo mahitaji ya chakula, ndivyo ilivyosema Sheria tuliyotunga hapa Bungeni. Isipokuwa tu pale kama aina za vyakula vinavyohitajika vinaendana na dawa anayotakiwa kupata mgonjwa. Kwa hiyo, Madaktari huchanganya vyakula vile katika *prescription* wanayoitoa.

Sasa swali la pili, kwamba kuna tofauti kati ya fedha. Mimi nadhani Mheshimiwa Mbunge, anachanganya kidogo. Kati ya walimu wanaohudumiwa au wanaosimamiwa na Wizara yangu na walimu wa shule za msingi ambao hao kutokana na utaratibu wa mageuzi ya Serikali za Mitaa, wao malipo yao yanapitia Wizara ya TAMISEMI. Kwa hiyo, labda amepima mafungu hayo na yale yaliyoko Wizarani. Jibu langu limezingatia wale wanaolipwa na *Vote 46,* ambazo ndizo fedha zinazokuja katika Wizara yangu. Nina hakika akiangalia kwa *Vote 46* atakuta fedha za matibabu zimewekwa katika fungu moja linalowahudumia walimu wote wanaosimamiwa na Wizara yangu.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, swali langu nililotaka kumwuliza linahusiana na walimu hasa wanapofariki, lakini kwa kuwa ameeleza kwamba, hiyo inashughulikiwa na Wizara ya TAMISEMI, ndiyo maana nikaona kwamba sina sababu ya kuuliza tena swali.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Na. 309

**Umeme Kuzimika na kurudishwa Ghafla**

**MHE. EDSON M. HALINGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Shirika la Ugavi wa Umeme *(TANESCO)* huzima umeme na kuurudisha ghafla na kusababisha vifaa vingi vinavyotumia umeme kama vile redio, majiko na *video* kuungua na kusababisha hasara kubwa kwa mteja:-

(a) Je, kosa hilo linapotokea nani alaumiwe?

(b) Je, nani anapaswa kugharamia uharibifu huo wakati *TANESCO* hujilinda kwa visingizio vingi?

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kuleta Muswada Bungeni ili ajali zinazosababishwa na kasoro za umeme ziwe zinafidiwa vilivyo na Shirika hilo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edson Mbeyale Halinga, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye vipengele (a), (b) na (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* hulipa wateja wanapoharibikiwa mali zao pale inapodhihirika kuwa uharibifu umetokana na uzembe wa *TANESCO* yenyewe katika utendaji wa kazi

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuomba fidia ni kwa mteja kuandika barua kwa Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa au Ofisi ya *TANESCO* ya jirani mara inapotokea ajali.

Pia ni vyema kwa Wananchi wafahamu kwamba, vitu vilivyoharibika wakati wa ajali vinaweza kuhitajika kwa ajili ya ukaguzi na uthibitisho, hivyo, ni vyema vitunzwe ili vithibitishwe wakati wa kuhakiki.

Mheshimiwa Spika, sheria inayohusu usambazaji wa umeme inamlinda mtumiaji wa umeme kama inavyomlinda mtoa huduma hiyo *(TANESCO)*. Sheria inampa nafasi mteja aliyeathirika na moto unaodhaniwa kuwa chanzo chake ni umeme kukata rufaa kwa Waziri endapo hataridhika na maelezo yaliyotolewa na *TANESCO* baada ya uchunguzi kufanyika. Waziri kwa sheria hiyo, anayo mamlaka ya kumteua mchunguzi wa kujitegemea *(Independent Inspector),* ambaye atachunguza chanzo halisi cha moto na kuwasilisha ripoti ya uchunguzi kwa Waziri mwenyewe, ambaye atafanya maamuzi ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, aidha, muathirika anayo nafasi ya kuomba msaada wa kisheria kutoka Mahakamani akiona hata uamuzi wa Waziri haumtoshelezi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha mipango ya kuunda Wakala wa Kusimamia Sekta za Umeme na Maji *(Energy and Water Utilities Regulatory Authority - EWURA),* ambao pia kwa mamlaka watakayopewa, watalinda maslahi ya watoa huduma na wapokea huduma wa sekta hizi mbili.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni mazuri.

La kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri, anafahamu kwamba wateja wengi huweka vyakula vyao kwenye mafriji na wanapozima umeme bila taarifa, vyakula vingi huharibika, je, nani adaiwe fidia katika hasara hizo?

La pili, kwa kuwa majengo mengi yanayopata ajali ya kuungua inasemekana ni tatizo la nyaya kwa kosa la kiufundi. Je, Shirika linahusika vipi katika hasara hizo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nafahamu kwamba, umeme unapozimwa na kama kuna chakula katika friji au *freeze,*

kama umeme utazimwa kwa muda mrefu huenda chakula hicho kikaharibika. Lakini nimesema katika ujumla wake kwamba, panapotokea hitilafu au uharibifu ambao unaonekana chanzo chake ni *TANESCO,* kwa uunguaji wa vifaa na huhitaji fidia, kwa ujumla mteja anayo haki ya kupeleka malalamiko yake *TANESCO*. Lakini ningependa pia ifahamike kwamba, *TANESCO* ni Shirika letu, ikiwa kila wakati ambapo umeme ukizimika pakiharibika samaki au nyama tutakwenda kuomba fidia *TANESCO,* itakuwa kazi kubwa sana. Lakini katika ujumla wake, nimesema hapo awali kwamba, pale ambapo pana uthibitisho kwamba kuna hasara kubwa imetokea, basi wapeleke malalamiko *TANESCO* na *TANESCO* imekuwa wakati hadi wakati, ikilipa fidia pale inapoonekana kwamba panastahili kulipwa fidia.

Kuhusu majengo, kama ambavyo nimejibu katika Bunge hili hili kama mara mbili hivi kuhusu suala la moto unaosababishwa na umeme, inategemea kama nilivyosema awali na chanzo chenyewe ni nini. Kama uunguaji wa majengo yale unatokana na hitilafu ambayo chanzo chake ni *TANESCO,* utaratibu kuhusu majengo ni mkubwa zaidi kwamba unahusisha hata Shirika la Zimamoto, unahusisha na hata Polisi. Kwa hiyo, ukaguzi katika eneo hili kwa kweli unakuwa ni wa uhakika zaidi katika kulinda maslahi ya mteja.

Na. 310

**Mradi wa Kusaidia Wachimbaji Wadogo Wadogo**

**MHE. NJELU E. M. KASAKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Waziri katika hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2001 alitangaza juu ya kuanzishwa kwa mradi wa kusaidia wachimbaji wadogo wadogo Wilayani Chunya kwenye Kijiji cha Matundasi:-

(a) Je, utekelezaji wa mradi huo umefikia wapi na ni lini utakamilika?

(b) Je, ni sababu zipi za kiuchumi au za kiufundi zinazosababisha kusiandaliwe mradi mkubwa wa kuchimba dhahabu Wilayani Chunya?

(c) Je, kuna ukweli gani kwamba Migodi ya Saza na Itumbi iliyofungwa muda mfupi kabla ya Uhuru mwaka 1961 ilifungwa kwa sababu za kisiasa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, shughuli za ufungwaji mtambo zimekwishakamilika na kinachoendelea hivi sasa ni kukamilisha hatua za mwisho za majaribio ya kiufundi ya mtambo wenyewe ikifuatiwa na mafunzo maalum kwa watumishi wa uendeshaji mtambo kituoni na baadaye kufanya makabidhiano ya

kituo kutoka kwa mkandarasi kwenda kwa Wizara husika. Taratibu za makabidhiano zimepangwa kufanyika mwezi Oktoba, 2004.

(b) Utafiti ambao umeshafanyika hadi sasa unaonesha kuwa hakujagunduliwa mashapo ya kutosha kwa uanzishaji wa mradi mkubwa wa uchimbaji dhahabu Wilayani Chunya, ni migodi mikubwa.

Mheshimiwa Spika, miamba ya dhahabu iliyopo Lupa ni miembamba na dhahabu haikuenea kwa kiasi cha kutosha kwenye miamba mingine hivyo kusababisha uhaba wa dhahabu ya kutosha katika eneo husika. Kwa sababu hiyo, sio rahisi kwa wawekezaji wakubwa kuwekeza eneo la Lupa. Lakini ningependa niongezee kuwa, kama Mheshimiwa Mbunge anao wawekezaji wakubwa ambao pamoja na mazingira hayo, wako tayari kwenda Lupa, sisi kama Wizara tuko tayari kushirikiana nao.

(c) Mwisho, si kweli kwamba, migodi ya dhahabu ya Saza na Itumbi ilifungwa muda mfupi kabla ya Uhuru mwaka 1961 kwa sababu za kisiasa. Sababu zinazofahamika ni kuwa mgodi huu ulifungwa kutokana na kushuka kwa bei ya dhahabu na kutokana na gharama za sasa za uendeshaji mgodi kuwa kubwa.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nilitaka niulize swali moja la nyongeza. Ule mtambo wa Gaga wa kusafisha dhahabu kwa wachimbaji wadogo tatizo hasa ni nini, hata baada ya mwaka mmoja baada ya ziara ya Waziri bado haujawa tayari kufanya kazi, shida yake hasa ni nini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa ufupi tu ni kwamba, mtambo ule ulikuwa ukikabiliwa na matatizo ya kiufundi ambayo yamekuwa yakifanyiwa kazi. Ningependa nichukue nafasi hii kwa kweli kumshukuru Mheshimiwa Njelu Kasaka, kwa kufuatilia sana suala hili na kushirikiana na Wizara katika kuhakikisha kwamba, mtambo huu unafanya kazi.

Na. 311

**Kambi ya Jeshi ya Makoko**

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kazi za kusimamia ulinzi wetu zinazofanywa na wapiganaji wetu ni kazi muhimu na nyeti; na kwa kuwa, ili wapiganaji na Makamanda wa Jeshi waweze kutekeleza wajibu wao ni lazima juhudi za dhahiri zifanywe ili kuwapatia huduma muhimu ikiwa ni pamoja na Maji, Makazi bora na kadhalika; na kwa kuwa, Kambi ya Jeshi Makoko ilikuwa na tatizo la makazi kwa kucheleweshwa kukamilika kwa ujenzi wa nyumba kwenye kambi hiyo:-

(a) Je, Serikali imefikia wapi katika mpango wa kuwapatia Maji Wanajeshi wa kambi hiyo na kama imekamilishwa ni gharama kiasi gani zimetumika?

(b) Je, ahadi iliyotolewa na Serikali wakati wa kipindi cha Bajeti ya 2003/2004 kuhusu kukamilisha nyumba za kambi hiyo imefikia wapi?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wapiganaji hao usafiri wa uhakika *(Public Transport)?*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (k.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahimu Wankanga Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mpango wa kuwapatia maji Makamanda na wapiganaji wa Kambi ya Makoko (Musoma) toka Ziwa Victoria, uko katika hatua za mwisho. Kwa kushirikiana na Mhandisi wa Maji wa Mkoa, bomba kubwa limewekwa toka ziwani hadi Kambini, pamoja na kujenga tangi kubwa la maji lenye ujazo wa lita laki mbili na ishirini na tano elfu. Kazi hiyo imekamilika mwishoni mwa Mei, 2004. Kazi inayoendelea hivi sasa ni kutandaza mabomba kutoka kwenye tangi kwenda kwenye maeneo mbalimbali kambini.

(b) Mheshimiwa Spika, zoezi la kukamilisha viporo vya nyumba za Kambi za Makoko linaendelea vizuri chini ya kikosi cha ujenzi cha JKT. Hivi sasa nyumba 84 zinajengwa ambazo zitakidhi mahitaji ya familia 336. Nyumba hizo zitakamilika ifikapo Desemba, 2004.

(c) Mheshimiwa Spika, Jeshini tatizo la usafiri na usafirishaji limezingatiwa katika mpango kamambe wa maendeleo wa miaka mitano ya uboreshaji wa Jeshi ulioanza mwaka 2003 - 2008. Mpango huu si kwa ajili ya kuimarisha usafiri wa nchi kavu peke yake, bali pia usafiri wa majini na angani. Kuhusu usafiri wa nchi kavu, ununuzi wa magari ya aina mbalimbali kwa ajili ya usafiri na usafirishaji utazingatiwa katika bajeti ya kila mwaka. Hata hivyo, jitihada kubwa zimefanywa, kuhakikisha karakana kuu ya Jeshi, Lugalo imekarabatiwa kwa ajili ya matengenezo na ufufuaji magari na pia karakana za vikosi zitakarabatiwa kwa kusudi hilo hilo.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri na pia kwa hatua ambazo Serikali imezichukua toka mwaka 2003 hadi sasa kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza.

Kwa sababu mradi huo wa maji unapita eneo ambalo kuna wakazi ambao ni raia na kwa kuwa ndugu zetu Wanajeshi wamekuwa wakisaidiana sana na raia kwa maana ya Wananchi wetu, je, Waziri ana mpango gani kuhakikisha kwamba, mradi huu wa maji unaotoka ziwani kuja kwenye nyumba za Jeshi utawanufaisha na wakazi wa Makoko linakopita bomba hilo la maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, tunashukuru kwa pongezi alizozitoa kwa Wizara yetu, zinatutia moyo na tunaomba tuendelee kushirikiana naye katika kuhudumia Wanajeshi wetu.

Kuhusu huu mradi kama utahudumia raia wanaoishi karibu na kambi, napenda kusema kwamba, kwanza, juhudi inayofanywa sasa hivi ni kuhakikisha kwamba, haya maji yanawafikia walengwa ambao ni Wanajeshi. Tukishakamilisha hilo sasa tutatazama uwezekano wa kuwasaidia majirani kama tunavyosaidia katika huduma mbalimbali kama huduma za afya, majirani wanapata huduma za afya katika vikosi vyetu vya Jeshi. Kwa hiyo, hata hili nalo linawezekana. Ngoja kwanza tumalize tuwafikishie Wanajeshi halafu hilo nalo litakuja tu. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Ibrahimu Marwa kwamba, uwezekano upo, tuwe na subira. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi napenda kuwapongeza sana Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kwa jinsi ambavyo wanashirikiana vizuri sana katika huduma za jamii kuwapa Wananchi maji pale inapowezekana.

Ningependa kumuahidi Mheshimiwa Ibrahimu Marwa kwamba, Wizara yangu italifuatilia jambo hili kuhakikisha kwamba Wananchi wanapata maji safi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakuona Mheshimiwa Membe lakini kambi ya Makoko iko Musoma haiko Lindi.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa katika majibu yake ya kifungu (c), Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuwapatia Wanajeshi usafiri wenye uhakika na kwa kuwa huko nyuma askari au Wanajeshi walikuwa wanapata mikopo kwa ajili ya kununua magari hasa mwaka 1995/96. Je, Waziri yupo tayari katika huo mpango wa kuhakikisha usafiri mzuri kwa Wanajeshi, waendelee kupatiwa mkopo wa magari ili kuwawezesha kusafiri kutoka kazini na kurudi majumbani kwao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu lilihusu hasa usafiri ule wa Serikali *(Public Transport).* Nilisema kwamba, hilo tunalitazama katika bajeti zetu kuhakikisha kwamba, vikosi vyetu vya Majeshi mbalimbali vinapata huduma ya magari na katika bajeti ambayo tutaomba wiki ijayo muipitishe humu ndani, tumeomba fedha za kununua magari kwa ajili ya vikosi vya Jeshi, nafikiri mtatupitishia.

Kuhusu suala la mikopo ambalo kusema kweli halimo moja kwa moja katika swali hili, utaratibu ule upo kwa Serikali nzima pamoja na majeshi haujafutwa. Kwa hiyo, nataka kuhakikisha kwamba, utaratibu ule bado upo.

Na. 312

**Ada ya Cheti cha Kuzaliwa**

**MHE. HAROUB SAID MASOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipokuwa ikijibu swali Na. 54 la Mheshimiwa Mutungirehi hapo tarehe 7 Novemba, 2003 ilisema kwamba, jukumu la kumhudumia mtoto anapozaliwa sio la mama peke yake bali ni la wazazi wote wawili na kwamba ni wajibu wao kutimiza wajibu huo kwa mtoto wao ikiwa ni pamoja na kumlipia ada ya Sh. 3,500/= kwa ajili ya cheti cha kuzaliwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa cheti cha kuzaliwa bure au kwa nusu ya ada kwa wale wanawake maskini waliokubuhu ambao wamezaa watoto bila kuwajua baba zao?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, kama ifuatavyo:-

Kwanza, napenda kumshukuru Mheshimiwa Haroub Said Masoud, kwa kutambua kuwa wajibu wa kumtunza na kumlea mtoto ni wa wazazi wote. Aidha, nakubaliana naye kwamba, wapo akina mama walioachiwa jukumu la kuwatunza watoto ambao hawafahamu baba zao. Akina mama hawa hufanya kazi kubwa ya kuwalea watoto wao wenyewe ikiwa ni pamoja na kuwatafutia chakula, mavazi, kugharamia elimu yao na mahitaji yao mengine mengi.

Hata hivyo, Serikali kwa sasa haina mpango wa kufuta au kupunguza kwa namna yoyote ile ada ya cheti cha kuzaliwa kwa sababu zifuatazo:-

- Ada yenyewe ni ndogo kwa mzazi mwenye nia na anayeelewa umuhimu wa cheti cha kuzaliwa. Utafiti wetu unaonyesha kuwa watoto wengi wameandikishwa na kupata vyeti katika kipindi hiki ambacho ada ya cheti ni Sh.3,500/= kuliko ilivyokuwa Sh. 5/= katika miaka ya 1990 na kurudi nyuma.

- Tayari zipo gharama za uchapishaji vyeti vya kuzaliwa na nyaraka nyinginezo zinazohusiana na utoaji wa cheti cha kuzaliwa kama vile *Registers* na *Forms* mbalimbali zihusuzo usajili.

- Aidha, Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu ambayo ina jukumu la usajili wa vizazi iko katika hatua za kuwa Wakala wa Serikali *(Executive Agency).* Vyanzo vya mapato yake ni pamoja na ada ya vyeti vya kuzaliwa.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, inaonesha anakubaliana nami kuwa wapo wanawake wanaozaa watoto bila kuwajua baba zao. Lakini juu ya hayo yote, amekwepa kutoa angalau unafuu wa malipo ya ada ya cheti. Sasa, je, Mheshimiwa Waziri anatoa tamko gani kwa wale akinamama wanaowadekeza wanaume wasio waaminifu ambao baada ya kuwapa mimba wanawaacha hoi na kuwakimbia? *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza sijakwepa kujibu swali lenyewe. Niliyoyasema ni sahihi na ndio utaratibu wenyewe. Lakini ningependa nichukue nafasi hii, kukubaliana naye kwamba, wako wanawake ambao wanadanganywa. Kwa mfano, Dar es Salaam unaweza ukakuta kwamba, vijana hata wazee wanawadanganya hawa wasichana kwamba watawaoa na wanadiriki hata kuwapeleka hawa wachumba kwa wazazi wao kuwatambulisha na wengine hata kutoa mahari kidogo. Lakini baada ya kufanya hayo pia humpa mwanamke yule masharti kwanza lazima utunge mimba halafu tutaona kama tutaoana na baada ya hapo kijana hubonyea. Mara utashtukia kwamba, amepata mchumba mwingine, anapiga matarumbeta anakwenda kuoa mwanamke mwingine.

Kwa hiyo, haya nakubaliana na Mheshimiwa Haroub Said Masound, lakini nasema kwa wanawake namna hiyo basi kama wamedanganywa, Mahakama zetu zipo, kuna *Affiliation Ordinance,* wanaweza kwenda kuwashtaki Mahakamani kwa udanganyifu. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Waziri, napenda anithibitishie aliposema kwamba malipo ya kuzaliwa watoto ni shilingi 3,500/=, ina maana wale wanaolipa shilingi 5,000/= hizo Sh. 1,500/= wanazipeleka wapi katika Wizara yake?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, fedha hizi zinagawanyika katika mafungu mawili. Kuna ada ya uandikishaji au ni shilingi 1,500/= na pia kuna ada ya cheti chenyewe ambayo ni shilingi 2,500/= jumla ni shilingi 3,500/= na hizi hukusanywa na Wakala wa Kabidhi Wasii katika Wilaya. Wenyewe baada ya kukusanya zile fedha basi huziwasilisha kwa Kabidhi Wasii.

Na. 313

***Mkomazi Game Reserve* Kuwa *National Park***

**MHE. JOHN E. SINGO** aliuliza:-

Kwa kuwa Wananchi wa Wilaya ya Same wanayo shauku kubwa ya kuona Hifadhi ya Wanyama ya Mkomazi *(Mkomazi Game Reserve)* ikifanywa kuwa Hifadhi ya Taifa *(National Park);* na kwa kuwa kuwepo kwa Hifadhi ya Taifa kutakuza uchumi wa Wilaya hiyo:-

(a) Je, ni lini Serikali itapitisha uamuzi wa kupandisha Mbuga za Mkomazi kuwa Hifadhi ya Taifa *(National Park)?*

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kujenga Bwawa la Chato katika Mbuga hiyo kufuatia ahadi ya Wizara katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge?

(c) Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kuweka mazingira ya ushindani na ya kuvutia ya Mbuga zetu dhidi ya yale ya hifadhi tunayopakana nayo ya Tsavo nchini Kenya?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imepokea mapendekezo ya Wananchi wa Wilaya ya Same ya kutaka kupandisha hadhi ya Pori la Akiba la Mkomazi kuwa Hifadhi ya Taifa. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wizara itayapa mapendekezo hayo uzito unaostahili na naahidi kwamba, suala hilo litaanza kufanyiwa kazi rasmi mwaka 2005/2006.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliahidi kuchangia sehemu ya gharama za ujenzi wa Bwawa la Chato, nilipokuwa najibu swali Na. 67 wakati wa Mkutano wa 15 wa Bunge la Bajeti ya 2003/2004. Kwa kuwa gharama za ujenzi wa bwawa hilo ni zaidi ya shilingi 415,541,600/=, Wizara ilimwandikia Mheshimiwa Mbunge, barua Kumb. Na. AB. 290/315/01 ya tarehe 27 Aprili, 2004 ili kuweza kujua mchango wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Same. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, kwa kushirikiana na pande husika, watuletee gharama hizo mapema ili Wizara iweze kutenga fungu katika bajeti ya 2005/2006.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Wahisani, tokea zamani imekuwa ikitoa maelezo kuhusu juhudi zinazofanyika katika kuyafanya maeneo ya hifadhi likiwemo Pori la Mkomazi kuwa ya kuvutia zaidi. Kwa Pori la Akiba la Mkomazi/Umba, juhudi zimeendelezwa katika kuweka mazingira bora ili kukuza na kudumisha utalii wa picha. Baadhi ya juhudi hizo ni pamoja na kujenga kituo cha habari kwa watalii *(Visitor Information Center)* kwenye lango la Zange ambapo jengo limekamilika. Aidha, samani na taswira za ndege zimewekwa na hivi sasa kituo hiki kinatumika. Vile vile, Mabwawa ya Dindira na Kavateta yamefanyiwa matengenezo kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa maji kwa ajili ya wanyamapori.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda kufahamu kwamba kuna sababu gani za uamuzi wa Mbuga ya Mkomazi kuwa *National Parks* kuchukua muda mrefu wakati kikao cha *RCC* Mkoani Kilimanjaro kilishapeleka maombi hayo kuanzia mwezi Septemba, 2003 na sasa karibu miaka miwili, mitatu itakuwa imekwisha?

La pili, kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, ameahidi kuchangia gharama za Bwawa la Chato na Halmashauri ya Wilaya ya Same iko tayari kuchangia. Je, Mheshimiwa Waziri anasema nini katika mwaka huu wa fedha kuhusu ujenzi wa bwawa hilo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwamba, tutakuwa tayari kuchangia, kwa sababu tunaelewa kwamba, bwawa hilo hasa ni kwa ajili maji kwa ajili ya mifugo. Wizara husika (Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo), ndiyo ambayo imeleta mapendekezo haya ya shilingi 415,541,600/=. Kwa kweli Mheshimiwa Mbunge, atakubaliana na mimi hivi juzi tu wiki iliyopita ambapo tulizungumza na nikapata makadirio hayo. Kwa sababu makadirio hayo kwa kweli hayajaletwa moja kwa moja kwetu sisi, kwa hiyo, kwa wakati huu bajeti ilikuwa tayari imeshafanyika na kwa maana hiyo isingewezekana. Lakini kama nilivyojibu ni kwamba, itawezekana kwa Wizara yangu kuweza kuchangia katika bajeti inayokuja na kwa kujua pia Wizara husika pamoja na Halmashauri itaweza kufanya hivyo.

Kuhusu suala la kupandisha hifadhi kwamba imechukua muda mrefu. Masuala haya ya kupandishwa hifadhi ni jambo ambalo si rahisi mara moja. Kwa sababu lazima tuangalie kwanza hifadhi ile ina wanyama wa aina gani, inawezekana kuwa hifadhi ya *National Park* na kadhalika. Nataka nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni kikao cha *RCC* kwa barua ya Mheshimiwa Mbunge, aliyoniletea tarehe 18 Machi, 2004. Kwa hiyo, ni mwezi wa Machi. Hapo anasema katika maongezi hayo uliahidi kupandisha daraja la *Mkomazi Game Reserve* kuwa *National Park* na kunitaka nikuletee mapendekezo ya Kamati ya Ushauri wa Mkoa *(RCC)*. Kwa msingi wa maelezo haya, naambatisha barua ya kikao cha *RCC* Kilimanjaro, Kumb. Na. D.30/100 Vol.11/55 ya tarehe 15 Januari, 2004, iliyoidhinisha pendekezo hilo. Kwa hiyo, kwa kweli ni Januari, 2004 ndipo *RCC* iliidhinisha suala hilo.

Na. 314

**Mipaka ya Hifadhi ya Liparamba**

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wizara ya Maliasili na Utalii imepeleka fedha kwa ajili ya kutengeneza mipaka ya Hifadhi ya Liparamba - Wilaya ya Mbinga, kazi inayofanyika na wataalam kwa shida kwa sababu ya ukosefu wa gari na kwa kuwa ulinzi umeimarishwa katika hifadhi hiyo hivyo wanyama wa kila aina wanaongezeka sana:-

(a) Je, Serikali iko tayari kupeleka gari kwa ajili ya hifadhi hiyo?

(b) Je, ujenzi wa majengo mbalimbali muhimu kwa ajili ya hifadhi hiyo utaanza lini?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, naomba kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Pori la Akiba la Liparamba lilitangazwa rasmi kuwa Pori la Akiba kwa tangazo la Serikali Na. 289 la tarehe 18 Agosti, 2000. Pori linasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kwa kushirikiana na Wizara yangu. Kuanzia mwaka 2002/2003 hadi 2003/2004, Wizara yangu imetoa jumla ya shilingi milioni ishirini na tatu ili kuwezesha usimamizi na uendelezaji wa Pori la Akiba la Liparamba. Shughuli hizi zimekuwa zinasimamiwa na Afisa Wanyamapori wa Wilaya ya Mbinga.

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia shughuli za uhifadhi kwenye Pori la Akiba la Liparamba, mambo yafuatayo yametekelezwa tangu mwaka 2002/2003 hadi sasa: Kufanya doria katika maeneo mbalimbali ya Pori zilizopelekea kutegua mitego 550, kukamata silaha 210, kukamata majangili 12 na kudhibiti ukataji wa miti na kupasua mbao ndani ya hifadhi, kushirikisha jamii kwa kuwapatia elimu ya uhifadhi, kutengeneza barabara zenye urefu wa kilometa 134, kKusafisha mipaka ya pori urefu wa kilometa 88 na kutengeneza madaraja sita pamoja na kuharibu madaraja yanayotumika kwa shughuli za uhalifu ndani ya pori.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu imejumuisha gharama ya kununua gari moja jipya kwa ajili ya kufanyia kazi katika Pori la Akiba la Liparamba katika bajeti ya mwaka 2004/2005.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa majengo mbalimbali muhimu kwa ajili ya Pori la Liparamba, utaanza katika mwaka 2005/2006 baada ya kufanya tathmini ya mahitaji ya majengo na gharama zake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, ameridhika na muda wa maswali umekwisha, kwa hiyo, tunaendelea na mambo mengine.

Kwanza, matangazo ya vikao vya leo. Kamati nne za Kudumu zimepangiwa kufanya vikao vyake leo. Ya kwanza, ni Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Dr. William Shija, anaomba Wajumbe wake wakutane saa 5.00 asubuhi hii katika ukumbi Na. 219 ghorofa ya pili. Kamati nyingine ni Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Njelu Kasaka, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo saa 5.00 asubuhi kwa madhumuni ya kupitia Muswada wa Fedha *(The Finance Bill)* katika chumba Na. 231 ghorofa ya pili.

Kamati ya tatu, ni Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, anaomba Wajumbe wakutane chumba namba 428 ghorofa ya nne kuanzia saa 7.00 mchana.

Kamati ya mwisho, aah hii siyo Kamati, hii ni *Common Parliamentary Associatian (CPA)*, Tawi la Tanzania, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jackson Makwetta, anaomba Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya *CPA* Tawi la Tanzania, wakutane leo kuanzia saa 7.00 katika chumba namba 432, ghorofa ya nne.

Kabla hatujaendelea, limekuja tangazo lingine wakati nimeshasimama limetoka kwa Mwenyekiti wa *TAPAC,* Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, anaomba niwatangazie Wanachama wa *TAPAC* kwamba, mafunzo kwa Wanachama kuhusu UKIMWI na Bajeti, yatafanyika kuanzia leo saa 7.00 mchana. Hivyo, Wanachama wa *TAPAC,* ambao wanapenda kushiriki katika mafunzo hayo waandikishe majina yao.

Mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper,* Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005
### Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, baada ya kupokea taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kisekta ya Ardhi na Kilimo, sasa Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuipongeza Kamati ya Bunge ya Ardhi na Kilimo, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika maandalizi ya bajeti hii. Kamati ilitoa ushauri, maoni na maagizo kwa Wizara yangu na hatimaye ikaidhinisha Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2004/2005. *(Makofi)*

Aidha, katika kuimarisha uhusiano baina ya nchi zinazotumia maji ya Bonde la Mto Nile, Waheshimiwa Wabunge tisa, Wajumbe wa Kamati hiyo walipata fursa ya kutembelea nchi ya Misri kuanzia tarehe 3 - 8 Juni, 2004 ili kujionea wenyewe matumizi ya maji ya bonde hilo. Ziara hiyo ilikuwa ni mwendelezo wa semina iliyoandaliwa na Wizara yangu kwa Waheshimiwa Wabunge wote kuhusu matumizi endelevu ya maji ya Bonde la Mto Nile.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini na hivi majuzi tena kifo cha mwenzetu Mheshimiwa *Captain* Theodos James Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki. Nachukua fursa hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa salamu za rambirambi kwa familia za Marehemu, ndugu na Wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini na wale wa Ulanga Mashariki. Namwomba Mwenyezi Mungu, aziweke roho za Marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Aidha, naomba nitumie fursa hii, kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge waliopata ajali na mikasa mbalimbali katika kipindi hiki akiwemo Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kwa matatizo aliyopata na Mheshimiwa Estherina Kilasi, kwa ajali aliyopata.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya waliojiunga na Bunge lako Tukufu katika kipindi cha mwaka 2003/2004, ambao ni Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, Mbunge wa CCM, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Danhi Makanga, Mbunge wa CCM, kwa kuchaguliwa kutoka Jimbo la Bariadi Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Ibengwe Mongella, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Dr. William F. Shija, Mbunge wa Sengerema, Mheshimiwa Dr. Amani W. A. Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, Mheshimiwa Remidius Edington Kissassi, Mbunge wa Dimani na Mheshimiwa Athumani S. M. Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kwa kuchaguliwa kwao kuwa Wabunge wa Bunge la Afrika. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Arcado Dennis Ntagazwa, Mbunge wa Muhambwe na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Kimataifa la Mazingira. Nampongeza pia Mheshimiwa Balozi Dr. Pius Yasebasi Ng'wandu, Mbunge wa Maswa na Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kwa kuteuliwa kuwa Rais wa Mawaziri wa Elimu Afrika. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kuchaguliwa kuiwakilisha Tanzania kwenye Bunge la *SADC (SADC Parliamentary Forum). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa jitihada zake za kuongoza, kusimamia na kuendeleza amani, utulivu na uchumi wa nchi yetu. Ni kutokana na jitihada hizo, Jumuiya ya Kimataifa, kwanza, ilimchagua kuwa Mwenyekiti Mwenza wa Kamisheni ya Utandawazi *(Co-Chairman of the World Commission on the Social Dimension of Globalization)* na pili, kwa kuteuliwa na Waziri Mkuu wa Uingereza kuwa Mjumbe wa Tume ya Kimataifa ya Blair kuhusu Afrika *(Blair's Commision for Africa).* Hali hii inadhihirisha imani kubwa waliyonayo kwake kutokana na utendaji wake wa kazi. Aidha, akiwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC),* ameweza kuitisha kikao cha dharura ambacho kilijadili na kutoa tamko juu ya kuimarisha kilimo na hali ya chakula na usalama wa chakula katika nchi hizo. *(Makofi)*

Kwa upande wa Sekta ya mifugo, tamko limebaini maeneo ya utekelezaji katika muda mfupi ambayo ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa mifugo inayoongezeka kwa muda mfupi *(Short Circle Stocks),* kuwa na mkakati na mipango ya kudhibiti magonjwa ya milipuko, kuongeza upatikanaji wa masoko ya mifugo na mazao yake, kuendeleza na kusambaza huduma za utafiti na ugani na kuchunguza athari za uingizaji wa mazao ya mifugo nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Mbunge wa Hanang', kwa hotuba yake nzuri ambayo kwa ufasaha

imetoa malengo ya Serikali na mwelekeo wa utendaji wa Sekta mbalimbali. Nawapongeza pia Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Mbunge wa Rombo, kwa hotuba zao zilizoainisha kwa makini mwelekeo wa Bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha 2004/2005. Pia, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Brigedia Jenerali (Mstaafu) Hassan Ngwilizi na Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja, kwa hotuba zao ambazo zimeainisha maeneo tunayoshirikiana kwa karibu katika kutoa huduma za maji na mifugo kwa Wananchi. Napenda pia, kutumia fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote walionitangulia kuwasilisha Hotuba zao ambazo zimetoa taswira ya ushirikiano wa kiutendaji kwa lengo la kukuza Pato la Taifa na kupunguza umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha Hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2004/2005, naomba nichukue fursa hii kutoa shukrani kwa Wananchi kwa michango yao ya hali na mali, wakiongozwa na wawakilishi wao Waheshimiwa Wabunge na Madiwani, katika kutekeleza programu za maji na mifugo. Wizara yangu itaendelea kushirikiana nao kwa lengo la kuboresha hali ya maisha yao na kuongeza uwezo wa Taifa letu kiuchumi. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao ya mawazo na ushauri wanaoutoa ndani na nje ya Bunge hili kwa nia ya kuboresha huduma za maji na mifugo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2003/2004, yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa nchi Wahisani, Mashirika ya Misaada, Taasisi za Hiari Zisizokuwa za Kiserikali, Mashirika ya Kidini na Taasisi za Kifedha. Hivyo, napenda kuzishukuru Serikali za nchi ya Ujerumani *(KfW* na *GTZ),* Japan, Ufaransa, Jamhuri ya Watu wa China, Uholanzi, Denmark, Sweden, Marekani, Canada, Uswisi, Ireland, Ubelgiji na Uingereza *(DFID).* Aidha, napenda kutoa shukrani kwa Taasisi za Fedha za Kimataifa, yaani Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika *(BADEA)*, Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya *(EIB),* Umoja wa Nchi zinazouza Mafuta Duniani *(OPEC)*, Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU),* Nchi za *NORDIC,* Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *UNDP, UNICEF, FAO, UNIDO, IFAD, Global Environmental Facility (GEF),* Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki na Taasisi ya Rasilimali ya Wanyama ya Umoja wa Afrika *(AU/IBAR)* kwa misaada na michango yao ya utaalamu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuyashukuru Mashirika ya Kidini ya *World Islamic League*, Shirika la *Al Munadhanat Al Dawa Al Islamia*, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Kanisa la Kilutheri la Ujerumani na Kanisa Katoliki Tanzania *(TEC),* pamoja na Taasisi nyingine za hiari za *WaterAid, VetAid* na *OXFAM* za Uingereza, *Austro -Project, Heifer Project International (HPI), World Vision,* Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili *(IUCN),World Wildlife Fund (WWF)* na wote wale ambao kwa njia moja au nyingine, wanaendelea kuisaidia Wizara yangu katika kutoa huduma

kwa Wananchi. Naomba, kupitia kwako nitumie fursa hii kuwashukuru wote hawa kwa dhati kabisa. Nawaomba waendelee kushirikiana na Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ninayowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu ni matokeo ya ushirikiano na mshikamano ninaoupata kutoka kwa wenzangu katika Wizara. Naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Anthony M. Diallo, Mbunge wa Mwanza Vijijini, kwa msaada na ushauri wake wa karibu. Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu, Ndugu Vincent Mrisho na Naibu Katibu Mkuu, Dr. Charles Nyamrunda, Wakuu wa Idara, Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara yangu pamoja na watumishi wote kwa kujituma katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Sekta hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana Wananchi wa Jimbo langu la uchaguzi la Monduli kwa ushirikiano walionipa katika kipindi hiki na kwa kunivumilia pale niliposhindwa kufika kwao kutokana na majukumu mengine ya Kitaifa yanayonikabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango na Bajeti ya mwaka 2003/2004 na Mpango wa mwaka 2004/2005, Wizara yangu inazingatia kikamilifu maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2000 kuhusu kuendeleza Sekta za Maji na Mifugo. Kwa upande wa maji na mifugo, Ilani inasisitiza juu ya ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji, kufufua na kujenga mabwawa ya maji, kushirikisha Wananchi katika ujenzi na uendeshaji wa miradi yao ya maji, kuvuna maji ya mvua na utunzaji wa vyanzo vya maji.

Aidha, Ilani inatilia mkazo ushirikishwaji wa Halmashauri za Wilaya katika kuweka miundombinu ya mifugo na uboreshaji wa ufugaji ili ubadilike kutoka ule wa kijadi na kuwa ufugaji wa kisasa na kibiashara unaozingatia ubora wa mifugo kuliko uwingi. Pia, Ilani inaelekeza kuweka Mkakati wa Kitaifa wa kuwaandalia wafugaji mazingira mazuri yatakayowahakikishia upatikanaji wa maji, malisho na majosho ili hatua kwa hatua waondokane na maisha ya kuhamahama.

Mheshimiwa Spika, Sekta za Maji na Mifugo ni kati ya Sekta zinazopewa kipaumbele katika Mkakati wa Taifa wa Kupunguza Umaskini Nchini *(PRS).* Mkakati huu unazingatia Dira ya Taifa 2025 na Malengo ya Kimataifa ya Kuondoa Umaskini *(Millenium Development Goals - MDGs).* Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu imefanya mapitio ya maeneo ya Sekta za Maji na Mifugo katika mkakati huo kwa kuhusisha wadau wa Sekta hizo katika ngazi mbalimbali kwa lengo la kupata maoni yao kuhusu maeneo muhimu ya kusisitiza ili Sekta hizi zitoe mchango mkubwa zaidi katika kuondoa umaskini. Mapitio hayo yameainisha malengo ya Sekta hizi kwa kipindi cha miaka mitano ijayo pamoja na viashiria vitakavyotumika katika kupima utekelezaji wa mkakati huo.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa maji ni kigezo na kichocheo muhimu katika kufanikisha jitihada za Serikali za kupambana na umaskini nchini. Maji ni muhimu

katika kuendeleza huduma za kijamii na kiuchumi zikiwemo Sekta za nishati, kilimo, mazingira, maliasili, viwanda pamoja na mahitaji ya binadamu na mifugo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo ina umuhimu mkubwa katika kumwondolea umaskini mwananchi, hususan maeneo ya vijijini. Mifugo hutoa ajira na inatumika kama benki hai ambayo ni chanzo cha mapato ya haraka na akiba ya chakula wakati wa hali ya ukame na njaa. Vile vile, katika kuendeleza kilimo, mifugo hutoa samadi ambayo ni muhimu katika kuongeza uzalishaji wa mazao na kwa maeneo mengi ya nchi ng'ombe na punda hutumika kama wanyama kazi. Aidha, uzalishaji wa mifugo na bidhaa zake huokoa fedha za kigeni ambazo zingetumika kuagiza bidhaa zitokanazo na mazao ya mifugo kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu hali halisi ya Sekta ya Maji nchini, napenda kutoa taarifa kuwa mwezi Aprili, 2004, Tanzania ilishiriki katika Kikao cha 12 cha Kamisheni ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ambacho kilifanya tathmini ya maendeleo ya utekelezaji wa malengo ya Kimataifa *(MDGs),* ya mwaka 2002. Moja ya makubaliano yaliyofikiwa ifikapo mwaka 2015 katika Sekta ya Maji ni pamoja na kupunguza kwa asilimia 50 idadi ya watu duniani wasio na huduma ya maji safi na salama, wasio na huduma ya usafi wa mazingira na kuweka mfumo shirikishi wa usimamizi wa raslimali za maji. Katika kikao hicho, ripoti ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Koffi Annan, ilizipongeza nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania kwa hatua zilizofikiwa katika kutekeleza malengo ya Kimataifa kwa kusema yafuatayo, nanukuu: -

*"Some countries are exceptional in their progress towards achieving the internationally agreed targets including the Central African Republic, Congo, Ghana, Kenya, South Africa and the United Republic of Tanzania in Sub Saharan Africa, India Nepal and Pakistan in South - East Asia: and Morocco and Tunisia in North Africa. Progress in those countries was due to increased funding from domestic and international sources, effective resource mobilization strategies through cost-recovery mechanisms, and integrated institutional frameworks, together with effective laws and regulations".*

Wizara yangu itaendelea na mikakati ya kutekeleza makubaliano hayo ili kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Spika, inakadiriwa kuwa kiasi cha maji yote duniani ni sawa na kilomita za ujazo 42,700. Kiasi hicho kikigawanywa kwa idadi ya watu duniani, wanaofikia bilioni 5.85, wastani wa maji kwa kila mtu ni mita za ujazo 7,300 kwa mwaka. Kwa Tanzania, kiasi cha maji yanayofaa kwa matumizi ya binadamu kwa sasa ni kilomita za ujazo 2,700 kwa mwaka. Kiwango kinachotosheleza ni mita za ujazo 1,700 kwa mtu kwa mwaka. Inakadiriwa kuwa, ifikapo mwaka 2025, kiasi hiki kitapungua na kufikia mita za ujazo 1,500 kwa mtu kwa mwaka, hali inayoashiria uhaba wa maji kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo ongezeko la watu. Katika mwaka 2003/2004, hali ya mvua katika maeneo mengi nchini ilikuwa chini ya wastani na kusababisha kupungua kina cha maji kwenye mito, mabwawa na chemichem. Kwa

mfano, katika Bwawa la Mtera, ujazo wa juu uliofikiwa mwaka huo ni mita za ujazo bilioni 1.3 ikiwa ni theluthi moja ya ujazo wake ambao ni mita za ujazo bilioni 3.6. Katika Bwawa la Nyumba ya Mungu, ujazo wa juu uliofikiwa ni asilimia 35 tu ya ujazo wake. Hali hii ilisababisha kushuka kwa uzalishaji wa umeme kwa kutumia nguvu za maji katika mabwawa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma ya maji duniani, takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba karibu watu bilioni 1.2 hawana huduma ya majisafi na salama na kati ya hao milioni 300 wako kwenye Bara la Afrika. Pia, inakadiriwa kwamba watu wapatao bilioni 2.6 duniani hawana huduma ya uondoaji majitaka na usafi wa mazingira na kati ya hao milioni 540 wako Bara la Afrika. Kwa upande wa Tanzania, asilimia 53.47 ya Wananchi waishio vijijini wanapata huduma ya maji safi na salama, ukilinganisha na asilimia 53 ya mwaka 2003. Huduma ya maji mijini imeendelea kuwa asilimia 73 ya wakazi wa mijini wanaopata huduma ya maji safi na salama. Mfumo wa uondoaji wa majitaka umeendelea kuwa asilimia 17 ya wakazi wote waishio mijini.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Maji inalenga katika kujenga mazingira ya kuwezesha Sekta hiyo kukua kwa haraka ili kuwawezesha Wananchi kuishi maisha bora zaidi na kuchangia zaidi katika kupunguza umaskini. Mafanikio ya utekelezaji wa Sera yanategemea sana uelewa na ushiriki wa Wananchi, Halmashauri za Wilaya na watendaji katika ngazi za utekelezaji. Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika lake la *GTZ* na Serikali ya Japan kupitia *JICA* ilichapisha na kusambaza nakala 16,250 za Sera ya Maji kwa wadau wa Sekta wakiwemo Viongozi, Wananchi, Taasisi zisizo za Kiserikali na Waheshimiwa Wabunge. Aidha, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la *WaterAid*, inaandaa tovuti ya Sekta ya Maji ambayo itatumika katika kueneza Sera na taarifa za Sekta hiyo kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kutekeleza Sera ya Maji, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika lake la *GTZ,* inaandaa Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Maji. Mkakati huo utaelekeza jinsi utekelezaji wa Sera hiyo utakavyoiwezesha Wizara kufanikisha malengo yake ya muda wa kati na mrefu. Rasimu ya mkakati huo inakamilishwa na itasambazwa kwa wadau ili kupata maoni yao. Aidha, Sheria za Maji zinafanyiwa marekebisho ili ziendane na Sera ya Maji na kuimarisha usimamizi katika utekelezaji wa mkakati huo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 22 Machi kila mwaka ni siku iliyochaguliwa na Umoja wa Mataifa kuwa Siku ya Maji Duniani *(World Water Day).* Nchi yetu huitumia siku hiyo kama kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Maji ambayo huanza tarehe 16 hadi tarehe 22 Machi. Maadhimisho haya yanafanyika katika ngazi zote kuanzia Kijiji hadi Taifa na yanalenga kutoa nafasi kwa wadau wa Sekta ya Maji kupata ufafanuzi kuhusu Sera ya Maji na kutathmini utoaji wa huduma ya maji nchini. Maudhui ya Wiki ya Maji kwa mwaka 2004 yalikuwa "Hifadhi Vyanzo vya Maji Kuepuka Majanga". Maadhimisho hayo Kitaifa yalifunguliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuzindua Awamu ya Pili ya Mradi wa Maji uliotekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali yetu na Serikali ya Japan katika Wilaya za Manyoni na Singida Vijijini. Kitaifa, maadhimisho hayo yaliendelea

kwa kufanya maonyesho, warsha na semina katika Mkoa wa Ruvuma. Maadhimisho hayo Kitaifa yalifikia kilele tarehe 22 Machi Mjini Songea ambapo Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, aliyafunga rasmi. Nawashukuru sana Viongozi hawa kwa kujumuika nasi.

Mheshimiwa Spika, ili kuhamasisha utekelezaji wa Sera ya Maji, kubadilishana uzoefu na kujifunza mambo mapya yanayojitokeza katika Sekta ya Maji, kila mwaka Wizara yangu hufanya Kongamano la Wataalam wa Maji Nchini *(Annual Water Experts Conference - AWEC).* Katika mwaka 2003/2004, Kongamano hilo lilifanyika Arusha kuanzia tarehe 23 hadi 27 Januari, 2004 na maudhui yalikuwa Utoaji Huduma ya Maji Katika Dunia ya Utandawazi. Wizara yangu inayafanyia kazi maazimio ya kongamano hilo kwa lengo la kuboresha utoaji huduma ya maji nchini.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Sita wa Mwaka wa Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini ulifanyika Jijini Mwanza kati ya tarehe 4 - 5 Machi, 2004. Mkutano huo huwakutanisha Watendaji Wakuu wote wa Mamlaka za Maji Mijini katika Tanzania Bara. Madhumuni yake ni kuhamasisha utekelezaji wa Sera ya Maji na pia hutoa fursa ya kubadilishana uzoefu kuhusu masuala ya kiufundi, kifedha na kimenejimenti. Katika mkutano huo, Mamlaka hizo pia hufanyiwa tathmini ya utendaji kazi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za maji mijini. Mkutano huo, ambao ulifunguliwa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, ulimalizika kwa kutoa maazimio ya kupunguza upotevu wa maji yasiyolipiwa, kukusanya madeni na kupunguza gharama za uendeshaji. Utekelezaji wa maazimio hayo, utafanywa na mamlaka zote katika mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa maji chini na juu ya ardhi ni jukumu la msingi la Serikali. Madhumuni ya uchunguzi huu ni kugundua na kutathmini vyanzo vipya vya maji vitakavyotumika kutoa huduma ya maji vijijini na mijini. Ili kukidhi azma hii, Wizara imeweka mtandao wa vipimo vya wingi wa maji, hali ya hewa na mtandao wa kufuatilia raslimali za maji chini ya ardhi katika mabonde. Lengo ni kupata takwimu sahihi na kwa wakati unaotakiwa kwa ajili ya kuratibu matumizi ya raslimali za maji nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu iliendelea kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za maji juu na chini ya ardhi kwa kukarabati vituo 25 katika mabonde ya Ziwa Rukwa tisa, Ziwa Tanganyika vinane na Bonde la Kati vinane. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itaendelea na ukarabati wa vituo 90 vya ukusanyaji wa takwimu za maji juu ya ardhi katika mabonde ya Kati 21, Ziwa Tanganyika 19, Ziwa Nyasa 34 na Mto Ruvuma 16. Aidha, ukarabati wa vituo 35 vya kupima wingi wa maji juu ya ardhi na hali ya hewa katika Bonde la Mto Wami/Ruvu utafanyika kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Maji katika Jiji la Dar es Salaam. Pia, Wizara yangu imefikia makubaliano na Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili *(IUCN),* ambapo Shirika hilo litatekeleza mradi wa usimamizi wa pamoja wa raslimali za maji *(Intergraded Water Resources Management - IWRM)* katika Bonde la Mto Pangani kwa miaka mitatu kuanzia 2004/2005, Mradi huu utagharimu Shilingi bilioni 2.3 utakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kutafuta vyanzo vipya vya maji, mwaka 2003/2004, Wizara yangu ilifanya utafiti ili kutambua maeneo yanayofaa kuchimba visima vya maji kwa matumizi mbalimbali. Maeneo 1,033 yalipimwa katika Mikoa yote na visima virefu 636 vilichimbwa, ambapo 516 ni kupitia Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa na 120 ni kwa kupitia Makampuni binafsi. Aidha, Wizara yangu ilisimamia kwa karibu shughuli za uchimbaji wa visima hivyo ili kuhakikisha kuwa taratibu za kitaalam zinafuatwa ambapo Makampuni binafsi 25 yanayochimba visima nchini yalikaguliwa. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itafanya utafiti katika maeneo 1,000 kwa ajili ya kutambua maeneo yanayofaa kuchimba visima virefu na vifupi. Vile vile, Wizara itaendelea na usimamizi wa uchimbaji visima vya maji nchini pamoja na ukaguzi wa Makampuni binafsi ya uchimbaji visima.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika mwaka 2003/2004, ilichunguza sampuli 281 kwa ajili ya kutathmini rasilimali za maji katika Bonde la Mto Wami/Ruvu, kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki. Aidha, Wizara ilipokea madawa na vifaa mbalimbali kwa ajili ya uchunguzi huo na watalaam watatu walipata mafunzo ya muda mfupi katika taaluma ya *Isotopes.* Warsha ya mafunzo ya kuanza kutathmini mizania ya Ziwa Victoria kwa kutumia takwimu zilizokwisha kukusanywa imefanyika tarehe 12 - 25 Juni, 2004, Kisumu Kenya. Wizara itaanzisha mtandao wa kuratibu mwenendo wa rasilimali za maji chini ya ardhi katika mabonde ya Wami/Ruvu na Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa kulinda na kuhifadhi Bonde dogo la Makutupora ambalo ni chanzo kikuu cha maji kwa Manispaa ya Dodoma, dhidi ya uchafuzi, Wizara yangu katika mwaka 2003/2004, imelipa nyongeza ya fidia ya Shilingi milioni 73 kama malipo ya mwisho kwa wakazi waliohamishwa toka eneo hilo. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itaendelea na kazi za kuhifadhi mazingira na kuimarisha mtandao wa kuratibu mwenendo wa rasilimali za maji chini ya ardhi kwenye bonde dogo hilo.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa, asilimia 43.4 ya rasilimali za maji katika nchi yetu ziko kwenye maji shiriki. Wizara yangu inashiriki katika majadiliano na nchi nyingine katika kuweka mfumo wa ushirikiano utakaoleta uwiano mzuri wa matumizi ya rasilimali za maji shiriki. Kwa upande wa Bonde la Mto Nile, nchi shiriki zimetambua umuhimu wa kuchukua hatua madhubuti za kutumia na kuendeleza rasilimali za maji ya Bonde la Mto Nile kwa manufaa ya kiuchumi na kijamii kwa ajili ya Wananchi wao.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inashirikiana katika matumizi ya maji ya Bonde la Mto Nile kupitia chombo cha mpito kiitwacho *Nile Basin Initiative (NBI).* Chombo hicho, kinasimamia haki na usawa wa matumizi ya rasilimali za maji za Bonde la Mto Nile. Katika mwaka 2003/2004, Kamati ya Majadiliano iliyoundwa na nchi shiriki ili kujadili rasimu ya chombo mbadala ilizinduliwa katika Kikao cha Kumi cha Baraza la Mawaziri wa Maji kilichofanyika Addis Ababa, Ethiopia. Katika mwaka

2004/2005, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na nchi za Bonde la Mto Nile katika utekelezaji wa miradi iliyobuniwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeshiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi iliyopo chini ya Mpango wa Kutekeleza Mkakati wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC - Regional Strategic Action Plan - RSAP).* Lengo la Mpango huu ambao ni wa miaka mitano ni kuboresha upatikanaji na uchambuzi wa takwimu na taarifa mbalimbali zinazohusu raslimali za maji shiriki na mazingira. Takwimu na taarifa hizi zitaziwezesha nchi za Jumuiya ya *SADC* kukuza ushirikiano katika uendelezaji, usimamizi na matumizi bora ya rasilimali za maji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, nchi za Tanzania, Msumbiji na Malawi zimekamilisha makubaliano ya awali *(Memorandum of Understanding)* ya uendelezaji wa Raslimali za Maji katika Bonde la Ziwa Nyasa na Mto Shire. Mikoa itakayofaidika na makubaliano haya ni ile iliyomo kwenye Bonde la Ziwa Nyasa ambayo ni Mbeya, Iringa na Ruvuma. Wizara yangu pia ilishiriki katika maandalizi ya Sera ya Maji ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika. Aidha, Tanzania na nchi nyingine zilizoko katika Jumuiya ya *SADC* ilishiriki majadiliano yenye lengo la kukamilisha Mkataba wa Makubaliano ya kuanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi *(Zambezi Watercourse Commission - ZAMCOM).* Mkataba huu umewekwa saini na Mawaziri wa Maji wa nchi zilizomo kwenye Bonde la Mto Zambezi tarehe 13 Julai, 2004 huko Kasane Botswana. Pia, upembuzi yakinifu wa Mradi wa Kudhibiti Kingo za Mto Songwe ulikamilika. Katika mwaka 2004/2005, jitihada za kutafuta fedha zitaendelezwa ili kugharamia usanifu wa kina wa miradi iliyotambuliwa katika Bonde la Mto Songwe ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa, kuendeleza miundombinu na upandaji wa miti ili kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imechukua hatua za kuanzisha Mfuko wa Maji Kitaifa kama ilivyoshauriwa na Bunge lako Tukufu mwaka jana. Mfuko huo utatumika katika kutekeleza miradi mbalimbali yenye lengo la kuendeleza Sekta ya Maji nchini. Hivi sasa, Wizara inakusanya maoni ya wadau mbalimbali nchini kuhusu namna ya kuanzisha na kuuendesha mfuko huu. Aidha, Wizara yangu inashiriki katika majadiliano yanayofanywa na Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika kuhusu uanzishaji wa Mfuko wa Maji Afrika *(The Africa Water Facility),* Mfuko huu utatumika kufadhili miradi mbalimbali kwa lengo la kuendeleza Sekta ya Maji. Katika Bara la Afrika wafadhili wengi wameonyesha nia ya kuchangia katika Mfuko huo zikiwemo nchi ya Sweden, Ujerumani, Canada na Uholanzi. Kiasi cha Dola za Marekani milioni 650 zinategemewa kupatikana kutoka kwa wafadhili.

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kusimamia matumizi bora ya raslimali za maji kwa uwiano mzuri, Wizara yangu inatekeleza Sera ya Maji ya Taifa ya mwaka 2002, ambayo inasisitiza usimamizi wa rasilimali za maji kwa kufuata mabonde, tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo usimamizi ulikuwa unafuata mipaka ya Mikoa. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu ilianzisha ofisi nne za Mabonde ya Maji ya Mto Ruvuma/Lukuledi, Ziwa Tanganyika, Rukwa na Bonde la Kati. Idadi hiyo inakamilisha uanzishwaji wa ofisi katika mabonde yote tisa nchini. Mabonde ambayo tayari yalikuwa

na ofisi ni mabonde ya Mto Rufiji, Pangani, Wammi/Ruvu, Ziwa Victoria na Bonde la Ziwa Nyasa. Majukumu ya ofisi za mabonde ni kusimamia matumizi bora ya maji, kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji na kutatua migogoro.

Katika mwaka 2004/2005, mabonde yaliyoanzishwa yataimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi pamoja na watumishi ili yaweze kutekeleza majukumu ya kupanga na kusimamia matumizi bora ya raslimali za maji katika mabonde yanayohusika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu ilikagua jumla ya vyanzo vya maji 1,026 katika mabonde ya mto Rufiji, Pangani, Wami, Ruvu na Mabonde ya Ziwa Victoria, Nyasa, Rukwa na Bonde la Kati, kwa lengo la kuhakiki matumizi bora ya maji na kuhamasisha watumiaji kuwa na hati za kutumia maji. Jumla ya hati 157 zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya maji katika mabonde hayo. Vile vile, kazi ya kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji ilifanyika katika bonde la Ziwa Victoria, mto Pangani na Wami/Ruvu. Jumla ya viwanda 46 na migodi mikubwa minne ilikaguliwa na kuagizwa kufanya marekebisho katika mifumo ya maji na majitaka ili kuimarisha na kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji.

Katika mwaka 2004/2005, jumla ya vyanzo 1,500 vitakaguliwa katika mabonde ya Rufiji, Pangani, Wami Ruvu, Ruvuma - Lukuledi, Bonde la Kati, mengine ni Mabonde ya Ziwa Victoria, Nyasa, Tanganyika na Rukwa. Jumla ya hati 262 zinatarajiwa kutolewa katika kipindi hicho kwa watumiaji mbalimbali wa maji. Vile vile, jumla ya viwanda na migodi 77 inatarajiwa kukaguliwa kwa lengo la kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji na kutoa vibali maalum vya kutupa majitaka. Aidha, migogoro yote itaendelea kushughulikiwa kwa karibu zaidi kupitia ushauri wa Bodi za mabonde zilizoanzishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia maabara za maji 15 zilizopo nchini, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu ilifanya ukaguzi na uchunguzi wa usafi na ubora wa maji katika Mikoa yote nchini ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji safi na salama. Wizara yangu ilifanya uhakiki wa madawa yanayotumika kusafisha maji ili kuona kama yapo katika viwango vinavyokubalika. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itaendelea kufanya ukaguzi wa vyanzo vya maji nchini ili kudhibiti uchafuzi wa maji na kuhakikisha kwamba majitaka yanayoingia katika vyanzo vya maji yana viwango vinavyokubalika. Wizara yangu pia itaendelea kuzifanyia ukarabati maabara za maji za Morogoro, Mtwara, Shinyanga na Ubungo na kutoa mafunzo kwa watumishi. Kupitia mradi wa Hifadhi ya Ziwa Victoria, ukarabati wa maabara ya Bukoba utafanyika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Kitengo cha Ubora wa Maji na Mfumo Ikolojia chini ya Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Viktoria kiliendelea na ukusanyaji wa takwimu za uwingi na ubora wa maji ya mito, mvua, majitaka kutoka viwandani na mijini na athari zake kwa maji ya ziwa hilo kwa upande wa Tanzania. Takwimu hizo hutumika katika kusanifu miradi ya maji, kwa mfano, Usanifu wa Mradi wa kutoa Maji Ziwa Victoria kwenda Shinyanga na Kahama umefanyika kwa kutumia takwimu hizo. Aidha, kitengo kilishirikiana na viwanda na wadau wengine husika katika kuendeleza programu ya uzalishaji unaojali mazingira. Katika mwaka 2004/2005 Wizara

yangu, kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda, itaendelea na Uratibu wa Ubora wa Maji na Mfumo Ikolojia katika Bonde la Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, ili kuandaa miradi ya usambazaji wa maji katika maeneo ambayo hayana huduma ya maji ya kuridhisha, mwaka 2003/2004, Wizara yangu ilifanya uchunguzi wa vyanzo vya maji kwenye vijiji vya Kayenze na Igombe (Mwanza), Tarime Mjini, Mafia, Ngara, Kiomboi na Sikonge. Aidha, Wizara yangu ilifanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya upanuzi na usambazaji wa maji kwenye Miji ya Tukuyu, Mbinga, Kasulu, Makambako na Tunduru.

Mpango wa mwaka 2004/2005, ni kufanya usanifu wa miradi ya maji kwa miji ya Geita, Masasi na Nachingwea na mradi wa maji wa Kijiji cha Itete, wilayani Rungwe. Usanifu wa miradi hii utazingatia matumizi ya maji ya Ziwa Victoria kwa ajili ya Mji wa Geita na chemichemi ya Mbwinji kwa Miji ya Masasi na Nachingwea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu ilifikia makubaliano na Serikali ya Japan kugharamia uchunguzi ambao unalenga katika kuongeza kiwango cha upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Pwani na Vijiji vya Mkoa wa Dar es Salaam. Katika mwaka 2004/2005, kazi zitakazofanyika ni kutambua maeneo ambayo yatafanyiwa uchunguzi wa kina na usanifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu iliendelea na maandalizi ya programu ya maji katika Miji midogo tisa ambayo ina lengo la kuziba pengo lililopo katika utekekelezaji wa miradi ya maji katika Miji mikubwa nchini na maeneo ya vijijini. Programu hii inayohusu Miji midogo ya Kilosa, Gairo, Turiani, Mvomero, Mpwapwa, Kibaigwa, Utete, Ikwiriri na Kibiti inafadhiliwa na Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la misaada la *AFD*. *(Makofi)*

Mhandisi Mshauri atakayesaidiana na Wizara kusimamia utekelezaji wa programu amekwishachaguliwa na ataanza kufanya kazi kuanzia mwezi Septemba, 2004. Katika kipindi cha miezi 16 ya mwanzo, Mhandisi Mshauri atafanya uchunguzi na usanifu wa kina wa mifumo ya maji na usafi wa mazingira na kuandaa makabrasha ya zabuni za ujenzi. Aidha, shughuli za uhamasishaji na utoaji wa elimu ya afya na usafi wa mazingira zitakuwa zikifanyika sambamba na kazi za uchunguzi na usanifu.

Katika mwaka 2004/2005, Shilingi milioni 220 zimetengwa kwa ajili ya shughuli za uchunguzi na usanifu kwenye programu hii. Ujenzi wa miradi unategemewa kuanza mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 tutatekeleza yafuatayo: -

- Kufanya usanifu wa mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya Mji wa Geita; *(Makofi)*

- Tutafanya usanifu wa mradi wa chemchem ya Mbwinji kwa ajili ya Masasi na Nachingwea na Mradi wa Maji wa Kijiji cha Ilete wilayani Rungwe; *(Makofi)*

- Tufafanya mazungumzo na Benki ya Kiarabu chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Basil Mramba; Waziri wa Fedha, ili wagharimie ujenzi wa Mradi wa Maji wa Mbwinji kwa ajili ya Miji wa Masasi na Nachingwea; na *(Makofi)*

- Tutaendeleza ushirikiano na Serikali ya Ufaransa kwa kutumia Shilingi milioni 220 kufanya uchunguzi na usanifu wa Miradi ya Maji katika Miji midogo tisa niliyoitaja. Mkataba wa kuanza uchunguzi wa kina na usanifu umewekwa saini tarehe 27 mwezi huu hapa Mjini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu mwaka jana, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya, ilifanya utambuzi wa miradi ambayo haijakamilika na haifanyi kazi. Jumla ya miradi 794 yenye kuhitaji Shilingi bilioni 43 kuikamilisha, ilitambuliwa. Fedha hizo ni nyingi kuweza kupatikana mara moja. Hivyo, Wizara yangu ilifanya kazi ya ukarabati. Katika mwaka 2003/2004, Wizara ilitenga jumla ya Shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya kukarabati miradi 31. Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ilifanya ukarabati wa miradi ya maji ya Migori na Kiponzelo (Iringa Vijijini), Lumeya (Sengerema), Misasi (Misungwi), Malya (Kwimba), Mugango - Kiabakari (Musoma Vijijini) Bunda Mjini, Gabimori (Tarime), Hedaru (Same), Lotima (Rombo), Biharamulo na Chunya. Aidha, miradi mingine iliyofanyiwa ukarabati ni Mwamapuli/Bulenya (Igunga), Singida Vijijini, Mahenge Mjini, Shinyanga Vijijini, Kilulu (Bariadi), Magugu (Babati), Korogwe Mjini, Nassa (Magu), Kitomondo (Lindi), Urambo mjini, Ndea (Mwanga), Majengo/Eslalei, Elerai/Longido na Mto wa Mbu (Monduli).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara imetenga jumla ya Shilingi bilioni 7.9 kwa ajili ya kukarabati miradi 44 ya maji ya Libango (Namtumbo), Misasi (Misungwi), Kilulu, Kiponzelo, Mto wa Mbu, Mugango - Kiabakari, Gabimori, Hedaru, Lotima, Magugu, Kayenze, Nassa, Shosholo, Sikonge, Kitomanga, Iwindi, Majengo/Esilalei, Chato, Nyang'hanga/Kabita na Elerai/Longido. Miradi mingine ni Kwanyange (Mwanga), Mpanda, Sengerema, Ngara, Chunya Vijijini, Njombe Vijijini, Mafia Vijijini, Makete Mjini, Bomba Kuu la Handeni *(HTM),* Mradi wa Maji Makonde, Tarime Mjini, Mwisanga/Ntomoko, Korogwe, Monduli, Shinyanga Vijijini, Bomba Kuu la Kilimanjaro Mashariki *(EKTM),* Nyakagomba, Mugumu, Tukuyu, Nzega Vijijini, Kamachumu, Tunduru na Chamwino. Ili kuongeza kasi ya ukarabati wa miradi ambayo haifanyi kazi, nazishauri Halmashauri za Wilaya ziweke kipaumbele kwenye miradi hiyo kwa kuweka kwenye mipango yao ya kila mwaka chini ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira inayotekelezwa kwa msaada wa wafadhili mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Wahisani na Taasisi za ndani na nje, imeendelea kuimarisha na kuboresha huduma ya maji vijijini kwa kupanua na kujenga miradi mipya ya maji katika maeneo mbalimbali nchini. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu iliendelea kujenga na kupanua miradi ya maji ya Nachingwea Mjini, Maswa, Rondo, Singida Vijijini, Manyoni Vijijini, Nanganga, Kitomanga, Kazilankanda (Ukerewe), Nyakagomba, Losinyai, Hai na bwawa la Mugumu. Aidha, uchimbaji wa visima viwili vya Serengeti na Dang'aida (Hanang')

uliokuwa kwenye mpango wa mwaka 2003/2004 utakamilika katika kipindi cha mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka uliopita ni ukamilishwaji wa mradi mkubwa wa maji wa Chalinze. Mradi huo uliogharamiwa kwa pamoja kati ya Serikali yetu na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, kwa jumla ya Shilingi bilioni 23.65, ulizinduliwa na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwezi Mei 2004. Mradi huo wenye mabomba yenye urefu wa kilometa 160, vituo vya kuchotea maji 332, matanki 10, kwa sasa unahudumia Wananchi 70,000 katika Vijiji 18 Wilayani Bagamoyo. *(Makofi)*

Mafanikio mengine ni ukamilishaji wa awamu ya pili ya mradi wa Hanang', Singida Vijijini, Manyoni na Igunga uliotekelezwa kwa kushirikiana na Serikali ya Japan na kugharimu Shilingi bilioni 3.9. Mradi huo ulizinduliwa na Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwezi Machi, 2004 katika Wilaya ya Manyoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara imepanga kuendelea na upanuzi wa miradi ya maji ya Chiuwe (Lindi), Igombe (Mwanza), Nyakagomba (Geita), Kilwa Masoko, Ilula (Kilolo), Malya (Kwimba) na Hai. Wizara kwa kushirikiana na *UNICEF,* imetenga jumla ya Shilingi milioni 80 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji, elimu ya afya na usafi wa mazingira katika Wilaya za Magu, Mbarali, Hai, Kibaha, Kilosa, Masasi, Misungwi, Kwimba na Mtwara Vijijini. Aidha, ujenzi wa matanki ya maji ya mfano na kuhamasisha uvunaji wa maji ya mvua katika Wilaya za Chunya na Magu utaendelea. Vile vile, katika mwaka 2004/2005, Wizara imepanga kuchimba visima virefu vitatu katika Vijiji vya Sangabuye viwili na Nyamwilolelwa (Mwanza) na vingine vitatu Mjini Tarime. Aidha, Wizara itendelea na ujenzi wa bwawa la Mugumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya, itaanza kutekeleza Mradi wa Maji katika Wilaya ya Monduli kwa msaada wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)*, kwa gharama ya Shilingi bilioni 24. Asilimia 90 ya fedha hizo zitatolewa na ADB na asilimia 10 itatolewa kwa pamoja na Serikali Kuu, Halmashauri ya Wilaya na Wananchi. Mradi huu utakapokamilika utawanufaisha Wananchi katika Vijiji 18, Mji wa Monduli na Mji mdogo wa Namanga. Kwa mwaka 2004/2005, Shilingi bilioni 1.53 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ukarabati wa mfumo wa maji wa Mji wa Monduli na baadhi ya Vijiji vya Wilaya hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Serikali ya Uholanzi, inatekeleza Programu ya Maji Vijijini katika Mkoa wa Shinyanga, inayohusisha Wilaya zote za Mkoa huo. Programu hii ambayo ilianza kutekelezwa kuanzia Julai, 2002 inahusisha uchimbaji wa visima vifupi na virefu, ujenzi wa miradi ya maji ya bomba na ujenzi wa mabwawa. Programu inatekelezwa kwa kuzingatia Sera ya Maji hasa ushirikishwaji wa Wananchi. Miradi inayotekelezwa katika programu ni ile ambayo

Wananchi wameibuni na wako tayari kushiriki kuitekeleza. Katika mwaka 2003/2004, mradi mmoja wa bomba ulijengwa na mabwawa saba kuchimbwa.

Aidha, visima virefu vinne na vifupi 341 vilichimbwa katika Wilaya zote za Mkoa huo. Jumla ya Shilingi bilioni 1.97 zimetumika kuanzia Julai 2002 hadi Machi 2004. Kwa mwaka 2004/2005, programu hii imetengewa Shilingi bilioni 2.9 kwa ajili ya utekelezaji katika Wilaya zote za Mkoa, ambapo visima vifupi 186 na virefu 16 vitachimbwa na mabwawa madogo 11 kujengwa. Aidha, miradi saba ya maji ya bomba itajengwa vijijini na upanuzi wa miradi ya maji katika Miji ya Bariadi, Mwanhuzi na Ushirombo utaanza.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu mwaka wa jana, Wizara yangu itatekeleza mradi wa maji katika Mikoa ya Mtwara na Lindi kwa kushirikiana na Serikali ya Japan. Mradi huo utakapokamilika utawanufaisha Wananchi wa Vijiji 64. Kati ya hivyo, Vijiji 31 ni vya Mkoa wa Mtwara na Vijiji 33 ni vya Mkoa wa Lindi. Katika mwaka 2004/2005, Shilingi bilioni 3.07 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa mitambo ya kuchimba visima virefu na vifupi, vifaa vya uchunguzi na magari. Vifaa mbalimbali, kama vile mitambo ya kuchimbia visima na magari vilianza kuwasili nchini tangu mwezi Juni, 2004 na ujenzi wa mradi utaanza katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inasimamia Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ambao unagharamiwa kwa mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia. Mradi ulianza kutekelezwa katika Wilaya tatu za Rufiji, Kilosa na Mpwapwa ambapo jumla ya Vijiji 29 vyenye watu 134,000 vinapata huduma ya maji hadi sasa. Mafanikio hayo yametokana na uchimbaji wa visima vifupi na virefu, pamoja na ujenzi wa miradi ya maji ya mtiririko. Katika mwaka 2002/2003, mradi ulipanuliwa na kufikia Wilaya 12 na mwaka 2003/2004, Wilaya nyingine 38 ziliongezwa hivyo kufikia Wilaya 50. Aidha, Wizara ilifanya warsha za uhamasishaji kuhusu maandalizi ya mradi huo katika Wilaya zote nchini. Lengo la warsha hizi lilikuwa ni kujadili na watendaji katika ngazi za Wilaya na Mkoa kuhusu taratibu na maandalizi ya utekelezaji wa mradi katika Wilaya husika.

Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu imetenga Shillingi bilioni 9.9 kwa ajili ya maandalizi ya mradi huo kwenye Wilaya 38 zilizoongezwa pamoja na ujenzi wa miradi katika Wilaya 12 za awamu ya kwanza. Pia, maandalizi ya kupanua mradi huu yamekamilika ili kuwa na Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini itakayotekelezwa katika Wilaya zote nchini kuanzia Julai, 2005. Narudia. Kukamilisha maandalizi ya upanuzi wa mradi huo ili kuwa na programu ya maji na usafi wa mazingira Vijijini itakayotekelezwa katika Wilaya zote nchini kuanzia Julai, 2005. *(Makofi)*

Maandalizi ya utekelezaji wa programu hii yanahusisha wadau mbalimbali wa Sekta ya Maji na kuzingatia uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi. Aidha, upanuzi wa miradi ya maji katika Miji ya Igunga, Kiomboi, Manyoni, Kondoa, Kongwa na Kibaya ulifanyika.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa huduma ya maji vijijini na katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji midogo umeendelea kuimarika mwaka hadi mwaka. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa miradi inayojengwa na kufanyiwa ukarabati inakabidhiwa kwa watumiaji ili waisimamie na kuiendesha kwa kutumia vyombo huru vilivyoundwa kisheria. Hadi sasa Kamati za Maji 8,469 zimeundwa na zina Mifuko ya Maji 7,254 yenye jumla ya Shilingi bilioni 1.28. Kiasi hiki cha fedha kinaonyesha mwamko uliopo kwa Wananchi katika kumiliki na kugharamia uendeshaji wa miradi yao. Vyombo vingine vya maji vijijini vilivyoundwa kisheria ni pamoja na Jumuiya za Watumiaji Maji 62, Makampuni ya Maji 23, Vyombo vya Udhamini vitatu na Vikundi vya Watumiaji Maji Vijijini 1,709. Vyombo hivyo vimeendelea kusimamia utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi katika maeneo yao. Hadi Aprili, 2004, Miji 92 ya Wilaya na miradi minne ya Kitaifa ya Maswa, *HTM,* Makonde na Mugango/Kiabakari ilikuwa imetangazwa kuwa Mamlaka za Maji na kati ya Mamlaka hizo, 39 zimeunda Bodi za Maji.

Lengo la Serikali ni kuanzisha mamlaka za maji kwenye Miji Mikuu yote ya Wilaya nchini pamoja na Miji mingine midogo ili kusimamia utoaji wa huduma ya maji katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa muda mrefu imekuwa ikiendesha miradi sita ya Kitaifa inayotoa huduma ya maji vijijini. Miradi hiyo ni Wanging'ombe, Makonde, Mugango/Kiabakari, Maswa, Handeni Trunk Main na Chalinze. Kwa kuzingatia Sera ya Maji, miradi hii itakabidhiwa kwa vyombo vya watumiaji maji. Maandalizi ya kukabidhi miradi hiyo yamekamilika na itakabidhiwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa *(DDCA),* ulio chini ya Wizara yangu, uliundwa kwa lengo la kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji kwa njia ya kuchimba visima na kujenga mabwawa nchini kote. Tangu Wakala uanzishwe umechimba visima virefu 3,527 vyenye uwezo wa kutoa maji kiasi cha lita bilioni 158 kwa mwaka. Kwa wastani kiwango cha mafanikio ya visima hivyo ni asilimia 84.

Katika mwaka 2003/2004, wakala ulilenga kuchimba visima virefu 400, lakini ilivuka lengo na kuchimba visima 516. Lengo la mwaka 2004/2005, ni kuchimba visima 420. Kwa njia hii ya visima virefu hali ya huduma ya maji katika Vijiji na Miji ya Singida, Shinyanga, Lindi, Arusha na Dar es Salaam imeboreshwa. Wakala pia umeanza ujenzi wa bwawa la Mugumu ambalo litakamilishwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, utendaji kazi wa wakala huu unaathiriwa sana na uchakavu wa mitambo ambayo ina umri kati ya miaka 30 na 70 na hivyo kupunguza kasi ya wakala ya kujenga vyanzo vipya vya maji nchini. Kwa hiyo, ni muhimu kwa wakala huu ukaimarishwa kwa kuupatia mitambo mipya na ya teknolojia ya kisasa. Mitambo hiyo inakadiriwa kugharimu Shilingi bilioni 20 ambapo katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu imetenga Shilingi milioni 310 kwa ajili ya kununua mitambo ya uchimbaji visima na ujenzi wa mabwawa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuanzishwa kwa Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini, kumekuwepo na mafanikio ya kuridhisha katika utoaji wa huduma ya maji katika Miji Mikuu ya Mikoa ambapo kwa sasa upatikanaji wa maji kwa wakazi wa mijini ni zaidi ya asilimia 73 ikilinganishwa na asilimia 68 mwaka 1998 wakati Mamlaka zilipoanzishwa. Uwezo wa uzalishaji wa majisafi kwa Mamlaka zote 18 uliongezeka kutoka lita bilioni 91 mwaka 1998 hadi lita bilioni 102 mwaka 2002/2003. Hata hivyo, kwa mwaka 2003/2004, uzalishaji halisi wa majisafi ulikuwa lita bilioni 99 kutokana na ukame ulioathiri vyanzo vingi vya maji. Ukusanyaji wa mapato uliongezeka kutoka Shilingi bilioni 13.2 mwaka 2002/2003 na kufikia shilingi bilioni 14.85 mwaka 2003/2004. Jitihada zinaelekezwa kwenye ukarabati wa mifumo ya maji inayofanya kazi chini ya uwezo wake, upanuzi wa mifumo iliyopo, kutafiti vyanzo vipya vya maji na pia kuimarisha uwezo wa uendeshaji na matengenezo ya mifumo hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU)* na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW),* inatekeleza mpango wa kuimarisha huduma za majisafi na uondoaji wa majitaka katika Jiji la Mwanza na Miji ya Mbeya na Iringa ambao utagharimu jumla ya shilingi bilioni 122.5. Katika mwaka 2003/2004 kazi zifuatazo zilifanyika: Kukamilisha usanifu na taratibu za zabuni ya mradi wa majisafi Mwanza, kukamilisha Usanifu na taratibu za zabuni ya awamu ya kwanza ya mradi wa majisafi na uondoaji majitaka Mbeya na upembuzi yakinifu wa mradi wa majisafi Iringa.

Katika mwaka 2004/2005 kazi zifuatazo zitatekelezwa: Kuanza ujenzi wa mradi wa majisafi Mwanza ikiwa ni pamoja na upanuzi wa kituo cha kusukuma maji, mtambo wa kusafisha maji, matanki mapya na upanuzi wa mtandao wa kusambaza maji, upanuzi wa mifumo ya majisafi na uondoaji majitaka pamoja na ufungaji wa dira 10,000 katika mji wa Mbeya na usanifu wa mradi wa maji Iringa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Serikali, kwa msaada wa Serikali ya Ufaransa, kupitia Shirika lake la Maendeleo *(AFD),* ilianza kutekeleza Mradi wa Uchunguzi *(Feasibility Study)* wa Majisafi na Majitaka katika Miji ya Bukoba, Musoma na Misungwi, kwa gharama ya shilingi milioni 226.1. Katika mwaka 2004/2005, uchunguzi utaendelea na unatarajiwa kukamilika Desemba, 2004 ambapo taratibu za ujenzi wa mradi zitaanza.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji Mjini Singida ambao utahusu ujenzi wa ukarabati wa mfumo uliopo, ujenzi wa chanzo kipya na uimarishaji wa mfumo wa usambazaji uliopo kwa jumla ya Shilingi bilioni 13.6 utaanza kutekelezwa mwaka 2004/2005. Fedha hizo zitatokana na mkopo wa Shilingi bilioni 5.5. kutoka Mfuko wa Nchi Zinazotoa Mafuta *(OPEC),* Shilingi bilioni 6.0 kutoka Benki ya ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Africa *(BADEA)* na kutoka Serikali yetu Shilingi bilioni 2.1. Pia, *BADEA* wametoa msaada wa shilingi milioni 280 kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa mradi wa uondoaji majitaka kwa mji wa Singida.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa miradi ya uchunguzi mwaka 2003/2004, Wizara ilifanya uchunguzi wa awali wa miradi ya majisafi na majitaka katika Miji ya Lindi, Sumbawanga na Babati. Lengo la uchunguzi huu ni kupata taarifa za

awali kwa ajili ya usanifu wa miradi ya maji safi na uondoaji wa majitaka. Aidha, kuwepo kwa taarifa hizi kutapunguza muda wa uandaaji wa miradi mipya.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inakarabati miundombinu ya majisafi na majitaka mijini kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utoaji huduma na pia kuziongezea uwezo Mamlaka za Maji Mijini katika kukusanya mapato ili hatimaye ziweze kujitegemea. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu ilitekeleza mradi wa dharura wa maji kwa mji wa Lindi ili kukabiliana na ukame uliosababisha kupungua vyanzo vya maji hadi kufikia asilimia 15% ya mahitaji yake. Mradi wa kufufua vyanzo vya maji ulitekelezwa kwa ajili ya mji wa Lindi ambapo visima 10 vyenye uwezo wa kutoa lita milioni 5 kwa siku vilichimbwa. Aidha, pampu tatu, jenereta moja na tanki lenye ujazo wa lita 500,000 vilinunuliwa na kufungwa kwa ajili ya visima vitatu, eneo la Kitunda. Kazi zote hizo ziligharimu shilingi milioni 555.3. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itaunganisha visima vitatu zaidi vilivyoko eneo la Kitunda kwenye mfumo wa kusambaza maji. Aidha, Wizara yangu itakarabati mifumo ya majisafi kwa gharama ya Shilingi milioni 70 kwa ajili ya miji ya Kigoma shilingi milioni 15, Mbeya shilingi milioni 5, Mtwara shilingi milioni 20, Musoma shilingi milioni 15 na Sumbawanga shilingi milioni 15.

Mheshimiwa spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika lake la fedha la *KfW*, ilianza awamu ya kwanza ya ukarabati wa mradi wa majisafi kwa mji wa Songea kwa gharama ya Shilingi bilioni 8.68. Hadi sasa kazi za ukarabati wa vyanzo vya maji vya mto Ruvuma, Liwoyowoyo, Lipasi, Mahilo, Luhira A na B na ukarabati wa mabomba zimekamilika. Kazi ya ujenzi wa mtambo wa kuchuja maji pamoja na tanki la maji yasiyosafishwa *(Raw Water Tank)* inaendelea na itakamilika mwezi Desemba, 2004. Katika mwaka 2004/2005, kazi ya usanifu na ujenzi wa awamu ya pili utaanza kwa gharama ya Shilingi bilioni 13.34.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu ilianza ujenzi wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka Miji ya Kahama na Shinyanga pamoja na vijiji 54 vya Mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Mradi huu una lengo la kuwapatia maji takribani wakazi milioni moja. Mkataba wa kwanza wa mradi unahusisha ujenzi wa chanzo kilichopo Ihelele, chujio na mitambo ya kusukumia maji, ulazaji wa bomba lenye urefu wa kilometa 10 kutoka chanzo cha maji hadi tangi kuu kwenye Mlima Mabale lenye lita za ujazo milioni 35. Mkataba huu wenye thamani ya Shilingi bilioni 27.5, ulisainiwa tarehe 03 Februari, 2004 Mjini Dodoma. Katika mwaka 2004/2005, Mkataba huo utaendelea kutekelezwa pamoja na kuanza utekelezaji wa Mkataba wa pili ambao unahusu ulazaji bomba kutoka tanki la Mabale hadi Solwa na Mwamashimba. *(Makofi)*

Aidha, kazi za ulazaji wa mabomba kutoka Solwa hadi Kahama na Shinyanga zitafanyika mwaka ujao wa fedha. Utekelezaji wa mradi mzima utachukua miaka miwili na unatarajiwa kukamilika kabla ya Oktoba, 2005 ambapo utakuwa umegharimu jumla ya Shilingi bilioni 85.1 kwa kutumia fedha za ndani. Huu ni mradi mkubwa tulioubuni na kuuandaa kwa muda mfupi na kwamba una changamoto kubwa ya kutumia maji shiriki.

Hivyo, kuanza utekelezaji wa mradi huu ni hatua muhimu katika kufikia dhamira yetu ya kujitegemea kwenye Sekta ya Maji na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi huu ni mkubwa na wa kihistoria, naomba kutumia fursa hii, kwa dhati kabisa, kumshukuru Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kusimamia mwenyewe na kutoa msukumo wa utekelezaji wa mradi huu kwa kutumia fedha zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina jukumu la kuanzisha, kuendeleza na kusimamia Mamlaka za Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa. Mwaka 2003/2004, Wizara ilianzisha Mamlaka mpya ya Maji kwa Mji wa Babati ambao ni Makao Makuu ya Mkoa mpya wa Manyara. Kwa sasa, Mamlaka hiyo inahudumia wakazi wa Mji wa Babati wapatao 30,000. Ili kuimarisha huduma ya maji kwa mji wa Babati, Wizara yangu imekamilisha ujenzi wa chujio la maji kwa lengo la kuongeza ubora wa maji yanayozalishwa katika chanzo kinachotumika hivi sasa. Kwa sasa, maji yanayozalishwa ni lita milioni 1.7 kwa siku sawa na asilimia 80 ya mahitaji. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itaendelea kujenga uwezo wa Mamlaka hii kwa kuinunulia nyenzo za kufanyia kazi, kulipia gharama zote za umeme na watumishi pamoja na kuwapatia mafunzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara ilitumia fedha za ndani kiasi cha Shilingi milioni 159.7 kuboresha huduma za majisafi katika Miji ya Tabora, Dodoma na Morogoro kwa kupanua mitandao ya kusambaza maji na kununua pampu za kusukuma maji katika Miji ya Kigoma na Mtwara. Pia, Wizara ilitumia kiasi cha Shilingi milioni 149.13 kupanua mtandao wa majitaka Mjini Iringa ili wakazi wengi zaidi waunganishiwe kwenye mfumo huo. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itatumia Shilingi milioni 125 kwa ajili ya kupanua mifumo ya majisafi kwa miji ya Mwanza, Dodoma, Singida, Iringa, Morogoro, Shinyanga, Tabora na Bukoba. Aidha, Shilingi milioni 50 zitatumika kupanua mifumo ya majitaka kwa miji ya Iringa, Morogoro, Tabora, Dodoma na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa maji yanayozalishwa yanatumiwa vizuri na pia katika kuhakikisha gharama halisi ya maji inalipwa na mteja kulingana na matumizi halisi, katika mwaka 2003/2004, jitihada ziliendelea kufanywa na Mamlaka za Maji Mjini kudhibiti upotevu wa maji na kuzuia matumizi mabaya kwa kufunga jumla ya dira za maji 7,000. Kwa sasa jumla ya dira za maji 100,000 zimefungwa kwa wateja wa maji wa Mamlaka zote. Hii ni sawa na asilimia 65 ya wateja 150,733, ikilinganishwa na asilimia 50 mwaka 2002/2003. Takwimu hizi hazijumuishi Jiji la Dar es Salaam na Mji wa Kibaha ambayo ina mpango wake maalum wa ufungaji dira 173,000 ulioanza kutekelezwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu iliendelea kuboresha huduma ya majitaka katika Miji ya Iringa, Dodoma, Mwanza na Tabora. Mamlaka za Majisafi na Majitaka katika Manispaa za Morogoro, Arusha, Moshi na Tanga ziliendelea kudhibiti utiririkaji ovyo wa majitaka kwa kukarabati miundombinu na kuongeza njia

ndogo za mabomba. Aidha, katika Mji wa Tabora wateja zaidi ya 200 waliunganishwa kwenye mtandao wa majitaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004 Wizara iliendelea kuwapatia mafunzo mbalimbali watumishi wa Mamlaka za Maji Mijini ili kuwaongezea uwezo kiutendaji. Mafunzo hayo yalihusu uandaaji na usimamamizi wa miradi pamoja na taaluma ya mawasiliano *(Project Identification Planning and Management and Communication Skills).* Mamlaka zilizoshiriki katika mpango huo ni Bukoba, Lindi, Kigoma, Mtwara, Tabora, Musoma, Mbeya, Sumbawanga na Songea. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itaendelea kuwapatia mafunzo watumishi wa Mamlaka za Maji katika nyanja za uendeshaji na usimamizi pamoja na taaluma za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, baada ya miundombinu ya utoaji wa huduma ya majisafi na majitaka kwa Jiji la Dar es Salaam kukodishwa kwa Kampuni ya *City Water Services Limited,* utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma hizo kwa Jiji na Miji ya Kibaha na Bagamoyo ambao utagharimu Shilingi bilioni 164.4 umeanza. Katika mwaka 2003/2004, mpango wa kazi zilizopewa kipaumbele *(Priority Works Programme)* wa kukarabati miundombinu ya kuzalisha maji kutoka vyanzo vya Ruvu Juu na Ruvu Chini pamoja na mabomba makuu yanayosafirisha maji kutoka mitambo hiyo imeanza. Kazi hii itagharimu Shilingi bilioni 6.0 hadi kukamilika. Kazi nyingine ni ukarabati wa vituo vya pampu za kusukuma majitaka baharini na kukarabati bomba kuu la kumwaga majitaka baharini utakaogharimu jumla ya Shilingi milioni 835.2.

Mheshimiwa Spika, mradi huu pia utahusisha ununuzi wa dira za maji ambapo jumla ya dira 173,000 zenye thamani ya Shilingi bilioni 5.4 zitanunuliwa na kufungwa katika kipindi cha miaka mitano ya mradi. Katika mwaka 2003/2004, jumla ya dira za maji 16,000 zimenunuliwa na kuanza kufungwa kwa kuanzia na mji wa Bagamoyo. Katika mwaka 2004/2005, Shilingi bilioni 34.6 zimetengwa kwa ajili ya kukarabati mitambo ya kusafishia maji na matangi ya kuhifadhia maji, mabwawa ya majitaka, pampu za kusukumia majitaka, mabomba ya kusambaza majisafi, ufungaji wa dira za maji 40,000, na kutekeleza mradi mdogo wa maji na usafi wa mazingira kwa Wananchi wenye kipato kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maji katika mto Ruvu, ambacho ndicho chanzo kikuu cha maji kwa Jiji la Dar es Salaam, yamekuwa yakipungua kutokana na ukame. Hali hii inasababisha upungufu wa maji kwa Jiji la Dar es Salaam pamoja na Miji ya Bagamoyo na Kibaha. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itafanya uchunguzi kwa lengo la kutafuta vyanzo vipya vya maji kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam, Miji ya Bagamoyo na Kibaha kwa gharama ya Shilingi bilioni 2.43 ikiwa ni mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuendelea kutekeleza mradi wa ukarabati wa miundombinu ya majisafi na uondoaji majitaka katika Jiji la Dar Es Salaam, Miji ya Kibaha na Bagamoyo, mwaka 2004/2005 Programu ya kuendeleza huduma za majisafi na uondoaji majitaka katika Miji Mikuu ya Mikoa 19 itaandaliwa kwa gharama ya Shilingi milioni 500 ikiwa ni mkopo kutoka Benki ya Dunia. Hii ni hatua muhimu na ya

mafanikio kwa kuwa programu hiyo itakuwa ni mwongozo kwa wawekezaji na wadau wengine katika uandaaji wa miradi kwenye Sekta ndogo ya maji mijini.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inayo rasilimali kubwa ya mifugo. Kulingana na takwimu za mwaka 2002, inakadiriwa kuwa Tanzania ina ng'ombe milioni 17.7, mbuzi milioni 12.5 na kondoo milioni 3.5, nguruwe 880,000 na kuku milioni 47. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu ilishiriki katika kufanya Sensa ya Sampuli ya Kilimo na Mifugo ili kuweza kupata takwimu sahihi za kuwezesha kuboresha mipango ya kuendeleza Sekta ya Mifugo. Zoezi hili limekamilika mwezi Januari, 2004 na hivi sasa takwimu hizo zinafanyiwa uchambuzi.

Pamoja na idadi hiyo kubwa ya mifugo, Sekta hiyo imechangia asilimia 4.3 katika Pato la Taifa mwaka 2002 kutokana na mfumo duni wa uzalishaji na ufinyu wa soko. Aidha, viwango vya ulaji wa mazao ya mifugo kama nyama, mayai na unywaji wa maziwa bado viko chini kulingana na viwango vya Kimataifa. Kwa sasa, kila Mtanzania kwa mwaka anakunywa wastani wa lita 35 za maziwa, anakula kilo 10 za nyama na mayai 27 tu. Viwango hivi vya ulaji ni vidogo ikilinganishwa na nchi nyingine. Aidha, viwango vinavyopendekezwa na Shirika la Kilimo na Chakula Duniani *(FAO)* cha lita 200 za maziwa, nyama kilo 50 na mayai 300 kwa mtu kwa mwaka. Lengo la Wizara yangu ni kubadilisha mfumo wa ufugaji nchini ili kuongeza uzalishaji na kuhamasisha ulaji wa mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa Sera ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1997 inalenga kuiwezesha Sekta ya Mifugo kuwa na tija kubwa zaidi, kuzalisha kibiashara na kuongeza pato la wafugaji na la Taifa kwa ujumla. Lengo la sera hiyo ni kuinua maisha ya Wananchi ambao msingi wa shughuli zao na namna yao ya maisha vinategemea mifugo. Msisitizo umeelekezwa kwa wafugaji wadogo ambao hawazalishi ziada ya kutosha kutokana na uzalishaji duni na tija ndogo. Katika kuhamasisha utekelezaji wa Sera hiyo, mbinu mbalimbali zimekuwa zikitumika, ikiwa ni pamoja na kusambaza nakala za Sera hiyo kwa wadau, kuendesha makongamano ya wataalam na wadau wa Sekta na kuandaa maonyesho mbalimbali. Aidha, kutokana na mabadiliko mbalimbali yanayotokea nchini na duniani kote, pamoja na maoni ya wadau wa Sekta, Sera ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1997 inahitaji kufanyiwa marekebisho ili iendane na mabadiliko hayo. Hivyo, katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itafanya mapitio ya sera hiyo, ili hatimaye kuwa na Sera kamili ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu ilishiriki kuandaa Maadhimisho ya Siku ya Wakulima na Wafugaji Nane Nane yaliyofanyika Kitaifa mkoani Mbeya. Maadhimisho hayo ambayo hufanyika katika ngazi ya kanda na Kitaifa, yanalenga kutoa nafasi kwa wadau wa Sekta ya Mifugo kupata ufafanuzi kuhusu Sera ya Mifugo, kutathmini utoaji wa huduma za mifugo nchini na kueneza teknolojia mpya za uendelezaji wa Sekta hii. Kwa mwaka 2003, maadhimisho hayo yalifunguliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na kilele kuhitimishwa na Rais Mstaafu, Mheshimiwa Alhaj Ali Hassan Mwinyi. Kaulimbiu ya Maadhimisho hayo ilikuwa ni "Ondoa Umaskini kwa Kuboresha Kilimo, Ufugaji na Ushirika". Katika maonyesho hayo, Wizara yangu ambayo pia ilionyesha

bidhaa na shughuli za ufugaji, ilipata ushindi wa kwanza Kitaifa. Wizara yangu pia ilishiriki katika kuadhimisha Siku ya Chakula Duniani ambayo hufanyika tarehe 16 Oktoba kila mwaka duniani kote. Maadhimisho hayo kitaifa yalifanyika Mkoani Ruvuma. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itaendelea kushiriki katika maadhimisho ya Nane nane ambayo Kitaifa yatafanyika mkoani Mbeya na kaulimbiu itakuwa "Zalisha Kibiashara na Hifadhi Chakula cha Kutosheleza Mahitaji ya Kaya".

Mheshimiwa Spika, makongamano ya Vyama vya Kitaalam vya Madaktari wa Mifugo *(Tanzania Veterinary Association - TVA)* na Wataalam wa Mifugo *(Tanzania Society of Animal Production - TSAP),* yameendelea kufanyika kwa madhumuni ya kueneza Sera ya Mifugo, kubadilishana uzoefu na kujifunza mambo mapya yanayojitokeza katika maendeleo ya Sekta hii. Kongamano la Wataalam wa Mifugo lilifanyika Tanga mwezi Agosti, 2003 na la Madaktari wa Mifugo lilifanyika Arusha mwezi Desemba, 2003. Wizara yangu inayafanyia kazi maazimio ya makongamano hayo ili yaweze kusaidia katika kuboresha maendeleo ya Sekta ya Mifugo nchini.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, mwezi Aprili, 2004 lilipitisha Sheria ya Maziwa *(Dairy Industry Act, 2004)*. Sheria hiyo itatumika katika kusimamia, kuboresha na kuhamasisha uzalishaji, usindikaji, utafutaji wa masoko ya maziwa na mazao yatokanayo na maziwa kwa lengo la kukidhi mabadiliko ya kiuchumi na kijamii yaliyotokea nchini. Chini ya Sheria hiyo, Bodi ya Maziwa Tanzania *(Tanzania Dairy Board)* inayoshirikisha wadau wa Sekta ya Maziwa itaundwa ili kuratibu na kusimamia shughuli za uendelezaji wa maziwa.

Mheshimiwa Spika, katika kupanua soko la ndani la unywaji wa maziwa na utumiaji wa mazao yatokanayo na maziwa, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali huadhimisha "Wiki ya Uhamasishaji Unywaji wa Maziwa" mwezi Juni kila mwaka. Sherehe za mwaka 2003/2004, zilifanyika Kitaifa Mkoani Mwanza, ambapo ujumbe ulikuwa "Glasi moja ya maziwa kila siku ni haki ya mtoto". Shughuli nyingine zilizofanyika katika wiki hiyo ni pamoja na Mkutano Mkuu wa Tatu wa Baraza Kuu la mwaka na Kongamano la Tano la Wadau wa Sekta ndogo ya Maziwa. Katika mwaka 2004/2005, sherehe hizo zitafanyika Kitaifa Mkoani Tanga. Nachukua fursa hii kuipongeza Mikoa ya Iringa, Pwani na Dar es Salaam kwa kuitikia wito wangu nilioutoa mwaka uliopita kuungana na Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha, kuwa na programu ya kuwapa wanafunzi maziwa. Nazidi kuiomba Mikoa iliyobaki nayo ifanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sekta ndogo ya maziwa ilikabiliwa wa matatizo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na uhaba wa maji na malisho, tija ndogo kutokana na aina ya mifugo na mifumo ya uzalishaji, magonjwa ya mifugo, ukosefu wa viwanda vya kusindika, masoko, mikopo, uwekezaji mdogo na elimu duni kwa wafugaji. Hata hivyo, kumekuwepo na maendeleo ya kuridhisha katika Sekta hii. Katika mwaka 2003/2004, uzalishaji wa maziwa uliongezeka na kufikia lita bilioni 1.2. Hili ni ongezeko la asilimia 20 kutoka lita milioni 980 mwaka 2002/2003. Ng'ombe wa kiasili walichangia asilimia 70 na ng'ombe wa kisasa, asilimia 30. Katika mwaka 2004/2005, lengo ni kuzalisha lita bilioni 1.3 za maziwa ambazo pamoja na jitihada zinazoendelea

kufanyika za kuhamasisha unywaji wa maziwa nchini, zitaongeza unywaji kutoka wastani wa lita 35 za sasa na kufikia lita 40 kwa mtu kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu iliendelea kuboresha mashamba 6 ya uzalishaji mitamba ya Mabuki, Sao Hill, Nangaramo, Kibaha, Kitulo na Ngerengere kwa kuongeza ng'ombe wazazi 400 aina ya Boran, kuyapatia vifaa muhimu na vitendea kazi. Lengo ni kuongeza uzalishaji wa mitamba ili isambazwe kwa wafugaji wadogo. Aidha, jumla ya mitamba 4,622, sawa na asilimia 96 ya lengo, ilisambazwa kwa wafugaji wadogo kupitia mpango wa "Kopa Ng'ombe Lipa Ng'ombe". Kati ya mitamba hiyo, 619 ilizalishwa katika mashamba ya Serikali na mitamba 4,003 ilitoka Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Aidha, jumla ya mitamba 165 ilipelekwa Mikoa ya Kusini kwa lengo la kuendeleza ufugaji. Vile vile, Mfuko wa *Tanzania Japanese Food Aid Counterpart Fund* ulitoa Shilingi milioni 107 kwa lengo la kuendeleza ufugaji wa ng'ombe wa maziwa Mkoani Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, mitamba 650 itasambazwa kutoka mashamba ya Serikali. Aidha, mitamba 4,200 itasambazwa kutoka katika Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Vile vile, mpango wa kuendeleza ufugaji katika Mikoa ya Kusini utaendelea kwa kupeleka ng'ombe 250. Kazi nyingine zitakazofanyika ni kuimarisha mashamba ya kuzalisha mitamba na kutathmini mahitaji ya kuimarisha miundombinu ya mashamba hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya *HPI, FARM Africa* na *World Vision* ilisambaza mbuzi wa maziwa 707 kwa wafugaji wadogo kupitia mpango wa "Kopa Mbuzi Lipa Mbuzi. Kati ya hao, mbuzi 105 walipelekwa mikoa ya Lindi na Mtwara. Mpango wa mwaka 2004/2005 ni kusambaza mbuzi wa maziwa 650.

Mheshimiwa Spika, asilimia 97 ya ng'ombe tulionao nchini ni wa asili wenye ukosaafu mdogo *(Low Genetic Potential)* na hivyo kuwa na viwango vidogo vya uzalishaji. Ng'ombe hawa huzalisha chini ya wastani wa lita 500 za maziwa kwa mwaka ikilinganishwa na lita kati ya 2,500 na 3,000 kwa ng'ombe chotara. Ili kufikia lengo hilo, Serikali imeendelea kuimarisha na kuboresha kituo cha madume cha *Usa River (NAIC)* cha kuzalisha mbegu bora za ng'ombe kwa ajili ya kuongeza ukosaafu wa ng'ombe wetu. Kwa sasa kituo hicho chenye madume 22 kina uwezo wa kuzalisha mbegu dozi 230,000 kwa mwaka. Ili kuongeza matumizi ya mbegu bora toka kituo hiki, Wizara yangu inaendelea kuhamasisha wafugaji wa ng'ombe juu ya matumizi ya teknolojia hii, kutoa mafunzo kwa wataalam na ununuzi wa vifaa vya kusambazia.

Katika mwaka 2003/2004, jumla ya ng'ombe 40,000 walihamilishwa sawa na asilimia 80 ya mbegu iliyozalishwa. Katika mwaka 2004/2005, kituo kitaimarishwa na kitazalisha dozi 60,000 za mbegu bora na ng'ombe 54,000 wanatarajiwa kuhamilishwa. Lengo la Wizara yangu ni kuimarisha huduma hii kwa kuanzisha vituo vya kanda vya usambazaji, kwa kuanzia na Kanda ya Juu Kusini na Kanda ya Ziwa ili kuweza kuwafikia wafugaji wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, usindikaji wa maziwa ni muhimu sana katika kuongeza thamani ya bidhaa, usalama, muda wa uhifadhi, ajira na mapato kwa wafugaji na wasindikaji. Wizara yangu inaratibu na kuhamasisha usindikaji wa maziwa nchini. Kwa sasa tunavyo viwanda 22 ambavyo vina uwezo wa kusindika lita 510,000 kwa siku, lakini vinasindika lita 150,000 kwa siku sawa na asilimia 30 ya uwezo. Hali hii imetokana na gharama kubwa ya ukusanyaji wa maziwa kutoka vijijini na gharama za usindikaji. Juhudi zinazoendelea kufanywa na Serikali ni pamoja na kulinda viwanda vya ndani, kuhamasisha wasindikaji na wazalishaji kuunda vikundi ili kuwa na nguvu ya pamoja katika usindikaji na kutafuta masoko.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, uzalishaji wa nyama uliongezeka kutoka tani 341,500 hadi kufikia tani 348,800 sawa na ongezeko la asilimia mbili. Kati ya tani hizo, nyama ya ng'ombe ilichangia asilimia 53, mbuzi na kondoo asilimia 22, kuku asilimia 18 na nguruwe asilimia saba. Ongezeko la uzalishaji wa nyama umeongeza wastani wa ulaji wa nyama kwa mtu kwa mwaka kufikia kilo 10.3 ambayo bado ni chini ya kiwango kinachotakiwa cha kilo 50 kwa mwaka. Aidha, mafunzo kwa wakaguzi wa nyama 210 yalitolewa.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza mbuzi wa nyama na kondoo, Wizara yangu inaandaa programu ya kuendeleza wanyama hao ili kuongeza uzalishaji na kupata ziada ya kuuza nje. Katika mwaka 2003/2004, shamba la mifugo la Ngerengere limeimarishwa kwa kupatiwa mbuzi wa asili 200 na wengine 65 aina ya *Boer* walinunuliwa kutoka Afrika ya Kusini ili kuzalisha kwa wingi mbuzi chotara ambao ni bora zaidi watakaosambazwa kwa wafugaji wadogo. Katika mwaka 2004/2005, lengo ni kuzalisha tani 378,510 za nyama na kutoa mafunzo kwa watumishi 400 wa ukaguzi wa nyama.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, uzalishaji wa ng'ombe wa nyama uliendelea katika ranchi za mfano za *NARCO* ambapo ng'ombe waliongezeka kwa asilimia 7.8, kutoka ng'ombe 42,187 mwaka 2002/2003 na kufikia 45,500. Katika kipindi hicho, *NARCO* ilizalisha na kuuza mitamba 2,000 ya maziwa, iliuza ng'ombe wa nyama 9,800 na ilinunua ng'ombe 3,000 kutoka kwa wafugaji kwa lengo la kuwanenepesha na kwa hivyo, kuwapatia wafugaji soko la mifugo yao.

Aidha, Kampuni ilizalisha mbuzi na kondoo 3,060 wa nyama katika ranchi za West Kilimanjaro, Kongwa na Mzeri. Katika mwaka 2004/2005, *NARCO* inatarajia kuwa na ng'ombe 48,000 ambapo itazalisha ndama 12,100 wa nyama na mitamba 3,000 wa maziwa. Vile vile, itanunua ng'ombe 4,000 wa kunenepesha kutoka kwa wafugaji na kuuza ng'ombe 11,300.

Mheshimiwa Spika, shughuli za uzalishaji kuku zimeendelea chini ya Sekta binafsi ambapo kwa sasa kuku wa kienyeji wameongezeka kutoka milioni 27 mwaka 2001 na kufikia milioni 30 mwaka 2003/2004 na kuku wa kisasa kutoka milioni 20 hadi kufikia milioni 25 katika kipindi hicho. Ongezeko hili limetokana na jitihada za kudhibiti magonjwa na hasa ugonjwa wa mdondo na uhamasishaji ufugaji bora. Katika mwaka 2003/2004, jumla ya vifaranga milioni 18.4 vya kuku wa kisasa vilizalishwa nchini.

Aidha, mayai ya kutotolea vifaranga milioni 5.5 na vifaranga milioni moja viliagizwa toka nje na hivyo kufanya uzalishaji wa vifaranga kuwa milioni 24.7. Uzalishaji huo ni mdogo ikilinganishwa na mahitaji ya vifaranga milioni 59 kwa mwaka. Hali hii inatokana na kupanda kwa gharama za uzalishaji vyakula, madawa na uhaba wa vifaranga na mayai ya kuangua vifaranga. Katika mwaka 2004/2005 lengo ni kuzalisha vifaranga milioni 34.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji mayai umeongezeka kutoka milioni 790 mwaka 2002/2003 hadi kufikia milioni 910 mwaka 2003/2004. Aidha, ulaji wa mayai kwa mtu kwa mwaka umeongezeka kutoka wastani wa mayai 23 mwaka 2002/2003 hadi kufikia 27. Ongezeko hili limetokana na uhamasishaji na elimu juu ya ufugaji bora wa kuku wa kienyeji na wa kisasa. Katika mwaka 2004/2005, lengo ni kuzalisha mayai bilioni 1.8 kwa kuwa wafugaji wengi wamehamasika kutumia chanjo.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya hivi karibuni, biashara ya ufugaji nguruwe imeshamiri katika sehemu nyingi nchini na hivyo kuongeza kipato cha wafugaji na wafanyabiashara. Uzalishaji wa nyama ya nguruwe umeongeka kutoka tani 23,000 mwaka 2002/2003 hadi tani 26,000 mwaka 2003/2004, ikiwa ni ongezeko la asilimia 13. Tatizo kubwa linalokabili uendelezaji wa nguruwe nchini ni pamoja na ukosefu wa mbegu bora unaofanya uzalishaji wa ndani ya ukoo mmoja utokee *(inbreeding),* lishe duni, magonjwa na mfumo dhaifu wa soko. Ili kuimarisha uzalishaji wa nguruwe, Wizara yangu inaimarisha shamba la mifugo la Ngerengere ili liweze kuzalisha na kusambaza mbegu bora kwa wafugaji. Lengo la mwaka 2004/2005 ni kuzalisha tani 27,000 za nyama ya nguruwe.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatoa kipaumbele katika usindikaji wa nyama ili kukuza soko la ndani na nje ya nchi kwa maendeleo ya Sekta hii. Kukosekana kwa viwanda na miundombinu muhimu ya masoko kunafanya sehemu kubwa ya biashara ya mifugo pamoja na mazao yake kuwa isiyo rasmi. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu, kupitia Mradi wa Uendelezaji Masoko ya Mifugo nchini *(TLMP),* iliendelea kukarabati miundombinu ya masoko ya mifugo nchini. Wizara ilikarabati vituo sita vya kupumzishia mifugo, kituo kimoja cha karantini, vituo viwili vya ukaguzi wa afya na mnada mmoja wa awali. Aidha, vituo viwili vya kupakilia na kupakua mifugo relini na mabehewa sita ya kusafirisha ng'ombe yalikarabatiwa.

Idadi ya ng'ombe waliouzwa katika minada nchini kutoka kwa wafugaji iliongezeka kwa asilimia 35 kutoka 487,181 mwaka 2002/2003 na kufikia 659,865 mwaka 2003/2004. Kutokana na mafanikio ya ukarabati wa miundombinu ya mifugo nchini, nchi yetu imeanza kuuza mifugo nje ya nchi. Katika mwaka 2003/2004 ng'ombe 1,807 na mbuzi 565 wenye thamani ya Shilingi milioni 652 waliuzwa nchini Comoro. Harakati za kutafuta masoko zaidi ya mifugo na mazao yake katika nchi za Ghuba chini ya *Red Sea Livestock Trade Commission* zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa idadi ya watu katika miji mbalimbali, kuanzishwa kwa maduka makubwa ya kisasa na mahoteli ya kitalii nchini, kunafanya mahitaji ya nyama iliyo bora na salama kuongezeka. Wizara yangu inatoa umuhimu wa

kuwa na machinjio yenye hadhi na yanayokidhi viwango vya uchinjaji ili kuongeza thamani ya mifugo na mazao yake. Hadi sasa tunayo machinjio ya kisasa ya Sakina (Arusha), Mwika (Moshi) na Lwamishenyi (Bukoba). Pamoja na kwamba shughuli za ujenzi na uendeshaji machinjio ni za Sekta binafsi chini ya Halmashauri za Miji/Wilaya, Serikali imefanya yafuatayo: -

- Imekamilisha ujenzi wa machinjio ya kisasa Mjini Dodoma yenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 214 na mbuzi na kondoo 200 kwa shifti kwa siku. Kukamilika kwa machinjio haya kutaongeza soko la uhakika la mifugo na bei nzuri kwa wafugaji na walaji wa zao la nyama. Machinjio yataajiri watu 60. Wizara yangu inaandaa taratibu za kumpata mwendeshaji binafsi wa machinjio hayo. *(Makofi)*

- Imekamilisha ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ukataji Nyama Dodoma. Chuo hiki kitatoa mafunzo kwa wataalam 74 kila mwaka katika ngazi ya ufundi sadifu wa kuchinja na kutengeneza mazao mbalimbali yatokanayo na nyama.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia inatoa umuhimu katika ujenzi wa viwanda vya kusindika nyama kama njia mojawapo ya ufumbuzi wa tatizo la soko la mifugo hapa nchini. Tofauti na sekta ndogo ya maziwa, uwekezaji katika usindikaji wa nyama ni mdogo na kufanya nchi iendelee kutokuwa na viwanda vya kusindika nyama. Hata hivyo, kuna viwanda vidogo saba vya kusindika nyama katika mikoa ya Dar es Salaam viwili, Arusha vitatu, Iringa kimoja na Ruvuma kimoja ambavyo vinatoa aina chache za mazao. Ujenzi wa viwanda zaidi vya kusindika nyama katika maeneo mbalimbali utasaidia wafugaji kupata soko la uhakika.

Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itaendelea na ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya mifugo, ikiwa ni pamoja na masoko ya mifugo katika Mikoa ya Morogoro, Iringa, Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Lindi na Mtwara ili kupanua biashara ya mifugo. Aidha, maandalizi ya kutunga Sheria ya Nyama *(Meat Industry Act),* ambayo itaunda Bodi ya Nyama nayo inategemewa kukamilika hivi karibuni ili ihusike na uendelezaji na usimamizi wa sekta ndogo ya nyama nchini.

Mheshimiwa Spika, ngozi ni zao muhimu la mifugo linaloliingizia Taifa fedha za kigeni. Katika mwaka 2003/2004 jumla ya vipande vya ngozi milioni 3.7 vyenye thamani ya Shilingi bilioni 6.5 vilikusanywa sawa na ongezeko la asilimia 37 zilizokusaywa mwaka 2002/2003. Aidha, vipande vya ngozi milioni 3.4 vyenye thamani ya Shilingi bilioni 5.7 viliuzwa nje sawa na ongezeko la asilimia 54 ya ngozi zilizouzwa mwaka 2002/2003. Hali hii imetokana na ongezeko la bei katika soko la nje na ubora wa ngozi unaotokana na juhudi za Wizara katika kutoa elimu juu ya mbinu bora za uwekaji chapa, uchunaji, uwambaji na hifadhi ya ngozi. Aidha, wafanyabiashara 17 walipatiwa leseni na wakaguzi wa ngozi 210 walipatiwa mafunzo.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha ufugaji nchini, Serikali ilianzisha Mfuko wa kuendeleza Sekta ya Mifugo kutokana na ushuru wa asilimia 20 unaotozwa ngozi ghafi zinazouzwa nje. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2004 zaidi ya Shilingi milioni 736 zilikuwa

zimekusanywa na Mamlaka ya Mapato nchini *(TRA)*. Aidha, Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa, kupitia Mfuko wa *Common Fund for Commodities (CFC),* limetoa dola za kimarekani 400,000 kwa ajili ya kuendeleza zao la ngozi hapa nchini katika kipindi cha miaka mitatu ijayo.

Katika mwaka 2004/2005, lengo ni kukusanya vipande vya ngozi milioni 4.1 vyenye thamani ya Shilingi bilioni 7.2 na kuuza nje vipande vya ngozi milioni 3.7 vyenye thamani ya Shilingi bilioni 6.3 na watumishi 400 watapatiwa mafunzo juu ya ukaguzi wa ngozi. Aidha, Sheria ya Ngozi Sura 544 ya Mwaka 1963 itafanyiwa marekebisho ili kukidhi mabadiliko ya kiuchumi yanayoendelea nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nchi yetu kuwa na ardhi ya kutosha kwa shughuli za ufugaji, ufanisi wa Sekta ya Mifugo unakwamishwa na matumizi duni ya ardhi na mifumo ya ufugaji. Katika kukabiliana na hali hii, Wizara yangu iliendelea kuzihamasisha Halmashauri za Wilaya kutenga maeneo ya mifugo na kuhakikisha wafugaji wanamilikishwa na kuyaendeleza ili kuwa na mipango ya ufugaji wa kisasa na endelevu kama inavyoelekeza Sheria ya Vijiji Namba 5 ya Mwaka 1999 na Waraka wa Rais Namba 1 wa mwaka 2002. Aidha, wafugaji wameendelea kuhamasishwa ili kubadili mfumo wa ufugaji wa asili ili uwe wa kibiashara kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na redio, vipeperushi, vijarida na mafunzo vyuoni. Vile vile, Wizara yangu ilitoa mafunzo kwa wafugaji wa ng’ombe wa asili 20 wenye ng’ombe wengi na maeneo binafsi wanaotaka kuanzisha ufugaji wa kisasa wa ranchi na tayari wameunda Umoja wa Wafugaji wa Kanda ya Mashariki (UWAKAMA) wenye wanachama waanzilishi 104. Kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Wizara yangu itatoa mafunzo ya aina hiyo kwa wafugaji wengine wa asili 70 katika mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Mikoa mingi nchini inakabiliwa na uhaba wa maji kwa ajili ya mifugo na hivyo kusababisha wafugaji kuhamahama ili kutafuta maji na malisho. Hali hii husababisha migogoro ya ardhi na kuenea kwa magonjwa ya mifugo. Ili kupunguza tatizo hilo, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu ilichangia jumla ya Shilingi milioni 238 kwa ajili ya kuchimba na kukarabati malambo 70 katika Wilaya 34 kwenye Mikoa 15 iliyo kame na yenye mifugo mingi. Hii inafanya idadi ya malambo yote yaliyochangiwa na Wizara yangu tangu mwaka 2001/2002 kufikia 298. *(Makofi)*

Ujenzi na ukarabati wa malambo 177 umekamilika na mengine yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wasaidie kuhamasisha Halmashauri za Wilaya na Wananchi ili wachangie kikamilifu gharama za ujenzi na ukarabati wa malambo katika maeneo yao ili kupunguza tatizo la upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo yao. Katika mwaka 2004/2005 Wizara itachangia ujenzi na ukarabati wa malambo 60 katika Wilaya 25 nchini.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa mbegu bora za malisho ni muhimu katika kuendeleza ufugaji nchini. Mbegu zinazozalishwa hazikidhi mahitaji kutokana na kuendelea kuzalishwa na Taasisi na mashamba yanayomilikiwa na Serikali. Katika mwaka 2003/2004, mashamba ya mbegu za malisho ya Vikuge (Pwani) na Langwira (Mbeya) yaliimarishwa. Jumla ya tani 7 za mbegu bora za malisho na marobota 78,000

ya nyasi kavu zenye lishe bora (hei) zilizalishwa. Kati ya hizo, Sekta binafsi ilizalisha marobota 28,000. Katika mwaka 2004/2005 lengo ni kuimarisha mashamba haya ili yaweze kuzalisha tani 9 za mbegu bora za malisho na marobota 60,000 hei. Aidha, Sekta binafsi inategemewa kuzalisha marobota 40,000 ya hei.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa vyakula vya mifugo vyenye virutubisho muhimu umeendelea kufanywa na Sekta binafsi. Hata hivyo, vyakula hivyo havizalishwi kwa viwango vya ubora vinavyotakiwa. Kutokana na hali hii, Wizara yangu inairekebisha Sheria ya Mbolea na Vyakula vya Mifugo Sura ya 467 ya mwaka 1962 kwa lengo la kusimamia ubora wa vyakula vya mifugo. Katika mwaka 2003/2004, mafunzo kuhusu ubora wa vyakula vya mifugo yalitolewa kwa wataalam wa mifugo 54 kutoka Kanda za Kaskazini, Mashariki, Nyanda za Juu Kusini, Ziwa na Kati. Lengo ni kuwawezesha wataalam hao kusimamia ubora wa vyakula vya mifugo. Aidha, uzalishaji wa vyakula vya mifugo ulifikia tani 492,000 ikilinganishwa na mahitaji ya tani 650,000. Katika mwaka 2004/2005, jumla ya tani 550,000 za vyakula vya mifugo zitazalishwa. Aidha, mafunzo yatatolewa kwa wataalam 260 wa vyakula vya mifugo na watumiaji wa vyakula vya mifugo 480.

Mheshimiwa Spika, huduma bora za afya ya mifugo zinapunguza kuenea kwa magonjwa ya wanyama, vifo vya mifugo na kulinda watumiaji wa mazao ya mifugo kutokana na maambukizo ya magonjwa. Aidha, kupungua kwa magonjwa kutaongeza soko la mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi. Jukumu la Serikali ni kudhibiti magonjwa ya milipuko na magonjwa yanayoambukiza binadamu, kufanya ukaguzi na kusimamia taratibu za afya ya mifugo. Udhibiti wa magonjwa yasiyo ya milipuko ni jukumu la mfugaji na anapaswa kugharamia huduma za madawa, chanjo na pembejeo. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu iliendelea kuzuia na kudhibiti magonjwa ya mifugo, hasa ya milipuko. Magonjwa hayo ni Sotoka, Homa ya Mapafu, Ugonjwa wa Miguu na Midomo, Ugonjwa wa Kuvimba Ngozi, Homa ya Nguruwe, Ugonjwa wa Mdondo wa Kuku, Kimeta na Chambavu.

Aidha, udhibiti wa magonjwa yaenezwayo na kupe, mbung'o na magonjwa ya mifugo yanayoambukiza binadamu kama vile Kifua Kikuu *(TB)*, Ugonjwa wa Kutupa Mimba *(Brucellosis)* na Kichaa cha Mbwa uliendelea.

Mheshimiwa Spika, shughuli za kutokomeza ugonjwa wa Sotoka ziliendelea kutekelezwa na Wizara yangu chini ya Mradi wa Kudhibiti Milipuko ya Magonjwa ya Mifugo *(Pan African Programme for the Control of Epizootics - PACE),* unaogharimiwa na Nchi za Jumuiya ya Ulaya *(EU)* na kuratibiwa na Umoja wa Nchi za Afrika chini ya taasisi yake ya Raslimali za Wanyama *(AU-IBAR).*

Katika mwaka 2003/2004 Wizara yangu ilifuatilia dalili za ugonjwa wa Sotoka katika Wilaya tisa zinazopakana na nchi ya Kenya na maeneo ya mbuga za wanyama katika wilaya hizo. Sampuli za damu ya ng'ombe 11,736, mbuzi na kondoo 3,600 na wanyamapori 41 zilichunguzwa kwa lengo la kubaini dalili za sotoka. Matokeo yalionyesha kuwa ugonjwa huo haupo nchini. Ugonjwa wa Sotoka ni miongoni mwa magonjwa yanayozuia nchi kuingia katika biashara ya mifugo duniani. Katika mwaka

huu wa fedha Wizara yangu itafanya uchunguzi wa dalili za sotoka kwa kuchukua sampuli za damu ya ng'ombe 12,500, mbuzi na kondoo 4,500 na wanyamapori 45 ili kuweza kuthibitisha kama ugonjwa huu umetokomezwa ili tuweze kutambuliwa na kutangazwa kwa Jumuiya za Kimataifa na Shirika la Shirika la Kimataifa la Afya ya Mifugo *(Office Internationale des Epizooties - OIE)*.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa Homa ya Mapafu *(CBPP),* ambao ulitangazwa na Serikali kuwa ni janga la Taifa mwaka 2001, bado ni tishio kwa maendeleo ya Sekta ya Mifugo. Ugonjwa huu upo katika Wilaya 55 za Mikoa 20 ya Tanzania Bara. Kutokana na juhudi za Serikali za kudhibiti ugonjwa huo, matukio ya ugonjwa huu yanaendelea kupungua kutoka 3,904 mwaka 2001/2002 hadi 1,463 mwaka 2003/2004. Aidha, katika kipindi hicho, vifo vya ng'ombe navyo vimepungua kutoka 3,275 hadi 696. Juhudi za kukabiliana na ugonjwa huu zinaelekezwa katika chanjo na udhibiti wa usafirishaji holela wa mifugo. Dawa za chanjo dozi milioni saba zenye thamani ya Shilingi milioni 490 zilinunuliwa na zinaendelea kusambazwa katika Wilaya 57 kwa ajili ya kuchanja jumla ya ng'ombe milioni 6.5.

Katika mwaka 2004/2005, jumla ya dozi milioni sita zitanunuliwa kwa Shillingi milioni 420 ili kuendelea na chanjo ya kudhibiti ugonjwa huu. Lengo ni kuchanja na kuweka ukanda usio na maambukizo katika Wilaya 13 Kusini na Kusini Magharibi mwa nchi yetu. Udhibiti wa ugonjwa huu huhitaji chanjo za kurudiwa kwa mfululizo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, kuna aina tatu za virusi vinavyosababisha ugonjwa wa Miguu na Midomo *(FMD; O, SAT1* na *SAT2)* hapa nchini na hivyo kufanya udhibiti wake kuwa mgumu. Katika mwaka 2003/2004, kumekuwepo na matukio 308 ambayo yalitolewa taarifa ambapo jumla ya ng'ombe 24,957 waliugua na 407 walikufa. Udhibiti wa ugonjwa huo ulihusisha uchanjaji na uzuiaji wa usafirishaji wa mifugo na bidhaa zake kutoka kwenye maeneo yenye ugonjwa. Programu za kudhibiti ugonjwa huu zimewasilishwa na kuombewa fedha kutoka kwa wafadhili kupitia mipango ya pamoja ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki *(EAC)*. Katika mwaka 2004/2005, Serikali itaendelea kushirikiana na nchi hizo katika kudhibiti ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na kuchanja mifugo, kudhibiti usafirishaji wa mifugo na mazao yake ili kuzuia ugonjwa huo usienee zaidi kama unavyoagiza Waraka wa Rais Namba 1 wa mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, ugonjwa huu ulitokea katika Wilaya za Arumeru, Manispaa ya Arusha, Kigoma, Kasulu, Kibondo na Tabora Mjini ambapo kulikuwa na jumla ya milipuko 7 yenye matukio 873 yaliyosababisha vifo 1,167. Nguruwe 9,394 walikuwa kwenye hatari ya kuambukizwa ugonjwa. Ugonjwa huo hauna tiba wala kinga na ni hatari katika uendelezaji wa ufugaji wa nguruwe hapa nchini. Hata hivyo, ugonjwa huo umedhibitiwa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Mbeya ambako ulikuwa tishio mwaka 2002/2003. Katika mwaka 2004/2005, jitihada kubwa zitawekwa katika kudhibiti usafirishaji holela wa nguruwe na mazao yake na kuchukua hatua za haraka kuutokomeza ugonjwa huo kila unapotokea. Hatua hizo ni pamoja na kuweka eneo lilioambukizwa chini ya karantini, kuchinja nguruwe wote katika eneo

lililoambukizwa, kusafisha mabanda kwa dawa maalum pamoja na kutofuga nguruwe kwa muda usiopungua miezi sita.

Mheshimiwa Spika, magonjwa yanayoenezwa na kupe husababisha kati ya asilimia 70 na 80 ya vifo vyote vya ng'ombe hapa nchini. Kati ya vifo hivyo asilimia 61 husababishwa na Ndigana Kali *(ECF),* asilimia 23 Ndigana Baridi *(Anaplasmosis),* asilimia tisa Maji kwenye Moyo *(Heartwater)* na asilimia saba Kukojoa Damu *(Babesiosis).* Katika mwaka 2003/2004, ng'ombe 163,333 waliugua, kati yao ng'ombe 44,100 wenye thamani ya shilingi bilioni 44.1 walikufa. Aidha, ugonjwa wa *Ormillo (Cerebral Theileriosis)* unaosababishwa na kupe uliua ng'ombe 110,000 katika mikoa ya Arusha, Manyara na Morogoro. Uchunguzi wa kitaalam bado unaendelea kufanyika kwa msaada wa Serikali ya Uingereza kupitia Shirika lake la *DFID* ili kujua kiwango cha usambaaji na madhara yatokanayo na ugonjwa pamoja na kutambua aina za kupe wanaoeneza ugonjwa huo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, chanjo dhidi ya Ndigana Kali ilifanyika katika Mikoa ya Morogoro, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Kagera, Mbeya, Tanga, Iringa na Mtwara. Jumla ya ng'ombe waliochanjwa waliongezeka kutoka ng'ombe 20,278 mwaka 2002/2003 na kufikia 55,000 mwaka 2003/2004. Kati ya hao, ng'ombe 35,000 ni wa asili ambapo kutokana na uchanjaji huu, vifo vya ndama vimepungua kutoka kati ya asilimia 40 - 50 hadi asilimia 5 -10 kwa wale waliochanjwa. Aidha, kampeni zaidi ya uhamasishaji wa matumizi ya chanjo hiyo kwa wafugaji wenye mifugo ya asili katika Mikoa mingine unaendelea kufanyika. Ili kuwa na mipango madhubuti na endelevu, Wizara inandaa Mkakati wa Kudhibiti Kupe na Magonjwa Yanayoenezwa na Kupe kwa lengo la kuhimiza matumizi sahihi ya dawa ya kuogesha inayozingatia hifadhi ya mazingira pamoja na kutumia chanjo.

Katika mwaka 2004/2005 Serikali itaendelea na ukarabati wa majosho, uchanjaji wa ng'ombe dhidi ya ugonjwa wa ndigana kali, kutoa mafunzo na uhamasishaji wa matumizi ya chanjo hiyo kwa wafugaji wa ng'ombe wa asili. Pia, ufuatiliaji wa matibabu kwa ng'ombe wenye dalili za ugonjwa wa *Ormillo* utaendelea ili hatimaye uweze kudhibitiwa. Aidha, Wizara itaendelea na uchunguzi wa ueneaji wa aina ya kupe, usugu wa kupe dhidi ya dawa za kuogeshea na kutathmini chanjo ya *ECF* kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, kama inavyoonekana katika maelezo yaliyotangulia magonjwa yanayoenezwa na kupe ndio chanzo cha vifo vingi vya mifugo. Njia ya kuzuia vifo hivyo ni uogeshaji wa mifugo kwa dawa zinazofaa. Lakini, pamoja na kulifahamu hili wafugaji wengi hawaogeshi mifugo kutokana na gharama kubwa za madawa ya mifugo. Katika kuondoa tatizo hili Serikali itatoa ruzuku ya kati ya asilimia 20 hadi 30 kwa madawa ya kudhibiti magonjwa yaletwayo na kupe (dawa ya uogeshaji) ili dawa hizo ziweze kumfikia mfugaji kwa bei nafuu. Ruzuku hii itaigharimu Serikali Shilingi 1.0 bilioni kwa mwaka. Hatua hii inategemewa kupunguza vifo vya mifugo na kwa hiyo kupunguza umaskini, lakini pia kutokomeza magonjwa ya mifugo nchini, ili hatimaye kutuwezesha kushiriki katika masoko ya mifugo Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asilimia 40 ya nyanda zinazofaa kwa malisho zina tatizo la mbung'o hivyo kuzuia ufugaji katika maeneo hayo. Hali hii imesababisha ufugaji kufanyika katika eneo dogo na kusababisha msongamano na uharibifu wa mazingira. Aidha, mbung'o hueneza ugonjwa wa Nagana kwa wanyama na kuathiri uzalishaji.

Kampeni ya kutokomeza Mbung'o na ugonjwa wa Nagana Barani Afrika imeendelea kufanyika chini ya Taasisi ya Raslimali za Wanyama wa Umoja wa Nchi za Afrika *(AU/IBAR)*. Aidha, mradi wa *Farming in Tsetse Controlled Areas (FITCA)* unaofadhiliwa na Jumuiya ya Nchi za Ulaya umeendelea kutekelezwa kwa lengo la kuwafundisha na kuwawezesha wafugaji kutumia mbinu shirikishi ya kutumia mitego na vitambaa vyenye sumu ya kuua mbung'o. Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya za Karagwe, Bukoba Vijijini, Pangani na Handeni. Katika mwaka 2003/2004, wataalam 49 kutoka katika Wilaya zenye mbung'o walipatiwa mafunzo na uchunguzi wa ueneaji wa mbung'o *(tsetse survey)* na utayarishaji wa ramani umefanywa kwa Wilaya zote za Mkoa wa Mara. Kutokana na juhudi hizi, ng'ombe waliopatwa na ugonjwa wa nagana wamepungua kutoka 14,406 mwaka 2002/2003 hadi 4,520 kati ya ng'ombe 527,658 walioko kwenye hatari ya kuambukizwa. Katika mwaka 2004/2005 shughuli za kuondoa mbung'o na kutokomeza nagana zitaendelezwa na watumishi 100 watapatiwa mafunzo juu ya teknolojia mpya ya kudhibiti mbung'o.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, ugonjwa wa mdondo umeendelea kudhibitiwa kwa kiwango kikubwa kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya chanjo ya mdondo inayostahimili joto. Jumla ya kuku milioni 5.4 walichanjwa katika Vijiji 255. Tathmini iliyofanyika katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kusini na Kati imeonyesha vifo vya kuku kutokana na mdondo vimepungua kutoka asilimia 90 hadi chini ya asilimia 10. Hivi sasa, chanjo inapatikana katika Vituo vyote vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo *(Veterinary Investigation Centres - VICs)* hapa nchini. Hivyo, natoa wito kwa Halmashauri za Wilaya na Waheshimiwa Wabunge kuwahamasisha wafugaji kutumia chanjo hii ili kutokomeza ugonjwa huu. Katika mwaka 2004/2005, uhamasishaji wa kutumia chanjo hiyo utaendelea kutolewa kwa wafugaji wa kuku. Katika mwaka 2004/2005 uhamasishaji wa kutumia chanjo hiyo utaendelea kutolewa kwa wafugaji wa kuku. Kutokana na athari kubwa inayosababishwa na ugonjwa huo, Serikali inaandaa utaratibu wa kutoa ruzuku ya Shilingi milioni 200 ili kuboresha usambazaji wa chanjo ya mdondo kwa lengo la kupunguza gharama kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo yanayoambukiza binadamu ambayo ni kutupa mimba, kifua kikuu, tegu, kimeta na kichaa cha mbwa. Katika mwaka 2003/2004, jumla ya ng'ombe 2,750 walichunguzwa ugonjwa wa kifua kikuu na 6,703 walichunguzwa ugonjwa wa kutupa mimba. Jumla ya dozi 60,000 za dawa ya chanjo ya kichaa cha mbwa zilinunuliwa na Serikali na kusambazwa katika Wilaya 30 zilizotoa taarifa za matukio ya ugonjwa huo. Halmashauri kwa kushirikiana na Sekta Binafsi wamechanja jumla ya mbwa 5,000 na ng'ombe 150,559. Vile vile, vipeperushi 5,000 viliandaliwa na kusambazwa katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Arusha, Manyara na Kilimanjaro kwa ajili ya kutoa elimu na kuhamasisha juu ya uzuiaji wa ugonjwa huu. Katika mwaka 2004/2005, Wizara

itanunua dozi 50,000 za chanjo zenye thamani ya Shilingi milioni 15, kuendelea na uchunguzi pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu athari za magonjwa hayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha vituo 6 vya kanda vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo *(VICs)* vya Mwanza, Tabora, Arusha, Iringa, Mpwapwa na Mtwara ili viweze kuongeza ufanisi katika uchunguzi na kutoa taarifa za magonjwa ya mifugo. Katika mwaka 2003/2004, vituo vyote vimepewa magari, vifaa vya maabara, vitendea kazi pamoja na mafunzo kuhusu utambuzi wa magonjwa kwa kutumia teknolojia za kisasa. Katika mwaka 2004/2005, Vituo vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo vitaendelea kuimarishwa kwa kuvipatia vifaa zaidi.

Mheshimiwa Spika, shughuli za kudhibiti uingizaji na utoaji wa mifugo na mazao yake zimeendelea kutekelezwa katika vituo 20 vya mipakani, 4 vya viwanja vya ndege, 13 bandarini na 381 vya ndani. Katika mwaka 2003/2004, Ofisi nne za *Mbamba Bay,* Isongole, Kasesya na Sirari zimeimarishwa. Aidha, wakaguzi wamepatiwa sare, mafunzo, vitendea kazi zikiwemo pikipiki 15. Katika mwaka 2004/2005, vituo vilivyobaki vitaendelea kuimarishwa kwa kujengewa ofisi, kupatiwa vitendea kazi na mafunzo ili viweze kudhibiti usafirishaji wa mifugo na mazao yake.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya utoaji wa huduma ya afya ya mifugo inatolewa na Sekta Binafsi. Kutokana na hali hiyo, sheria mbili muhimu, zinazohusu magonjwa ya mifugo na huduma za mifugo *(Veterinary Act No. 16, 2003* na *Animal Disease Act No. 17, 2003)* zimepitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Novemba, 2003 ili kudhibiti na kusimamia vyema mienendo ya utoaji huduma ya afya ya mifugo. Chini ya Sheria ya Huduma za Mifugo, Baraza Kuu la Huduma za Afya ya Mifugo *(Veterinary Council)* ndilo lenye mamlaka ya kusimamia utoaji wa huduma za afya ya mifugo zinazotolewa na watumishi wa umma na Sekta binafsi. Taratibu za kuunda Baraza hilo zinaendelea. Aidha, kila Wilaya itaorodhesha na kutunza kumbukumbu za wataalam wa ngazi za stashahada na astashahada na kutakuwa na mfumo wa mawasiliano na Baraza Kuu. Wizara imeandaa rejista na kanuni husika kwa ajili ya uorodheshaji.

Katika mwaka 2003/2004, Bodi ya Madaktari wa Mifugo ilisajili madaktari wa mifugo 36 na kufanya jumla ya madaktari waliosajiliwa nchini kufikia 495, kati ya hao, madaktari 225 wanafanya kazi Serikalini na Taasisi za Umma na waliobakia 270 wanafanya katika Sekta binafsi. Vile vile, vituo vinne vya kutolea huduma ya afya ya mifugo na kliniki 2 za mifugo zilisajiliwa na kufanya jumla ya vituo na kliniki kufikia 89.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa sehemu kubwa ya utoaji wa huduma za afya ya mifugo inatolewa na Sekta binafsi. Hata hivyo, Sekta hiyo bado haijaimarika vya kutosha kuweza kutoa huduma hiyo vijijini walipo wafugaji wengi. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu iliendelea kuhamasisha Halmashauri za Wilaya kuhusu ushirikishwaji wa Sekta binafsi katika kutoa huduma za Mifugo. Halmashauri zilishauriwa kutumia utaratibu wa mikataba na kuzingatia sheria zinapohusisha Sekta binafsi ili huduma zinazotolewa ziweze kuhakikiwa.

Kwa mwaka 2004/2005, Wizara itaendelea kusimamia maadili ya utoaji huduma na matumizi ya dawa za mifugo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Chakula na Dawa *(TFDA)*. Aidha, Wizara itaendelea na urekebishaji wa sheria za zamani, kuandaa kanuni za sheria mpya, kusimamia uorodheshaji wa wataalam na kuhamasisha ushirikishwaji wa Sekta binafsi katika utoaji huduma kufikia ngazi za Vijiji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu iliendelea kuboresha utoaji wa huduma za ugani kwa kujenga uwezo wa Maafisa Ugani wa Wilaya ili waweze kutoa huduma hizo kwa kushirikisha Wananchi. Jumla ya Maafisa Ugani 312 wa ngazi za Wilaya, Kata na Vijiji katika Halmashauri za Wilaya 22 za Kanda ya Mashariki walipatiwa mafunzo ya Upangaji Mipango shirikishi ya shughuli za ugani *(Participatory Extension Programme Planning).* Aidha, wafugaji wameendelea kuelimishwa kuhusu ufugaji bora kwa kuwapatia vijitabu na vipeperushi na kupitia vipindi vya redio. Zaidi ya nakala 20,000 za vipeperushi mbalimbali kuhusu ufugaji bora vilisambazwa. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kuhusu ufugaji bora na wa kibiashara kwa kutumia mbinu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa mifugo nchini umeendelea kwa kutumia mbinu shirikishi ili kutafuta teknolojia sahihi na endelevu yenye kuweza kutatua matatizo yanayowakabili wafugaji. Lengo kuu likiwa ni kuhakikisha matokeo ya utafiti yanawafikia wafugaji kupitia kwa washauri wa mifugo ili kuongeza uzalishaji, tija na mapato yao.

Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu iligharamia utafiti wa mifugo katika Taasisi na Vituo vya Utafiti vya Mpwapwa, *ADRI* Temeke, Kongwa, Tanga na *West Kilimanjaro.* Aidha, utafiti wa mifugo hufanyika kupitia Taasisi nyingine ikiwemo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Utafiti unaofanywa unahusu magonjwa ya mifugo; uzalishaji wa maziwa, nyama, mayai, uendelezaji wanyama wadogo na nyanda za malisho.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, utafiti katika Taasisi ya Uzalishaji na Utafiti Mpwapwa uliendelea kwa kununua mitamba 300 ya ng'ombe aina ya Boran kutoka Ranchi ya Kongwa kwa ajili ya kuendeleza uzalishaji wa ngo'mbe aina ya Mpwapwa kwa msaada wa Shilingi milioni 126 toka *JICA.* Jumla ya ndama chotara 154 walizalishwa kwenye Taasisi hiyo. Lengo ni kuongeza ng'ombe aina ya Mpwapwa hadi kufikia zaidi ya 1,000 katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Idadi ya ng'ombe aina ya Mpwapwa hadi Mei 2004 imefikia 361 ikilinganishwa na ng'ombe 173 waliokuwepo mwaka 2002/2003. Jumla ya ng'ombe 120 aina ya Mpwapwa wamesambazwa kwa wafugaji katika Wilaya za Mpwapwa, Singida, Manyoni, Ngorongoro na Monduli kwa lengo la kuwafanyia tathmini kwa kushirikiana na wafugaji. Jumla ya ndama chotara 350 wamezalishwa katika mwaka 2002/2003 na 2003/2004. Mahitaji ya madume ya Mpwapwa yameongezeka kutoka 89 na kufikia 276 baada ya kuanzishwa kwa mpango huu.

Kati ya mwaka 2001/2002 na 2003/2004, utafiti shirikishi wa mbuzi bora aina ya *Blended Goat* uliendelea katika Taasisi ya Mpwapwa kwa kusambaza mbuzi 600 Mkoani

Dodoma na Singida. Hadi sasa mbuzi hao wameongezeka na kufikia 1,826. Mpango wa usambazaji mbuzi vijijini umefanyika kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la *Dodoma Micro Projects Programme- DMPP),* ambalo lilitoa Shilingi milioni 37 za kununulia mbuzi na kufundisha wafugaji. Aidha, tathmini itaendelea kufanyika kwa mbuzi aina ya *Boer* toka Afrika ya Kusini pamoja na chotara ya wale wa asili katika mazingira ya mfugaji wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Utafiti wa Mifugo Tanga kiliendelea kufanya tathmini ya uwezo wa mifugo bora wa ng'ombe chotara *($F_1$-Bull),* majogoo chotara na mbuzi bora waliopelekwa katika Vijiji vya Wilaya za Bagamoyo na Handeni. Katika mwaka 2004/2005, tafiti za ng'ombe aina ya Mpwapwa pamoja na mbuzi aina ya mchanganyiko *(Blended)* na kuku zitaendelea kwa kushirikiana na wafugaji vijijini. Hii ni pamoja na kusambaza madume bora ya mbuzi na kutoa ushauri kwa wafugaji kwa kushirikiana na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, kazi za utafiti, uchunguzi na utambuzi wa magonjwa ya mifugo ziliendelea katika Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Mifugo *(ADRI - Temeke).* Utafiti ulihusu magonjwa yanayoathiri mifugo yakiwemo yale yanayoenezwa na kupe, Homa ya Mapafu na Homa ya Matumbo ya Kuku *(Fowl Typhoid).* Uchunguzi wa magonjwa yanayosambaa kwa mlipuko pia uliendelea. Magonjwa hayo ni pamoja na Sotoka, Mdondo, Homa ya Nguruwe na Ugonjwa wa Miguu na Midomo. Ushauri juu ya udhibiti wa magonjwa hayo ulitolewa kwa wadau mbalimbali.

Wizara yangu inafanya majaribio ya uzalishaji wa chanjo za kuzuia ugonjwa wa Kimeta, Chambavu na Mdondo. Utafiti juu ya chanjo ya ugonjwa wa Kutupa Mimba na Ndui ya Kuku unaendelea. Katika mwaka 2003/2004, *ADRI Temeke* ilitengeneza jumla ya dozi milioni 5.1 za chanjo ya mdondo wa kuku na kusambazwa katika Mikoa yote. Dozi 256,000 za chanjo ya Kimeta na nyingine 245,000 za Chambavu zilitengenezwa na kusambazwa kwa majaribio. Aidha, ukarabati wa maabara ya kutengenezea chanjo ya mdondo umekamilika. Katika mwaka 2004/2005, utengenezaji wa chanjo hizi utaendelea pamoja na kukiimarisha kitengo cha chanjo ili kukiwezesha kuendelea na utafiti wa chanjo mbalimbali za magonjwa ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Utafiti wa Ndorobo na *Malale Tsetse and Trypanosomiasis Research Institute (TTRI)* - Tanga imeendelea na Utafiti wa kutokomeza mbung'o kwa kutumia teknolojia ya kuhasi madume ya mbung'o kwa kutumia mionzi *(Sterile Insect Technique - SIT).* Katika mwaka 2003/2004, Taasisi iliendelea na upembuzi wa awali kuhusu maeneo yenye mbung'o ya Kondoa, Simanjiro, Same na Tanga kwa kuainisha aina mbalimbali za mbung'o ili kuangamiza mbung'o hao. Aidha, kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki *(International Atomic Energy Agency),* Taasisi iliendelea na ukarabati na ununuzi wa vifaa vya maabara ambavyo vitaiwezesha Taasisi kufuga mbung'o waliohasiwa wa kupeleka Ethiopia na Botswana. Katika mwaka 2004/2005, utafiti kuhusu njia mbalimbali za kufuga na kulisha mbung'o utaendelea. Aidha, Taasisi hii itaendelea kuimarishwa zaidi ili iweze kutoa huduma nzuri ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kuimarisha miundombinu ya vituo vya utafiti wa mifugo kwa kukarabati ofisi, maabara, nyumba za watumishi na mashamba ya mifugo. Aidha, kazi ya kumalizia ujenzi wa maabara kwa ajili ya Utafiti wa Ugonjwa wa Miguu na Midomo umeendelea na umefikia asilimia 85. Ukarabati wa Vituo na Taasisi za Utafiti wa Mifugo utaendelea katika mwaka wa 2004/2005, ili kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Benjamin William Mkapa alipokuwa anafungua rasmi Bunge hili tarehe 20 Novemba, 2000, alisema yafuatayo na ninanukuu: "Mkakati wa kuwawezesha kiuchumi ni njia tuliyoibuni kuwafanya Watanzania walio wengi nao waweze kumiliki na kuendesha uchumi katika nchi yao. Dhana kuu hapa ni uwezeshaji, yaani kuunda mazingira muafaka yatakayowapatia fursa za kumiliki ardhi, viwanda na zana za kazi, kupata mitaji na kuwekeza katika shughuli za kiuchumi, na kupata elimu na maarifa ya kuendesha biashara na miradi ya kiuchumi".

Mheshimiwa Rais alisisitiza kwamba: "Watanzania (Waafrika), hawana uwezo wala mitaji na uzoefu. Lakini kama tunataka kujenga uchumi wa nchi ambao ni endelevu kundi hili ambao ndio wengi halina budi litafutiwa njia za kuwashirikisha katika ujenzi wa uchumi wa nchi yao".

Katika kutekeleza maagizo haya ya Rais, katika Sekta ya Mifugo tunafanya yafuatayo: -

- Ranchi za Mkata, Mzeri na Dakawa zimekwisha kutangazwa na wawekezaji wa Kitanzania wanaofaa tayari wamepatikana. Jumla ya ranchi ndogo 11 katika ranchi ya Mkata na tisa katika ranchi ya Mzeri zimepatikana.

- Ranchi za Kalambo na Usangu zimekwishapimwa na kutangazwa. Jumla ya ranchi ndogo ndogo 29 zimepatikana katika ranchi hizo.

- Ranchi za Kitengule, Kikulula Complex na Misenyi zote zilizopo Mkoani Kagera zimepimwa na zitatangazwa mwezi huu wa Julai, 2004.

- Ranchi za Uvinza na West Kilimanjaro zitapimwa na kutangazwa kabla ya mwezi Oktoba, 2004.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wamiliki wapya wa ranchi hizo kufuga kibiashara na kisasa, majadiliano yanaendelea na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika *(BADEA),* chini ya Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri wa Fedha, kwa lengo la kuwapatia wafugaji hao mikopo kwa masharti nafuu ili waweze kufuga kibiashara na kisasa. Inakadiriwa kuwa kiasi cha Shilingi bilioni 2.4 zitahitajika. *(Makofi)*

Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu iliendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM, kwa kushirikiana na Wizara ya Ushirika na Masoko kwa kuwahamasisha wafugaji na wadau wengine wa Sekta ya Mifugo kuunda vikundi ili kuwa na nguvu ya

pamoja katika kutatua matatizo ya ufugaji na utafutaji wa masoko. Jumla ya vikundi 231 vya wafugaji vimeanzishwa ikilinganishwa na vikundi 193 vilivyoanzishwa mwaka 2002/2003. Kati ya hivyo, vikundi 41 vimesajiliwa na vinahusika na uendeshaji wa majosho, uuzaji wa mifugo, usimamizi wa malambo, ufugaji wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa. Madhumuni ya kuanzisha vikundi hivyo ni kuviwezesha kusimamia na kuendesha Vyama vya Ushirika na Bodi za Mazao yatokanayo na mifugo kwa manufaa yao. Katika mwaka 2004/2005, Wizara itaendelea kuhamasisha uundaji wa vikundi na vyama vya wafugaji pamoja na kusimamia uundaji na uimarishaji wa Bodi mbalimbali za mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inasimamia Chuo cha Maji cha Rwegarulila ambacho kinatoa mafunzo katika fani za ufundi mchundo na sadifu ambazo zinahitajika katika Sekta ya Maji nchini. Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu iliendelea kutoa mafunzo katika fani hizo ambapo wanafunzi 36 walihitimu katika fani za ufundi mchundo na 160 katika ufundi sadifu. Katika jitihada za kuboresha mafunzo katika fani hizo kulingana na mahitaji ya soko la ajira, hatua ya kwanza ya kufanya mapitio ya mtaala wa mafundi mchundo imefanyika. Aidha, chuo kimeanza utaratibu mpya wa kupeleka mafunzo kwa walengwa wa Sekta ya Maji katika Halmashauri za Wilaya. Pia, sehemu ya kwanza ya kazi za ukarabati wa mabweni ya wanafunzi na karakana za mafunzo ilikamilishwa.

Katika mwaka 2004/2005, Chuo kitaendelea na utoaji wa mafunzo kwa Mafundi Mchundo na Mafundi Sadifu wa Sekta ya Maji na kitaandaa mpango mkakati utakaokipa mwelekeo mpya wa kutoa mafunzo kulingana na mabadiliko ya Sera ya Maji. Kazi ya ukarabati wa miundombinu ya chuo itaendelea.

Aidha, hatua ya pili ni kupitia mtaala wa mafunzo, ikiwa ni pamoja na kutathmini mahitaji ya mafunzo na raslimali zitakazohitajika kuanzisha Stashahada ya Usimamizi wa Raslimali za Maji *(Diploma in Water Resources Management).* Serikali imetenga Shilingi milioni 559.2 kwa ajili ya kuimarisha miundombinu na uendeshaji wa chuo hicho.

Meshimiwa Spika, Wizara yangu inaendesha vyuo vitano vya mafunzo ya mifugo vya Morogoro, Mpwapwa, Tengeru (Arusha), Buhuri (Tanga) na Madaba (Songea). Madhumuni ya kutoa mafunzo ya mifugo ni kupata wataalamu wenye ujuzi na mbinu za kuwawezesha kuhudumia wafugaji kwa ufanisi zaidi. Pia, kutoa mafunzo kwa wafugaji kwa lengo la kuwapa mbinu bora za ufugaji. Ili kufikia azma hii, Wizara yangu katika mwaka 2003/2004 ilifanya ukarabati wa vyuo hivyo na kuvipatia vitendea kazi muhimu kwa gharama ya Shilingi milioni 125. Kutokana na kuboreshwa kwa mazingira katika vyuo hivyo na kurejeshwa kwa utaratibu wa Serikali wa kufadhili watumishi, idadi ya wanachuo imeongezeka kutoka 629 mwaka 2002/2003 hadi 719 mwaka 2003/2004 ikiwa ni asilimia 73 ya uwezo wa vyuo hivyo. Idadi ya wanachuo wanaochangia gharama za mafunzo yao kutoka ndani na nje ya nchi imeongezeka kutoka 210 mwaka 2002/2003 hadi 496 mwaka 2003/2004. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya wanachuo 315 walihitimu mafunzo, kati yao 221 ni wa stashahada na 94 ni wa astashahada.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Asasi mbalimbali iliweza kutoa mafunzo ya muda mfupi ya rejea kwa wataalamu waliopo na mafunzo kwa wafugaji. Katika mwaka 2003/2004, wafugaji 1,434 walipatiwa mafunzo ikilinganishwa na 1,557 katika mwaka 2002/2003. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni kupitia mitaala ya Stashahada ya Uzalishaji wa Mifugo *(Diploma in Animal Production)* ili kuboresha mafunzo kulingana na mabadiliko ya sera na mahitaji ya soko la wataalam.

Aidha, ili kudhibiti ubora wa mafunzo kulingana na viwango vinavyotakiwa, Wizara yangu inafanya ukaguzi wa kitaaluma kwenye vyuo na kutunga mitihani ya pamoja kwa mwaka wa mwisho kwa vyuo vyote vinavyofundisha kozi za muda mrefu za Astashahada na Stashahada.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itaendelea kuboresha na kuimarisha mazingira katika vyuo vya mifugo na kugharamia wanafunzi 229, kati yao wanafunzi 130 watasajiliwa kwa mwaka wa kwanza na 99 ni wa mwaka wa pili. Vile vile, kwa kushirikiana na asasi mbalimbali wafugaji 1,500 watapewa mafunzo. Pia, Wizara itafanya tathmini ya mafunzo yanayotolewa kwa wafugaji ili kubaini jinsi mafunzo hayo yanavyowanufaisha. Aidha, Wizara itaanzisha Stashahada ya Ufundi Sanifu Maabara ya Mifugo *(Diploma in Veterinary Laboratory Technology)* na kuandaa moduli za kozi za ufugaji bora wa nguruwe, mbuzi wa maziwa na kuku na pia, kuchapisha kitabu cha uzalishaji wa mifugo na uhamilishaji.

Wizara yangu ina jumla ya watumishi 3,605 ambapo kati yao watumishi 1,793 ni wa Sekta ya Maji na 1,812 ni wa Sekta ya Mifugo. Katika mwaka 2003/2004 jumla ya watumishi 1,795 walipandishwa vyeo, 97 waliajiriwa na watumishi 186 walipata mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi kwa kuzingatia mahitaji ya kazi zao. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu imepanga kuwapandisha vyeo watumishi 1,200 na watumishi 110 watapatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Aidha, Wizara yangu itawathibitisha kazini na kuwabadilisha vyeo *(recategorization)* baadhi ya watumishi kulingana na miundo yao ya utumishi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu imeendelea kuziba mianya ya rushwa katika Sekta za Maji na Mifugo sambamba na kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kuzuia Rushwa. Katika kutekeleza Mkakati huu, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Kitengo cha Utawala Bora pamoja na Taasisi ya Kuzuia Rushwa, imetoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi kwa njia ya semina kwa lengo la kuwaelimisha madhara ya kujihusisha na vitendo vya rushwa. Katika mwaka 2004/2005, Wizara itaendelea kuziba mianya ya rushwa na kuboresha huduma kwa wateja ili kufikia malengo yaliyoainishwa katika Mkakati wa Kitaifa wa Kuzuia Rushwa na Mpango wa utekelezaji kisekta. Aidha, Wizara yangu itaendelea kusimamia kikamilifu Sheria ya Ununuzi Na. 3 ya Mwaka 2001, ambayo kwa kiasi kikubwa inapunguza mianya ya rushwa katika manunuzi ya vifaa na huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu iliendelea na uhamasishaji wa watumishi kuhusu mbinu za kujikinga na ugonjwa hatari wa UKIMWI.

Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu imetenga jumla ya Shilingi milioni 132 kwa ajili ya kuendelea na juhudi za kuelimisha watumishi juu ya umuhimu wa kuzuia maambukizi mapya ya ugonjwa wa UKIMWI. Pamoja na mambo mengine yafuatayo yanategemewa kufanyika: Kuendeleza semina za uhamasishaji wa watumishi kuhusu namna ya kukwepa maambukizi mapya ya UKIMWI, kutoa mafunzo kwa Kamati ya UKIMWI ya Wizara, kuunda kikundi cha waelimisha rika na kukipa mafunzo ya kazi zao, kununua na kusambaza vifaa vinavyosaidia kujikinga na UKIMWI, kutengeneza na kusambaza vipeperushi na magazeti kuhusu UKIMWI na kuendelea kushirikiana na tume ya Taifa ya kudhibiti UKIMWI kuona kuwa ni namna gani waathirika wanaweza kupunguziwa makali ya ugonjwa na kuboresha afya zao.

Mheshimiwa Spika, suala la jinsia ni jambo linalosisitizwa na Wizara yangu katika utekelezaji wa kazi zake za kila siku. Katika mwaka 2003/2004, Wizara imefanya uhamasishaji wa masuala ya jinsia kupitia magazeti, redio na television. Aidha, Wizara yangu ilishiriki kwenye mafunzo, semina na kuanzisha Dawati la Jinsia ambalo litaratibu kwa kina masuala yote ya Jinsia katika Wizara. Katika mwaka 2004/2005 Wizara yangu inatarajia kufanya yafuatayo: Kuimarisha Dawati la Jinsia kwa kulipatia vitendea kazi muhimu, kuendesha semina kwa ajili ya kuhamasisha viongozi na wafanyakazi, kuunda Kamati ya kuratibu masuala jinsia, kutoa miongozo kwa wadau kuhusu kukusanya takwimu na kutengeneza taarifa zenye michanganuo ya kijinsia, kuratibu na kufuatilia masuala yatakayowezesha kuwepo kwa usawa na haki za kijinsia katika Idara mbalimbali na kuhamasisha na kupendekeza mabadiliko katika mfumo wa utawala, uendeshaji na ajira katika Wizara ili kuhakikisha kuwa mfumo huo unazingatia usawa wa jinsia.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii kwa mwaka 2004/2005, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh.124,206,069,100/= kwa ajili ya matumizi ya Wizara yangu kwa kipindi cha mwaka 2004/2005 kama ifuatavyo: -

(i) Fedha za Matumizi ni Sh.19,636,549,900/=, ambapo Sh.5,270,790,000/= ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi *(PE)* na Sh.14,365,759,900/= ni kwa ajili ya matumizi mengine *(OC)*.

(ii) Fedha za Miradi ya Maendeleo Sh.104,569,519,200/=, zinazojumuisha fedha za ndani Sh.31,196,856,000/= na fedha za nje Sh.73,372,663,200/=.

Mheshimiwa Spika, naomba tena kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taaadhima naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Wachangiaji wa mwanzo watakuwa ni hawa wafuatao: Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa Kisyeri Chambiri, wao hawajachangia.

Waliokwishachangia mara moja ni Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Benedict Losurutia na Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, wajiandae. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua makadirio ya Wizara hii atoe taarifa ya Kamati, Mheshimiwa Eliachim Simpasa.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 81(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa na Maoni ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, juu ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa Mwaka wa Fedha uliopita na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa, hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumpongeza Mheshimiwa Danhi B. Makanga, kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine tena kuwa Mbunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki na nampongeza kwamba, safari hii amepitia Chama cha Mapinduzi na nawapongeza Wananchi wote wa Bariadi kwa kutumia haki yao ya Katiba. *(Makofi)*

Aidha, kwa niaba ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, napenda kutoa pole kwa Wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kutokana na kifo cha Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego na pia nachukua nafasi hii kutoa rambirambi za Kamati kwa Wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kwa kumpoteza Mbunge wao, Marehemu Mheshimiwa Theodos Kapisapira hivi karibuni. Mwenyezi Mungu aziweke pema peponi roho za Marehemu wote. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, Wajumbe ambao walichambua hoja ya Kamati hii ni hawa wafuatao naomba niwatambue:-

Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Robert Mashala, Mheshimiwa Paulo Makolo, Mheshimiwa Masoud Salim, Mheshimiwa Ali Salim, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Salama Khamis Islam, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Philip Magani na Mheshimiwa Eliachim Simpasa, ambaye ni Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio na matatizo katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2003/2004. Kamati yangu ilipata maelezo ya kina juu ya majukumu ya Wizara, malengo ya utekelezaji wake kwa mwaka uliopita. Kamati ilifahamishwa kwamba, katika

utekelezaji wa mipango iliyowekwa kwa mwaka wa fedha uliopita, yalipatikana mafanikio mengi ya kuridhisha katika sekta zote mbili, yaani Maji na Mifugo. Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na haya yafuatayo:-

Sekta ya Maji: Ongezeko la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa kiwango fulani kwa wakazi wa vijijini na mijini, kukamilika na kuanza kutekelezwa kwa miradi mbalimbali ya maji na kukamilishwa kwa maandalizi ya kuanzishwa chombo cha huduma cha usimamizi wa matumizi na utunzaji wa rasilimali za maji ya Mto Nile kutoka *Lake Victoria. (Makofi).*

Sekta ya Mifugo: Kuongezeka kwa mauzo ya mifugo nje ya nchi na hivyo kuongeza pato la Taifa na kuanzishwa kwa Mfuko wa Kuendeleza Mifugo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo yaliyopatikana, Kamati yangu pia ilielezwa matatizo yaliyojitokeza ikiwa ni pamoja na tija ndogo katika uzalishaji wa mifugo hasa kwa wafugaji wa sekta ya asili, uhaba wa viwanda vya kusindika mazao yatokanayo na mifugo, pamoja na miundombinu ya kuwezesha kuuzwa bidhaa za mifugo katika soko la Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inatoa pongezi kwa jitihada za Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, katika kufanikisha malengo yake licha ya matatizo waliyokabiliana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusikiliza maelezo hayo, Kamati imetoa ushauri na maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, hali ya vyanzo vya maji nchini ni mbaya. Pamoja na kuwepo kwa Sheria Ndogo ndogo bado ukataji miti unaendelea kwa kasi kubwa kiasi cha kuhatarisha vyanzo hivyo na upatikanaji wa maji kwa ujumla. Kamati inashauri kuwe na ushirikiano wa karibu kati ya Wizara hii na Wizara ya Maliasili na Utalii, kutokana na ukweli kwamba, maji na miti ni vitu vinavyotegemeana. Aidha, kwa kuwa kuwepo kwa sheria ndogondogo kumeonesha kushindwa kuzuia ukataji ovyo wa miti, ni vyema itungwe Sheria kabisa yenye nia ya kuvilinda vyanzo vya maji kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Kamati inashauri kuwe na Mkakati Maalum wa kubainisha vyanzo vyote vya maji vya asili katika Halmashauri kwa kushirikiana na Wizara hii ili kuviendeleza vyanzo hivyo na kurahisisha kupatikana kwa huduma hii ya maji. Pia itawezesha utafiti na utunzaji wa vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kasi ya ongezeko la watu katika maeneo ya miji hasa kama Mji wa Dar es Salaam na miji mingine, haiendani na upatikanaji wa huduma ya maji, kwani pamoja na mambo mengine, mitambo ya maji inayotumiwa kwa mfano, Ruvu bado ni ile ile ya miaka mingi iliyopita. Kamati yangu inashauri ukarabati unaofanywa uhusishe na kuongezwa kwa mitambo mipya ili kuondoa matatizo ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa Wananchi wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado kuna umuhimu wa elimu ya uvunaji wa maji ya mvua kuzidi kutolewa kwa Wananchi hasa katika yale maeneo makame, kwani maeneo hayo hupata mvua kwa wingi wakati wa msimu na baada ya mvua kumalizika maji yanakosekana kabisa. Hivyo, Kamati inasisitiza elimu ya uvunaji maji kwa njia nyepesi izidi kutolewa katika maeneo yote nchini. Uanzishwe mradi maalum kuhusu suala hilo. Kamati inashauri wataalam wawafuate Wananchi katika makao yao na kutoa elimu hiyo, pia zitumike taratibu nyingine kama vile vipindi vya redio na kadhalika kwa ajili hiyo. Pamoja na kutoa elimu ya uvunaji maji kwa njia ya mabati, Kamati inashauri Wizara ianzishe na kusimamia zoezi la kuchimba visima virefu na kujenga mabwawa.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu kwa dhati kabisa, inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Mfuko wa Maji. Tunaamini Mfuko huu ni ukombozi wa matatizo ya maji kwa Wananchi. Kamati inashauri kuwe na utaratibu madhubuti wa utunzaji na ufuatiliaji wa matumizi ya Mfuko ili walengwa wapate faida iliyokusudiwa. Aidha, Kamati inaomba Waheshimiwa Wabunge wote, tushirikiane na wahusika katika maeneo tunakotoka ili Mfuko huu ufanikiwe kama Mfuko wa Barabara ulivyofanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imebaini kuwa mara nyingi mabwawa yanachimbwa katika maeneo yaliyo wazi na kusababisha mabwawa hayo kutokuwa na uwezo wa kuhifadhi maji kwa muda mrefu. Hivyo, Kamati inashauri kuwe na Mkakati wa kupanda miti katika maeneo ya mabwawa ili kutunza mazingira na kusaidia vyanzo vya maji. Hata hivyo, utafiti ufanyike ili miti itakayopandwa iwe ni ile inayosaidia kuhifadhi maji na siyo inayokausha maji.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imeendelea kutoridhishwa na gharama kubwa za kuunganisha maji mijini. Hali hii siyo tu inawanyima Wananchi wengi haki ya kupata maji safi na salama, bali pia inasababisha hasara kwa taasisi husika, kwani baadhi ya watu wasio waaminifu hujiunganishia maji kwa njia zisizo halali kwa kukwepa gharama. Kwa kuwa inaonekana watu wengi wanashindwa kutoa fedha zinazohitajika kwa mkupuo, Kamati inashauri kuwe na utaratibu wa watu kuunganishiwa maji halafu gharama husika zikatwe pole pole kwa kuchanganywa katika ankara zao za maji kila mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa ni nadra sana suala la maji taka kuzungumzwa katika Wiki ya Maji ambayo pamoja na mambo mengine, hutumika kwa kutoa elimu ya matumizi bora ya maji. Aidha, katika baadhi ya maeneo hasa Jijini Dar es Salaam, maji machafu hutiririka ovyo mitaani, sasa linaonekana ni jambo la kawaida. Pia bila kujali uwezekano wa kutokea magonjwa ya milipuko, kuna baadhi ya watu ambao hutumia vipindi vya mvua kufungulia vyoo vyao na kutiririsha maji machafu kuelekeza kwenye mabonde au mito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inashauri Serikali sasa ifuatilie jambo hili badala ya kuziachia Serikali za Mitaa pekee. Itolewe elimu ya kina kuhusu athari za maji machafu kwa afya ya binadamu na mazingira. Wiki ya Maji inaweza pia kutumika katika utoaji elimu hii. Aidha, Wizara iboreshe miundombinu kuhakikisha maji machafu

yanaondolewa katika makazi ya watu ikiwa ni pamoja na kuzibua mifereji iliyopo na magari vilevile ya kubeba maji machafu yaweze kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado Wananchi vijijini wanakabiliwa na matatizo kuhusiana na majosho. Ni ukweli kwamba, Halmashauri zetu zinajitahidi lakini uwezo wao bado ni mdogo hivyo ni vigumu kukabiliana na matatizo yote yanayohitaji ufumbuzi kifedha. Kamati yangu inaishauri Wizara isaidie fedha ili majosho yaliyopo yafufuliwe na kuanzisha mengine mapya. Hii pia itasaidia wafugaji kuogesha mifugo yao, kukabiliana na magonjwa kama vile kupe na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kamati imearifiwa kuwa, Mkakati unaandaliwa wa chanjo dhidi ya ugonjwa wa miguu na midomo kwa kushirikisha nchi Wanachama wa *SADC* na Jumuiya ya Afrika Mashariki, kutokana na ukweli kuwa ugonjwa huu husambaa haraka na hauna mipaka. Kamati inapongeza hatua hii, hata hivyo, tunashauri Mkakati huu uendane na Sheria au Maazimio kwa ajili ya kutilia nguvu na kuondoa uwezekano wa nchi nyingine kuafiki tu lakini bila kuingia kwenye utekelezaji. Aidha, ikiwezekana Mkakati uhusishe na nchi nyingine za Umoja wa Afrika, kwani iwapo Tanzania na Kenya zikipata chanjo hiyo na Ethiopia isiwemo, itakuwa ni kazi bure.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imearifiwa kuwa katika kuwawezesha wafugaji na wataalam wenye taaluma ya mifugo kuendesha shughuli za mifugo kibiashara, Wizara imeanza kupima maeneo ya Ranchi za Taifa na kuwapatia ili waziendeshe. Kamati inashauri Wizara isigawe tu Ranchi hizo na kuziachia bali iwapatie mwongozo na utaalam zaidi wa namna ya kuziendesha na kuziendeleza, kwa mfano, masuala ya malisho, uzalishaji. Pia wapewe mikopo ya kuwasadia kuziendesha kibiashara kwani bila hivyo ranchi hizi zinaweza kufa kabisa na hivyo kuua nia na malengo mema ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msukumo zaidi unahitajika katika kuendeleza malambo. Kwa kuwa Mpango wa MMEM unaonesha mafanikio makubwa katika sekta ya elimu, Kamati inashauri Wizara ibuni mbinu zitakazosaidia masuala kama haya na hasa kwa huduma za maji mijini na vijijini, yaani uzoefu wa Wizara ya Elimu kuhusu MMEM ndiyo utumike.

Mheshimiwa Spika, tumearifiwa kuwa mojawapo ya hatua zilizochukuliwa na Wizara katika kuboresha sekta ya mifugo nchini ni kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo, kutokana na ushuru wa asilimia 20 wa ngozi ghafi zinazouzwa nje na kwamba hadi kufikia Mei, 2004 zaidi ya shilingi milioni 500 zimekusanywa.

Kamati yangu inaamini tunao uwezo wa kuongeza Pato la Taifa kupitia uuzaji wa ngozi nje ya nchi. Hii itawezekana kama wataalam wa ngozi wataongezeka kwa kuboresha vyuo husika ili wawasaidie wafugaji katika utayarishaji na usindikizaji wa ngozi. Aidha, Kamati inashauri viwanda vya ngozi vifufuliwe.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa suala la uboreshaji wa afya ya mifugo kwa kiasi kikubwa linakwamishwa na gharama kubwa ya madawa ya mifugo na huduma

za wataalam. Sio jambo la ajabu kukuta mfugaji anatakiwa kugharamia usafiri wa kumpeleka mtaalam wa mifugo ili akatoe huduma, pia baada ya kupata ushauri inambidi mfugaji huyo atoe fedha nyingine nyingi kwa ajili ya madawa, hali hii inawakatisha tamaa wafugaji. Katika kukabiliana na hali hii, Kamati inashauri wataalam wa mifugo waendelee kusomeshwa kwa wingi na ushuru wa dawa za mifugo uondolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa kichaa cha mbwa umeenea kwa kasi hasa katika Mikoa ya Magharibi na sasa umeathiri hata binadamu hasa watoto. Kamati inashauri Wizara ichukue hatua madhubuti ili kukabiliana na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kupima maeneo ili kutenga yale ya Kilimo na Ufugaji, Kamati inaamini kuwa pamoja na tatizo la wataalam pia kuna tatizo kubwa la wahusika wenyewe, yaani wakulima na wafugaji kukubaliana. Hata hivyo, suala hili limewahi kufanikiwa Mkoani Rukwa kwa kupitia Azimio la Mto Wisa. Kamati inashauri njia zilizotumika kuwezesha kufanikiwa kwa azimio hili pia zitumike katika Wizara hii kuhusu wakulima Wakulima na Wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa kwamba, katika baadhi ya maeneo nchini Wafugaji walipoteza ng'ombe wao ambao walikufa baada ya kuchomwa sindano za chanjo, jambo linalofanya baadhi yao wafikiri kuwa chanjo hiyo ni mpango wa Serikali wa kupunguza mifugo yao.

Kamati inashauri Wizara, ifanye utafiti kuhusu jambo hili na kupitia wataalam wa mifugo, watoe elimu kwa wafugaji kabla ya zoezi la chanjo yoyote, hasa kuhusu matatizo yanayoweza kujitokeza baada ya chanjo na namna ya kukabiliana nayo. Aidha, jambo kama hili linapotokea kwa uzembe wa wataalam, Wananchi walioathirika walipwe fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa, Wizara imetenga fedha kwa ajili ya masuala ya UKIMWI. Hata hivyo, tunashauri kuwa badala ya fedha hizo kutumika kwa semina, warsha na mafunzo tu, basi utafutwe utaratibu wa kuwasaidia moja kwa moja watumishi wa Wizara hii ambao wameathirika kwa Ugonjwa wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kilimo na Ardhi, inawapongeza sana Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Antony Diallo na wasaidizi wao wote, kwa jitihada zao katika kusimamia vizuri masuala ya maji na mifugo. *(Makofi)*

Aidha, Kamati inatambua juhudi zilizofanywa na Wizara hii kwa kushirikiana na Serikali ya Watu wa China katika ujenzi wa mitambo ya maji kwenye Mto Wami, ili kuwapatia Wananchi wa Chalinze maji ya kuaminika. Kamati inaishukuru sana Serikali ya Watu wa China kwa msaada huo mkubwa kwa Wananchi. Tunatoa pia shukrani kwa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa kuzinduzi rasmi wa mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imetambua juhudi kubwa zinazofanywa na Wizara kuhusu mipango mizuri ya mradi mkubwa wa matumizi ya Ziwa Victoria kwa

Mkoa wa Shinyanga na Wilaya ya Kahama. Aidha, Kamati inampongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuwashirikisha Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Waheshimiwa Wabunge tisa, katika ziara yake ya hivi karibuni nchini Misri ili kubadilishana uzoefu na kujenga mahusiano mema kati ya Tanzania na nchi hiyo katika matumizi mazuri ya maji ya Mto Nile katika Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Kamati pia inapongeza juhudi zilizofanywa na Wizara kujenga Chuo cha Mafunzo ya Machinjio ya mifugo na kujenga vilevile machinjio yenyewe nje kidogo ya Mji wa Dodoma mahali panaitwa Kizota. Hizi zote ni jitihada ambazo kamati inazitambua kwamba, Mheshimiwa Edward Lowassa amejitahidi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati yangu, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu, Dr. Vincent Mrisho na watalaam wengine, kwa jinsi walivyoweza kufafanua hoja mbalimbali zilizotolewa na Wajumbe wakati Kamati yangu ilipokuwa inachambua Bajeti hii. *(Makofi)*

Pia nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati yangu na Makamu Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, katika kazi njema ya kunisaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, napenda kuishukuru Ofisi yako hususan Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka Msemembo Mussa na wasaidizi wake hasa Makatibu wa Kamati, hasa Bi. Nenelwa Mwihambi na Ndugu Hancha Abdallah, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi kufikia kutoa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kilichoombwa na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ni Sh.124,206,069,100/= zikiwa ni Sh. 19,636,549,900/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh.104,569,519,200/= kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, napenda kutamka kwamba, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vilivyomo ndani yake, kwa kutupa uhai na afya njema tukaweza kukutana hii leo ndani ya jengo hili kutekeleza wajibu wetu tukiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maoni, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5)(b)(c), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuungana na wenzangu ili kwa kauli yangu na kwa niaba ya Wapiga kura wa Jimbo langu la Utaani, kutoa rambirambi zetu za dhati

kabisa kwa Wananchi na familia za Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini na Marehemu Mheshimiwa Theodos James Kasapila, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, kwa msiba mkubwa wa kuondokewa na wenzetu hawa. Mwenyezi Mungu, aweke roho zao za Marehemu hawa mahali panapostahili. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, sasa nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Naibu Waziri Mheshimiwa Anthony M. Diallo Mbunge, pia Katibu Mkuu wa Wizara hii, pamoja na timu yake ya wataalam, kwa kuandaa na kuwasilisha bajeti hii ambayo kwa namna moja au nyingine, inaeleza bayana namna watakavyotekeleza majukumu yao waliyopangiwa ili kuwaondolea kero Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie utangulizi wangu kwa kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi pamoja na Wajumbe wake wote, kwa namna ambavyo wameandaa na kuwasilisha mapendekezo ambayo zaidi yamelenga katika kuboresha hotuba ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kuchangia mambo muhimu yafuatayo katika bajeti ya mwaka huu kwa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na kwa kuwa Wizara hii ina sekta kuu mbili ambazo ni Sekta ya Maji na Sekta ya Maendeleo ya Mifugo, basi Kambi ya Upinzani inatoa mchango wake kwa kila sekta kipekee:-
.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maji ni sekta muhimu sana kwa maisha ya viumbe. Mwenyezi Mungu, amekuwa anawaruzuku waja wake riziki hii ya maji ili kuendeleza mfumo wao wa maisha. Kwa hiyo, ni wajibu wa Wizara hii kuhakikisha kwamba, wakati wote maji safi na salama yanapatikana kwa matumizi ya binadamu. Hatua hii ichukuliwe hasa ikitiliwa maanani kwamba, sehemu nyingi za Tanzania hukumbwa na upungufu mkubwa wa maji kwa kipindi kirefu. Aidha, wakati mwigine upungufu huo hujitokeza hata wakati wa kipindi cha mvua za masika ama za vuli.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya maji huongezeka sambamba na ongezeko la idadi ya watu na shughuli za uzalishaji viwandani na kilimo. Pamoja na kwamba Tanzania ina rasilimali kubwa ya maji, mito, maziwa na bahari, hata hivyo, usimamizi madhubuti wa rasilimali hizo ni muhimu katika kuondoa umaskini, kuboresha afya za jamii na kuhakikisha usalama wa chakula, maendeleo ya kiuchumi na uendelevu na mazingira. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuandaa sera nzuri na kuona kuwa hatua madhubuti zinachukuliwa kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wengi wanaathirika na matatizo ama ya wingi au uhaba wa maji. Ukweli ni kwamba, maji ya mvua yanayopatikana kila mwaka ni mengi, hata sehemu zinazoitwa za ukame kama vile Dodoma, Handeni na nyenginezo. Tatizo ni kwamba, maji ya mvua yanapatikana kwa kipindi kifupi sana.

Mheshimiwa Spika, bila kutumia mbinu ya kuyahifadhi maji hayo hupotea kwa haraka sana ambapo hayawezi kutumika tena. Hivyo basi, hata kama tutapata mvua nyingi, iwapo maji yake hayatahifadhiwa tutaendelea kuwa na upungufu wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapata faraja kuona kuwa hatua zimeanza kuchukuliwa katika kujaribu kuboresha hifadhi na matumizi ya maji ya mvua. Kambi ya Upinzani, inachukua nafasi hii kuwapongeza Wataalamu wa Chuo Kikuu cha Sokoine, kwa kuanzisha Mpango wa Utafiti juu ya hifadhi na matumizi bora ya maji ardhini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya mpango huu ni kubuni, kufanya majaribio na kusambaza mbinu za kuboresha uhifadhi na matumizi ya maji ya mvua. Kufanikiwa kwa mpango huu, utakua ni ukombozi mkubwa kwa Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa kushirikiana na asasi nyingine, kuhakikisha mpango huo unaendelezwa na unapatiwa fedha na nyenzo za kutosha ili baadae mbinu zilizobuniwa ziweze kusambazwa kwa wadau wote. Mpango usiishie kwenye makaratasi tu kama yalivyo mazoea ya mipango mingi ya Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na maji ya mvua, nchi yetu ina utajiri mkubwa wa mito na maziwa. Hazina hii hutumika katika shughuli mbalimbali za maendeleo kama vile kilimo cha umwagiliaji, uzalishaji nishati ya umeme, uvuvi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tarehe 17 Aprili, 2004 Waheshimiwa Wabunge, tulifanyiwa semina kuhusu matumizi ya maji katika nchi zilizo kwenye Bonde la Mto Nile. Tulielezwa kwamba, kwa muda mrefu sasa kumekuwa na utumiaji wa rasilimali hii katika nchi zilizomo katika bonde hili kwa njia isiyo ya haki na usawa.

Mheshimiwa Spika, nchi hizo sasa zimeona umuhimu wa kukaa pamoja kujadili namna ambayo wataweza kutumia rasilimali hiyo kwa njia ya haki na usawa kwa manufaa ya wakazi wa nchi hizo. Kambi ya Upinzani, inaona sasa ni wakati muafaka pia kutumia ipasavyo maziwa na mito mingine iliyomo Tanzania ili kupanua kilimo cha umwagiliaji kwa manufaa ya Wananchi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwanzoni mwa mwezi wa Juni, 2004, ujumbe wa Tanzania ukiongozwa na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, akifuatana na Waheshimiwa Wabunge tisa na waandishi wa habari, walitembelea nchi ya Misri. Madhumuni ya ziara hiyo, pamoja na kukuza mahusiano ya nchi mbili hizi, bali pia ilikuwa ni kujifunza namna Wananchi wa Misri wanavyotumia maji kwa ajili ya kukuza kilimo cha umwagiliaji. Tunaipongeza Wizara kwa hatua hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujumbe huu umejifunza mengi, lakini kubwa kuliko yote ni vile namna ambavyo maji yanaweza kutumika kuleta maendeleo makubwa kwa Wananchi. Ujumbe huu uliwajibika baada ya kurejea nyumbani kuielimisha jamii ya

Watanzania, umuhimu wa matumizi ya rasilimali ya maji ambayo Tanzania tumejaaliwa nayo kuleta mapinduzi ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Serikali iliwashirikisha kwa kiasi kikubwa, Waandishi wa Habari katika ziara hiyo. Kama ambavyo waliifanya kazi nzuri ya kutolea taarifa ya ziara hiyo hata kabla ya ujumbe kurejea nchini, ni vyema kuendelea na juhudi hizo za kuelimisha jamii juu ya suala la matumizi bora ya maji katika kujiletea maendeleo. Nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kabisa, waandishi wa habari walioshiriki katika msafara huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kimekuwa ni kilio kikubwa kinachoelezwa na Waheshimiwa Wabunge kwamba, kilimo cha umwagiliaji kipewe umuhimu wake unaostahili ikiwa kweli tunataka kuiondoa nchi hii katika balaa la njaa na kuwaletea Wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji, fedha kwa ajili ya kukuza miundombinu ya umwagiliaji na kukarabati *scheme* za maji vijijini ni ndogo sana. Iwapo Serikali haitawekeza ipasavyo katika kukuza miundombinu ya Umwagiliaji, kilio hicho kitakuwa ni nyimbo ya mwaka hadi mwaka. Ni aibu kubwa kwa nchi kama Tanzania yenye vyanzo vya maji chungu nzima kukumbwa na njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni utamaduni uliozoeleka wakati Wizara zinapoandaa makisio yao katika bajeti za mwaka Serikali huziwekea kikomo cha makadirio *(ceiling).* Utaratibu huu hurudisha nyuma juhudi za baadhi ya Wizara kutokana na uzito wa majukumu yao ukilinganisha na fedha walizopangiwa. Kutokana na sababu hiyo na kwa kuzingatia umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwasilisha Bungeni Muswada wa kuomba bajeti ya ziada kila utakapotokea umuhimu kwa ajili ya kukuza na kusambaza miundombinu ya umwagiliaji, kadhalika na kukarabati *scheme* za umwagiliaji vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutakumbuka kwamba, katika Ziwa Victoria kulizuka gugu maji ambalo lilikuwa linatishia uhai na matumizi ya ziwa hilo. Pamoja na kwamba, juhudi za pamoja za nchi zinazopakana na ziwa hilo zilichukuliwa kuliangamiza gugu hilo, hali inaonekana kuwa inajirudia hasa baada ya juhudi hizo kusita kwa muda mrefu. Kambi ya Upinzani inaitahadharisha Wizara kwamba, iwapo hatua madhubuti na za ziada hazikuchukuliwa kuliangamiza gugu hilo, matumizi endelevu ya Ziwa Victoria yatakuwa ni ndoto.

Mheshimiwa Spika, hali halisi ya maji nchini na matatizo yaliyopo si ya kumalizwa kwa msimu mmoja au miwili ya bajeti, tatizo hili linaendana na upanukaji wa miji yetu ambayo inachangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko la haraka la watu, hii inasababisha miundombinu ambayo iliwekwa wakati wa enzi za kikoloni kushindwa kuhimili ongezeko hilo la watu na matumizi ya maji kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sekta ya maji katika maendeleo ya nchi yetu ndicho kitu kikubwa na chenye umuhimu wa aina yake, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliangalia upya suala la miundombinu ya maji safi na maji taka ili kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha ili iende sambamba na mahitaji yanayotokana na ongezeko la idadi ya watu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaona bado kuna mapungufu kwenye utoaji wa elimu kwa watumishi wa Serikali na Wananchi kwa ujumla, kuhusu utunzaji na uendelezaji miundombinu ya maji ambayo imewekwa na Serikali au wafadhili kupitia vikundi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tulisikia kwamba, kule Wilayani Karatu, Mkoa wa Arusha, kumefanyika uharibifu mkubwa na wa makusudi wa miundombinu ya maji, Serikali inaombwa kuchukua hatua za makusudi kukomesha vitendo hivyo kwa kuielimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuhifadhi, sio tu vyanzo vya maji, lakini na miundombinu ya kusambaza maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maendeleo ya Mifugo ina idara tatu, Idara ya Uzalishaji Mifugo, Huduma za Afya ya Mifugo, Utafiti na Mafunzo. Kwa ujumla sekta hii ni muhimu sana hapa nchini na hasa ukizingatia kuwa asilimia 40 ya kaya za wakulima ni wafugaji.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina ng'ombe milioni 17.7, mbuzi milioni 12.5, kondoo milioni 3.5, nguruwe 880,000 na kuku milioni 47. Lakini pamoja na wingi wa mifugo yetu, bado takwimu zinaonesha kuwa ulaji wa nyama, maziwa na mayai, kwa Mtanzania uko chini ukilinganisha na viwango vya nchi nyingine ulimwenguni, jambo ambalo linafanya soko la mifugo nchini kudidimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila Mtanzania kwa wastani hula kilo tisa za nyama kwa mwaka ukilinganisha na wastani wa viwango vya kilo 50 kwa mwaka katika nchi nyingine ulimwenguni. Aidha, kwa wastani Mtanzania hula mayai 27 na maziwa lita 35 kwa mwaka, wakati nchi nyengine hula mayai 160 na maziwa lita 200 kwa mwaka. Viwango vinavyopendekezwa na *FAO* kwa afya ya mwanadamu ni kilo 50 za nyama, lita 200 za maziwa na mayai 300 kwa mwaka. Hali hii inavunja moyo pamoja na umaskini tunaojua kwamba umekithiri, lakini ni lazima Serikali ifanye utafiti wa kutosha kujua sababu zinazopelekea Mtanzania kutumia mazao ya mifugo kwa kiwango kidogo sana ili hatua madhubuti zichukuliwe kuondoa tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, karibu asilimia 90 ya ng'ombe, mbuzi na kondoo, wanachungwa kienyeji na kwa bahati mbaya hapa nchini mwetu hatujatenga maeneo ya kutosha maalum kwa ajili ya kuchungia, matokeo yake wakati mwingine hutokea migogoro mikubwa baina ya wakulima na wafugaji. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliangalia kwa makini suala hili na kulipatia ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, *The Winroch International* katika utafiti wao wamegundua kwamba, Sekta ya Mifugo katika nchi zilizo chini ya jangwa la Sahara inakua kwa

wastani wa asilimia 2.2 kwa mwaka. Bali ongezeko la watu linakuwa kwa asilimia 2.8 kwa mwaka. Sasa ili kuhakikisha ongezeko la upatikanaji wa mahitaji ya mwanadamu, hakuna budi Sekta ya Mifugo ni lazima ikue kwa asilimia 4.0 kwa mwaka. Kambi ya Upinzani inaona kuwa hii ni changamoto kwa Serikali kuandaa mikakati madhubuti na inayotekelezeka ili kuikuza Sekta hii ya Mifugo kukidhi mahitaji ya ongezeko la watu nchini. Hatuna budi tukiri kwamba, baadhi ya hatua zimeanza kuchukuliwa na Wizara, ila Kambi ya Upinzani tunaona ipo haja ya kuongeza kasi ili lengo lililokusudiwa lifikiwe kwa muda mfupi. Mipango yetu isiwe ya kuwa mbioni wakati wote.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ng'ombe wa maziwa, dalili zimeonekana kuongezeka kwa uzalishaji katika miaka ya hivi karibuni. Wizara imekuwa inachukua juhudi ya kuzalisha mitamba ya maziwa kwa ajili ya kuisambaza kwa wafugaji. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara inayo mashamba sita ya kuzalisha mitamba. Mashamba hayo ni *Sao Hill,* Mabuki, Kibaha, Nangaramo, Ngerengere na Kitulo.

Mheshimiwa Spika, kikwazo kikubwa kilichojitokeza ni bei ya mitamba hiyo ambayo ni kubwa ukilinganisha na uwezo mdogo wa wakulima walio wengi. Tunaiomba Serikali kuzingatia upya bei hizo za mitamba ili kupanga bei itakayomwezesha mfugaji kuimudu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hiyo, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuweka msukumo katika ile mipango inayoelekezwa kwa Wananchi maskini kukuza shughuli za uzalishaji maziwa. Miongoni mwa mipango hiyo ni ule wa *Heifer-in-Trust,* ambao umechangia kwa kiasi kikubwa, kuongeza idadi ya ng'ombe wa maziwa nchini.

Mheshimiwa Spika, ufugaji wa mbuzi nao huchangia katika uzalishaji wa nyama na maziwa. Hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la mahitaji ya mbuzi wa maziwa. Ili kukidhi haja hiyo, miradi kadhaa imeanzishwa katika sehemu mbalimbali, kama ule wa Mgeta *(Mgeta Dairy Goat Project)* na *Farm Africa Dairy Goat Project* huko Babati. Ufugaji wa mbuzi wa maziwa ni ukombozi kwa Wananchi ambao hawana ardhi ya kutosha na wenye mtaji mdogo ukilinganisha na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, kwani mbuzi wa maziwa humpatia mfugaji maziwa, nyama, mbolea, manyoya na ngozi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya utafiti wa kutosha ili kufungua maeneo zaidi ya kusambaza mitamba ya mbuzi wa maziwa na kwa sababu ufugaji huu kwa baadhi ya sehemu ni mgeni, huduma ya ugani itangulizwe kabla ili kuhakikisha kwamba, taaluma ya kutosha inatolewa kabla ya kusambaza mitamba hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ufugaji kuku, inaonyesha kwamba, wakulima wanao uzoefu wa kiasi fulani, kwa sababu karibu kila kaya inafuga kuku. Pamoja na kuwa kuku wanafugwa kila mahali, lakini mchango wake katika uchumi wa kaya haujanakiliwa ipasavyo *(Poorly Documented).* Ni hivi miaka ya karibuni tu mchango wa kiuchumi kwa kaya utokanao na kuku, umebainika pamoja na athari zake katika kupiga vita umasikini. Kwa mfano, mkulima mwenye kuku 20 anaweza kuingiza kipato cha

Sh.540,000/= kwa mwaka ikiwa atawatunza vizuri kupunguza vifo vitokanavyo na gonjwa la *Newcastle.*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuwapa nguvu na motisha wasomi wanaojaribu kutafuta chanjo za kuku kwa kutumia mitishamba inayopatikana hapa nchini. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumepata ufumbuzi wa kupata chanjo sahihi na kwa wakati zinapohitajika. Ili tuwe na mifugo mingi na iliyo bora ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba, huduma za chanjo na utabibu wa mifugo zinapewa umuhimu mkubwa. Mifugo yetu nchini inakabiliwa na maradhi mengi kama vile homa ya mapafu, *East Coast Fever,* Kimeta, *Newcastle* na mengineyo. Maradhi haya husababisha kupungua uzalishaji na kuleta vifo.

Mheshimiwa Spika, maradhi hayo yanaweza kutibika ama kuzuilika iwapo hatua madhubuti zitachukuliwa zikiwemo matumizi ya chanjo kwa muda maalum, kutumia dawa za kuogeshea pamoja na kuangamiza *vectors* wanaoambukiza maradhi hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya nyuma, Serikali ilijenga majosho mengi katika sehemu mbalimbali. Kwa bahati mbaya mengi ya majosho haya kwa muda mrefu hayakukarabatiwa na hatimaye yameharibika. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha majosho haya yanafufuliwa na mengine mapya yamejengwa kwa zile sehemu ambazo hazina majosho ili kudhibiti maradhi yaambukizwayo na kupe.

Mheshimiwa Spika, kadhalika tunaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, chanjo mbalimbali zinapatikana za kutosha na kwa wakati ili kuweza kudhibiti mlipuko wa maradhi ya mifugo. Ili kufanikisha hili, ni vyema basi Serikali yetu ikajiunga kikamilifu na mpango uliobuniwa na nchi za *SADC* wa kutoa chanjo kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa na mipango mizuri ya udhibiti wa maradhi ya mifugo, ikiwa dawa na chanjo zitaendelea kuwa ghali sana, Wananchi watashindwa kuhudumia ipasavyo mifugo yao. Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba, bei za chanjo na dawa za mifugo zinadhibitiwa ili mfugaji wa kawaida aweze kuzimudu.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini tulikuwa na Kiwanda cha Nyama cha *Tanganyika Packers* pale Dar es Salaam. Kiwanda hiki kilikuwa kinasindika nyama na kuuza katika soko la ndani na nje ya nchi. Kwa bahati mbaya kiwanda hicho kimekufa muda mrefu, lakini sasa tunapata faraja kuona kwamba, hatua zinachukuliwa kuanzisha upya Viwanda vya Nyama. Mfano mzuri ni hiki Kiwanda cha Nyama kinachojengwa hapa katika Manispaa ya Dodoma. Huu ni ukombozi mkubwa kwa wafugaji. Sambamba na hatua hiyo, Serikali pia imejenga Chuo Maalum kwa ajili ya kuwafundisha vijana namna bora ya kuandaa na kusindika nyama kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi. Chuo hiki kipo hapa jirani na majengo ya Bunge na kinatarajiwa baada ya kukamilika kwake kitakabidhiwa kwa Chuo cha *VETA* kuendesha mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaipongeza Wizara kwa hatua hii na tunaiomba Wizara kuandaa utaratibu na miundombinu ya kutosha kuona kwamba, Chuo hicho kinakuwa cha manufaa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mifugo mingi hususan ng'ombe na mbuzi huchinjwa kila mwaka. Miongoni mwa rasilimali itokanayo na wanyama hawa ni pamoja na ngozi. Hapa nchini tulikuwa na viwanda vitano vya ngozi na kama nilivyosema awali kwamba, tuna ng'ombe milioni 17.7 na kondoo na mbuzi karibu millioni 16, ukilinganisha na Kenya ambao wana viwanda vya ngozi vinane, wakati idadi yao ya ng'ombe ni milioni 13, mbuzi na kondoo milioni 5.9. Uganda wao wanaviwanda sita vya ngozi, wakati idadi yao ya ng'ombe ni milioni 5.6, mbuzi na kondoo ni milioni 7.8.

Takwimu hizi zinatuonyesha tofauti iliyopo kati ya idadi ya mifugo kwa nchi yetu na majirani zetu na viwanda walivyonavyo vya ngozi. Inatuonyesha ni jinsi gani Tanzania bado hatujaweza kutumia vizuri rasilimali ya ngozi kwa manufaa ya wafugaji na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatujui ni viwanda vingapi hapa Tanzania vinafanyakazi na vingapi vimekufa kati ya vitano tulivyonavyo. Labda Mheshimiwa Waziri, atakapofanya majumuisho atatueleza ni vingapi vinafanya kazi na ni vingapi vimekufa. Lakini la msingi hapa ni kuwa hakuna asiyefahamu kuwa ngozi ni mali, basi ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba, viwanda vyote vya ngozi vinafanyiwa ukarabati ili viweze kufanya *processing* ya ngozi kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hatua hii itamsaidia mfugaji kuongeza pato katika kaya yake na kukuza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, huduma nyingine muhimu kwa wafugaji ni upatikanaji wa mbegu bora za malisho ili kukuza uzalishaji wa mifugo. Serikali inayo mashamba machache kwa ajili ya madhumuni hayo. Pamoja na mchango mkubwa unaotokana na mashamba hayo katika kukuza Sekta ya Mifugo, bado mashamba hayo yanakabiliwa na matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa zana, vipuri, wafanyakazi pamoja na mafuta ya kuendeshea mitambo, ni miongoni mwa matatizo sugu yanayokwamisha juhudi za mashamba hayo. Kambi ya Upinzani inaiomba Serikali kuyatupia macho matatizo yanayoyakabili mashamba hayo na juhudi za makusudi zichukuliwe kuyapatia vifaa na nyenzo muhimu ili kukuza ufanisi wa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, upandishaji bora wa mifugo ni njia moja na muhimu ya kukuza uzalishaji. Ni dhahiri kwamba, iwapo hatua madhubuti za upandishaji kwa njia ya kuunganisha damu *(Cross-breeding)* hazikuzingatiwa, badala ya kukuza uzalishaji matokeo yake ni kuyadumaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sera ya Upandishaji *(Breeding Policy),* tuliyonayo nchini ni ya z amani imekuwa haikidhi haja iliyokusudiwa. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuandaa upya *Breeding Policy* ambayo inaendana na wakati tulionao ili kukuza tija katika shughuli za ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 wakati nawasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii, nilitoa malalamiko yangu kwamba, nilikuwa sipati ushirikiano wowote kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake alisema kwamba, hiyo haikuwa nia yake ila tu alizongwa na kazi nyingi.

Mheshimiwa Spika, mwiba uingiapo ndipo utokeapo. Kwa sababu nililamika hapa Bungeni, naomba leo niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kuanzia wakati ule nimekuwa napata ushirikiano wa kutosha na mkubwa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na kuwa ushirikiano wetu umetuwezesha kufanya kazi yetu kwa ufanisi zaidi. Naomba ushiriano huu uendelee na udumishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa tunaanza mjadala wa jumla, lakini kabla sijamwita Mheshimiwa William Shellukindo, mimi nimepangiwa kuonana na mgeni niliyemtambulisha asubuhi. Kwa hiyo, namwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Eliachim Simpassa aje anipokee Kiti.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hoja hii ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, lakini awali ya yote, napenda kutamka kwamba, naunga mkono hoja hii kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa mchango wangu, napenda kuchukua nafasi hii kuwapa pole sana familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, kwa msiba mzito walioupata. Naomba tu wawe wavumilivu, wenye subira na ninamwomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya Marehemu mahali pema Peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, pamoja na Wasaidizi wake, Mheshimiwa Anthony Diallo, Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu, Bwana Vicent Mrisho, kwa kazi kubwa sana ambayo wameifanya ya kuliwezesha Taifa hili kutumia rasilimali muhimu ya maji ya Ziwa Victoria. Kazi hii waliyoifanya ni kazi ambayo ilitaka utulivu, kusoma Mikataba na kuelewa athari zinazoweza kutokea kama Mikataba hiyo tafsiri yake itakuwa sio sahihi. Lakini wameifuatilia vizuri na kwenda kugundua kwamba, kitendawili ambacho kilikuwepo kwa muda mrefu kinaweza kuteguliwa na wamekitegua. Tunawashukuru sana. Nadhani hapa la kusisitiza kwa kweli ni kwamba, wenzetu ambao wako jirani kabisa na rasilimali hiyo, waitumie vizuri sana ili tusije tukaonekana tumehitaji rasilimali kwa kuendeleza Taifa letu, lakini utakuta rasilimali hiyo haitumiki vizuri. *(Makofi)*

Mimi ningependa sana kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa mpango huu aliouanzisha wa miradi ya maji na usafi wa mazingira. Kwa kweli ni *concept* nzuri sana na mpya. Mimi nimefanya kazi Mkoa wa Mwanza kwa miaka mitatu, naelewa, Wasukuma ni watani wangu, hawataki miti na iko sababu nitaeleza. Hawataki miti kwa sababu pamba inahitaji maeneo yaliyo wazi, kwa hiyo mti hautakiwi.

**MBUNGE FULANI:** Aombe radhi!

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Siwezi kuomba radhi, mtani haombi radhi. Mkitaka mwende Lushoto mkaombe radhi kule. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naizungumza hii na iko wazi kabisa, kwa mfano, ukitoka Mwanza pale ukielekea Misungwi, sehemu iko wazi kabisa. Sasa kama maji yanakuja, basi na miti ipandwe, ndio hasa ninalotaka kusema mimi. Kama mnahitaji utaalam, uko mwingi sana. Kule Lushoto kuna watu wengi sana wangeweza kusaidia namna ya kupanda miti ambayo itasaidia kuhifadhi na kutunza maji hayo vizuri sana. Sasa sizungumzi utani, hii nasema ni amri kwa nyie Wasukuma, maji na utunzaji wa mazingira na hifadhi ya mazingira. Nitakuja kuwakagua huko. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Bumbuli lina matatizo makubwa sana ya maji. Kama mnavyojua sehemu ile ni milimani, kwa hiyo, kuna vyanzo au chemichemi ambazo kama hazikuhifadhiwa vizuri, basi kuna uwezekano maji yale yakakauka na kukauka kwake kutaathiri hata ujazo wa maji katika Mto Pangani. Sasa mimi namwomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara yake kwa ujumla, huu utaratibu wa miradi hii ya maji sasa uzingatie hiyo hifadhi ya mazingira. Yaani mradi wa maji ukipangwa basi hapo hapo uwepo mradi wa kuhifadhi mazingira ili tuhakikishe kwamba maji kule milimani hayakauki na kuathiri nchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Katika Jimbo langu la Bumbuli kuna miradi ambayo imekwisha fanyiwa michoro na ninapenda sana kumshukuru Mhandisi wa Maji wa Wilaya akisaidiwa na Kiongozi wake katika Mkoa kwa kazi ambazo wamezifanya kwa bidii kabisa. Kila nilipoomba kwamba mahali fulani Wananchi wanahitaji kutekeleza mradi wa maji, haraka sana walifanya kazi hiyo. Kwa hiyo, kuna miradi ifuatayo ambayo imekwishamaliza kufanyiwa michoro.

Mradi wa KWAKIDOLE ambao uko katika Kata ya Mamba, ambao gharama yake ni milioni 253. Mradi huu ulikamilika kuchorwa mwaka 1996, nadhani unahitaji kupitiwa tena maana gharama zitakuwa zimebadilika na ninadhani kwa sababu ndio wa kwanza huu, basi ungepewa kipaumbele ungekuwa *priority project* ili kusaidia Wananchi wale maana yake wamejitolea kufyeka mashamba yao, kufyeka kutoa njia itakayopita mabomba ya mradi huo.

Mradi wa pili, ni *Kweninyasa Water Project* ambao gharama yake ni Shilingi milioni 168. Gharama hizi nazo zinahitaji vilevile kuangaliwa kwa hali ya sasa.

Mradi wa tatu, ni Manga Funta katika Kata ya Funta. Mheshimiwa Edward Lowassa, anaufahamu sana huu mradi na alishawahi kuutolea jibu. Mradi huu gharama yake ni Shilingi milioni 247.

Mradi wa nne, ni Mpalalu Ngwelo katika Kata ya Tamota. Mradi huu gharama yake ni Shilingi milioni 114.

Mradi wa tano, ni *Mbuzii/Soni Water Project.* Unahusu Kata mbili na gharama yake ni Shilingi milioni 556.

Halafu kuna Mradi wa *Bumbuli Water Project* ambao gharama yake ni Shilingi milioni 498.

Sasa nadhani miradi hii kwa sababu imeshafanyiwa michoro isikae muda mrefu kwa sababu Wananchi wamehamasika, wanangojea wapate nguvu kutoka nje na sisi tunajitahidi kuimarisha Mifuko ya Maji. Tunahimiza michango iwepo ili miradi hii inapokamilika kwa kweli tusirudi tena Serikalini kwenda kuomba mtu wa kuja kuitengeneza, iwe ni kazi ya Wananchi wenyewe kuendelea kuitengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Wizara hii pamoja na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, alitoa ahadi kwa Mradi wa Mgwashi, kwamba atausaidia na gharama yake ni Shilingi milioni 84 lakini wameshapata Shilingi milioni 16. Ombi letu hapa ni kwamba, utoaji wa fedha huu kidogo kidogo una gharama kubwa. Kwa hiyo, ni vizuri kama mradi umetengewa fedha, kama ni awamu mbili basi ziwe ni awamu ambazo haziongezi gharama. Kwa sababu kama utanunua vifaa nusu nusu, usafiri utakuwa ni ule ule, kwa hiyo, utakuwa na gharama zaidi. Ningeomba hili lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kitabu cha Hotuba cha Mheshimiwa Waziri, katika ukurasa wa 140, Jedwali la Tano, Wilaya ya Lushoto imewekwa kama Wilaya ya upanuzi wa awamu ya pili kwa mwaka 2005. Sasa nilitaka kufahamu hapa katika hii miradi sita niliyoitaja ni mingapi ambayo itatekelezwa katika mwaka huu. Nitashukuru sana, maana wakati nikiwa hapa nilipata barua ya Mwenyekiti wa Mradi wa KWAKIDOLE, Bwana Bushiri pale Mamba, ananiambia nisisahau kumkumbusha Waziri wa Maji kwamba, Mradi wa KWAKIDOLE umekaa muda mrefu, kwa hiyo, autazame. Wanamkaribisha Mheshimiwa Waziri akaone KWAKIDOLE palivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara hii chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Edward Lowassa kwamba, haya mawazo mapya ya maji na hifadhi ya mazingira, nadhani isingekuwa ni wimbo sasa. Kwa sababu mvua nyakati za sasa inanyesha kwa taabu sana, sasa hivi vyanzo vichache vyenye uhakika wa maji tulivyonavyo ni vizuri tukaviwekea hifadhi nzuri ya mazingira na kuviimarisha ili tuweze kuwa na maji wakati wote. Kwa hiyo, mimi napenda kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba, hata kwenye Halmashauri zetu, kuna miradi midogo midogo ya maji ambayo haihitaji kupelekwa kwa Mheshimiwa Edward Lowassa vya Sh.50,000/=, Sh.100,000/= na kadhalika, basi hii upangaji wake uzingatie vilevile upangaji wa namna ya kutunza mazingira katika eneo hilo kwa maana vyanzo vile kwa

kweli ni vitu muhimu sana kuhifadhiwa, vinginevyo tutapata matatizo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza tena Wizara hii kwa kuweka utaratibu mzuri sana wa mashamba ya mifugo. Mimi nilikuwa na wasiwasi mkubwa sana kwamba kama hatukuwa waangalifu, rasilimali ya ardhi ni rasilimali ya msingi, kama tutaichezea itakuja kuingia kwenye mikono ya watu wachache halafu tupate matatizo kama wanayoyapata wenzetu wa Zimbabwe. Sasa ni vizuri tuchukue masomo tuliyoyapata Zimbabwe tuweke mipango ambayo haitupeleki kwenye hatua hiyo.

Mimi napenda kuwapongeza sana kwa kuwasaidia Watanzania hawa kuweza kumiliki maeneo ya ufugaji wa kisasa, maeneo ambayo wana uwezo nayo. Hapa ningependa kusema kwamba, ni vizuri hata yale maombi yakafuatana na Mpango wa Maendeleo *(Strategic Investment Plan)* wa eneo hilo. Tusije tukatoa ardhi tu, kwa sababu mtu anaweza asitumie eneo lote alilopewa na sisi tumeweka katika maendeleo yetu kwamba, tutaweza kuzalisha mifugo katika maeneo yafuatayo na mifugo kiasi fulani, kumbe ni kuhodhi tu ardhi ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili suala la *strategic investment plans* liwe ni kitu cha muhimu kabisa, mtu anapoomba eneo la ardhi. Vilevile ardhi mtu anayoomba basi angepewa kwa awamu kwamba katika mpango wake amesema katika miaka mitano hii ataweza kuzalisha kiasi hiki. Basi kwa kuanzia tunakupa hilo eneo la kuweza kulitumia kwa miaka hiyo mitano, hili lingine uonyeshe kwanza kwamba hili unalitumia vizuri ndipo tukuongezee, kuliko kuwapa watu ardhi halafu yakawa mapori na baadaye watu wengine wakiihitaji tunasema ana hati ya kumiliki. Kwa sababu ukishampa mtu Hatimiliki, kumnyang'anya inakuwa ni kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi sina zaidi kwa sababu Wizara hii sina matatizo nayo kwenye Jimbo la Bumbuli, sina kabisa. Kama nilivyosema miradi imekwishafanyiwa michoro, iliyobaki kwa kweli tushirikiane ili tuweze kuwasaidia Wananchi waweze kuitekeleza miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja hii kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kupata nafasi kusudi niweze kutoa mchango wangu kwa Wizara hii ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina haja ya kusisitiza umuhimu wa maji. Wale wote waliojifunza Shule wanaelewa kwamba, kila mwanadamu robo tatu ya mwili wake umekuwa *composed* na maji. Lakini pamoja na umuhimu wa maji kwamba ni mazuri, tunaweza kunywa, kupikia na kuoga, lakini pia ni hatari yanapokuwa machafu na yakitumiwa na watu, yanaweza kuleta magonjwa kama vile kipindupindu na shida nyingi. Kwa hiyo, moja ya matatizo makubwa tuliyonayo sisi hasa katika Mji wetu wa Tarime katika Jimbo la Tarime ni kupata hayo maji safi.

Maji ambayo mpaka sasa hivi tunapata ni machafu kwa maana kwamba, maji yote yanayotumika katika Mji wetu wa Tarime hayasafishwi wala hayawekewi dawa. Yanachukuliwa kama yalivyo halafu yanakwenda katika matumizi moja kwa moja. Ni kwa sababu hiyo ndio maana katika mwaka 2000 Rais, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa alipotembelea Tarime, alipouliza wananchi kwamba tatizo gani kubwa zaidi mlilonalo, wakamwambiwa Bwana Rais, sisi kura zote tutakupa ilimradi kama tutapewa maji. Rais akaahidi akasema kwamba, hakuna tatizo, Tarime mtapewa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka mwaka 2001, Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba, nilishamwona kuhusu ahadi hii ya Tarime, mwaka 2002 nilimwona, mwaka 2003 nilimwona, 2004, nimemwona na sio mimi tu, pamoja na Mkuu wetu wa Mkoa na watu wengine mbalimbali. Kwa hiyo, angalau kwa mwaka huu wa 2004, labda nishukuru tu kwamba, katika hotuba ya Waziri nimeona hata jina la Tarime limeonekana. Miaka hiyo mingine nyuma hata kugusiwa wala kusemwa ilikuwa hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nataka kusema ni kwamba, tuna matatizo mawili makubwa, kwanza, hatuna maji ya kutosha, halafu yale yaliyopo ni machafu. Kwa sababu hiyo, yanadhuru watu wanapoyatumia. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Mheshimiwa Waziri, atushughulikie kwa namna mbili. Kwanza, nashukuru alituma mtu akaenda akaona vyanzo vya maji ambavyo ni vingi kwa sababu toka Ziwa Victoria mpaka Mji wa Tarime, sehemu ya karibu zaidi ni Kilometa 38, kutoka mto mkubwa ambao haukatiki mwaka mzima, Mto Mori, mpaka Mji wa Tarime ni Kilometa mbili.

Lakini *source* za Tarime mpaka sasa zimekuwa mbili. Moja ni hili lililojengwa na Wakoloni, walichimba bwawa ambalo sasa lilishajaa matope na linatunza maji machache. Halafu tuna *gravity scheme* ambayo inachukua hayo maji machafu ambayo tunatumia kwa ajili ya matumizi Tarime.

Kwa hiyo, katika awamu ya kwanza wakati tunangojea huo mpango wa kudumu ambao Mheshimiwa Rais alituahidi, tulikuwa tunaomba kwamba, maji ambayo sasa yanachukuliwa, yanayokuja Tarime kutoka katika ile *gravity scheme,* ile njia ikarabatiwe kusudi iweze kuleta maji ya kutosha japo hayatatosha hata tukifika asilimia 30 au 40 kwetu ni kitu.

Ukitoka 10 ukaja 20 au ukitoka 10 ukaja 30 ni bora kuliko unapobaki pale kwenye 10. Lakini sana ni kwamba, hayo maji yakija yawe *treated* kabla hayajatumiwa na watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu katika *speech* ya Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba, sehemu ambazo zitafanyiwa ukarabati ni pamoja na Tarime, nilifikiri pia atachukua nafasi hii na kuagiza Wizara yake kwamba, lile bwawa ambalo walijenga Wakoloni zamani huko, sasa lisafishwe matope yaishe tuweze kupata maji mengi yanayobaki pale mvua inaponyesha.

Halafu katika mpango wa kudumu, tunaamini kabisa na Mheshimiwa Waziri atakubaliana na sisi kwamba, watakapoamua kutoa mabomba Ziwa Victoria mpaka Mji wa Tarime, sio kwamba tutasaidia Mji wa Tarime tu, bali pia tutasaidia na Vijiji vya jirani ambavyo vipo njiani kabla hatujafika Tarime.

Kwa hiyo, ningetaka kusisitiza tu na kusema kwamba, ni vizuri Mheshimiwa Waziri, watu wake wameshatembelea Tarime na mradi hauwezi kuanza mpaka kwanza usanifu ufanyike, *design, costs* ijulikane, maji yatakuwa namna gani na kila kitu kitafanyika namna gani.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba katika kipindi hiki na katika muda mfupi iwezekanavyo basi, atufanyie usanifu kwa ajili ya maji ya Mji wa Tarime. Baada ya huo usanifu, angalau tuelewe kwa hakika kwa kutangazwa, kwa kusemewa kwamba, sasa haya maji ni hakika hata kama sio mwaka huu wa 2004, basi mwaka 2005, lakini kwa muda mfupi iwezekanavyo tutaweza kukamilisha na kurekebisha tatizo la maji katika Mji wa Tarime. *(Makofi)*

Halafu tunashukuru kwamba, pia kama temporary measure nimeona kwamba katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kati ya visima vitakavyochimbwa tutapata visima virefu vitatu. Nataka pia kushukuru kwa sababu ninaamini vitatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nataka kusisitiza na ambacho nataka kusema ni kwamba, maji tuliyonayo Tarime ni machafu na kwamba katika huu muda wa mpito, kabla hatujapata maji ya kudumu, wakati inaamuliwa kufanywa ukarabati, basi tufanyiwe ukarabati kusudi maji haya yawe masafi, mabomba yaongezwe, yazibuliwe tupate maji ya kutosha katika Mji wa Tarime na kwamba hivyo visima vitakavyojengwa viwe *distributed* vya kutosha katika Mji kusudi maeneo mengi zaidi yaweze kupata maji.

Kwa hiyo, kwa kumalizia tu nataka nisisitize kwamba viwe *distributed* vya kutosha katika mji kusudi maeneo mengi zaidi yaweze kupata maji. Kwa hiyo, kwa kumalizia tu nataka nisisitize kwamba naamini kwamba wote hapa tunaajiri naamini pia na Mheshimiwa Rais anaajiri, anawaajiri nyie Mawaziri hapa kwa kuwapa kazi naamini kwamba ile kauli yake ni kauli ya mwajiri na kwamba akisema naamini ni lazima mtii. *(Makofi)*

Kwa hiyo na kwa sababu alishafika mkiwa Tarime naomba tu kwamba hiyo kauli ya mwajiri ingawa anaajiri watu wote lakini kazi aliwapa nyie mumsaidie. Kwa hiyo, naomba umsaidie ahadi hii ya kwetu ya Tarime ikamilike kwa wakati muafaka. Nashukuru sana kupata nafasi ya kuchangia. *(Makofi)*

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika hoja hii ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Sekta ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya Watanzania na hususan katika harakati zetu za kuupunguza umaskini katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijafanya hivyo ningeomba nami nitoe salamu za pole kwa wafiwa wa aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Hayati Mwalyego na aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, Hayati Capt. Theodos James Kasapira, kwa kupotelewa na ndugu zao ambao ni wapenzi wetu sisi wote. Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahala pema peponi. *Amini.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nianze kwa kutamka kwamba naiunga mkono hoja hii mia kwa mia. Naunga mkono na ningewaomba Waheshimiwa Wabunge wote kwa kweli tuunge mkono kwa sababu Mheshimiwa Edward Lowassa, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu, Ndugu yangu Vincent Mrisho na wasaidizi wao wametoa hotuba nzuri, yenye kina na mantiki na yenye kuleta matumaini kwa Watanzania.

Lakini pia napenda kuwapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya. Sisi ambao tumebahatika kushirikiana na Mheshimiwa Lowassa hatutasita kumsifu, na hatutaacha kumshukuru kwa jitihada zake za kuleta maendeleo katika Sekta ambazo anazisimamia. Mbali ya mipango mizuri, Mheshimiwa Lowassa ni mwepesi wa kupokea ushauri na pia anapojulishwa kwamba yapo matatizo, basi huwa hasiti anafika katika maeneo yale yenye matatizo badala ya yeye kutoa maagizo kutoka mezani. Hufika katika maeneo kama hayo akiwa ameambatana na wataalam wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maagizo yake yeye hutolewa mahali pa tatizo *on the spot.* Kwa hiyo, basi pale kwenye Ibara ya nane ya hotuba anapotushukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango ambayo inamsaidia yeye nadhani tunafanya hivyo kwa sababu yeye mwenyewe ni mwepesi wa kupokea ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vielelezo vya hayo ninayoyasema viko wazi. Katika Wilaya yangu ya Kisarawe tulikuwa na tatizo la maji Mjini Kisarawe na nimelizungumza hapa Bungeni. Lakini baada ya Kikao cha Bunge kile nilichozungumzia tatizo hilo, Mheshimiwa Lowassa alifika na Wataalam wasiopungua 10 na kwa kweli wakati huo huo akasaidia chanzo cha maji cha mahala kinachoitwa Dalu na sasa hivi maeneo ya mji wa zamani wa Kisarawe hayana matatizo ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunasikia katika vyombo vya habari jinsi jitihada zake katika Mikoa mingine. Kwa mfano, nimesoma na kusikia katika vyombo vya habari alipotembelea Mtwara amefika vijijini ambako wamemshukuru kwamba alikuwa Waziri wa kwanza tangu tumepata uhuru. Nadhani alikuwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo wa kwanza kufika kwenye vijiji hivyo. Huyo ni Mheshimiwa Lowassa na timu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Mheshimiwa Lowassa apokee shukrani za Wana Kisarawe kwa jitihada alizozifanya na mpaka akafika katika chanzo cha maji cha Bwawa la Minaki ambako ndiyo tegemeo kuu la Mji wa Kisarawe na Shule ya Sekondari ya Minaki na kwa taarifa yako Mheshimiwa Waziri juzi tu nimeongea na wenzangu kule Kisarawe, mradi ule sasa unaenda vizuri sana, bwawa karibu litamazilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuchelewa kwa kweli nimesema nimemwomba Mheshimiwa Waziri azipokee hizo shukrani na ni mategemeo yangu kwamba jitahada zake ataziendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia Wizara hii miaka miwili iliyopita, nilielezea tatizo la ardhi katika Wilaya za Kisarawe na Kibaha. Hapa lazima niwasemee wenzangu. Kwa sababu wale Mawaziri wa Bagamoyo na Kibaha hawawezi kujisemea wenyewe mbele ya Bunge hapa. Nilisema kwamba Wilaya hizi zina matatizo ya miamba ambayo hayawekezi maji ya visima vifupi na nikamshauri Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano wa kutumia njia nyingine kama za kutega maji ya mvua, visima virefu na kuchimba malambo. Nafurahi kusema kwamba katika mpango wake wa mwaka jana kati ya malambo machache ambayo yamepatikana, Waziri hakusita kunipatia malambo matatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kuwa alishauri nguvu za wananchi zitumike, kwa taarifa yake wananchi, Halmashauri na mchango wa Mbunge wamesaidia badala yahivyo badala ya kuchimba malambo matatu kwa fedha ile ambayo imetolewa, tumechimba manne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwarifu Mheshimiwa Waziri kuwa malambo manne katika Wilaya yenye vijiji 76 vyote vyenye matatizo ya maji ni tone katika bahari. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, tunakuomba ujitahidi katika bajeti hii na zijazo utuongezee malambo kusudi tuweze kupunguza matatizo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kuwa hili litawezekana kwa sababu kama nilivyosema Mheshimiwa Waziri yeye ni hodari wa kupokea ushauri na ni hodari wa kutimiza ahadi zake. Katika bajeti ya mwaka wa 2003/2004, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Waziri, ahadi ambayo alikuwa amezitoa. Alisema kwamba mwaka huo Wizara yake ingefanya utafiti wa maji chini ya ardhi kwenye maeneo 700 nchini ili kutambua yale yatakayochimbwa visima vya maji.

Kwa bahati mbaya, kwa mujibu wa Jedwali Na. 2 ya hotuba yake ya mwaka huu, naona Kisarawe haimo. Lakini nafarijika kwamba nilipoangalia katika kiambatisho Na. 5(b) niliona kuwa kati ya Wilaya 38 ambazo zimewekwa katika awamu ya pili, Kisarawe imo. Ni mategemeo yangu kwamba Mheshimiwa Waziri atahakikisha yote niliyoyasema yanatekelezwa na kuwa malambo matatu hayatoshi hivyo atatilia mkazo wa kutupatia malambo zaidi katika bajeti ya mwaka huu na miaka ijayo.

Napenda pia nimkumbushe Waziri ahadi zake mbili za miaka iliyopita na ninaamini ilikuwa kama si mwaka 98 ulikuwa 99. Ya kwanza katika bajeti ya miaka hiyo aliahidi kufufua mradi wa maji ya Mzenga katika Wilaya ya Kisarawe ambao ulisimama kutoka miaka ya 1978.

Lakini baada ya hapo wananchi wa Mzenga bado wanasikiliza kuona kwamba ni lini mradi huu utafufuliwa. Hapa napenda tena nimkumbushe Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ya nyuma alisema kuwa angeweza kusaidia kuchimba malambo madogo.

Mabwawa, siyo malambo sasa. Mabwawa makubwa matatu dams mawili Kisarawe na moja Kibaha katika maeneo ya Titu na Homboza; kule Kibaha katika eneo la Kitanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika bajeti zilizofuatilia ahadi hiyo haikutekelezwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri uwezakno ukipatikana aikumbuke ahadi hiyo kwa sababu bado wananchi wanapata shida katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, basi atakapojibu hoja zetu ni mategemeo yangu kwamba Mheshimiwa Waziri atatoa tamshi juu ya malambo ya Mzenga, Titu na Homboza kule Kitanga. Isitoshe, kutokana na taarifa yake katika bajeti iliyopita, Mheshimiwa Waziri, alisema mradi wa maji vijijini unaotumia mikopo nafuu ya Benki ya Dunia, angeweza kuhakikisha kwamba maeneo ambayo yako kando kando ya njia za maji kutoka Ruvu Juu na Ruvu Chini yatakuwa yameshughulikiwa.

Nimezingatia taarifa ya Mheshimiwa Waziri katika Ibara ya 50 ukurasa wa 35 kwamba mradi wa kupanua maji vijijini utahusisha Wilaya zote na ni mategemeo yangu kuwa maeneo haya yatafikiriwa. Kuhusu maji mijini, katika hotuba yake ya mwaka uliomalizika, Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba ataharakisha huduma za maji ili kuwafikishia wenye kipato cha chini. Maeneo yatakayohusika ni yale yaliyo kando kando ya mabomba makuu na maeneo yaliyo pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam, Kibaha na Bagamoyo.

Aliahidi kuanza kutekeleza programu ya usambazaji wa maji safi na majighafi. Nataka kumkukumbusha Mheshimiwa Waziri wala sijui kama anayo taarifa kwamba sasa hivi kuna maeneo mengi katika Jiji la Dar es Salaam na miji ya Kibaha hayafiki maji. Kule ninakoishi mimi miezi mitatu sasa hakuna maji. Na sielewi tatizo ni nini. Ni *Mbezi Beach,* maeneo ya Tangi Bovu na kule *Jangwani Beach* hakuna maji na ambapo kuna hoteli za kitalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo juu ya Mifugo. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba ingawa Mkoa wa Pwani tulikuwa nyuma ya Wasukuma kwa mifugo, ashukuru kwamba kwa jitihada zake, sasa hivi tumeanza kufuga ng’ombe wa maziwa na alipotembelea Kisarawe aliwahi kupitia wafugaji wachache na wataalam wake wakatupa maelekezo na sasa hivi, baadhi ya Wanakisarawe wanakunywa maziwa ambayo yanatoka katika maeneo hayo. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kengele isinigongee nasema kwamba katika mchango wangu nimesema mambo makuu matatu: nimempongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kwa kazi nzuri na jitihada zao na kuukubali ushauri na kwa niaba ya Wana Kisarawe nimemshukuru kwa jinsi alivyoshughulikia kero za maji na kuanza kutuendeleza katika mifugo ya ng’ombe hasa wa maziwa.

Mwisho nimeeleza matumaini yangu na ya Wana Kisarawe kuwa Mheshimiwa Waziri atashughulikia matatizo ambayo nimeyataja juu ya maeneo ambayo mpaka sasa hivi bado hayajapata maji. Ni mategemeo yangu kwamba hili litakuwa limefanyika.

Baada ya kusema hayo nisingependa kengele ya pili isinigongee. Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipa nafasi. Ahsante sana na naunga mkono tena mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Lakini kabla ya kufanya hivyo, naomba nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kutoa rambi rambi na pole nyingi kwa familia ya Mheshimiwa Theodos Kasapira aliyefariki hapa wiki iliyopita na Mwenyezi Mungu awape subira katika hili lililowatokea ambalo ni gumu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kuchangia pia nami naomba kwa awali kabisa niunge mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina sababu kwa kweli zote za kufanya hivyo kwa kuunga na bila kuchelewa kwa kweli naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Naibu wake na wafanyakazi wao wote kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya na ambayo imeonyesha matumaini kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetupa matumaini kwa Watanzania wote si mijini kwa kweli mpaka vijijini hali sasa ya maji inaendelea kubadilika siyo kama wakati ule ambao tulikuwa tunapata tabu. Pamoja na ukame, lakini juhudi na mipango yake anayoionyesha Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa kweli inatupa matumaini mazuri ya kuendelea kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu au katika mji wangu wa Singida Mjini nina aina mbili ya mshughuliko wa maji. Nina Kata 13 lakini Kata 7 ni za vijijini na Kata 6 ni za Mjini. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kweli katika kujali sehemu zote za aina mbili. Katika Kata za Vijijini karibu sasa hivi kila Kijiji au kila Kata tuna visima vya maji. *(Makofi)*

Kila Kijiji kina kisima cha maji na tunaendelea kupata kupata visima vya maji karibu kila kitongoji. Bahati mbaya tu labda katika kitongoji hicho maji yasiwepo. Nashukuru Shirika moja lisilo la kiserikali *Water Aid* ambao kwa ushirikiano na wananchi wetu kwa sababu wametupa mradi ambao unashirikisha wananchi wameweza kushughulika na kutuchimbia visima vyote hivyo ninavyovitaja kwa muda wa miaka mitatu sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru wananchi wa Kata hizo kwa kuitikia mradi huu. Kwa sababu walikuwa wanatakiwa kuchanga au kuanzisha mifuko ya maji kila Kijiji na Kitongoji ambacho kimepatiwa kisima. Niwashukuru sana kwa kuchangia mifuko ya maji ili kuweza kupata visima vya maji. Kwa kweli ni kama kitu bure kwa sababu tunachochangia fedha hiyo tunayochangia bado ni fedha yetu kuanzisha

mfuko wa maji na katika kuchangia labda shilingi 50,000/= au 100,000/= unapata kisima cha milioni 5 au 7, milioni 3. Sasa ni kwamba tunakushukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Shirika hilo ili kupatiwa maji hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru pia Shirika hili kwa sababu licha ya kuchimba visima vipya, visima vyote vile ambavyo vilikuwa vimeharibika, vimekarabatiwa na kuanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kazi nzuri ambayo imefanywa vijijini bado na mjini pia, mji wa Singida kuna kazi ambayo inaendelea kazi nzuri ya kuinua upatikanaji wa maji mjini. Bado tuna matatizo ni asilimia 48 mpaka 50 tunapata maji. Lakini tukiangalia mahala tulipotoka tunaona kwamba hali inaendelea kuwa nzuri. Tunaendelea kupata maji na hali inaendelea kuwa nzuri kwa sababu yanaendelea kuongezeka. Lakini tabu ni kwamba tangu mwaka jana nafikiri na mwaka huu tutakuwa na tatizo kwa sababu ya ukame, visima vyetu vinakuwa na ukame na kwa hiyo maji yanakwenda chini zaidi kuliko uwezo wa kutoa maji.

Lakini mradi mkubwa zaidi kwa mji wa Singida ambao unautegemea, kwa bahati nzuri tena nimeuona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, mradi wa kutoa maji kutoka Bwawa la Itamka, unaotegemewa kuwa ni mradi wa bilioni 13. Mheshimiwa Waziri nashukuru kwa hatua iliyofikiwa na nashukuru kwa kweli kwamba bado unaukazania kuusukuma. Lakini niombe Serikali iendelee kwa sababu imeshakuwa miaka mitatu tangu mradi huu tuendelee kusikia na tumeupigia debe kweli kweli pale mjini kwa sababu ni mradi unaotegemewa kutukomboa kwa maji.

Sasa hivi maji tunayoyapata ni maji ya visima kiasi ambacho sasa ukomo wa visima au uwezo wa visima unafika mwisho. Sasa haya ndiyo tunayotegemea yatukwamue. Lakini pamoja na utayari wa wafadhili na watu wengine kutoa hizo fedha pamoja na Serikali bado tatizo ni kwamba sasa hivi liko nje ya uwezo wako, ni tatizo ya Sheria ya Manunuzi *(Procurement Act)* ambayo kwa kweli inachelewesha miradi mingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ningeiomba Serikali katika hilo ilete kama ni uwezekano, ilete marekebisho haraka ili tuweze kurekebisha. Kwa sababu kama vitu vinakuwa tayari lakini kwa sababu tu ya Sheria ya Manunuzi mradi unakaa miaka mitatu, minne bila kuendelea kufanyiwa kazi. Sasa wafadhili wanaweza wakati mwingine wakashtuka na kuzuia fedha kwa sababu wanaona wametoa fedha lakini fedha haifanyiwi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vinginevyo ni kwamba Wizara inajitahidi katika kukamilisha shughuli zote. Kwa hiyo, naishukuru Wizara kwa harakati hizo za kuweza kutukamilishia hilo. Ninachoomba sasa kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba katika Kata zangu zingine hizi saba za vijijini kuna Kata tatu, Kata ya Mtipa, Mtamaa na Mungumaji, miaka mitatu minne iliyopita walikuwa wamejitahidi kuchimba mabwawa. Lakini kwa sababu mabwawa hayo yamechimbwa na watu wenyewe kwa mkono kwa kujitolea, kwa kweli mabwawa ambayo ni madogo na yanahitaji msaada wa Wizara ili tuweze kupata

mabwawa yatakayosaidia. Naomba Mheshimiwa Waziri hebu nijalie katika hayo niweze kupata angalau mabwawa mawili matatu katika Kata hizo. Nitakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiachana na hilo naomba niongee kidogo kuhusu masuala ya mifugo. Mheshimiwa Waziri ana mipango mizuri sana kuhusu masuala ya mifugo na hasa suala moja linalotupa tabu na ambalo kwa kweli inakuwa ni vigumu kwa mifugo yetu kukubalika nje pamoja na nyama pengine ambayo tungetakiwa kuuza kwa ajili ya magonjwa. Mipango yake ya kuwezesha kutibu wanyama wetu naiona. Amejitahidi kwamba ametoa ruzuku ya bilioni 1 kwa ajili ya kutoa ruzuku kwenye madawa ya uogeshaji na hilo ni tatizo, kupe ndiyo tatizo ambalo linafanya wanyama wetu wakati wote waendelee kuwa na hali mbaya. Lakini kwa vile huu ni mwanzo, ningeomba sana na nashukuru kwamba mwanzo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ingekuwa inawekana wafugaji hawa ambao sasa hivi bado hali yao si mzuri na hata elimu yao katika hili katika magonjwa, ni tatizo. Kama ingekuwa inawezekana tungeweza kukarabati haya majosho na kuweka sheria kila mfugaji aweze kuogesha na aogeshe bure ili tuondokane na magonjwa haya ya kupe kwa sababu vinginevyo kwa kweli bila kutilia mkazo na bila kuweka Sheria ili wananchi waweze kuogesha kwa lazima tutaendelea kuwa na tatizo la hawa wadudu kupe na magonjwa yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara nasema mwanzo si mbaya wa kutoa ruzuku ya bilioni 1, si haba. Lakini jinsi tunavyokwenda kule ili tuweze kukomesha suala hili hebu tufikirie kuongeza ruzuku hiyo na hatimaye tuweze kuwapa hawa waogeshe bure lakini Sheria iwekwe ili kila mtu aweze kuogesha tuhakikishe tunaondoa matatizo haya ya kupe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uogeshaji kuna tatizo moja, kuna sehemu zingine kuna majosho. Lakini majosho hayo yanakabiliwa na uhaba wa maji. Kwa sababu maji yanakuwa hamna. Ili uweze kuogesha uweze kuweka dawa lazima pawepo na maji ya kutosha katika josho. Sasa maji yanakuwa ni tatizo. Aidha yanakuwa mbali. Sasa naomba basi Mheshimiwa Waziri, kama inawezekana katika kila majosho pawepo na visima ili uwezekano wa kukosa maji hayo usiwepo. Pawepo na visima vya kuwarahishia hawa wananchi ili waweze kupata maji karibu na waweze kuogesha kila wakati inapotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninaloliomba ni kwamba upande wa chanjo liangaliwe ili wafugaji wetu waweze kupata chanjo kama si bure basi pia waweze kupata kwa bei ndogo inayowawezesha wafugaji wote waweze kuchanja mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninataka kulizungumzia katika eneo hili ni njia za kupitisha mifugo inayopelekwa kwenye minada yetu *stock routes.* Mwaka jana Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Rais alikuwa ametoa Waraka wa kuhakikisha kwamba tusiendelee tena kuswaswaga ng'ombe barabarani na sehemu zingine kwa sababu kwa kweli tunaendelea kueneza magonjwa. Nimwombe Mheshimiwa Waziri ili *stock routes* ambazo zilikuwa zimeanzwa kutengenezwa basi

zikamilike bado hazijakamilika, kwa hiyo, wafugaji au bado wanapata pata visababu vya kuendelea kupitisha ng'ombe mahala ambapo hapatakiwi na kwa kweli tunajikuta tunaendelea kueneza magonjwa kwa hilo. Naomba *stock routes* zikamilishwe ili tuendeleee kulinda ng'ombe wetu.

Mara nyingi ninapokuwa ninakuja Dodoma nakutanakutana na ng'ombe ambao bado wanaswagwa barabarani, bado hii hali kwanza inaharibu barabara zetu pamoja na sisi Singida tulikuwa tumepiga marufuku muda mrefu na kulalamika juu ya hili. Lakini bado Sheria hajaimarishwa ili kuhakikisha kwamba hali hii inaondoka.

Mhesheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nilikuwa na hayo machache ya kuweza kuongea katika Wizara hii. Niendelee kumshukuru Ndugu yangu huyu na kumsifu kwa sababu kazi yake kwa kweli inaonekana kwa muda mfupi ambaye ameichukua Wizara hii inaonekana anakulika kabisa aendelee kuungwa na Wizara zingine kwa sababu hivi vyote vinategemeana, kama mwingine atafanya vizuri na huyu akafanya vizuri kwa kweli tunajikuta tumejikamua katika matatizo yetu. Baada ya kuzungumza hayo Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono tena hoja ya Mheshimiwa Waziri huyu ili bajeti hii iendelee, ipite apate fedha na aweze kufanya kazi yake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia machache kuhusu Wizara hii ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salaamu za rambi rambi kwa wananchi wa Majimbo ya Mbeya Vijijini na Ulanga Mashariki kwa vifo vya Waheshimiwa Wabunge wenzetu, Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego na Theodos James Kasapira, tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hao mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nitumie hii nafasi vile vile kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. Mheshimiwa Waziri Lowassa kwa kweli amefanya kazi nzuri sana katika Wizara yake na inaonyesha wazi kwamba kwa Tanzania tunapiga hatua kwa suala la maji na suala la maendeleo ya mifugo. Kwa hiyo, napenda nimpongeze sana pamoja na Naibu Waziri wake kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo hata amediriki kufika kwangu Meatu kwenye maeneo ambayo ni magumu sana kufika lakini amejitahidi mpaka akafika. Lakini kwa jitihada za Wizara hii ikiongozwa na Mheshimiwa Lowassa kwa kweli nampongeza na kuwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda niwashukuru sana Watendaji Wakuu, Katibu Mkuu na wengine ambao wanamsaidia Mheshimiwa Lowassa. Pongezi nyingi sana na kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii ambayo kwa kweli ni vigumu kuikosoa. Baada ya pongezi hizo Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nijielekeze kwanza kutumia nafasi hii vile vile kwa dhati kabisa kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa msukumo wa pekee wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kuja Kahama hadi Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ni ukombozi mkubwa sana kwa mradi huu na ningeomba tu ili uweze kutekeleza vizuri tupate Mhandisi ambaye anafaa, mambo mengine hua yanaenda kwa mradi kwa kusuasua, watu ambao pengine si wataalam zaidi kwa kusambaza maji. Na ningeomba Mradi huu kwa sababu ni mkubwa uweze ku-*cover* maeneo ambayo mradi huu unapitia. Na ingefaa sana usimamiwe kwa karibu sana na Wizara yenyewe hata kama kutakuwa na tenda ya watu ambao wanakuja kutujengea huo mradi. Naomba Mheshimiwa Lowassa kwa uhodari wake na Naibu wake waweze kusimamia kwa karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais. Kwetu Meatu tulikuwa na shida sana ya maji lakini kwa bahati nzuri, Mheshimiwa Rais ametupatia mradi wa maji ambao ni mkubwa sana Bwawa la Mwanyahina. Bwawa hilo sasa hivi lina maji mengi tu. Naomba kama inawezekana Wizara hii ifanye kila linalowezekana ili mradi huo ukamilike na kusambaza maji kwa watumiaji na ikiwezekana Rais mwenyewe aliyeuanzisha mradi huo aje aufungue mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maji hayo yafike sehemu mbalimbali lakini yasisahauliwe kufika kwenye Hospitali ya Wilaya. Hospitali ya Wilaya iko kando kidogo ya mji wa Mwanuzi ikipatiwa maji naamini kwamba wale wanaokwenda pale kupata huduma za afya watafaidika na hasa upande wa akina mama wanapojifungua maji huwa ni ya kununua kutoka kwenye vijito vidogo vidogo kwa kweli ni usumbufu mkubwa sana. Naomba maji yafike kwenye Hospitali ya Wilaya pamoja na shule za sekondari, Meatu Sekondari, Kimali Sekondari na maeneo mengine muhimu. Mradi huu kwa kweli utatuokoa kutumia maji sio salama. Sasa hivi wanategemea maji kutoka kwenye vijito na ni maji ambayo sio safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, napenda nijielekeze kwenye sehemu nyingine upande wa mifugo. Mkoa wa Shinyanga una ng’ombe wengi sana na mara nyingi huwa tunapeleka kwenye minada ya Arusha, Mara na Dar es Salaam. Minada hiyo kwa kweli iko mbali na wale wanaopeleka ng’ombe hao huwa wanasafirisha kwa njia ya reli. Ng’ombe kumsafirisha kwa njia ya reli ni kero, huchukuliwa ng’ombe 60 kwenye behewa moja. Katika kuwasafirisha huchukua siku 3 mpaka 4 kutoka Shinyanga kwenye Dar es Salaam. Wakati huo huwanywi maji, hawachungwi na wamesimama mpaka wakifika wamekonda na wana afya mbaya. Nadhani Serikali ingebuni utaratibu mwingine wa kuwasafirisha vizuri, hawa ni wanyama hai wanahitaji huduma ambazo zinawafanya wakae katika hali nzuri wakati wakisafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu ni kuwa pawe na vituo, kwanza Shinyanga penyewe pawe na kituo, halafu Tabora, Dodoma mpaka Dar es Salaam ili kama kuna uwezekano katika vituo hivyo wapate maji ya kunywa kuliko kuwasafirisha kwa njia hiyo, ni mateso. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani kulikuwa na chombo cha kuzuia unyanyasaji au utesaji wa wanyama ambacho kilikuwa kinajulikana kwa jina la Kiingereza *Tanganyika Society for Prevention of Cruelty to Animals,* hata kumning'iniza kuku kichwa chini ni makosa, kumtumia ng'ombe kwa kulima mpaka akachubuka shingoni au punda kuvuta kamba mpaka akachubuka shingo ilikuwa ni marufuku na ukikamatwa miezi miwili jela.

Lakini sasa watu wanadiriki kuwabeba hivyo wanyama kwa kuwapiga, kuwachubua migogoni, kuwaning'iniza kuku vichwa chini, ng'ombe wakati analima anavuta mpaka shingo inachubuka mpaka nyama zinaonekana damu inatoka, huo ni utesaji wa wanyama. Sasa nalinganisha pamoja na ule usafirishaji wa mnyama ambaye ametoka maeneo mbalimbali kwa kuswagwa halafu aje awekwe kwenye njia ya reli, anasafiri siku 3,4 bila kunywa maji kwa kweli hayo ni mateso kwa wanyama. Naomba Wizara hii ifanye mpango wa namna ya kuwasafirisha wakiwa na hali nzuri, wafike salama, wasije wakakonda njiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba Mheshimiwa Lowassa kwa sababu kulikuwa na mradi wa Kiwanda cha Nyama Shinyanga, kiwanda hicho tangu mwaka 1975 kinajengwa hadi leo hakijakamilika. Naomba kama inawezekana safari hii kwa sababu tumepata mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria basi kile kiwanda kikamilishwe ili wakati mwingine tuwe tunasafirisha nyama kuliko usumbufu uliopo sasa. Naomba Kiwanda cha Nyama Shinyanga kikamilishwe ili kiweze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwa sababu ya kuwa na ng'ombe wengi katika Mkoa wa Shinyanga, naomba tuwe na minada ya Kitaifa ambapo mnunuzi anaweza kuja kununua. Ukichukulia Wilaya ya Bukombe kuna mnada mkubwa sana wa Bukombe ungechukuliwa uwe mnada wa Kitaifa. Kuna mnada mwingine Nhungumarwa, Wilaya ya Kwimba ni mnada mkubwa sana ambao unaweza kuchukua ng'ombe 500 mpaka 1000 kwa siku moja.

Kwa hiyo, watu wangekuwa wanakuja kununua ng'ombe pale ni vizuri sana. Kuna mnada wa Wilaya ya Kishapu ni mkubwa sana unaitwa Nhunze unafaa sana kuwa mnada wa Kitaifa. Vile vile Wilaya ya Meatu tuna mnada wa Bukundi ni mpakani mwa Shinyanga na Singida unachukua ng'ombe wengi sana. Badala ya kuswaga ng'ombe kutoka Meatu kwenda Arusha kwa wiki tatu basi watu wawe wanakuja kununua pale Bukundi na kusafirisha wao wenyewe wale matajiri wanaokuja kununua. Hilo litawezekana kama kweli jitihada hizi zitaonyeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kulikuwa na mpango mahususi wa malambo ambayo kwa kweli kwangu Wilaya ya Meatu, mawili yamekamilika, matano bado. Kuna lambo la kijiji cha Bukundi, Mwanjolo, Chambala na Nkhoma. Maeneo hayo ndio yenye wafugaji wengi lakini hawana mahali pa kunyweshea mifugo yao. Naomba Mheshimiwa Waziri alione hilo ili miradi hii aliyoianzisha imekamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Lowassa ni mtendaji mzuri na Naibu wake na watendaji wake wakuu basi haya mambo ambayo nimeyazungumza naomba yazingatiwe. Lakini bado namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa jitihada zake na napenda niishie hapo, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba niungane na wenzangu kutoa pole na rambirambi kwa wananchi wa Wilaya ya Mbeya Vijiji pamoja na Ulanga Mashariki kwa kufiwa na Mheshimiwa Kasapira na Mwalyego na Mungu ailaze mioyo yao mahali pema, amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Waziri, Edward Lowassa na Naibu wake, Anthony Diallo na Ndugu yetu Vincent Mrisho na wataalam wake wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na hotuba nzuri ambayo kusema kweli haina maneno, ime-*cover the whole country,* nadhani kila mji, kijiji, Wilaya kimeguswaguswa, kweli nawapa pongezi kwa kazi nzuri sana, sana. Wanapambana na uhai na suala zito la maji. Maji ni uhai kwa binadamu na mifugo kwa hiyo wanapambana na suala ambalo ni zito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kumpongeza Rais wetu Benjamin William Mkapa kwa kusaidia Wizara hii na kujitolea kwa kila hali. Ametimiza ile ahadi yake ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kwanza kabisa kwamba atajitahidi kuondoa matatizo haya makubwa. Ahadi yake ya kwamba ataunda Wizara hii ya Mifugo ndio sasa hivi tunaizungumzia, nampongeza sana Rais wetu kwa sababu amefanya kazi nzuri na Watanzania hatuwezi kusahau kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii ni ngumu sana. Mwaka jana wakati akisoma hotuba yake hii nilikuwa na furaha sana kwa kazi ambayo ilifanyika. Mwaka huu nina shida kubwa sana lakini yeye hakusababisha shida hii ni hali ya hewa.

Pale kwangu sasa hivi hatuna maji, mwaka jana mabwawa yote yalikuwa na maji, ng'ombe wanafurahi lakini mwaka huu hatuna tone la maji, binadamu hawafurahi, ng'ombe hawafurahi hali ni mbaya. Lakini sio kosa la Wizara ni hali ya hewa, mabwawa yapo lakini hayana maji. Juzi katika *ITV* mmeona jinsi sisi tunavyopata taabu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kibaya kuna mradi wa *World Bank,* nampongeza sana lakini watu wanavyohangaika na ukiambiwa kuna *World Bank* hapa utashangaa. Maana yake lile lidude likiwepo pale halafu unazungumzia *World Bank* halafu hakuna maji, hapo unapata matatizo. Kwa hiyo, naomba wataalam wakaangalie, kwanza hili jina la *World Bank,* kijiji kikishasikia Benki ya Dunia iko pale ni msisimuko mkubwa sana, Benki ya Dunia, *Washington DC* ndio iko pale halafu bado wanahangaika, lugha hiyo inakuwa ngumu sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnasema mwakani vijiji vyote ni Benki ya Dunia inachukua sisi ambao tumeshaanza utaratibu ni mzuri sana, wakiingia wanaingia na ma-*contractor,* wanaingia kweli ki-*World Bank,* ma-*tender* sijui manini hata kijijini huwezi kuelewa, yale makaratasi moja inakwenda *Washington* mpaka mradi upatikane, mpaka

hiyo *World Bank* uishike, ni kazi ngumu sana. Sio sawasawa na Mungai tukisema MMEM basi hela imeingia hapo hapo na kagawa vijijini ile bwana ina mikataba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kijiji changu cha Dosidosi sasa hivi wananunua maji Sh.300 kwa ndoo moja, wanalima na tumepata chakula lakini hatuna maji lakini kuna kijiji kilichoko karibu cha Suguta naomba Wizara hasa rafiki yangu kabisa yule wa maji washirikiane na Mwandisi wangu wajaribu kutafuta mashine ya haraka kuokoa, pale hakuna mboga tena, kuku unabandika ndio unajaribu kutafuta maji kidogo ya ugali yaani kiu ni kali sana, Dosidosi.

Mhandisi wangu wa Wilaya *Engineer* Mohamed Maghembe ni mfanyakazi hodari sana lakini akikuta ng'ombe 300,000 au 400,000 wanahangaika hakuna maji na binadamu amechanganyikiwa, kusema kweli naomba mkamsaidie, anachanganyikiwa Maghembe kutokana na shida ya maji iliyoko pale sasa hivi. Naomba Wizara ikashirikiane naye na kuona ni namna gani wanaweza kutatua tatizo hili maana ni maafa makubwa kabisa, sasa hivi tunapozungumzia maji Kiteto ni maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue hii nafasi kuwashukuru *Water Aid* kwa kazi yao nzuri. Wenzetu wa *Water Aid* wametufanyia kazi Njoro, Ndedo na wameokoa sehemu kubwa. Vile vile napenda niwashukuru Shirika la Swedish la *LAMP* kwa kusaidia miradi ya maji katika Wilaya ya Kiteto, wamefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo, sina haja kubwa, kama huu mradi wa Benki ya Dunia kila mwaka ukichukua vijiji 10 mpaka 20 *at least* Wilaya ya Kiteto au nchi nzima itakuwa na hali nzuri ya maji kama wataingia kwa nguvu zote. Tunamshukuru Rais pamoja na wataalam katika Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado tuna tatizo moja. Katika tatizo hili la mabwawa sisi bado hatujapata mabwawa. Nimeangalia takwimu hizi inatia motisha lakini hakuna Kiteto hapa sijui *World Bank* ndio imemeza na mabwawa, sina uhakika.

Naomba uongeze pesa ya mabwawa badala ya shilingi milioni tatu kwa kweli inatupa taabu sana, tupe kuanzia shilingi milioni 10 mpaka 15 kwa bwawa. Kuna mabwawa ambayo unachimba kwa milioni 200, 300 sisi hatujawahi kupata hiyo bahati lakini utuongezee fedha za mabwawa badala ya milioni 3 unaweza kusema ninachimba mabwawa 20 kwa milioni 3 hazisafirishi hata *bulldozer* unakwenda pale unafukuafukua tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna bwawa la Indrikish nimekuandikia ka-*note* nadhani umepelekea wataalam wako, lakini kuongezea nguvu. Indrikish nimekuta wananchi wametoa shilingi milioni 3, Halmashauri milioni 3 mimi nikatoa ahadi nikiringia katika Wizara yangu nikasema basi na mimi nitawaletea milioni 3 mpaka 4 sasa nimetoa, jibu hamjapata huko sasa nimetoa ahadi sijui ninyi wenyewe mtanifikiria namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo suala la maendeleo ya mifugo. Kwanza tatizo la malisho bado liko pale pale halina ufumbuzi, katika nchi hii hakuna *National Master Plan,* bado tuna matatizo. Sasa hivi hatujajua mfugaji yuko wapi, anatangatanga, hatujafanya *Master Plan* ya nchi yetu kwamba sio kila mahali unaweza kufuga, hapana lazima tugawe ardhi yetu kwamba hili ni eneo la ufugaji, hili ni eneo la kilimo tuwe *serious* huwezi kuchanganyachanganya namna hii. Kwa hiyo bado hatuna *Master Plan* ya hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la majosho, tunashukuru sana tumepata hiyo, tuna hakika kabisa tutakuwa na ufugaji mzuri. Baada ya kilio cha muda mrefu sana lakini Serikali imeweza kutusikia katika hili suala la majosho, tunaishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha nyama ni ajira, jengeni Shinyanga kiwanda kingine cha nyama nzito ili tuweze kupata ajira. Maana karibu 58% ng'ombe wanatoka kule wanatuharibia na soko huku waelekee kule na sisi tuelekee huku. Tujenge kule tena kiwanda. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ni ombi langu la kila siku, unywaji wa maziwa kwa watoto. Sisi tunatumia lita 33 Kenya wanatumia lita 84 kwa mtu kwa sababu ya watoto bado hatujawa serious na suala hili watoto wa shule wanywe maziwa tufikie na sisi lita 84, watu wazima hawawezi kung'ang'ania magudulia ni watoto ndio wanakunywa maziwa wapate afya.

Kwa hiyo, bado hamjaweka katika bajeti, leo ungekuja na bajeti kwamba maziwa kwa watoto wetu wa shule ni bilioni 2 au 3. Eeh, Waziri wa Watoto ananiangalia na Elimu yuko hapa na wote ni marafiki zangu, naomba sana mshughulikie suala hili. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sifa bado zipo kemkem, kazi ya Serikali ya Awamu ya Tatu ni nzuri, wala sina mabishano yoyote, hakuna Waziri ambaye amening'inia angani wa Mianvuli wote wameshatua na wanafanya kazi. Kwa hiyo, sitakuwa na maneno mengi lakini naomba uyazingatie mambo haya na pongezi tutakupa tena na tena na wote mmejitahidi na tutajihidi kushirikiana na wewe vizuri kabisa na uwe *aggressive* kama ulivyoanza endelea na nguvu hiyo usirudi nyuma pamoja na matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Musoma Mjini, naomba nitoe salamu zangu za rambirambi kwa familia ya ndugu yetu Comrade Kasapira ambaye tumempoteza katika Mkutano huu unaoendelea. Pia napenda nichukue fursa hii kuwapa pole Wapiga Kura wote wa Jimbo la Ulanga Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchawi kama nitajaribu kuzungumza tofauti na wachangiaji wote ambao wametangulia. Kwa hiyo, awali ya yote kabisa, naomba nichukue fursa hii kusema kwamba naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu kwa asilimia mia moja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli mbiu ya zamani wakati nikiwa kijana mdogo kuliko hivi sasa kwa sababu bado ningali kijana tulikuwa tunaelezwa kwamba maji ni uhai na sidhani kama kuna mabadiliko bado maji ni uhai na ni kauli ambayo itabidi tubakie nayo kwa muda mrefu mwingine. Nilikuwa najaribu kujiuliza hivi haya maji tukiwapa matajiri wachache wakayauza nadhani wengi tuliopo hapa tunaweza kufa. Nilikuwa sikusudii kuchangia kwenye Wizara hii lakini nikasema nichangie kwa sababu unapozungumzia uhai lazima uzungumzie maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama *speed* hii ya upatikanaji wa huduma ya maji ingekuwa imefanyika hivi kwa miaka 15, 20 iliyopita sasa hivi tungekuwa na maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Losurutia, amesema kitu kimoja sasa hivi kwamba Askari hawa wa Mianvuli hawajakwama juu ya miti wameteremka na wanafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ambazo zinachukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tatu chini ya uongozi wa Rais wetu kuhakikisha kwanza Watanzania wanapatiwa maji, kwa kweli kwa kipindi ambacho ndugu yetu Waziri wa Maji, Lowassa na *Deputy* wake wamefanya kazi kubwa ambayo kwa kweli lazima tuwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma hii ya maji ni muhimu lakini wasiwasi wangu ni kwamba bado gharama za uzalishaji ziko juu sana hasa kwa sisi ambao tuko mijini kwa sababu miundombinu mingi ni ya muda mrefu. Kwa hiyo, gharama za uendeshaji ni kubwa na zinapelekea upatikanaji wa maji kwa maeneo ya mjini kuwa ghali.

Kwa mfano ukienda pale Musoma watumiaji wengi wa maji ni pamoja na wastaafu, wazee vikongwe lakini unakuta gharama za maji ziko juu sana. Familia ya watu wawili, watatu kama wanaweza kudaiwa Sh.6,000 au 7,000 kwa ajili ya kulipia maji kwa mwezi nadhani kiwango hicho ni kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuliona hilo na kuuingia Mji wa Musoma katika mradi wa maji safi na taka. Nina uhakika mradi huu ndio utaweza kuondoa kero hii ya upatikanaji wa mji kwa bei kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ione kwamba hii ni huduma muhimu na baadhi ya makundi yakasamehewa kulipia maji au yakapewa unafuu fulani katika upatikanaji wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili iliyopita nilitembelea Namibia. Wakati nikiwa kule kulikuwa na Muswada wa sheria ambao ulikuwa unapelekwa kwenye Bunge la Namibia kwamba wale wazee wastaafu, vikongwe na walemavu waondolewe katika kundi la watu wanaostahili kulipia huduma ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri ikiwezekana tuangalie ni jinsi gani tunaweza kuwapa unafuu hawa wazee vikongwe na hata wastaafu. Kwa mfano hata wastaafu tunaweza tukawa na mpango wa kuwatoza kiasi ambacho si sawasawa na wale watumiaji wa kawaida angalau wapate unafuu kwa sababu tunasema maji ni uhai watu wa mjini lazima wapate maji kwa kuchangia watu wa vijijini unaweza kukuta dimbwi, kisima ukachota bila kuyalipia lakini kwa mjini lazima kulipia maji.

Kwa hiyo, kwa kundi hili la wastaafu, vikongwe na walemavu tunaweza kuangalia ni namna gani tunaweza kuwasaidia kupata maji kwa gharama nafuu au kuwaondoa kabisa kwenye kundi hili la watu ambao wanaweza kupata huduma hiyo kwa kulipia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupatikana kwa maji alizungumza mchangiaji mmoja hapa kwamba bado kuna maeneo ambayo Watanzania wanatumia maji ambayo si safi na salama. Sasa ni lazima kuwe na mpango madhubuti ambao utaandaliwa kwamba baada ya miaka kadhaa tuongeze kiwango cha ustaarabu wa Mtanzania kumtenganisha kutumia maji ambayo yananywewa na ng’ombe, maana kuna Watanzania ambao bado wana-*share* maji na mifugo. Sasa huu si ustaarabu kwamba binadamu bado anaendelea kutumia maji ambayo yanatumiwa na mifugo. Kwa hiyo nadhani tuwe na mkakati ambao utajaribu kuwaondolea Watanzania tatizo hili la kunywa maji yasiyo safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilikuwa napenda nichangie ni kwamba Wizara imefanya kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba kwenye maeneo ya Mjini zinapatikana mita, zinafungwa ili watumiaji waweze kutumia maji ambayo yanaweza kupimwa na wakadaiwa kiasi ambacho wametumia.

Lakini sijui kama Wizara ina taarifa kama kuna maeneo ambayo mita zimefungwa lakini bado watumiaji hawalipi kulingana na zile mita zinavyosomeka. Sasa nadhani hili ni tatizo kwa sababu kama tayari mteja amekwishafungiwa mita, nadhani halali yake ya kulipia maji ni kiwango kile ambacho kitakuwa kinasomeka kwenye mita na si vinginevyo. Sasa naiomba Wizara iliangalie hilo kwamba kama mteja amekwishafungiwa mita, basi alipie kiwango cha maji ambacho kitakuwa kinasomeka katika mita hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona mengi yamekwishazungumzwa na wenzangu, lakini nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa ahadi yake leo asubuhi kwamba atawawezesha wale wakazi wa Kata ya Makoko pale Musoma Mjini waweze kupata maji katika mradi ule wa maji ambao unapeleka maji katika kambi yetu ya Jeshi pale Makoko. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niseme kitu kimoja, Mheshimiwa Waziri wa Maji pamoja na Naibu wake nadhani wamezunguka sana kwenye nchi hii na kujua tatizo kubwa ambalo lipo ni maji na nadhani wanakuwa na upeo mkubwa wa kuelewa tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji katika nchi hii kwa sababu wamepita kwenye hizo sehemu na kujua jinsi tatizo lilivyo. Nadhani hiyo ingefanywa pia na Mawaziri wengine kwamba watembelee hii nchi waone matatizo ambayo Watanzania wanayo, maana tunaweza kuwa na Mawaziri hapa wamemaliza miaka mitano hawajafika hata nusu ya Mikoa ya nchi hii. Sasa watajuaje matatizo ya Watanzania! Lakini nasema huu mfano ambao wenzetu wameuonyesha ungeigwa pia na Mawaziri wengine kwamba watembee waone matatizo ambayo yanawakabili Watanzania, maana kwa sisi tukikaa tu Dar es Salaam na Dodoma haitakuwa rahisi kujua kwamba Watanzania wanakabiliwa na matatizo gani. Lakini leo ukichukua kitabu cha hotuba, utaona nchi nzima imeguswa. Sasa huu ndio Utanzania, kwa hiyo hatuwezi kusema kuna sehemu imependelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaposema kuna sehemu zina upendeleo hatusemi kwa sababu tunataka kumwonea Waziri anayehusika. Tunasema kwa sababu kweli upendeleo umo mle hata kwenye bajeti zao wanazotuletea hapa. Kwa hiyo mimi naungana na wenzangu kwa kweli kumpongeza sana Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi waliyotuletea kupitia hotuba yao na ni matumaini yetu kwamba mwaka kesho tutakapokutana hapa sehemu kubwa ya nchi yetu itakuwa angalau ina huduma kidogo kidogo ya upatikanaji wa maji safi na salama. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba haya ambayo tumeahidiwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri yatatekelezwa kwa kadri itakavyowezekana. Nami kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Musoma Mjini nawatakia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yao yote ya Wizara hii afya njema ili waweze kusimamia utekelezaji wa haya ambayo wametuletea hapa katika hotuba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kurudia kuunga mkono hoja hii na nawatakia kila la kheri katika kutekeleza mipango hii waliyotuletea hapa Bungeni. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuzungumza katika hoja ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuungana na wenzangu kwanza kutoa pole kwa marehemu Kasapira, Comrade mwenzetu ambaye ametuacha kwa masikitiko. Namwombea kheri Mwenyezi Mungu aiweke pema roho yake. *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisha napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Edward Lowassa, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wametuonyesha katika Wizara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ametumia vizuri sana mwavuli wake, ametimiza kauli ambayo ilitolewa na Rais wetu Mtukufu kwamba watendaji wake safari hii watatumia miavuli. Si yeye peke yake tu aliyetumia mwavuli wake vizuri, ni Wizara nyingi na Mawaziri wengine pia. Nasema hivyo kwa sababu Mawaziri ambao

wametumia vizuri miavuli yao wamefanya kazi nzuri ya kutekeleza sera za CCM na pia kuwapa unafuu Wabunge wenzao Wapinzani pamoja na wa CCM wanaposimama kutetea haki na kazi za Bunge hili mbele ya wananchi wanazungumza kwa ukweli, kwa kujigamba na kwa vitendo. Mfano, Waziri wa Maji amefanya kila njia, amefika kila Mkoa na kila sehemu amesambaza maji kwa kadri alivyoweza.

Hakuna anayeweza kila kitu, lakini naweza kusema kwamba karibu robo tatu ya nchi ametimiza. Kwa hali hiyo hata nikisimama kwa wenzangu nikitetea kazi ya Bunge nasema hamwoni maji katika sehemu fulani yamepatikana na kweli yapo. Nasema hamwoni simu zimepatikana katika sehemu ambazo simu zilikuwa hazipatikani, wanasema kweli mwavuli umeteua hapo.

Nikisema hamwoni wafanyakazi sasa hivi wanapata madawa katika hospitali kwa upande wa afya, wanasema kweli. Basi hao ni watu ambao wametumia miavuli yao kihalali. Si kwamba wengine hawakutumia, wote wametumia, hata wa Mambo ya Ndani, juzi silaha nyingi zimechomwa ambazo zingeachwa kwa maadui wangedhuru wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli wanastahili sana pongezi za hali ya juu lakini bado kama Wizara na sisi kama Wabunge lazima tutoe machache ambayo tunaona kwamba yanahitaji kutimizwa na Wizara hii. Mfano, maji upande wa Mkoa wa Dar es Salaam, tulikuwa tukitumia maji ya bomba kutoka Ruvu Juu na Ruvu Chini. Ni kweli katika hotuba yake amezungumzia kwamba kuna ukarabati wa mabomba makubwa, lakini napenda tu kuijulisha Wizara hii kwamba wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam wana matatizo makubwa sana ya maji pamoja na kwamba wamechimbiwa visima lakini angalia mkazi wa Dar es Salaam anakwenda kuchota maji sawasawa na mwanakijiji ambaye hana uwezo wa kupata mabomba, wapi na wapi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya nyuma kulikuwa na mabomba ambayo yanatoka Ruvu Juu mpaka Magereza. Sasa hivi Magereza Ukonga wanapata shida ya maji, wanatumia maji ya visima. Wananchi kutoka Buguruni, Vingunguti, Kipawa, Majumba Sita kwa wanajeshi na hata Gongolamboto, wakati watu walikuwa na mabomba ya maji, mtu anajivutia mwenyewe maji, sasa hivi maji hayo hayapo.

Mimi naiomba Wizara kwa sababu imesema yenyewe kwamba inafanya ukarabati wa mabomba makuu, basi waongeze tena nguvu kuweka mabomba ili wananchi wenye uwezo waweze kuvuta maji, watumie maji yaliyo salama ambayo tayari huwa yanawekwa dawa ndio yanawafikia walaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kuzungumzia habari ya maji ya chupa. Nimekuwa nazungumza ndani ya Bunge hili sasa hivi kwa mara ya pili, kuna maji ya chupa ambayo yanauzwa. Mara nyingi hasa Mkoa wa Dar es Salaam, maji mengi ambayo yanayouzwa yanaleta matatizo kwa wananchi, ugonjwa wa *typhoid* unatokana na maji haya ya uhai na nilishasema tangu mwanzo. Ni kweli si kana kwamba mwenye kutengeneza haya maji ya uhai ndiye anayesababisha *typhoid* lakini watu ambao wanapenda utajiri wa haraka haraka na kujipatia fedha kwa haraka haraka wanamwiga

utengenezaji wa maji. Hapa nimekuja na mfano wa chupa ili leo Mheshimiwa Waziri aone ninalolisema kwamba ni la hakika.

*(Hapa Mheshimiwa Mbunge alionyesha Bungeni vielelezo husika)*

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakwisha na *typhoid* watu wa Dar es Salaam. Ukilinganisha chupa ya uhai na chupa ya Afrika na chupa za Kilimanjaro. Muundo huu wa uhai nikimaliza natoa maji kwa njia ya sindano, maji yanatoka aliyoweka mwenzangu kama yalinywewa, chupa iko wazi, naichukua nakwenda kuchukua sindano na bomba lake naongezea maji humu kisha na-*seal*, nauza hayo maji. Mlaji anachukua anajua ni maji yaliyo hai na ukiiangalia chupa kweli imepita kwenye *TBS,* kwa hiyo mtu unakuwa na uhakika kwamba maji ni hai.

Lakini nakuthibitishia maji haya sio hai kwa sababu watu wanaiga na ukiyanywa mfululizo utapata typhoid. Kwa hiyo naomba hii Wizara iliangalie kwa makini. Sina ubaya na mtengeneza maji, lakini ajue hivyo na watu ambao wanafanya fujo kiasi hicho ni watu wa Buguruni. Kwa hiyo naomba mlifikirie ili muweze kuwasaidia wananchi hasa wa Mkoa wa Dar es Salaam na maji haya yamesambaa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nazungumzia na yale maji ya paketi, paketi zimezidi sana, aombwe mmiliki atumie vichupa vidogo vidogo. Tunazungumzia habari ya mazingira. Tunaposema mazingira si kwa Wizara ya Mazingira peke yake, vikaratasi au vipaketi vya maji ya sh. 50/= vinapomaliza kutumiwa vinasambaa ovyo, kwa hiyo uchafu unaongezeka na mazingira tunazidi kuyaharibu. Jambo lingine, naomba nizungumzie habari ya kuchimba malambo. Bahati nzuri mimi ni Mbunge wa Taifa, kwa hiyo huzunguka sana. Pamoja na ukulima wangu, lakini huzunguka pia kuangalia jinsi gani wananchi wanavyopata shida. Kuna shida sana ya maji. Kuna Mheshimiwa Mmoja amezungumzia hapa kuhusu jinsi wananchi wanavyo-*share* maji na wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi na macho yangu nimehakikisha na hasa atanisemehe Mheshimiwa Waziri, hasa kabila lake la Wamasai. Utawahurumia sana, utafikiri hawapo Tanzania pamoja na kwamba upande mmoja amefunika, upande mmoja ni wa CCM, upande mmoja ni wake, nasikia watoto wanachekesha hivyo, lakini nasema hivi naomba Waziri awahurumie wenzake, maji ameyapeleka huko anakoishi yeye lakini Dosidosi, Magungu, Kibaya Kiteto, Olukashmeti, Siza Kongwa na Matulangu Hogolo hakuna maji na malambo yaliyopo hapo nikieleza ukweli mtasikitika. Maji kwanza yanakauka, yanapatikana wakati wa masika, yakiisha masika punda ndio wanafuata maji karibu maili ishirini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu jiulize huyu mwananchi anaoga lini? Anaoga mara moja au mbili kwa mwezi kwa sababu ya kukosa maji, anahitajika kuoga lakini ataoga vipi. Malambo hayana maji ya kuhimili muda mrefu. Naomba tafadhali Mheshimiwa Waziri aliangalie hili, pamoja na kumsifu kote tunamsifu kweli kwa sababu mwavuli wake ameutumia, lakini si kweli kwamba utaona kila sehemu ukapajua wapi palipo na matatizo. Kwa hiyo, haya tunayozungumza naomba tafadhali uyafuatilie ili uweze kuwasaidia wananchi wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakwenda kwa upande wa majosho ya mifugo. Nashukuru mwenzangu pia hapa amezungumzia, zamani kulikuwa na majosho ya mifugo, kwa hiyo hata mwananchi hakuwa na shida, anajua siku fulani nitapeleka ng'ombe zangu kuosha, lakini sasa hilo halipo, wananchi wanapata shida.

Hizi dawa za kuoshea nyumbani kama utaosha labda ng'ombe mmoja wenye kufuga ng'ombe mmoja *(zero grazing)* mpaka ng'ombe kumi lakini wakizidi pale unategemea nini, zaidi utategemea kifo tu. Halafu hawa ndugu zangu Madaktari wanaokuja kutibia ndani ya nyumba zetu, gharama zao zinakuwa kubwa, anasema *labour* na dawa analeta. Hebu na hilo pia Mheshimiwa Waziri aliangalie kama kweli amekubali kutuletea ruzuku ya dawa ambazo zitatusaidia kwa magonjwa halisi ambayo yanawasumbua ng'ombe wetu au wanyama wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba habari ya madaktari aingalie kwa makini, ni kweli kabisa ukimwuliza kwa nini bei imekuwa kubwa, anasema ujue mama kuna *labour,* sijui kuna nini, sasa hiyo labour mimi mfugaji siijui. Kwa hiyo na hilo naomba pia mliangalie kwa sababu huyu mtu analipwa na Serikali au hiyo pia imeshabinafsishwa ndio maana mtu anataka alipwe *labour* yake kwa sababu hatapata mshahara kutoka Serikalini?

Naomba hilo liangaliwe ili kusudi liweze kusaidia wafugaji katika madawa kama nilivyosema, madawa ya ng'ombe na dawa za kuku, kwa sababu ninaposema habari ya madawa si ng'ombe tu, kuna ufugaji wa kuku pia, wananchi wanapata shida. Halafu unakuta kwamba kuku unawaleta wanakuwa na magonjwa labda toka wanakotoka, ukienda kuwanunulia dawa nako hivyo hivyo, huku umeshawanywesha Gombolo au umeshawanywesha nini. Naomba hilo nalo pia liangaliwe kwa ajili ya kusaidia ndugu zetu wanaofuga kuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, mimi nazidi tu kuipongeza Wizara hii kama nilivyosema, iendelee na kazi njema, lakini iangalie malambo. Kwa kweli malambo yanahitajika, Waheshimiwa wenzangu, wapo kweli binadamu wanaochangia maji na ng'ombe, punda, mbwa, wanakunywa humo humo na binadamu anakwenda kuyanywa. Sasa hilo naomba pia liangaliwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wa mawazo yangu. Awali ya yote naomba nitumie nafasi hii kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Mbunge wa Ulanga Capt. Kasapira. Namwombea Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Naibu wake pamoja na viongozi wote kwa kazi nzuri wanayoifanya kutumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba nitumie nafasi hii kutoa mchango wa mawazo yangu nikielekeza hasa kwenye eneo ambalo natoka. Kama walivyozungumza Mheshimiwa Losurutia na wengine, katika nchi yetu yapo baadhi ya maeneo ambayo kweli yana matatizo makubwa ya maji likiwemo eneo ambalo natoka Jimbo la Kishapu.

Jimbo la Kishapu ni kame na lina wafugaji, kwa mfano, katika Jimbo hilo tuna ng'ombe 163,734; tuna mbuzi 80,766; tuna kondoo 44,304 na vile vile Jimbo hilo lina jumla ya watu karibu 234,000. Sasa kama nilivyozungumza ni kwamba tatizo letu kubwa hapa ni upatikanaji wa maji.

Sasa nimesimama hapa kumwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie ili tuondokane na tatizo la maji. Yapo maeneo kwenye Jimbo langu ng'ombe wanakunywa maji mara moja au mbili kwa wiki kwa sababu ya tatizo la maji na si hilo tu hata ule upatikanaji wa maji yenyewe unachukua umbali hata wa kilomita nane kwa ng'ombe na binadamu. Sasa Mheshimiwa Waziri kwanza jambo hili linatuchelewesha hata katika shughuli zingine za kimaendeleo.

Kwa mfano, mtu kaamka asubuhi, anafuata maji kilomita nane, inamchukua muda mrefu kurudi, sasa hafanyi shughuli zingine isipokuwa maji tu. Sasa nilikuwa napenda nimwombe Mheshimiwa Waziri atusaidie katika eneo letu la Kishapu juu ya tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kulizungumza ni upande wa maji ya chumvi, *fluoride.* Mimi katika eneo langu moja la Mji wa Maganzo lina tatizo la *fluoride,* tulichimba visima vizuri na tunashukuru Wizara ilitupa mashine.

Baada ya kukamilisha uchimbaji, wataalam walivyokuja wakapima, waligundua kwamba maji yale yana *fluoride* na hayafai kutumiwa na binadamu. Tulijitahidi kuomba pengine tuweke ile mashine ili tuyatumie haya maji kwa shughuli pengine hata za ufuaji nguo na mambo mengine lakini tulizuiliwa, tukaambiwa mkifanya hivyo tutashitakiwa.

Sasa Mheshimiwa Waziri nadhani niliwahi kuuliza swali, nikaahidiwa kwamba Serikali itajitahidi kuleta mtambo wa kupunguza *fluoride* katika eneo hilo. Sasa sijajua kama Mheshimiwa Waziri atakuwa amejiandaa kunisaidia kwa hilo, lakini nilipenda kumwomba sana anisaidie katika suala hilo tumeshachimba kisima na hakitumiki kipo na mashine ipo lakini maji ndio yana chumvi na hayafai kutumiwa na binadamu.

Sasa kwa kweli inaniwia vigumu, pengine nimwombe Mheshimiwa Waziri kama kuna uwezekano basi anisaidie, wataalam hawa waje, aliniahidi wataalam kutoka Chuo Kikuu wataletwa ili mitambo inisaidie kunipunguzia tatizo hilo la *fluoride.* Huo Mji ni mkubwa, una watu wengi na una matatizo makubwa. Sasa kwa kweli namwomba sana Waziri anisaidie kwa suala hilo la mtambo wa maji ili wananchi wa eneo hilo waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka niombe kupitia Wizara hii nina eneo moja katika Tarafa yangu ya Mondo, kuna Kata moja ya Bubiki na Bunambiju. Maeneo haya yana tatizo kubwa la maji na si rahisi kuchimba visima vya maji na kupata maji kwa karibu, halafu hata unapochimba malambo maji yapo chini zaidi.

Sasa pengine kwa kutumia wataalam waliopo hapa, naomba Wizara ifanye utafiti na ijaribu kuangalia namna ya kusaidia wananchi wa eneo hili, wana tatizo kubwa sana la maji na tumejitahidi kwa njia zote kama kuchimba visima lakini haiwezekani. Lakini tunategemea kwamba kwa kutumia wataalam Waziri anaweza kutusaidia kwa kujaribu kuangalia namna ya kusaidia eneo hili ili liondokane na tatizo la upatikanaji wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka niliseme ni juu ya hii minada. Ipo baadhi ya minada ambayo sasa hivi imechukuliwa na Wizara hii. Kwa mfano, pale kwangu nina mnada mmoja wa Mhunze upo chini ya Wizara hii.

Lakini pengine nilikuwa nataka nishauri kwamba ni kwa nini Mheshimiwa Waziri minada hii asiiachie Halmashauri za Wilaya nazo zikaweza kujisaidia kwa sababu zina matatizo mengi na tunahitaji vile vile kwa kweli maendeleo, lakini kwa hali ya sasa ilivyo, pesa zote zinazopatikana katika hii minada zinachukuliwa na Wizara hii.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba pengine Mheshimiwa Waziri alifikirie hili na kama ikiwezekana basi aruhusu Halmashauri za Wilaya nazo ziweze kupata mapato ili kusukuma shughuli za maendeleo katika maeneo yetu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa kweli mimi sikuwa na maelezo marefu sana, naunga mkono hoja na nawatakia mafanikio mema katika utendaji wa kazi zao. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Katika kuweka rekodi sawasawa, tuna Wabunge wa Viti Maalum, sasa bado hatujapata Wabunge wa Taifa, kwa hiyo ni vizuri tuweke rekodi vizuri kwamba tuwe tunajua kuna Wabunge wa Majimbo na Wabunge wa Viti Maalum na Wateuliwa.

Tangazo lingine ni kwamba, tunafahamu Wizara hii inachangiwa kwa siku moja. Kwa hiyo wachangiaji ni wengi sana na wale waliochangia mara moja wamebaki saba, tunawaandika wote kwenye orodha, sasa itategemea wachangiaji watachangia kwa dakika ngapi baadaye jioni lakini ni saa moja tu. Kwa hiyo, tunaomba mumwaarifu Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa John Mwakipesile na Mheshimiwa Njelu Kasaka kama watawahi, wasipowahi basi tutachukua orodha hii hapa chini.

Baada ya matangazo hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni. *(Makofi)*

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia naomba kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kutoa pole kwa wananchi wa Wilaya ya Ulanga Mashariki na familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira aliyefariki wiki iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Naibu Waziri na timu yake nyote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kupunguza kero ambazo zilikuwa zinawakabili wananchi hasa wakiwemo wanawake. Kwa sababu wanawake ndiyo wanaohangaika kupata huduma za maji, lakini si hilo tu kuweza kutatua kero kwa wafugaji hasa kwenye kujenga mabwawa kwa ajili ya wananchi kuweza kunywesha mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ilikuwa na kero kubwa na kwa kweli nami naungana na wenzangu kwamba baada ya kuingia Mheshimiwa Edward Lowassa kwa kweli tumeona Askari Mwavuli ametua kweli na parachuti yake na tunayaona mabadiliko makubwa ambayo yametokea katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee upatikanaji wa maji Mijini na niangalie katika Miji yetu ikiwemo Manispaa ya Wilaya ya Iringa. Manispaa ya Iringa ilikuwa na shida ya maji sana, lakini kwa sasa hivi huduma zimeboreshwa maji ni masafi na vyanzo zimepanuliwa na ninaomba niwapongeze wafanyakazi wote wa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Manispaa ya Iringa, na nipongeze juhudi zinazofanywa na Wizara. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ametuonyesha na ninafahamu kwamba *feasibility study* imeshafanyika katika Manispaa ya Iringa ili kupanua mradi wa maji. Nina uhakika huo mradi utapanuliwa mapema ili wananchi wote waweze kupata maji safi na pia kuweza kuunganishwa kwenye mtandao wa maji taka. Nina uhakika kwamba Mheshimiwa Waziri atafanya hivyo haraka sana kabla hata ya kufika mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalopenda kuliongelea ni suala la elimu kwa watumia maji hasa uvunaji wa maji wakati wa mvua. Ninafikiri jambo hili pamoja na kwamba Wizara inalizungumzia linahitaji kutiliwa maanani na kuzingatiwa. Ni maji mengi sana yanapotea wakati wa masika tunapokuwa na mvua. Mkoa wa Iringa ulikuwa na mradi ambao ulikuwa unahifadhi maji hasa kwenye mitungi ambayo ilikuwa inajengwa kama matanki, ninaomba Wizara irudi ifufue utaratibu huu maji yaweze kupatikana ili kupunguza kero ya maji hasa wakati wa kiangazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia nimwombe Mheshimiwa Waziri aunganishe nguvu na mradi unaoendelea mashuleni wa kuboresha huduma ya elimu ya

msingi na huduma ya elimu ya sekondari ili pale elimu ya sekondari inapoboresha majengo basi uwepo utaratibu pia wa upatikanaji maji mashuleni. Kwa sababu watoto wanakunywa maji saa nyingine ya kwenye madimbwi, lakini kama tunaweza kuunganisha majengo yanayojengwa mashuleni tukaunganisha na huu mradi wa kuvuna maji ya mvua, shule zinaweza kuwa na matanki ambayo yanaweza yakahifadhi maji.

Lakini pia ukawepo utaratibu wa kuchimba visima virefu ambavyo vitakuwa na maji ya uhakika katika shule hizi kwa mwaka nzima na kupunguza kero. Kwa mfano, shule nyingine za sekondari unakuta watoto wanahangaika kutafuta maji nje ya shule. Kwa hiyo nafikiri pia huo ni utaratibu ambao unaweza kusaidia kuboresha huduma za maji kwenye shule zetu za msingi na shule za sekondari ili kuhakikisha kwamba tunapunguza matatizo ya magonjwa yanayoambukizwa kutokana na kunywa maji machafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie utunzaji wa vyanzo vya maji. Naipongeza Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa juhudi kubwa ambazo zinafanyika hasa kutumia Wiki ya Maji kutoa elimu kwa watumia maji, lakini pia kutoa elimu vijijini kuhusiana na utunzaji wa vyanzo vya maji. Ninaomba niiombe Wizara iendelee kusisitiza suala hili kwa sababu tumekuta mara nyingi watu wanalima katika vyanzo vya maji. Kwa hiyo elimu iendelee kutolewa juhudi ambazo Wizara inafanya iendelee nazo ili elimu iweze kuwafikia wananchi wote ili waweze kuelewa umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji na pia inaweza kuwa ni sababu kubwa inayofanya vyanzo vinakauka na kuleta matatizo ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, ninaomba sasa nizungumzie sekta ya mifugo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu nyote kwa kazi nzuri wanayofanya kufufua mifugo na kuweza kufanya Tanzania pia ionekane inauza nje mazao yanayotokana na mifugo, kwa sababu tuna mifugo mingi sana, lakini tumekuwa tunaitumia kwa kuweza kuonekana kwamba tuna mifugo lakini hatufaidiki nao. Nashukuru sana na kupongeza juhudi ambazo zinafanywa na Wizara kuhakikisha kwamba sasa wananchi wanafaidika na matunda ya mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninalopenda kumshauri Mheshimiwa Waziri ni kwamba aongeze majosho huko vijijini. Tatizo kubwa ni majosho. Wananchi wanahangaika kuogesha mifugo yao na saa nyingine wengine hawaogeshi matokeo yake mifugo yao inakufa kutokana na magonjwa. Kwa hiyo juhudi zinazofanywa sasa hivi ziendelee kufanyika ili kuhakikisha kwamba tuna sehemu za kuogeshea mifugo, majosho yale yanakamilishwa yanayokarabatiwa na mengine mapya pia yanajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la wataalam wa ugani. Naipongeza Wizara kwa mafunzo mbalimbali ambayo wameyatoa kwa wataalam wa ugani. Lakini ninaomba mafunzo hayo yaendane pia na vitendea kazi ili wataalam wa ugani waweze kufanyika kazi yao vizuri ni muhimu wawe na vitendea kazi vinavyoweza kuwafikisha kwenye maeneo mpaka ya vijijini. Naelewa kwamba kata nyingi zina wataalam wa mifugo, lakini unakuta saa nyingine kata ni kubwa sana mtaalam hawezi kuitembelea nyote kama hana usafiri wa uhakika.

Kwa hiyo, juhudi za kuwapatia wataalam vitendea kazi ukiwemo usafiri wa uhakika kama pikipiki lakini pia nyumba za kuishi ili kuwafanya waonekane na wao kwamba wana haki ya kuweza kuishi kama wafanyakazi wengine. Kwa sababu saa nyingine unakuta mtaalam anakaa kwenye nyumba ambayo kwa kweli hailingani na hadhi yake na inamkatisha tamaa katika kufanya kazi zake vizuri.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri hilo pia aliangalie na maslahi ya hao wataalam wa ugani ili waweze kutoa huduma vizuri. Lakini si hilo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Wizara kwamba ina utaratibu wa kuweza kufanya hizi kazi ziweze kufanyika kibiashara. Lakini wasiwasi wangu ni kwamba utaratibu gani umewekwa wa kuhakikisha kwamba wakianza kufanya shughuli hii kibiashara ni wazo nzuri, lakini utaratibu gani umefanywa wa kuwaandaa wao wataalam na kuwaandaa wananchi.

Mimi nilikuwa napenda niishauri Wizara kwamba ianze kuweka utaratibu. Kwa sababu itafika mahali utaalamu unaweza kuwa ni wa ghali sana kiasi kwamba mfugaji wa kawaida mwananchi aliyeko kijijini akashindwa kuweza kufaidika na huduma hiyo kwa sababu hawezi kumudu kumwita Daktari wa mifugo aweze kuihudumia mifugo yake. Kwa hiyo, Wizara iangalie utaratibu na ikianzisha huo utaratibu iweke kabisa gharama inayoeleweka kumtibu mnyama, ng'ombe, mbuzi, kwa ugonjwa huu gharama itaanzia hapa ili iweze kuelewe isije ikatokea huduma hiyo sasa ikawa huria na gharama zikawa kubwa sana na wananchi wakashindwa kumudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalopenda kulizungumzia na ambalo sikuliona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni jinsi ya kuwasaidia wafugaji wadogo wadogo ambao wako vijijini. Wafugaji kama akinamama wanaofuga kuku 10, 5 vijijini hawakuongelewa kwenye hii hotuba na hao ndiyo wengi. Inapofika wakati wa kifuku wengi mifugo yao hasa kuku wanakufa kwa magonjwa.

Sasa nafikiri tena amenifurahisha sana amewaweka wanawake hapa mbele kwenye *cover* ya hotuba yake, basi na humo ndani napenda awaangalie na mifugo yao midogo midogo. Uwepo utaratibu ambao Wizara inaweza kufanya hata mara wakati wa kutoa chanjo, basi wananchi wahamasishwe wale wenye kuku wachache kijijini wakikusanywa wakaambiwa kwamba tarehe gani wataalam wanakuja kutoa chanjo ya kuzuia kideri wafugaji wote wadogo wadogo wakusanye mifugo yao wote waweze kupewa dawa kwa wakati ule.

Kwa sababu sasa hivi tunahimiza kwamba akinamama wawe na mifugo midogo midogo, tunazungumzia akinamama wazee wanaolea watoto yatima hawawezi kufanya ufugaji mkubwa, wanaweza kuwa na huduma za kuku wa kienyeji au kuku wa asali ambao wachache, lakini inapofika wakati wa kifuku kuku wote wanakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri hawa nao pia awaangalie, asitizame tu hawa wafugaji wakubwa awaangalie na hawa walioko vijijini kwa sababu wengine hawana hata mbuzi wanao hao kuku na ndiyo wanaowategemea. Uwepo utaratibu wa kuhakikisha kwamba na wao huduma ya ugani inawafikia hasa kwa kutibiwa mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika kwamba haya yakiboreshwa mifugo kwa kweli itakuwa ina mchango mkubwa hapa nchini na wafugaji wa kawaida vijijini pia wanaweza kupata hizi huduma. Na kama nilivyosema kwamba utaratibu uangaliwe kwa kutoa huduma hii na kuweka utaratibu ambao itakuwa ni rahisi mtaalam wa ugani kuweza kufika kwenye ngazi kijijini kwa sababu saa nyingine siyo lazima hata hao wafugaji ninaozungumzia kwamba waweze kufikiwa inakuwa ni vigumu sana kuwafikia kama utaratibu mzuri hautawekwa wa kuweza kuhakikisha kwamba wanapata huduma za uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii pia itasaidia kama kutakuwa na utaratibu wa kuanzisha Ushirika wa Ufugaji wadogo wadogo ninaelewa kwamba kuna jitihada kubwa zinazofanyika za kuanzisha Ushirika. Lakini Ushirika huo unakuwa wa wafugaji wakubwa tu, tuangalie pia na Ushirika wa wafugaji wadogo wadogo.

Wafugaji wa ng'ombe wa maziwa, wafugaji wa kuku wa nyama na kuku wa mayai ili waweze kuwa na uhakika wa kuuza mifugo yao kwa kushirikiana. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili pia Wizara ilishughulikie watafanyaje ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na Ushirika tunazungumzia sasa ushirika wa mazao je, ushirika wa wafugaji wadogo wadogo huko vijijini tunawaandalia mazingira yapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuwepo na utaratibu wa kuangalia mazingira ambayo hao wafugaji wadogo wadogo wanaweza kuanzisha ushirika wao na huu utawasaidia hata akinamama walioko vijijini kuweza kuhakikisha kwamba mifugo yao ya kuku inaweza kuuzwa na pia suala la mbuzi wa maziwa. Nimeona kabisa jitihada kubwa imefanyika Mheshimiwa Waziri nakuomba sana ujitahidi kutusambazia mbuzi wa maziwa hao ndiyo wanaoweza kuwa ukombozi mkubwa kwa sababu wanawake wengi hawafugi ng'ombe, lakini mbuzi wanaweza kufuga.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninakuomba sana hili ulitilie maanani mifugo hasa mbuzi wa maziwa waweze kuenezwa vijijini na sasa hivi humu ndani ya Bunge Waheshimiwa Wabunge tunapiga kelele kuhusiana na lishe bora kwa wagonjwa wa UKIMWI ambao wanauguzwa majumbani. Kama Mbuzi wa maziwa watasambazwa vijijini wataweza kusaidia pia kuhakikisha kwamba lishe bora inapatikana kwa watoto lakini pia kwa wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile sipendi kugongewa kengele, ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia na fedha zote apewe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Kyela kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira kwa kifo kilichotokea wiki iliyopita hapa Bungeni. Wote tunaelewa Marehemu Capt. Theodos Kasapira alikuwa ni Mbunge mahiri, alikuwa ni Mbunge makini na alikuwa ni Mbunge ambaye alikuwa na mahusiano mazuri sana karibu na Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda na mimi kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo pamoja na wenzake wote katika Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Nimesoma hotuba yake Mheshimiwa Waziri kutoka ukurasa wa kwanza mpaka mwisho mchana wa leo na nikaona kwa kweli Kitaifa Mheshimiwa Edward Lowassa na Wizara yake wanafanya kazi nzuri sana. Lakini nilipokuwa natazama hali halisi ya maji katika Wilaya yangu ya Kyela nikaona kuna matatizo makubwa na mchango wangu utaelekezwa katika Wilaya ya Kyela kwa hali halisi ya maji ilivyo katika Wilaya hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kyela ni Wilaya ndogo sana kieneo. Ina ukubwa wa kilomita za miraba 1,350 tu, ina wakazi hivi leo 185,000, Wilaya ina mito minne mikubwa ambayo haikauki. Mto Songwe, Mto Kiwira, Mto Mbaka na Mto Rufilio na mito yote hiyo inatoka kwenye miteremeko ya milima ya Wilaya jirani Wilaya ya Rungwe, Wilaya ya Ileje na Wilaya ya Makete. Wilaya inapata mvua kwa wingi. Matatizo makubwa ni kwamba Wilaya hii ni tambarare ina matatizo ya kupata mafuriko kila mwaka kati ya mwezi Machi hadi mwezi Mei na wakati wa mafuriko kuna milipuko ya kila aina ya magonjwa kama vile kipindupindu, kuharisha damu, na magonjwa yote yako pale. Ndiyo maana kunako mwisho wa miaka ya sitini na mwanzoni mwa miaka ya sabini Serikali ya Awamu ya Kwanza ilijenga miradi mitano ya maji. Mradi wa *Kanga group* ambao ndiyo mradi muhimu sana katika Wilaya ya Kyela, Mradi wa *Ngana group,* Mradi wa *Sinyanga group*, Mradi wa *Ngamanga group* na Mradi wa *Makwale/Matema group.*

Sasa miradi yote hii ina sifa mbili zinazofanana. Sifa ya kwanza ni kwamba miradi imezeeka. Tangu imejengwa miaka ya sitini na mwanzoni mwa miaka ya sabini mpaka leo miradi imezeeka na huduma kwa miradi hii ni kama hakuna. Kwa hiyo, nusu ya maji ambayo yanatiririka katika bomba hizo yanapotea njiani hayawafikii walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Edward Lowassa mwaka 2002 alitembelea Wilaya ya Kyela. Nilifarijika sana kumwona na tulimpeleka vijijini akatazama kisima kimoja ambacho kimechimbwa na mradi wa *TASAF.* Halafu tukapeleka kutazama na kukagua mradi wa maji wa Makwale/Matema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachotaka kusema na kumkumbusha Mheshimiwa Waziri ni kwamba alipokuwa anazungumza na wananchi na hasa viongozi yeye mwenyewe alitamka kwamba Serikali hailali usingizi na itahakikisha kwamba mradi wa *Kanga group* unakarabatiwa. Sasa ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba huu mradi ni lazima ukarabatiwe kwa sababu ni mradi muhimu sana wa maji katika Wilaya ya Kyela.

Mradi wa *Kanga group* chanzo chake ni milima ya Wilaya ya Rungwe na unapita katika Kata sita za Wilaya yangu, Kata ya Ipinda, Kata ya Ikama, Kata ya Muungano, Kata ya Mwaya, Kata ya Kyela yenyewe na kata ya Kalinyumele. Kata zote hizo sita zina vijiji zaidi ya 80. Kwa hiyo, kama mradi huu utakarabatiwa basi inawezekana kabisa tutatatua tatizo kubwa la maji siyo tu kwa mji wa Kyela, lakini vilevile kwa vijiji 80 hivi ambavyo viko katika Kata sita ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisoma hiki kitabu katika ukurasa wa 142 ukurasa wa 140 ni Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira, sasa Kyela imetajwa ukurasa wa 142 Wilaya za Upanuzi Awamu ya Pili mwaka 2005. Ningependa Mheshimiwa Waziri anieleze huo mwaka 2005, je, ni miradi yote mitano ambayo nimeitaja itanufaika na programu hii au ni miradi mipya mingine ambayo Serikali imeibuni?

Ningependa kujua mapema kwa sababu hizi takwimu sasa siyo mali ya Wizara ni mali ya Taifa na ni mali ya watu wa Kyela na nitakwenda na hotuba hii kuwaeleza kwamba yale yote ambayo Mheshimiwa Waziri aliahidi alipokuja huku mwaka 2002 atayatimiza mwaka kesho mwaka 2005. Nikisema bila kuonyesha hiki kitabu watafikiri ni kampeni ya mwaka kesho. Kwa hiyo nitakwenda na hii hotuba na jinsi wanavyomuelewa Mheshimiwa Waziri wataamini, lakini ningependa hapa nielewe ni miradi ipi ambayo itakuwa *affected* katika programu hii. Kama ni miradi mipya au miradi hii hii itakarabatiwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa vilevile kuomba kuna mradi wa maji unaoitwa *Ngana group* huu mradi unahudumia Kata tano, Kata ya Ngana yenyewe, Kata ya Ikolo, Kata ya Bujonde, kata ya Ngonga na Kata ya Katumba Songwe. Lakini katika sehemu hii kumejitokeza Mji mdogo wa Kasumulu, miaka 10 iliyopita huu mji mdogo haukuwepo. Ni Mji mpya mpakani mwa Malawi. Miaka 10 iliyopita Kasumulu ilikuwa inakaliwa na siyo zaidi ya familia 100 leo ina wakazi zaidi ya 15,000. Sasa maji ya mradi huu ambayo yalitakiwa yatiririke kutoka kwenye chanzo cha milima ya Ileje yaende kuwahudumia wananchi katika Kata hizi tano ambazo nimezitaja yamedakwa na Mji mdogo wa Kasumulu. Hayafiki huko kwa wananchi. Ni maendeleo mazuri kwa sababu Mji mdogo umepanuka na unakua, lakini umeleta tatizo kwa mradi huu wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu na hili linatoka kwenye sakafu ya moyo wangu, ninamwomba Mheshimiwa Waziri alichukue. Ombi langu ninaiomba Serikali ituchimbie kisima kirefu cha kisasa pale. Wilaya ya Kyela haijapata kuchimbiwa hata kisima kimoja miaka 10 iliyopita. Mheshimiwa Eliachim Simpasa ana bahati alichimbiwa pale mpakani Tunduma. Lakini nasikia kuna kata zake kule Msangano sijui kunaitwa nini kule, hakuna maji hata kidogo. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri ombi

langu hilo ulichukue hata ukidanganya kwa maneno napo nitaridhika. Ulichukue nipate kisima pale ili watu wangu wa Kata hizo tano nilizozitaja wapate maji na mji mdogo wa Kasumulu upate maji. *(MakofiKicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ombi la pili ambalo linafanana na hilo ni kupatiwa kisima *bore hole* pale mjini Kyela. Kwa sababu ninaamini kabisa huu mradi ambao umetajwa katika hotuba yako unaweza ukachukua miaka mitatu, minne *on the short term* nakuomba sana nipatiwe *bore hole* kisima cha kisasa mjini Kyela ili wananchi wangu wafaidike.

Hivi sasa wanapata matatizo makubwa sana. Kwa hiyo, narudia maombi yangu makuu ni hayo. Kisima pale Kasumulu na kisima cha kisasa ambacho kitasambaza maji Mjini Kyela. *(Makofi)*

Mwisho, Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nataka nikwambie kwamba katika Wilaya ya Kyela lugha ya majosho hakuna, tumesahau. Miaka 10 iliyopita tulikuwa na josho katika kila Kata, leo Wilaya nzima hatuna josho hata moja. Lugha ile haipo katika Wilaya ya Kyela. Ni ombi langu la tatu kwako na unanielewa mimi Mheshimiwa Waziri inaweza ikapita miaka mitatu, minne nisikusumbue kwa lolote sina tabia ya kusumbuasumbua Mawaziri.

Lakini kwa hili visima hivyo viwili na kufikiria kuleta majosho katika Wilaya yangu ya Kyela ni maombi matatu ambayo nimeweka mbele yako na nimeyaweka mbele ya Serikali yote ninaamini kabisa kwa jinsi ninavyokuelewa kwamba ni msikivu utanisaidia hayo maombi yangu matatu.

Mimi sina tabia ya kuzungumza maneno mengi hasa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambaye ninajua ni mchapakazi. Kwa hiyo ninakuomba sana hayo niliyoyazungumza uyazingatie na nitaendelea kushirikiana na wewe katika yote ambayo yatakuwa mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. NJELU E.M. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie. Nami nichukue nafasi nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na timu yake yote. Sikutazamia kama ningepata nafasi hii nilifikiri nimeshakosa, lakini kwa kuwa nimeipata basi nitaitumia kwa kusema machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nizungumzie katika sekta mbili hizi. Katika sekta ya mifugo nilipokuwa naangalia takwimu toka hotuba ya mwaka jana na hotuba ya mwaka huu inaonekana kwamba katika upande wa afya ya mifugo ambapo magonjwa hasa yanayoenezwa kwa kupe udhibiti wake ni kwa njia ya kuogesha mifugo.

Lakini nilipokuwa naangalia takwimu alizozitoa Mheshimiwa Waziri mwaka jana inaonyesha kwamba katika majosho 2050 katika nchi nzima yalikuwa kama asilimia 23 tu ndiyo yanayofanya kazi mengine yote hayafanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa naangalia zaidi takwimu hizo ilionyesha kwamba katika baadhi ya Mikoa ambako kuna ufugaji mkubwa sana hali ilikuwa mbaya. Kwa mfano, Shinyanga katika majosho yote ilikuwa asilimia 8 tu ndiyo yanayofanya kazi na Mkoa kama Singida ni asilimia 9, Mkoa kama Mbeya ambako mifugo mingi imehamia hivi miaka ya karibuni lakini majosho yaliyokuwa yanafanya kazi ilikuwa kama asilimia 27.

Sasa hiyo ilikuwa inanipa picha kwamba eneo la kudhibiti magonjwa kwa upande wa sekta ya mifugo ilikuwa bado ni hafifu sana na kwa kuwa katika Wizara yake na kabla ya hapo katika Wizara ya Kilimo na Mifugo wakati ule.

Suala la kwamba washirikishe sekta binafsi lilianza kuzungumzwa toka mwaka 1996/1997 na mpaka leo bado sekta binafsi haijaingia kikamilifu katika ku-*own* na kuendesha majosho ya kudhibiti magonjwa ya mifugo. Je, Serikali inafikiri bado sera ya kushirikisha sekta binafsi katika eneo hili la kuendesha majosho ina mafanikio au haina mafanikio.

Ningependa Serikali wajaribu kufanyia *review* kwa sababu kama sera ukishaianzisha baada ya miaka 7 karibu miaka 10 bado haijaonyesha mafanikio unajiuliza je sera bado inaonyesha mafanikio au itakuja kuwa na mafanikio siku moja au ndiyo tumekwama. Kwa sababu mpaka leo uuzaji wa mifugo nje ya nchi, uuzaji wa nyama nje ya nchi umekuwa ni hafifu kutokana na kwamba mifugo yetu inakabiliwa na magonjwa mbalimbali na kwa hiyo haiwezi kupata soko nchi za nje. Bado sekta moja, eneo moja ambalo ingeweza kuboresha zaidi hili la kuhakikisha kwamba majosho yanakuwepo na mifugo inakogeshwa. Sasa kwa kuwa hakuna mafanikio katika eneo hili kwa nini msilifanyie *review* na kwamba Serikali yenyewe ijiingize kikamilifu katika kusaidia kuboresha na kuendesha au kuzipa nguvu Halmashauri za Wilaya ili ziweze kuendesha vizuri majosho ya kuogesha mifugo. Hilo nilitaka nizungumzie.

La pili, katika eneo hilo hilo ni kwamba katika takwimu ambazo amezitoa Mheshimiwa Waziri uzalishaji wa nyama, hasa nyama ya ng'ombe bado ni kidogo sana. Tani alizozieleza mwaka 2000/2001 ilikuwa tani kama 182,000 na ziliongezeka kidogo kufika 2003/2004 ilikuwa inakisiwa kwamba ingezalisha tani 184,000. Hii ni ongezeko la kama asilimia 1.6. Katika nchi yenye mifugo mingi 17,000,000 ya mifugo bado inazalisha nyama tani 184,000 tu. Kuna nini, kikwazo ni kitu gani? Nilitaka nijue kikwazo ni nini. Inaonyesha ni ulaji hafifu wa nyama ama watu wa Tanzania hawana mazoea ya kula nyama. Asubuhi ulipokuwa unawasilisha hotuba yako Mheshimiwa Waziri ulisema Watanzania wanakula kilo 10 tu za nyama kwa mwaka badala ya kula kilo 50 kwa mwaka. Je, hii inatokana kwamba nyama haipatikani ama watu hawana tabia ya kula nyama au watu ni maskini kiasi kwamba hawawezi kumudu kununua nyama?

Mheshimiwa Waziri suala hili labda mliangalie kwa kulinganisha na hali ya umaskini wa wananchi wetu. Tunapozungumza kwamba wananchi wetu wana hali mbaya hawana kipato cha kutosha nadhani inaweza ikajieleza au ikajionyesha kwa jinsi ambavyo wanashindwa hata kumudu kununua nyama inayopatikana hapa nchini kwetu. Kwa hiyo, nalo ni vizuri kwamba mnapoangalia mambo haya muangalie kikwazo ni nini na kwa nini wananchi wetu hawawezi kula nyama ya kutosha. Ni umaskini au nyama yenyewe haipatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka pia niongelee suala la malambo. Katika Wilaya yangu ya Chunya ambako mifugo mingi imekuja kutoka mikoa ya Kaskazini. Tunakabiliwa na tatizo kubwa sana kwanza mgongano kati ya wafugaji na wakulima, ambao inawezekana kwamba maeneo yale machache yenye maji ndiyo ambayo wananchi wakulima wanakwenda kulima mazao hasa wakati wa kiangazi na wafugaji ndiko wanakopeleka mifugo yao kwenda kulisha. Matokeo yake kumetokea mgongano mkubwa kati ya wafugaji na wakulima hasa katika Bonde la Songwe kwa ujumla. Sasa sisi tuliamua kuwahamisha hawa wafugaji kuwapeleka katika Nyanda za Juu ambako kuna maeneo ya kutosha hawakuweza kutokea mgongano kati ya wafugaji na wakulima. Kweli hali ni nzuri. Lakini eneo hilo linakabiliwa na mambo mawili makubwa. La kwanza kuna upungufu mkubwa sana wa maji. Tuliomba Serikali ijitahidi tuchimbe malambo makubwa matatu katika maeneo hayo ili kupunguza tatizo la maji na kuwawezesha wafugaji tukishawaelekeza huko waende wakatulie wafanye shughuli zao za kufuga mifugo yao.

Lakini la pili katika Wilaya Chunya maeneo mengi yana mbung’o. Kulikuwa siku za nyuma tulianzisha wa kuondoa mbung’o katika eneo la Wilaya ya Chunya hasa katika eneo la Luika. Lakini mradi ulikwishakufa siku nyingi na nimejaribu kuulizia hapa ni lini mnaweza mkaufufua tena ili kuwawezesha wafugaji wanaofuga mifugo yao iweze kukaa kwa usalama na wao waweze kutulia katika maeneo yao. Wanashindwa kutulia kwa sababu kwanza wanakosa maji, lakini la pili pia magonjwa yanayoambukizwa na mbung’o yanakuwepo. Lakini hatuoni dalili zozote au Serikali kuchukua hatua zozote za kuliondoa tatizo la maji kwa kujenga malambo makubwa na pili kuondoa mbung’o ambao ndio wanashambulia hiyo mifugo.

Kwa upande wa malambo tunashukuru kati ya mwaka juzi na mwaka jana tulipata fedha kidogo ya kujenga vilambo vidogo vidogo. Vitatu katika hivyo vimeshika maji lakini hivi vingine vimeshindwa. Mengine yameshindwa mengine yamebomoka. Sielewi kwa nini yalijengwa halafu yalipopata maji yakabomoka. Inawezekana ama fedha zilikuwa kidogo mno ama ujengaji ulikuwa hafifu ama si fedha yote ilikwenda kujenga hayo malambo. Labda wamejenga kidogo yalipopata maji yamebomoka. Lakini kuna malambo kama matatu hivi ambayo ndiyo yanatoa matumaini kwamba yanaweza kuweka maji na kuwapatia mifugo yetu maji. Ninachoomba kwa kweli Mheshimiwa Waziri ni suala zima la kutupatia fedha tujenge mabwawa yale ambayo tunapendekeza yajengwe katika eneo la Mpembe Mapogoro kule na bwawa lingine upande wa Mbangala. Haya ndiyo maeneo tuliyoyatenga kwa ajili ya kuweka mifugo ambayo imeingia kwa wingi katika Wilaya yetu ya Chunya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la maji kwa ujumla kwa binadamu. Nilikuwa nimemjulisha Waziri alipokuja mwaka 2002 alikuja kutembelea Wilaya ya Chunya. Alipokuwa pale mjini Chunya tulimpeleka kumwonyesha eneo letu tunapopata maji kwa ajili ya Mji wa Chunya, *Water Supply* ya Chunya. Pale tunacho kisima kimoja ambacho kisima kimoja ambacho kinafanya kazi na tulikuwa tumeomba tupate kisima cha pili ili kiwango cha maji yanayopelekwa kwa wananchi wa Mji wa Chunya kiweze kuongezeka na idadi ya watu imeongezeka sasa hivi sasa. Kiwango cha maji nacho kiongezeke.

Sasa tangu tulipoongea na Waziri na akatuahidi kwamba suala hili atalishughulikia kwa kupitia kwenye bajeti hatujapata bado fedha za kuwezesha kuweza kuchimba kisima cha pili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunakuomba sasa utupatie hizo fedha au uanzishe utaratibu wa kupata fedha ili kisima kiweze kuchimbwa na Wilaya ya Chunya ipate maji na wananchi wetu wapate maji.

La pili katika eneo la maji ni Kijiji cha Matwiga. Mwaka 2001/2002 nilikuwa nimeomba hapa kulikuwa na mradi wa maji wa zamani ulioanzishwa na *World Bank* na baadaye wakaacha. Kwa hiyo eneo lile halina maji na walikuwa wameanza kujenga bwawa katika Mto Mkowiji ukasema ungetuma wataalamu. Kwa kweli Wizara ilituma wataalamu wakaenda eneo hilo wakaangalia na walipochunguza mwaka uliofuata wakatenga shilingi 3,000,000 kwa ajili ya kufanya uchunguzi zaidi kwa lengo la kulifufua hilo bwawa lijengwe upya ili liweze kuwapatia wananchi wa Kata za Matwiga na Mtanila maji kutoka kwenye lambo hilo. Lakini mpaka sasa ninapozungumza Mheshimiwa Waziri hakuna hatua nyingine iliyochukuliwa tangu wakati ule.

Mwaka juzi uliniambia ulikuwa unatenga fedha kwenye bajeti lakini baadaye zile fedha hazikuweza kuonekana na sasa hivi nilikuwa naangalie kwenye bajeti hii ya sasa hivi labda nimeangalia haraka haraka sijaona mradi wa Mto Mkuwiji kwa ajili ya Kata ya Matwiga. Ningeomba na lenyewe liingizwe katika programu zako. Wananchi hawa kwa miaka zaidi ya 20 huu mradi umesimama na wa maji wanapata kwa shida sana kwenye visima mbalimbali. Kama haiwezekani kupata lile bwawa basi tupatiwe fedha ili visima vichimbwe vya kutosha katika Kata hiyo kuondoa tatizo ambalo linawakabili wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipenda pia nisisitize kwamba tuna bado Vijiji vingine vingi licha ya Kata ya Matwiga lakini tuna matatizo katika Kata za mbugani, Kata ya Chalangwa, Kata ya Chokaa na Kata ya Makongolosi ambako pia tunahitaji kuchimba visima kwa ajili ya kuwapatia wananchi wetu maji. Niliwahi kusema mwaka jana hapa hali ya maji katika Wilaya ya Chunya itazidi kupungua kwa sababu mvua katika miaka ya karibuni tangu wakati wa *el-nino* Wilaya ya Chunya haijapata mvua ya kutosha ili kujaza hata mito. Mito yenyewe haijai vya kutosha na baada ya mvua kumalizika mara tu mvua ikishamalizika miezi michache baadaye mito huwa imeshakauka.

Kwa hiyo, hata kiwango cha maji yaliyoko chini ardhini nayo inazidi kuteremka chini. Tunahitaji kupata visima virefu kwa ajili ya kuwezesha wananchi wetu wapate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namwomba Waziri aingize Wilaya ya Chunya kwenye programu zake za kuipatia visima vya maji vya kutosha na tuanze kuchimba. Tunachotaka najua programu zimekuwa zikitokea mara kwa mara visima hamchimbi. Mwaka jana mlipima visima saba mlipata site saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka hizo *site* saba zianzwe kuchimbwa sasa tupate vile visima saba. Mwaka jana mmepima *site* moja pale katika Kanisa la *Roman Catholic* pale Lupa Tingatinga tunachotaka tu ni kwamba maeneo hayo yachimbwe vipatikane visima ili wananchi wetu waondokane na adha ya kufuata maji kwenye mito, maji ambayo usalama wake ni hafifu ambayo pia si masafi sana kama ambavyo tungependa wananchi wetu wayapate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa kengele imegonga nilipenda na mimi niyaseme haya nimtakie kila la kheri Waziri na nimpongeze kwa kazi nzuri anayofanya aendelee kuifanya kwa bidii hivyo hivyo na hatimaye na sisi tupate visima ambavyo tumeviomba hasa kwanza akija pale Mjini Chunya ambapo kuna matatizo ni makubwa sana hivi sasa. Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi nataka niungane na wenzangu Wabunge kutoa rambirambi kwa familia, ndugu na wapiga kura wenzetu ambao wametutoka hivi majuzi, Mheshimiwa Yete Mwalyego pamoja na Mheshimiwa Theodos Kasapira na tuwaombee wote Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema peponi. *(Amin)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nataka nitamke kuanzia sasa ya kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Lakini pia nataka nitumie nafasi hii kumpongeza kwa mambo makubwa manne. Sisi pamoja na mwenzangu Kasaka tulipokuwa Wizara ya Kilimo na Mifugo wakati huo hali ilikuwa si nzuri. Haikuwa nzuri kwa sababu kubwa. Kwanza lazima niwapongeze *TRA* kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kukusanya mapato. Mapato ya nchi hii yameongezeka ndiyo maana tunaweza kufikia mahali fulani tukamwambia Waziri tunaomba tuongezewe kisima, tufanyie hili na hili.

Wakati huo Mheshimiwa Kasaka akiwa Naibu wangu mapato tulikuwa tunakusanya ilikuwa ni bilioni 28 tu, ukilinganisha na mapato ya hivi sasa ni bilioni 100 na zaidi. Hivyo lazima niipongeze Serikali, Waziri wa Fedha utupelekee salamu kazi nzuri inafanyika na *TRA* hata kusema haya tuliyonayo. *(Makofi)*

La pili, nataka kusema nimpongeze Mheshimiwa Lowassa kwa jinsi anavyotumia vizuri vyombo vya habari. Nalisema hilo kwa sababu Lowassa popote atakapokuwa

utamsikia. Akienda Ulaya Lowassa utajua, akija Sumbawanga utajua na hii ndiyo kazi ya Uwaziri lazima tujue wanafanya nini. Mimi nakupongeza kwa sababu kuna baadhi ya Wizara kweli unaweza kukaa hata miezi miwili husikii wanafanya nini.

Lakini kwa ajili ya utaratibu tu ni mimi nadhani tulipokuwa tunazungumzia, Mheshimiwa Rais alipozungumzia ya kwamba anateua Baraza la Askari ya Miamvuli alikuwa na maana tuwasikie wanateremka mahali popote, vijijini, mijini na akawasaidia akawapa magari ambao tunasema ndege za ardhini *VX*. Kwamba saa yoyote kukitokea tatizo tusikie Waziri yuko pahali fulani. *(Makofi)*

Mimi ningeomba Waheshimiwa Mawaziri Watanzania wangependa kujua kila Wizara inafanya nini. Najua jitihada ambao kila Wizara inafanya na nawapongeza Mawaziri wanafanya lakini wengi hatujui wanafanya nini. Ndiyo maana wananchi kila wakati wanasema kwamba mbona hatujamwona Waziri huku, mbona tunamsikia kwenye kongamano tu au kwenye mikutano. Lakini ni kazi nyingi tunaomba kazi hizo zijulikane kwa wananchi ili wananchi sasa wajue kila Wizara inafanya nini katika maendeleo yake. *(Makofi)*

Tatu, nataka nimpongeze Mheshimiwa Lowassa kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kuhakikisha matumizi ya maji ya Ziwa Victoria hayaleti mgogoro tena katika nchi hii. Tulikuwa na kigugumizi kikubwa sana lakini pamoja na jitihada yake ametufikisha mahali ambapo mimi naridhika kwamba kazi nzuri imefanyika mpaka sasa wakubwa wame-*salendar* kwamba sasa yaanze kutumika. Hongera sana kwa kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mwisho katika shukrani zangu ni kazi nzuri ambayo nilikuwa nimeiomba katika kikao cha bajeti kilichopita. Nilimwomba Mheshimiwa Waziri, nakumbuka na Mheshimiwa Namkulala aliniunga mkono hoja ya kuanzisha Mfuko wa Maji wa Kitaifa. Mwanzoni nilisita kwamba hivi kuna nini na nilikuwa bado nataka kuleta hoja nyingine ili mfuko huu uanzishwe lakini leo sikufichi umenifurahisha baada ya kuona kwamba mfuko huu sasa unaanzishwa rasmi na naomba wadau tushirikiane ili kuweza kuhakikisha unafanikiwa. *(Makofi)*

Mimi nina bahati nimezunguka sana ilizidi kunitisha kwa sababu taarifa ambayo hata Waziri amezungumzia katika kitabu chake ni kwamba hali ya maji si nzuri. Inazidi kupungua. Maji yanazidi kuteremka na kuwa chini zaidi kuliko utaratibu ambao tulizoea. *Surface water* itakuwa haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kipindi cha miaka 20 hali inakuwa mbaya na tukiendelea kutegemea wahisani watusaidie kila kazi hatufiki popote wana *agenda* zao. Ndiyo maana katika suala la ujenzi wa barabara tuliamua kuwa na Mfuko Maalum wa Barabara. Ndio maana tunaanza kufanikiwa kaitika shughuli za Barabara kwa sababu tuna mfuko wetu ambao tunaweza kuringia wakituwekea kigongo pale tunajua mfuko wetu utafanya kazi hiyo.

Ndiyo maana nikasema Mfuko wa Maji ni lazima tuwe nao kwa sababu utatufikisha mahali fulani sasa baadhi ya miradi ile ambayo tunaona ingekwama hata hiyo ya Victoria wanaweza kutuwekea ngumu usipokuwa na mfuko utakuwa ndio mwisho. Lakini mfuko utatukwamua.

Mimi nina imani kabisa huu ni mwanzo mzuri na mimi nimefurahi kwa sababu bajeti iliyopita ilinitisha. Mheshimiwa Waziri uliposema kwamba kulikuwa na miradi 794 kama nitakumbuka ambayo imebaki ni *pending* na inahitaji shilingi 43,000,000 ili iweze kukamilika na ukatoa taarifa ya kwamba miradi ambayo kwa kweli inaendeshwa na Wizara yako sasa ya maji na kadhalika imepata shilingi 37,000,000,000 kama nakumbuka mwaka jana. Lakini kati ya 37,000,000,000 zilizopatikana 34,000,000,000 ni za nje, sisi tumetoa 1.2 bilioni.

Sasa kama unategemea nchi ikupe 1.2 bilioni wengine ni wahisani siku wakisema hatutoi ndiyo mwisho wa programu zako. Sasa hilo ndilo naomba kwa kweli tulikazanie. Mfuko uanze na mimi Mheshimiwa Waziri nimekwishaanza kuandaa utaratibu ambao utasaidia ili kufanikisha na tutashirikiana kama ulivyokuwa umeniomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nizamie pale pale kwangu Sumbawanga Mjini. Mimi nimekuwa Mbunge wa Sumbawanga Mjini kwa vipindi viwili. Lakini nimekuwa Mbunge wa Bunge hili kama *front bencher* kwa vipindi zaidi ya vitatu au vinne. Lakini *front bencher* una *limit* yako. Tukipata nafasi na sisi ndio tunasema tukiwa huku.

Sasa yako mambo ambayo nilitaka Mheshimiwa Waziri anisaidie. Mji wa Sumbawanga unapata maji yake kutoka vyanzo vya mito saba. Tuna mito saba pale Sumbawanga midogo sana na mito hiyo ndiyo inatuwezesha kupata maji pale Mjini Sumbawanga. Wakati wa masika wakati wa mvua mito yote hiyo saba inatusaidia kupata mita za ujazo za maji 6,000 kwa siku. Mahitaji ya Mji wa Sumbawanga ni mita za ujazo 8,000 kwa siku.

Lakini wakati wa kiangazi ndiyo tatizo linaanzia hapo. Mito yote hiyo ina uwezo wa kutoa mita za ujazo 2,500 tu ambao ni robo tu hakuna *source* nyingine. *Source* nyingine tuliyonayo katika Mji wa Sumbawanga ni visima ambavyo vimechimbwa vidogo vidogo. Kuna visima pale Mjini kama 18. Vile athari yake kwa sababu kama unachimba katikati ya makazi ya watu hujui kitu gani kinaingia katika visima hivyo. Ndiyo maana tukamwomba Mheshimiwa Waziri aone uwezekano wa kutusaidia.

Mwaka 1998 Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu akiwa Waziri wa maji alikuja Sumbawanga. Tukazungumza naye na akaona tatizo hilo akaahidi kwamba atatuchimbia angalau kisima kimoja kama kianzio. Mpaka leo hakuna kisima. Tumeendelea tukaambiwa kuna Wachina wamekubali kuanzisha mradi maalum pale Sumbawanga wa kusaidia katika kuhakikisha kwamba sasa tunakuwa na mtandao unaofahamika wa maji katika Mji huo. Programu hiyo hatuelewi imeishia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2001mpaka 2003 tumekuwa tukipata taarifa ambazo zipo katika taarifa ya bajeti ya Waziri ya kwamba ilikuwa sasa tusaidiwe na *Africa Development Bank (ADB )* kusaidia Mji wa Sumbawanga kupata maji na uhakika wa mtandao. *(Makofi)*

Lakini mwaka jana tukaambiwa kwamba *ADB* kwa ajili imehama kutoka Makao Makuu yake ya zamani imehamia kwingine mradi wote utasita kidogo mpaka hapo baadaye. Sasa nini maana yake? Hivi kweli tuendelee kungoja *ADB*. Ndiyo maana nimesema Mheshimiwa Waziri hawa wahisani wakati mwingine tukiwategemea sana baadhi ya miradi yetu inaweza kukwama kwa sababu ambazo watazitoa wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa kujua Mheshimiwa Waziri anisaidie kujua hivi hatma yake sasa ni ipi. Nini hatma ya *ADB* kusaidia Mji wa Sumbawanga, hilo la kwanza. La pili katika misingi hiyo tulikuwa na mradi wa *NORAD*. *NORAD* walikuwa wanasaidia katika Mkoa wa Rukwa suala zima la visima na vyanzo mbalimbali vya maji.

Lakini tangu waondoke ni muda mrefu. Ule mradi ulianza mwaka 1975/76. Tangu waondoke Sumbawaanga katikati hatuna msaada wowote. Na Vijiji vinavyozunguka Mji wa Sumbawanga kwa ujumla viko 25. Mji wa Sumbawanga *proper* una Vijiji 25 ambavyo vinazunguka mji wenyewe. Na Vijiji hivyo vilikuwa na miradi mizuri sana *NORAD* walihakikisha kwamba vinapata navyo huduma ya maji sawa na Mjini.

Lakini katika hali ya mazingira ya sasa hatuna. Hivyo nakuomba Mheshimiwa Waziri uone namna ya kusaidia pia Vijiji ambavyo vinazunguka Mji wa Sumbawanga ambavyo havina msaada wowote, Havina Mhandisi wa Maji kwa sababu Mamlaka ilipoanzishwa pale Mjini Sumbawanga ikaonekana Mhandisi na wataalamu wake wanashughulikia zaidi pale Mjini kuliko Vijiji vinavyozunguka mji huo. Sasa tukasema tuombe tuone namna ya kuwasaidia hao ambao wanazunguka maeneo hayo.

Sasa ili kutekeleza hayo mimi nilikuwa na maombi matatu. La kwanza Mheshimiwa Waziri nakuomba uendelee na jitihada yako ya kuhakikisha kwamba tunapata vyanzo vingine vipya vya maji katika Mji wa Sumbawanga. Ombi la kwanza. La pili, utusaidie kuchimba angalau visima vitatu au vinne tunahitaji visima vitano kwa Mji wa Sumbawanga na ni mji peke yake katika Tanzania unaokua haraka sawa na Dar es Salaam. Ni mji unakuwa haraka kuliko miji yoyote ni Sumbawanga hivyo mahitaji yake ya maji yatakuwa ni makubwa zaidi. Tuombe uwezekano wa kupata msaada wa kuchimbiwa visima angalau vitano kama itawezekana.

La tatu, utusaidie kufufua miradi ile ya *NORAD*. Ambayo *NORAD* walikuwa wameanzisha. Tunajua kwamba uwezo wetu ni mdogo sisi hatuwezi lakini tuna imani kabisa sisi tungeweza kusaidia kwa msaada upande wetu lakini pia na upande wa Wizara mkatusaidia. La nne, ni kusaidia tupate Mhandisi wa Maji atakayeshughulikia specifically kwa Vijiji vinavyozunguka mji wa Sumbawanga. Utatusaidia ili tuwe na

uhakika kwamba kweli Mhandisi atakuwa kazi yake ni kuangalia nini kifanyike katika Vijiji vinavyozunguka mji ambavyo viko nje ya mamlaka yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nataka nikuombe ya kwamba ikiwezekana tuendelee kukuomba Mheshimiwa Waziri uone uwezekano sasa wa kuhakikisha kwamba huu utaratibu wa Mamlaka za Maji ambao tumezianzisha katika Miji yetu ya kugharamia kila kitu pamoja na mishahara ya watumishi wao tujaribu kuangalia upya kwa sababu kama hali ya maji itakuwa namna hiyo katika Mji wa Sumbawanga mapato yake yatatoka wapi. Tutapata wapi fedha za kuwalipa hao. Tungeomba mliangalie hili kuahirisha uamuzi huo tuangalie baada ya kuchimba visima hivi vitakavyokuja kutusaidia.

Mwisho nataka nitumie nafasi hii kuwapongeza wataalamu wako wote. Wataalamu wako *they are doing very good job* wote wa Mifugo na wa Maji kwa sababu mimi walio wengi tumefanya nao kazi. Lakini *speed* sasa ambayo wanakwenda nayo imenivutia sana naona hata vituo vyetu na Vyuo vya Mifugo vinaanza kuchangamka kidogo, mambo yanakwenda vizuri.

Kinachotakiwa tuwape kila aina ya *encouragement* wafanye kazi yao vizuri. Na wale wanaostaafu watafutiwe angalau miradi ya kuwa *keep busy.* Wanaostaafu ningeomba ndio uwasaidie katika kugawa zile dawa ambazo tunazileta kwa ajili ya kutibu magonjwa ya mifugo huko Vijijini wapate nafasi na wenyewe washiriki katika kusukuma maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Nikutakie kila la kheri Mheshimiwa Waziri lakini usitusahau Sumbawanga tatizo la maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nakushukuru sana. Labda nianze kwa kutoa rambirambi zangu kwa niaba ya Wapiga Kura wa Kigoma Mjini kwa kifo cha Ndugu yetu Comrade Kasapira, tunaomba Mungu ailaze pema peponi roho ya Marehemu wetu. *(Amin)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mengi nimejaribu kumwandikia tu Mheshimiwa Waziri kero zetu kubwa. Napenda tu niseme naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Naelewa kabisa kwamba sasa hivi Wizara hii kwa kweli iko tayari kupambana na tatizo la maji na nadhani ni uamuzi sahihi. Sasa mimi kwa Kigoma Mjini niseme tu kwamba tatizo letu kubwa ni umeme lakini tungependa Wizara hii itusaidie jamani tupate matanki ya ziada ili suala la kupampu maji lisije kuwa ndio nguzo kuu ya upatikanaji wa maji Mjini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika takwimu alizotoa Mheshimiwa Waziri hapa imeonekana dhahiri kuwa sasa hivi upatikanaji wa maji Tanzania umekuwa kutoka asilimia 68 mpaka 70 na kidogo. Pale kwangu Kigoma Mjini tuna wateja 6,000. Tukichukua wastani wa watu hata kama ni 8 kwa sababu Kigoma ndio wanazaana zaidi

kuliko mahali popote pengine. Utakuta kwamba ni watu 48,000 tu wanaopata maji ya uhakika na Mji wetu una watu 145,000.

Sasa ningesema kwamba pamoja na nia nzuri ya takwimu hizo lakini kwa mji wangu ni kuwa sisi tunapata maji kwa kiwango cha chini ya asilimia 50. Tunadhani si kosa la Wizara hii kwa kweli ni tatizo la umeme kwa sababu kama hakuna umeme maji hayapatikani na wananchi wanaendelea kuteseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme vile vile jambo moja ambalo amezungumzia Mheshimiwa Kimiti nalo ni muhimu sana. Katika zoezi hili la kuwahamisha wafanyakazi kutoka Wizarani kwenda kwenye Mamlaka. Pale Kigoma Mjini wafanyakazi 23 wa Bodi ya Maji wamekataa kujiunga kwa sababu wana wasi wasi kwamba wanaweza wakakosa mishahara yao kwa vile Bodi ya Maji haina kipato cha kutosha.

Habari nilizozipata ni kwamba wameandikiwa barua tayari waondoke na kwa kweli sasa hii inawatia wasi wasi waende wapi. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri tuliangalie hilo na tuangalie vile vile matatizo ya uchafuzi wa vyanzo vya maji Kigoma Mjini kama *TANESCO* wanaendelea kumwaga mafuta hata kama umeme haupo, Magereza na Polisi, naomba Serikali itusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa msaada wako na mimi niweze kuwatetea ndugu zangu wa Kigoma Mjini. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ABDULKARIM E. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nitoe shukrani zangu kwa niaba ya wananchi wa Mafia kwa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na kumpongeza sana Waziri Mheshimiwa Edward Lowassa, Naibu Waziri Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu na wasaidizi wake pamoja na Wakurugenzi wa Idara zake zote na watumishi wote wa Wizara na Idara zake kwa jitihada kubwa wanazozifanya katika kuhakikisha kuwa tatizo kubwa la maji linaondoka au kupungua hapa nchini na hasa vijijini ambako Watanzania walio wengi ndiyo wanapoishi na ndiyo wanaopata shida kubwa sana na kupata maji safi na salama. Mwenyenzi Mungu awabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Wizara pale alipofanya ziara Mheshimiwa Anthony Diallo, Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo katika Wilaya ya Mafia katika vijiji vya Jibondo na Juani na kutuahidi kutupatia fedha za ukarabati wa Malambo ya vijiji hivyo na tunashukuru kuwa fedha hizo tulizoahidiwa tulizipata shilingi 5,000,000/= *Alhamdulillah.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitoe shukrani kwa Mkurugenzi wa *DDCA* Dr. Mohammed, kwa kuonyesha nia ya kutusaidia wananchi wa Wilaya ya Mafia hasa katika Kijiji cha Jibondo kwa kutukubalia kuchimba visima vitatu katika eneo la

chemchem kwa ajili ya kuandaa mradi mkubwa wa kuvusha maji hayo kutoka Kijiji cha Chemchem hadi Kijiji cha Jibondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana niongeze kwa kuiomba Wizara pale inapokua na miradi katika Mkoa wa Pwani basi sisi Wabunge tunaomba tupewe taarifa za kimaandishi. Hii ni sababu kubwa sana ambayo mimi binafsi huwa inanitia wasiwasi mkubwa maana miradi mingi inapokuja pale Kibaha Mkoani Pwani basi huishia pale pale au katika Wilaya zilizokua karibu na Kibaha sisi Mafia huwa ni taabu sana kuipata miradi hiyo. Hivyo tunaomba msaada wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchunguzi uliofanywa na Wizara mwaka 2003/2004 katika Wilaya ya Mafia basi Wizara ihakikishe kuwa utafiti huo unafanyiwa kazi na unatekelezwa pia hasa katika kuboresha mipango ya kuupatia mji mdogo wa Kilindoni maji ya uhakika ili wananchi wote wanaoishi katika mji mdogo huo wapate huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nawashukuru na kuwapongeza pia Idara ya Mifugo lakini bado Mafia tunahitaji Mitamba ya ng'ombe wa maziwa na sasa basi watuletee pia na mbuzi wa maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja ya Wizara hii mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Mafia tunaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. LAWRENCE. M. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi ya kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna, Wakurugenzi na watendaji kazi wote waliosaidia kwa njia moja au nyingine na kufanikisha hotuba hii ya bajeti. Mpangilio wa hotuba ni wa kisayansi. Hongera sana kwa Serikali ya Rais Mheshimiwa Benjamin Mkapa, kama kweli kuna askari wa mianvuli basi nataka kumpasha Mheshimiwa Waziri kwamba yuko katika orodha yangu maana anaamua na kutenda. Hongera na naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 42 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kuhusu mradi wa maji wa Songea Mjini ni kweli unaendelea vizuri kwa kufuatana na ratiba. Wananchi wa Songea Mjini pamoja na Mbunge wao wana wasiwasi na kusema kwamba bila ujenzi wa Bwawa kuu kama ndiyo chanzo kikuu cha maji katika milima ya Magoro, mradi huu unaweza usiwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mradi huu ni msaada sio mkopo, tumamwomba sana Mheshimiwa Waziri awaombe wafadhili wakubali kulijenga Bwawa hilo kama awamu ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukataji, uchomaji wa miti na misitu una mahusiano na swala la maji. Tabia hii ni lazima sasa ukomeshwe. Nashauri sasa ianzishwe Idara itakayoshughulikia uchomaji na ukataji ovyo wa miti na misitu na vyanzo vya mito. Sheria ambazo zinahusu mambo hayo zipitiwe upya na kurekebishwa.

**MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa jinsi Wizara ilivyojitahidi na kuhakikisha huduma ya maji imeboreshwa. Pia pongezi kwa wafanyakazi wa Idara ya maji jinsi wanavyowajibika kikamilifu na kutupunguzia adha, taabu mbalimbali ikiwemo ankara za maji na usomaji mita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia yafuatayo:-

Kwanza maji safi ya kunywa, wananchi wengi wameshapata mwamko juu ya umuhimu wa maji safi kwa matumizi ya kunywa. Kwa hali hiyo, wananchi wengi wa mijini wameanza kutumia maji ya kunywa yanayouzwa madukani yakiwemo *Kilimanjaro, Africa, Cool Breeze,* Safi, Uhai na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo inasemekana ya kwamba baadhi ya haya maji si salama. Inasemekana baadhi yanachimbwa kwenye visima ambamo kuna madini mengi yanayochanganyika na maji na si mazuri kwa matumizi ya kunywa au kupikia. Maji hayo yenye madini yakiwemo yale ya Jina la Uhai, Masafi na mengineyo. Naomba Wizara inihakikishie ukweli huo ili tubaini yapi yanaweza kununuliwa kwa kunywa na pia kwa yale ambayo hayafai Wizara ina mpango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, eneo la Manzese kuna hali nzuri kiasi kwamba mabomba ambayo kwa muda wa miaka kadhaa yalikuwa hayatoi maji, sasa angalau yanatoa mara nne kwa wiki, na wananchi wamefurahishwa na hali hiyo. Ni matumaini yangu itafikia hatua wakazi wa maeneo hayo wapate maji siku zote za wiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, eneo la *Mbezi Beach,* tatizo la mabomba yaliyopasuka bado ni mbaya na inasababisha uharibifu wa barabara. Nashauri Wizara itoe maelekezo ya kuwezesha idara zake husika ziwe na ratiba ya kufanya *visits* kwenye sehemu mbalimbali ili kukagua mabomba yaliyopasuka barabarani na kuyafanyia matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya maji ya Mto Rufiji na Mto Kagera katika miaka ya 1977 kulianzishwa Shirika liitwalo *Rufiji Basin Development Authority (RUBADA)* ambalo hadi sasa wanajengo kubwa la ghorofa liko Ubungo karibu na Benki ya *NBC.* Shirika hili lilipewa jukumu la kuendeleza bonde la mto Rufiji kwa ajili ya kilimo cha kumwagilia. Wafadhili wa awali walikuwa ni Serikali ya Iran. Je mradi huu uliishia wapi? Tatizo la kukwama ni nini? Na lile jengo kwa sasa linatumia kwa kazi gani? Wafanyakazi wa *RUBADA* hatma yao ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nijibiwe kuhusu *Kagera Basin Development Authority* ambayo ilianzishwa kwa Mantiki kama ya *RUBADA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Bajeti hii, ila naomba kujibiwa hayo niliyochangia.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Sekta ya Maji na Mifugo.

Pili, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wote kwa kazi nzuri ya kutoa huduma kwa wananchi. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia maeneo yafuatayo: Sekta ya Maji, kwanza napenda kuishukuru sana Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kwa kuvipatia huduma ya maji vijiji vya Igoji II (Isalaza), Sazima, Berege, Chisayu, Mazae. Vijiji hivyo hivi sasa vinapata huduma ya maji na tayari *pump* zimeshaletwa na kufungwa katika vijiji vya Sazima, Berege na Chiseyu. Kijiji cha Igoji II (Isalaza) na Mazae wanapata huduma ya maji ya mtiririko *(Gravity Scheme)* kuhusu kuchangia mifuko ya maji Wilaya ya Mpwapwa hadi sasa wamechangia mifuko ya maji shilingi 20,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi watunze miradi hiyo wasitarajie Serikali/Benki ya Dunia kuendelea kukarabati miradi hiyo na miradi yao na wao ndiyo wanufaikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi waendelee kuchangia mifuko ya maji kama Sera ya Maji inavyosema. Wananchi watunze vyanzo vya maji ili maji hayo yasikauke. Pia napenda kuishukuru Serikali kwa kuwa na mpango wa kuboresha huduma ya maji. Mpwapwa Mjini na Vinghawe. Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa wameonyesha nia ya kusaidia mradi huo kwa gharama ya shilingi milioni 700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji katika Mji wa Mpwapwa na Vinghawe limeathiri sana maendeleo ya mji huo zikiwemo Taasisi mbali mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya mifugo, kwanza napenda kuishukuru Serikali kwa kuvikarabati vituo vya utafiti wa mifugo Kanda ya Kati, Mpwapwa na kukipatia vitendea kazi lakini bado lipo tatizo la upandishwaji vyeo, hata hivyo watumishi wengi wamepandishwa vyeo, bado wachache ambao Serikali ingekamilisha kuwapandisha vyeo na kurekebisha mishahara yao na hii inahusu watumishi wote wa Kituo cha Utafiti wa Mifugo Kanda ya Kati, Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa *(VIC)* Mpwapwa na Chuo cha Mifugo *(LITI)* Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuishukuru Serikali kwa ukarabati wa Chuo cha Mifugo Mpwapwa na kuanzisha kozi mbali mbali za Astashahada na Stashahada za Mifugo. Naomba ukarabati huo uendelee ili Chuo hicho kiwe na mazingira mazuri ya kusomea/kujifunzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa yapo magonjwa ambayo yanaweza kuzuilika kwa kuogesha mifugo kama vile *Anaplasmosis, ECF, Heart Water, Babesiosis,* magonjwa haya yanaweza kuzuilika kama mifugo itaogeshwa, nashauri Serikali iweke

mikakati kukarabati majosho ili mifugo iweze kuogeshwa. Mkoa wa Dodoma una majosho 123 ni majosho 33 tu ndiyo yanafanya kazi na 90 hayafanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vya Afya ya Mifugo *(Veterinary Centres)* ni muhimu sana kwa tiba na chanjo ya mifugo hasa vijijini. Mkoa wa Dodoma una vituo vya afya ya mifugo 34 na vyote havifanyi kazi lakini kama vituo hivyo vingefanya kazi nzuri ya kuzuia magonjwa kama vile *Anthrax* ambao ni ugonjwa hatari unaoweza kuambukiza mifugo na binadamu *Anthrax is a communicable disease, anthrax is a contiguous disease, anthrax is a Modifiable disease,* unaweza kuzuilika na kutibika, pia vituo hivi vingeweza kutumika kuzuia chanjo na tiba, magonjwa mengine ya *Black quarter, FMD, CBPP, Worms (Tameness paginate) file.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu zinazofanya majosho yasifanye kazi ni kwanza, ukosefu wa maji kwa baadhi ya maeneo, pili, bei kubwa ya madawa ya kuogeshea na tatu, mwamko mdogo wa wafugaji katika suala zima la kuunda ushirika wa wafugaji kuhusu uogeshaji wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri iliyoifanya kwa muda mfupi tangu ianzishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingi zimwendee Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Edward Lowassa, Naibu wake, Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Geita, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kupata angalau mwanga wa mji wa Geita kupatiwa maji ya Ziwa Victoria. Hii imetokana na majibu ya swali langu la tarehe 16 Julai, 2004 ambalo niliuliza kuhusu kupatiwa huduma ya maji katika mji wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alitamka wazi kuwa Mji wa Geita utapata maji kabla ya kumalizika mwaka 2005. Wananchi kwa ujumla wamefurahi sana kupata taarifa hizo za ujio wa maji katika mji wao. Naiomba Serikali itekeleze ahadi hii kama ilivyoahidi, kwa kuwa wananchi wanafuatilia kwa karibu sana suala hili la maji katika mji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia shida waliyonayo wananchi wa Geita Mjini ambao idadi yao ni zaidi ya 50,000 na huduma ya maji wanayoipata ni visima kumi na moja tu, visima hivi havitoshelezi matumizi ya wananchi hawa. Naomba kwa unyenyekevu mkubwa Serikali iuangalie mji huu kwa kuwa umevamiwa na watu kutoka sehemu mbalimbali kuja kutafuta ajira katika mgodi wa Dhahabu uliopo mjini Geita. Kutokana na idadi kubwa ya watu walio na wasio kuwa na kipato, kumejenga matabaka hivyo kuwa na tabaka kubwa la watu wasiokuwa na uwezo wa kununua maji ambayo yana bei kubwa sana mjini Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri wakati akijumisha taarifa yake asisahau Mji wa Geita kuupatia maji kwa kutenga fedha kutoka sehemu yoyote katika mafungu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono asilimia mia moja hotuba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii japo namwomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi wa mambo yafuatayo:-

Kwanza, ni kipindi cha zaidi ya miaka mitatu sasa wananchi wa Mji wa Bukoba tulielezwa kuanza kwa mradi mkubwa wa maji ambao ungeendeshwa na Kampuni ya Kifaransa *(AFD)*. Ni kwa nini kumekuwepo na ucheleweshaji wa namna hiyo na mradi huo unategemea kuanza lini na kama inavyoeleweka uwezo wa ujazo wa *Tank* za maji zinazotumika kuhifadhi na kusambaza maji kwa ajili ya wananchi wa Mji wa Bukoba ni mdogo ukilinganisha na idadi ya wakazi wa miji inayokua kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, mradi huo utarekebisha hali hiyo kwa kujenga *tanks* kubwa zenye kukidhi haja ya sasa na mtazamo wa siku za mbele?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya chanzo kunakochukuliwa maji kwenye Ziwa Victoria kwa ajili ya matumizi ya wakazi wa Mji wa Bukoba iko karibu na mahala ambapo upo mkondo wa maji machafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ina hatarisha afya za watumiaji maji kwani katika hali halisi upo uwezekano mkubwa kwamba maji wanayotumia ni machafu mno. Kwa nini Serikali isihamishe *pump* na kuziweka sehemu nyingine na hasa tukizingatia ukweli kwamba Ziwa Victoria lina maeneo mengi ya kuwekwa *pump* tofauti na zilipo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri anifafanulie ni kwa nini Mamlaka ya maji Mji wa Bukoba imeamua kuanza kuwatoza watumiaji maji gharama za maji kwa kutumia taratibu za *flat rate* hata kama watumiaji hao wameshafungiwa mita za maji na zinafanya kazi. Namwomba Mheshimiwa Waziri aitolee tamko hali hiyo kwani imewakanganya watumia maji wa mji wa Bukoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikipewa ufafanuzi murua wa mambo niliyoyaainisha hapo juu nitaiunga mkono hoja ya Waziri kwa nguvu zangu zote. Nawasilisha.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Lalamiko langu kila mwaka ni usambazaji maji katika Jimbo langu na Wilaya ya Mbozi kwa ujumla. Wahisani wa dhehebu la Konde la KKKT walikwishatoa msaada wa maji ya kutiririka Iyula, mradi ambao ungekuwa kwa manufaa kwa vijiji nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahisani wameahidi kutoa shilingi milioni 800 na wamefanya upembuzi na kukamilika kwa michango ya wananchi wote wanategemea kunufaika na mradi huo. Wahisani wanadai zinahitajika shilingi milioni 1600. Suala hili nimelifikisha Wizarani na Mheshimiwa Waziri amekuwa akiniahidi kuwa *World Bank* inakubali kugharamia. Tumewahamasisha wanavijiji wote kuwa na mfuko wa maji na wamefanya hivyo na wanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri sioni maelezo yoyote kuhusu mradi huu ambao wananchi wameusubiri kwa muda sasa. Naomba Mheshimiwa Waziri anifafanulie ili wananchi waeelewe utaratibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewahamasisha sana wananchi kuhusu ufugaji wa kisasa Wilayani Mbozi na umeanzishwa ufugaji na uuzaji mazao ya mifugo kwa pamoja na usindikaji wa siagi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwamba sioni msisitizo wa Wizara ili kuwapa moyo waliojiunga na kuwapatia wataalam ili kuboresha zao la mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri anisaidie maelezo ya ufasaha hasa dhamira ya *World Bank* katika kufanikisha mradi huu. Naunga hoja mkono kwa moyo wangu wote.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa na Wasaidizi wake kwa ushirikiano wao mzuri unaoipa Wizara taswira ya mafanikio na kupiga hatua kubwa katika mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kukubali kuukarabati mradi wa maji Kamachumu ambao kwa kipindi kirefu ulikufa kabisa. Nami naiomba Wizara ikishirikiana na TAMISEMI, Halmashauri ya Wilaya ya Muleba isimamie utunzaji wa Mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia katika mpango wa awamu ya pili ya maji na usafi wa mazingira vijijini *(Rural Water Supply and Sanitation Programme)* itakayoanza 2005 katika Wilaya ya Muleba, Vijiji vifuatavyo vipewe kipaumbele ambavyo ni Nyakashenye (Mahutwe), Izigo, Katoke (Izigo), Buhaya, Kagoma Mjini (Kagoma), Kata nzima ya Rushwa iliwahi kuwa na mradi wa maji Omurunazi ulioharibiwa na kufa kwa mradi wa Vijiji nchini, naomba urejeshwe maana eneo lenyewe lina miamba, watu na mifugo wanapata shida ya maji safi, Kishiro, Ngenge, Rwigembe, Rutoro (Ngenge), Mradi wa Bulyakishajui pia urekebishwe na kukarabatiwa ili uenee kote maana yapo maji ya *gravity* hapa, Makongora, Ruhanga, Mafumbo (Ruhanga).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaoishi katika Visiwa vya Bumbire na Goziba pia wasisahaulike. Visiwa vina wakazi wengi lakini hawana huduma nzuri ya maji. Watu hutumia maji ya Ziwa ambayo si salama kwa afya. Naomba walau vijiji

vitano viangaliwe katika mpango huo, napendekeza vijiji vya Kerebe, Makibwa (Goziba) na Iroba, Amushenye na Kituo (Bumbire).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ranchi za Misenyi, Kitengule na *Kikuhula Complex* yakishapimwa na kutengwa katika maeneo madogo madogo, wananchi wanaokaa humo wapewe umuhimu wa kwanza. Aidha, suala zima kwamba, Ranchi hasa Misenyi ziko mpakani lizingatiwe ili ulinzi na usalama wa mipaka yetu lisiachwe kwa watu binafsi. Nashauri pia wananchi wazalendo wapewe umiliki na uendeshaji wa Ranchi za mipakani. Serikali izitazame kwa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kuhusu ongezeko la ukataji miti na kasi ya kupotea kwa vyanzo vingi vya maji. Masikitiko yangu yanazidi pale ninapoona mpango wa kupungua matumizi ya nishati ya kuni na mkaa, ni kitendawili. Umeme unaongezeka bei na gharama, hata wale wa mijini wanategemea kuni na mkaa, kwa kuogopa gharama. Aidha, mpango wa kupeleka umeme vijijini ni kitendawili maana kama mwenye kipato anashindwa kulipia umeme, ni wanavijiji wangapi watamudu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio cha miti na vyanzo vya maji yanahitaji kutazamwa upya na kuweka mkakati ambao utakuwa endelevu na *more realistic* badala ya maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nitoe tamko rasmi kuwa naunga mkono hoja hii bila matatizo yoyote. Naomba pia nimpongeze kwa namna ya pekee Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa juhudi zake zenye tija. Vile vile nawapongeza sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Antony Diallo, Katibu Mkuu na Maafisa wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa maoni au maombi yoyote ningependa nitoe shukrani zangu kwa uongozi wa Wizara hii kwa kuingiza Kijiji cha Kiponzelo katika Miradi 44 ya ukarabati wa maji vijijini. Nitashukuru sana kama mradi huu utakarabatiwa kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka miwili mfululizo nimetoa maombi yangu yenye msisitizo juu ya kutoa maji kutoka mlima wa Nyamlenge na kutawanya kwa vijiji karibu 18 katika Kata za Magulirwa na Mgama ndani ya Jimbo langu la Kalenga, Iringa. Wahandisi wa Maji walikwishajitosheleza kwa kufanya utafiti kuwa maji yanayotokea katika mlima huo wa Nyamlenge ni mengi sana ya kutosha na kusaza na kwamba yanaweza kutawanywa katika vijiji mbali mbali kwa njia ya *gravity.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo Wahandisi wa maji wamefanya *survey* kwa vijiji vyote juu ya namna maji hayo yanavyoweza kutawanywa katika vijiji vya Kata hizo mbili. Kazi hii imefanyika kwa muda wa miaka miwili. Wananchi wamehamasika sana kuona *survey* hiyo inafanyika na Wahandisi wa Serikali. Hivyo wananchi wana matumaini makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wangu kuikumbusha Serikali juu ya maombi yetu haya muhimu. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri sikuona *commitment* ya Serikali hata kwa baadaye juu ya mradi huu. Kwa heshima, namwomba Mheshimiwa Waziri na uongozi wote wa Wizara watusaidie juu ya suala hili. Tunaomba fedha za wafadhili zianze kutafutwa maana gharama yake itakuwa ni kubwa, lakini watu watakaonufaika ni wengi sana. Ni matumaini yangu kuwa maombi yangu haya yamepokelewa kwa moyo wa huruma juu ya kilio cha wananchi wa Kata za Magulirwa na Mgama. Naomba nami maombi haya yashughulikiwe ipasavyo

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RAMADHAN H. KHALFAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Edward Lowassa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Mrisho, Naibu Katibu Mkuu Dr. Nyamrunda, pamoja na wataalam wote wa Wizara hii. Kwanza kabisa kwa maandalizi ya Bajeti ya Wizara na vile vile kwa namna wanavyosimamia kwa ufanisi mkubwa utekelezaji wa majukumu mazito ya sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Bagamoyo wanafarijika sana na huduma za maji katika maeneo mbalimbali Jimboni/Wilayani. Tunaipongeza sana Wizara kwa kuijumuisha Wilaya ya Bagamoyo miongoni mwa Wilaya 38 za upanuzi wa awamu ya kwanza katika mwaka 2004. Aidha, naipongeza kwa dhati kabisa Wizara kwa kutekeleza mpango wake wa ufungaji wa dira za maji kwa kuanzia na Mji wa Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali mbaya sana ya upungufu wa maji katika maeneo ya vijiji na vitongoji vya Vigwazo, Buyuni, Visezi, Mnindhi, Kisogo, Kivungwi, Kwazoka, Kitonga, Kengeni, Milo/Migude, (Kata ya Vigwaza) Makurunge, Boza na Kitome, (Kata ya Magomeni) Nyakahamba, Kimere, Kihalaka na Mapinga (Kata ya Zinga), pia maeneo ya Chamakweza Makombe, Masuguru, Mwetemo, Kiwangwa (Chalinze) yote haya na mengine mengi Wilayani yatapatiwa ufumbuzi mzuri katika kuitekeleza programu ya Kitaifa ya maji na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuishukuru Wizara kwa namna ilivyoandaa mazingira mazuri sana ya mahusiano mema miongoni mwa Utawala wa Ranchi ya Ruvu na sisi tuishio pembezoni mwa Ranchi hii. Kwa niaba ya wananchi wote waishio katika maeneo husika naomba nimpongeze sana Meneja wa Ranchi ya Ruvu, Ndugu Mangazini, kwa moyo wake wa upendo, huruma na ushirikiano anaouonyesha kwa wananchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Naibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu na watendaji wengine

kwa kazi nzuri wanayoitenda kwa ufanisi mkubwa. Aidha, nawapongeza kwa hotuba yao ya bajeti ambayo imejaa matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, ingawa Wizara ilitoa msimamo wa kufufua na kukamilisha miradi iliyotekelezwa miaka ya huko nyuma kwanza kabla ya kuanzisha mipya. Mradi wa maji wa Lifua, Manda hadi leo haujatekelezwa. Mradi huu uliotazamiwa kuhudumia vijiji kumi vya wakati huu Luilo, Lifua, Kipangala, Lihagule, Kingole, Nsungu, Ilela, Ngelenge Kipingu na Mbongo, lakini hadi sasa licha ya Wilaya kusukuma tatizo hilo ili Wizara iweze kusaidia katika miradi ya fedha za Serikali au kuwekwa kwenye miradi ya wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mradi huu ulipangwa kutatua tatizo la maji kwa ajili ya shule ya sekondari ya Manda ambayo kwa muda mrefu sana imebaki bila maji hali inayosababisha usumbufu mkubwa kwa walimu na wanafunzi haswa baada ya zoezi/shughuli iliyosimamiwa na Wizara ya kutafuta visima kusitishwa tangu mwaka 2002 bila ya kuipatia ufumbuzi mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa Wilaya imeleta maombi maalum ya kupata shilingi 30,000,000/= kwa ajili ya mradi wa maji wa Kata ya Ludende. Mradi huu mwaka 2002/2003 ulipitishwa Kimkoa lakini fedha zenyewe hazikuletwa. Tunaomba Wizara itazamie upya miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono asilimia mia moja hotuba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hobuba aliyoiwasilisha inajitosheleza, inaeleza yaliyofanyika na yatakayofanyika. Haya aliyoyaeleza endapo shilingi 104,569,519.200 zitapatikana bila matatizo basi utekelezaji wa miradi ya maendeleo itaenda sambamba kama matarajio yalivyo. La kuzingatia ni upatikanaji wa fedha za nje shilingi 73,372,663,200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, watendaji wake wakuu kwa kufanya vyema, lakini nampongeza Waziri kwa ujasiri mkubwa aliouonyesha, hizo ndizo sifa za kiongozi bora, anao upeo mpana, uwezo wa kupima na kuamua na ujasiri wa kutenda, yeye si mwoga wa kuamua au mashaka katika kutenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya kero kubwa kwa wananchi na kikwazo katika njia ya kujiendeleza ni ukosefu wa maji safi na salama na ndiyo maana maji ni miongoni mwa vipaumbele katika mkakati wa kupiga vita umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mageuzi yetu ya uchumi na usahihi wa sera zetu, usahihi wa sera ya taarifa ya maji ya mwaka 1991 na ilivyorekebishwa mwaka 2002 ndiyo chachu ya mafanikio ya kuendeleza miradi ya maji kwani kutokana na uchumi wetu kukua ipo miradi mbalimbali mfano, mradi wa ujenzi wa awamu ya kwanza kutoka Ziwa Victoria - Kahama hadi Shinyanga, mradi ambao utatumia fedha zetu wenyewe jumla ya shilingi bilioni 85.1. Huo ndio ujasiri wa kutenda na kuamua. Nami naungana na Mheshimiwa Waziri kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kulisimamia na kuliamulia suala hili la mradi wa maji wa Ziwa Viztoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo mkubwa tunaoutekeleza kwa fedha zetu wenyewe na ambapo utapita katika vijiji mbalimbali vya mkoa wa Mwanza kati ya Ihelele hadi Mhalo naomba kwa sababu huo ni mradi unaoendelea katika awamu ijayo maeneo ya Sumve, Ngudu na Malya yawe kwenye programu ya kupatiwa maji yanayotokana na Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Sumve tuna upungufu wa Malambo kwa ajili ya mifugo, naleta ombi la kuchimbiwa Malambo kama yalivyoainishwa na Afisa Mifugo wa Wilaya ya Kwimba Dr. Kibisa, anayefanya kazi kwa umakini kama ilivyo kwa watendaji Wakuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya katika mwaka 2003/2004. Aidha, nawatakia kila la kheri katika mwaka mpya wa 2004/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii lakini ninayo yafuatayo:-

Kwanza, maji kutotosha katika Mji wa Kasulu na vijiji kadhaa vya Jimbo la Kasulu Mashariki. Mji wa Kasulu una wakazi zaidi ya 30,000 na unakua haraka sana kiasi kwamba maji hayatoshi kabisa. Aidha, vijiji kadhaa kama vile Kitagata, Makere, Mvugwe, Shungulibha, Mtundu na Nyarugusu vinakabiliwa na upungufu mkubwa wa maji na hivyo kuathiri maisha ya wakazi wake. Naiomba Wizara ianzishe miradi ya kuwapa maji wakazi wa maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu visima vilivyochimbwa 2003/2004, nimeangalia Jedwali Na. 3 katika hotuba ya Wizara hii na kuona kuwa Mkoa wote wa Kigoma haukupata hata kisima kimoja. Je, hali hii inatokana na nini? Ina maana Mkoa huu hauna maeneo yenye shida ya maji? Siyo kweli hata kidogo! Nimeonyesha hapo juu maeneo yenye matatizo makubwa ya maji. Naiomba Wizara ishughulikie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapambano dhidi ya mbung'o. Kuwepo kwa mbung'o wengi katika maeneo kadhaa ya Jimbo la Kasulu Mashariki, siyo tu huwaathiri afya za wakazi, bali vile vile kuwazuia ufugaji wa mifugo mbali mbali na hivyo kuleta athari kiafya na kiuchumi kwa wakazi. Naiomba Wizara isaidiane na vyombo vingine

kwa mfano *UNHCR,* Wizara ya Afya na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu katika vita dhidi ya wadudu hao!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Edward Lowassa na Naibu wake, Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri inayoendelea kufanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Ranchi za Taifa, katika kuwawezesha wananchi kufuga kibiashara, Ranchi za Mkata, Mzeri, Dakawa, Kalambo, Usangu, Kitengule, Kikukula, Uvinza na *West Kilimanjaro,* zimegawanywa, zimepimwa na baadhi ya maeneo kugawiwa kwa wamiliki wapya Watanzania ili wafuge kibiashara na kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Wilaya ya Kongwa wangependa pia ranchi yao inafanyiwa utaratibu kama huu. Ombi kwa Wizara ni kukubaliana kuwa hiyo ndiyo sera sahihi kwa ranchi zetu. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapojibu hoja alisemee hili na akubaliane nasi kuwa sera zake ni sahihi kabisa na zitekelezwe kote nchini, *there should not be exceptions.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi maalum kwa Wizara, ikiwa kuna ziara za mafunzo katika nchi za Kenya na au Botswana naomba kuwemo ili kuwawezesha wananchi wa Kongwa wafuge kisasa kama katika nchi hizo mbili.

Pili, ni kuhusu majosho, Wizara itenge fedha mahsusi kwa ajili ya kufufua majosho, kujenga mapya na ku-*subsidize* huduma za uendeshaji wa majosho hasa dawa za kuogeshea mifugo. Jambo hili ni muhimu sana.

Tatu, kuhusu maji, tunaishukuru sana Wizara kwa mradi wa Benki ya Dunia wa huduma ya maji kwa vijiji vya Wilaya ya Kongwa (vijiji 10). Pia tunashukuru sana kwa mradi wa mji mdogo wa Kibaigwa kupaitia fedha za *AFD* za Wafaransa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni *paper work* inachukua sehemu kubwa sana ya mradi na muda mrefu, wananchi wanachotaka ni maji, siyo miezi kwa miezi ya kuandikiana Wilaya, Wizara, *World Bank* na kadhalika. Pia waliopewa kazi ya *survey* kabla ya uchimbaji wa maji wa mradi wa *World Bank,* Kongwa, sio kampuni nzuri, ina wababaishaji na hawawashirikishi wanakijiji na wanafanya kazi haraka haraka. Wananchi wameilalamikia sana kampuni hii na tunaomba kwa Kijiji cha Manungu waende kurudia ku-*survey.* Kazi waliyoifanya si nzuri pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza pia programu ya uchimbaji Mabwawa vijijini japo baadhi ya Mabwawa yamechimbwa sehemu ambazo hayatakinga maji

kamwe sababu ni kuwa kule mitambo ya kuchimbia inakokodishwa, ni watu wapenda fedha za haraka haraka kuliko kufanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalamu wa Wilaya wabanwe kuwa *accountable* na fedha hizi za uchimbaji wa mabwawa. Naunga mkono hoja 100%.

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa maji kwa binadamu maji pia ni hatari ya kuwa machafu. Mji wa Tarime kuna tatizo la maji na maji yanayopatikana hayasafishwi na dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais mwaka 2000 alielezwa kuwa kuna tatizo la maji na Rais aliahidi kuwa maji yatapatikana. Katika hotuba ya mwaka 2004/2005 angalau Tarime imetajwa. Hakuna maji ya kutosha na yaliyopo ni machafu.

Nashukuru kwa kutuona wataalam Mto Mori kilometa mbili toka Tarime, Bwawa la Wakoloni halitoshelezi. Wakati tunasubiri mradi mkubwa njia ya bomba kuu ifanywe ukarabati na yasafishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarime itafanyiwa ukarabati (bajeti ya mwaka 2004/2005). Bomba kutoka Ziwa Viztoria lihudumie vijiji vya njiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi kwa usanifu na ukarabati wa mradi uliopo, jambo la muda ambao hatua zitachukuliwa. Nashukuru kwa mpango wa kuchimba visima vitatu kwa mwaka 2004/2005, kauli ya Rais ni ya mwajiri.

**MHE. TEMBE K. NYABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nimeona Bunda tulipewa pesa kukarabati maji Bunda Mjini kwa mwaka 2003/2004. Lakini hukutoa nakala ya mgawanyo wa fedha kwangu Mbunge kama wanavyofanya Wizara za Ujenzi, TAMISEMI ili kufuatilia. Nijuavyo Bunda bado tuna tatizo kubwa la maji ili kufuatilia kwa karibu, naomba unipe barua *(official)* inayoonyesha tulipewa kiasi gani mwaka uliopita ili nifuatilie.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono kwa asilimia mia moja. Aidha, naomba msaada wa kuanzisha *water storage (reservoir)* kubwa zaidi kwa ajili ya Kijiji ambako sasa ni mji mkuu wa Wilaya mpya ya Namtumbo ambao *population* yake ni zaidi ya wakazi 100,000. Hii inaweza kufanyika au kwa kupanua chanzo cha maji cha Matogoro (cha sasa) kupitia Kijiji cha Libango. *Reservoir* sasa iwe juu ya Mlima Libango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikishindikana basi maji toka Mto Rwinga chanzo cha zamani kiimarishwe na kupanuliwa na kutandaza mabomba hadi *site* mpya ya mji mkuu wa Wilaya Namtumbo, mji ambao upo katika barabara kuu ya Songea - Tunduru - Masasi - Mtwara. Ujenzi ya Makao Makuu yanaanza kujengwa sasa Julai, 2004.

Pili, tafadhali tafuteni fedha za kufufua na kupanua chanzo cha maji baridi, matamu toka chanzo cha asili cha Msisi katika Milima ya Hombolo. Maji ya Bwawa la

Hombolo sasa hayafai maana yana chumvi kali sana. Wakati huo huo, mabomba yakifufuliwa, maji ya Msisi yaliyojengwa na Padri wa Hombolo (Muitalia) mwaka 1981 yatafaa kwa matumizi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Hombolo chenye wakazi 10,000. tayari yapo matanki sita toka Msisi kilomita tisa hadi Hombolo kijijini, Kanisa la Hombolo na Nyumba ya Masista, *Health Centre* ya Hombolo, *Primary Schools* mbili, Kambi ya Wakoma, Kijiji cha Hombolo Makulu, Kituo cha utafiti kilimo Hombolo, Chuo cha TAMISEMI cha Taifa Hombolo, Hoteli ya Kitalii inayotarajiwa kujengwa karibuni *(site* ipo tayari), Kiwanda cha kusindika Divai cha Mwekezaji toka Italy katika majengo ya zamani ya Kiwanda cha *NAFCO,* kituo cha watoto yatima na makazi ya wazee wasiojiweza, shamba la Zabibu la Parokia Hombolo,shule ya sekondari ya Hombolo, matumizi ya mifugo Hombolo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza jitihada zifanywe ili *Water Aid Tanzania* yenye tawi Dodoma wasaidie kufufua *Water Supply* ya Msisi, Hombolo ambayo ipo tayari lakini inahitaji kupanuliwa ili ifae wananchi hadi ifikiapo wakazi 30,000.

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa hotuba yake nzuri na ya kutia moyo na matumaini kwa sisi tulio na matatizo makubwa ya maji kwenye maeneo yetu. Naunga mkono hoja kwa mategemeo kwamba matatizo ya maji kwenye Jimbo langu la Gairo yatapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ndicho kilio kikubwa cha wananchi wa Jimbo la Gairo na hasa katika Mji Mdogo wa Gairo. Kuna upungufu mkubwa kwa maji Gairo na suala la maji Gairo limekuwa ni hoja ya kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mji mdogo wa Gairo na vijiji vya Kisitwi, Rubeho, Kwipipa, Msingisi, Luhwaji, Ukwamani, Majawanga, Ibate, Ngiloli, Kibedya na Chakwale wanategemea maji ya mtiririko kutoka kwenye chanzo kilichoko Masenge katika milima ya Ukaguru. Mradi wa maji hayo ya mtiririko ulikamilika mwaka 1973 na ukafanywa ukarabati mwaka 1982. Tangu wakati huo haujafanyiwa ukarabati wowote mkubwa. Mabomba mengi yameharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo katika mwaka 1985 ulikuwa unawahudumia wananchi 30,600 na ulikuwa unatoa kiasi cha lita 617,700 kwa siku sawa na lita 16 tu kwa kila mtu kwa siku. Hicho kilikuwa kiasi pungufu kulingana na kiasi kinachostahili cha lita 25 hadi 30 za maji kwa mtu kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya watu wanaohudumiwa na utaratibu huo wa maji ya mtiririko hivi sasa imeongezeka sana. Kwa mujibu wa Sensa ya watu ya 2002 idadi hiyo ya watu imefikia 97,512. Kwa idadi hiyo ya watu kiasi cha maji yanayopatikana ambayo hayajaongezeka na hasa yamepungua ni lita 6 tu ya maji kwa kila mtu kwa siku na hakuna chanzo kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahairi kabisa kuwa kiasi hicho cha maji ni kidogo mno. Ni kawaida kabisa kwa mkazi wa Gairo kukosa maji ya kuoga na kufulia nguo kwa wiki nzima. Upungufu huu wa maji umefikia kiwango cha kutisha. Kwa maelezo hayo nina hakika Mheshimiwa Edward Lowassa na Naibu wake, Mheshimiwa Anthony Diallo, wataelewa kwa nini nimekuwa ninawasumbua kila nilipokutana nao kuwaomba watusaidie kutatua tatizo la maji Gairo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tegemeo letu la kupata ufumbuzi wa tatizo la maji Gairo liko kwenye Mradi wa kupanua chanzo cha maji hayo ya mtiririko ambao utatekelezwa kwa msaada wa Shirika la Ufaransa la *AFD* kwa kushirikiana na Serikali, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa na wananchi husika katika mradi huo. Wananchi wamekwisha kukamilisha mchango wao wa shilingi 8,250,000/=. Hivi sasa wananchi wanasubiri kwa hamu kubwa kuona kwamba utekelezaji unaanza kwani nimekuwa nawapa matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyomwelewa Mheshimiwa Edward Lowassa na utendaji wake wa kazi ulivyo mahiri hatatuangusha mimi na wananchi wa Gairo. Inatia moyo kwamba Mhandisi Mshauri atakayesaidiana na Wizara kusimamia utekelezaji unaohusisha miji midogo tisa ukiwemo mjimdogo wa Gairo amekwishachaguliwa. Kwa ukubwa wa tatizo Gairo naomba mjimdogo wa Gairo upewe kipaumbele na Mhandisi mshauri huyo aanze na Gairo. Nina hakika nimeeleweka.

Pamoja na kilio changu hicho hapana budi niishukuru Serikali kuwezesha vijiji vya Nguyami, Meshugi na Mkalama kuchimbwa visima vyenye pampu za kusukumia maji kwa fedha zilizotoka Benki ya Dunia pamoja na michango ya fedha na nguvu kazi ya wananchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tarafa ya Gairo ni Tarafa yenye ukame na inapata kiasi cha 600mm tu za mvua kwa mwaka, wananchi wanahitaji kuhamasishwa watumie teknolojia nyepesi na rahisi ya kukinga na kutumia maji ya mvua kutoka kwenye mapaa ya nyumba. Bahati mbaya wananchi hawajaanza kutumia teknolojia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mifugo katika Jimbo langu la Gairo, juhudi zinafanywa kwa msaada wa wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Sokoine kueneza mbegu bora za ng’ombe na mbuzi wa maziwa na wameanza kututafutia masoko ya kuuzia mifugo hiyo. Lakini lipo tatizo la kukosekana majosho ya kuogeshea mifugo. Katika Tarafa ya Gairo yapo majosho matatu tu na yote hayafanyi kazi. Hivyo tishio la maradhi yanayotokana na kupe lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi zinafanywa kuyafufua majosho hayo yafanye kazi lakini lipo tatizo la bei kubwa ya dawa za kutumiwa kwenye majosho. Hivyo hatua ya Serikali kutoa ruzuku ya kati asilimia 20 hadi 30 kwa madawa ya kudhibiti magonjwa yaletwayo na kupe yaani dawa za uogeshaji inastahili kupongezwa. Vile vile kwa upande wetu kwa kusaidiana na Wizara tunachimba lambo kwa ajili ya mifugo Gairo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo namalizia kwa kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii nzuri mno ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, japo kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kazi nzuri anayofanya ya kuiongoza Wizara hii vizuri sana na jitihada kubwa anayofanya kuhakikisha kuwa Watanzania wote wanapata maji safi na salama kwa karibu iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu kwanza, napendekeza Mheshimiwa Waziri afanye kila awezalo kwa mwaka 2004/2005 maji mengi yaliyoko kwenye chemchem za Kilema Kaskazini kwenye Jimbo la Vunjo yamewafikia wananchi wa Kilema Kusini hasa maeneo ya Himo - Njiapanda, *Muungano Secondary School,* Chekereni na *Ghona Seondary School.* Kabla ya Uhuru na baada ya Uhuru hadi leo wananchi hao wa dhiki kubwa ya maji.

Pili, Kahe Magharibi na Kahe Mashariki kwenye Jimbo la Vunjo wana adha kubwa ya maji japo juu yake kidogo tu pana chemchem ya maji maangavu ya Miwaleni. Inaombwa ifanyike juhudi za makusudi za kuwawezesha wananchi hawa kupata maji safi na salama ikizingatiwa kuwa hapo awali walikuwa wanapata maji ya bomba kutoka Moshi Mjini ambayo yamekatwa na kuacha bomba ardhini bila maji na matanki yaliyopo kutokuwa na kazi ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naipongeza Wizara nzima kwa kazi nzuri mno wanayoifanya na naunga mkono hoja. Wapate pesa wazifanyie kazi.

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Kigoma Kaskazini, naomba vijiji vya Nyanda za Juu, Kalinzi, Nyarubanda, Mkigo, Matiazo na Mkabogo vipatiwe maji ya uhakika na vyanzo vipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Fedha wa Benki ya Dunia kwa Mkoa wa Kigoma una utaratibu gani wa kumaliza tatizo la maji? Naomba mradi huo uongeze tanki la maji kutoka Kijiji cha Kidahwe kwenda Kijiji cha Simbo na Kamala pamoja na Msimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tanki lingine lijengwe kutoka Kijiji cha Kizenga kwenda Kijiji cha Chankabwimba mpaka Kijiji cha Mahembe. Kigoma Mjini tatizo ni kubwa sana. Sijui tatizo nini hasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa baadhi ya vijiji vyangu ambavyo vimepata maji na misaada yako ambayo alinisaidia kupata mabomba kando kando ya Ziwa Tanganyika ijapokuwa bado vijiji viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja tena kwa nguvu zote.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Siha naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa hotuba yake nzuri na ya kuvutia sana, ambayo imetolewa leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kuwa kazi nzuri imefanyika katika Wizara hii hasa katika upatikanaji wa maji safi na salama katika nchi nzima. Jimbo la Siha na hususan Wilaya ya Hai limenufaika sana na huduma ya maji safi na salama kufuatilia msukumo uliowekwa na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na ule uliotokana wahisani wetu wa Serikali ya Ujerumani kupitia *Kfw* yaani Benki ya wananchi na Maendeleo ya Ujerumani. Kazi ile ni ya kupongezwa na ni ya kutia moyo. Maeneo mbalimbali ambayo yalikuwa hayana maji hasa maeneo ya tambarare ya Siha kati na Siha Kusini sasa yana maji safi na salama. Tutaishukuru Serikali ya Tanzania na ile ya Ujerumani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nalishukuru kanisa la KKKT Dayosisi ya Kaskazini kwa msukumo, uhamasishaji na hata mazungumzo ya awali ya kuhakikisha kuwa miradi ya Maji Wilaya ya Hai inapatikana. Miradi hiyo ni pamoja na ile ya Uroki - Bomang'ombe, Losaa - *KIA,* Lawate - Fuka na ule wa Magadini - *Makiwaru Water Supplies.*

Kuhusu mifugo, bado naomba Wizara iendelee kutusaidia katika uchimbaji wa Malambo na ukarabati wa majosho kwani uwezo wa Halmashauri ni mdogo.

Nakumbushia ujenzi/uchimbaji wa Malambo katika vijiji vya Donyomoruak, Magadini na Lekrimuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba wananchi wafugaji wadogo wadogo wapewe kipaumbele katika umilikaji wa Ranchi ndogo ndogo ambazo zitapimwa mwezi Oktoba kama hotuba ya Waziri ilivyoeleleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwasahau wananchi wadogo wadogo kwa maoni yangu litakuwa ni chimbuko la migogoro ambayo haina ulazima. Siamini kuwa wafugaji wadogo wadogo watakaa kimya tu hivi hivi huku wakiwaangalia *strategic investors* wanachukua maeneo yote. *Compromise* nzuri ni kuhakikisha na hawa wadogo wanapatiwa maeneo.

Mimi kama mwakilishi wa wananchi, nimewashauri wafugaji wajiunge katika makundi madogo madogo ya ushirika ili nao waweze kupata maeneo kwa ajili ya mafugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupongeza kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Edward Lowassa, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ROBERT J. BUZUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza mchango wangu kwa kumpongeza kwa dhati Waziri, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa juhudi zake dhahiri za kupenda kuwatumikia Watanzania na moyo wake wa kupenda maendeleo ya Taifa letu na ari ya kuwainua wanyonge ili waishi maisha nadhifu kwa kupitia kazi za Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawapongeza Mheshimiwa Anthony Diallo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na watendaji wengine wote kwa namna wanavyoshirikiana na Waziri kwa kuwakomboa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni nyenzo muhimu sana katika harakati za kuleta maendeleo ya nchi yetu na kwa kutambua hilo naamini kuwa kadri tunavyojitahidi kuweka mipango mizuri ya namna ya kuyatumia kama Wizara inavyofanywa sasa, hakika hatua za maendeleo ziko dhahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani kwa Mheshimiwa Benjamini William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi huu madhubuti ambao naamini ushauri mzuri aliopata kwa Waziri, umefanya kukubalika kuanza mara moja kwa kutumia fedha ya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Wizara/Serikali kwamba wakati mradi huu wa kupeleka maji katika miji ya Shinyanga na Kahama ni vyema vijiji na taasisi zilizopo kando ya bomba litakakopitia vipewe huduma ya maji kwa kuacha vituo ambavyo wananchi watachota maji na aidha, matoleo ambayo wananchi walio mbali na eneo linakopita bomba nao waweze kuvuta maji hayo kwenda vijiji hivyo kwa gharama zao. Hii itasaidia sana kuondoa tatizo la ukame, lakini pia kuwafanya wauone kuwa mradi huu ni kwa ajili yao na watakuwa walinzi wazuri wa miundombinu itakayowekwa. Aidha, itaondoa dhana kwamba wananchi wa mijini tu ndiyo wanaolengwa pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia Wizara ianze mapema kutaja bayana vijiji vyenyewe katika Jimbo la Solwa kwa kuwaandikia vijiji au mwakilishi (Mbunge) ili kuanza kuwaandaa wananchi wawe tayari kushiriki katika kazi za mkono zitakazowahusu kwani wao ni wadau. Hii ni pamoja na kuanzisha vikundi vya watumiaji maji *(WUA'S)*. Hapa mapendekezo haya nayatoa kwa kulenga Jimbo langu la Solwa ambapo nusu yake litanufaika na mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mifugo, katika eneo hili napongeza juhudi zinazoendelea kufanywa na Wizara kuendeleza zao la mifugo. Nashauri maeneo ya kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa na masoko ya mifugo yaendelee kupewa uzito ili kuleta ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala la dawa za mifugo zienezwe katika maeneo mbalimbali ya wafugaji. Aidha, katika Jimbo langu, naomba Serikali isaidie kuchimba Malambo/Mabwawa katika Kata na vijiji vya Sayu, Mwamadilamha, Bunambiyu, Nghomango Lyamidati, Lyabukande, Ng'wajiji na Kwakitoryo. Maeneo haya ni ya wafugaji wengi na wakubwa ambao wanakabiliwa sana na ukame hasa nyakati za kiangazi na mifugo mingi sana hufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kupongeza na kushukuru Serikali kwa juhudi zake, nawatakia utekelezaji mwema wa kazi zilizo mbele yao mwaka huu. Naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa maombi ya kuchangia hotuba hii kwa kuzungumza lakini inawezekana nikakosa nafasi. Naomba nitoe mchango wangu kwa kifupi sana.

Kwanza nataka kusema kwamba hotuba ya Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, ni hotuba nzuri sana, hotuba inayotoa matumaini kwa Watanzania wengi. Ni hotuba inayojielekeza kikamilifu katika suala zima la vita dhidi ya umaskini. Maji ni maisha na ndiyo chimbuko la maendeleo ya binadamu. Pasipo na maji safi na salama kama ilivyo katika sehemu kubwa ya Wilaya yangu ya Kyela, hapana maisha marefu ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kyela ni ndogo sana kieneo, ina ukubwa wa kilometa za mraba 1,350 tu, Wilaya nzima ni tambarare na ina mvua nyingi ambayo husababisha mafuriko makubwa kati ya mwezi Machi hadi mwezi Mei, kila mwaka. Kipindi hiki cha mafuriko ni kipindi cha milipuko ya magonjwa mbalimbali kama vile homa ya tumbo, kuhara damu, kipindupindu, kukohoa na kadhalika.

Kutokana na hali hii ndiyo maana Serikali ya awamu ya kwanza, chini ya Marehemu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, miaka 30 iliyopita ilijenga miradi mitano ya maji. Miradi hiyo ni *Kanga group, Sinyanga Group, Ngana Group, Ngamanga Group* na *Makwale/Matema Group.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi yote hii inasukuma maji kwa nguvu za *gravity.* Miradi yote nitano imezeeka na inahitaji *total overhaul.* Katika miaka ya 1970 miradi hii mitano ilikuwa inakidhi asilimia 30 tu ya wananchi wa Kyela ndiyo wanapata maji safi na salama ya bomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa ningependa Mheshimiwa Waziri atusaidie wananchi wa Kyela kwa mambo yafuatayo:-

Kwanza, mradi wa maji wa *Kanga Group* ukarabatiwe, ulijengwa kwa madhumuni ya kupeleka maji katika mji wa Kyela miaka 30 iliyopita. Mabomba ya mradi huu hupita katika Kata za Ipinda, Muungano, Ikama, Mwaya na Kyela. Kata zote hizi hazipati maji kutoka kwenye bomba hili. Mradi huu ukikarabatiwa na kutandika bomba kubwa. Kata zote nilizozitaja zitapata maji zikijumuisha vijiji zaidi ya 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu hili siyo geni mbele ya Mheshimiwa Waziri. Mara nyingi nimezungumza naye hapo Bungeni na ofisini kwake. Alipotembelea Wilaya ya Kyela Oktoba, 2002 wananchi wa Kyela pamoja na viongozi wake walimwomba Mheshimiwa Waziri kukarabati mradi huu wa Kanga na alikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kupitia upya mradi wa maji wa *Ngana Group.* Mradi umevamiwa na mji mdogo wa Kasumulu. Miaka 20 iliyopita hapakuwepo mjimdogo wa Kasumulu. Mradi huu ulijengwa kwa madhumuni ya kuwapa maji safi wananchi wa Kata za Ngana, Katumba Songwe, Ikolo, Ngonga na Bujonde. Leo Kata hizi hazipati maji kwani maji yote yamedakwa na mji mdogo wa Kasumulu. Kama haitawezekana kukarabati mradi huu basi naomba kisima kirefu cha kisasa kichimbwe. Wilaya ya Kyela haijapata kuchimbiwa kisima cha maji miaka kumi iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kyela imetajwa katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 142, je, upanuzi huu wa awamu ya pili unahusu miradi mipya au ukarabati wa miradi iliyopo ambayo nimeizungumzia hapo juu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia mchango wangu kwa kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri ingawa kwa miaka mingi Wilaya yangu imekuwa mtazamaji na sio mshiriki katika maendeleo ya sekta ya maji na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize basi kwa kuiomba Serikali kunichimbia visima katika mji wa Kyela na mjimdogo wa Kasumulu kujibu matatizo ya muda mfupi huku tukisubiri mipango ya muda mrefu. Asante.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na maafisa wote wa Wizara hii, mimi mchango wangu naomba niuelekeze katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, kuhifadhi maji ya mvua, pili chanjo kwa ajili ya mifugo na tatu, kutunza Mabwawa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja katika matatizo yanayotukabili hapa nchini ni ukosefu wa maji kwa ajili ya matumizi ya kilimo wakati nchi yetu inapokabiliwa na ukame yaani ukosefu wa mvua, watu wengi wanahangaika na kutafuta maji kwa ajili ya kilimo, ingekuwa vizuri Serikali ikaweka utaratibu wa kuvuna maji ya mvua ili yasipotee bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuepukana na usumbufu huo, nashauri maji ya mvua yahifadhiwe kwenye mahodhi maalum na baadaye yatumike katika kilimo cha umwagiliaji na pia yatumike katika kilimo cha mboga mboga. Vyanzo vya maji ni muhimu sana, hivyo naomba uwepo mkakati maalum wa kuhifadhi maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dawa za chanjo kwa ajili ya mifugo dawa hizo ziwe za kutosha na zipunguzwe bei ili wafugaji wawe na uwezo wa kuzinunua. Lakini

pia wafugaji wahamasishwe namna ya kutumia dawa hizi kwa ajili ya mifugo ikiwemo na umuhimu wa kutumia chanjo. Inaonekana baadhi ya wafugaji hawajalitia maanani umuhimu wa chanjo na dawa za kuoshea mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu yawepo mabwawa ya kutosha kwa ajili ya kuhifadhia maji. Mabwawa hayo siyo tu yatasaidia kwa matumizi ya binadamu, lakini pia yatasaidia kwa matumizi ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kazi yake nzuri sana anayoifanya katika Wizara hii. Aidha, nampongeza sana Naibu wake, Mheshimiwa Anthony Diallo, kwa kazi yake nzuri anayoifanya bila kumsahau Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Vicent Mrisho, ni mchapa kazi, naamini kabisa kutokana na ushirikiano mzuri na wataalamu wa Wizara hii ufanisi mkubwa utapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Edward Lowassa na Naibu wake ni viongozi ambao wanashirikisha vyema viongozi wenzao katika kazi zao na mfano kamili umeonekana pale alipowashirikisha Wabunge katika ziara ya kikazi nchini Misri. Ni Wizara ngapi na Mawaziri wangapi wameiga mfano huu wa Mheshimiwa Edward Lowassa. Kila siku wanasafiri lakini hawajawashirikisha Wabunge kama hivi. Nampongeza sana Waziri na kuomba Wizara zingine ziige mfano wake huu mzuri wa ushirikishwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tatizo la maji Tabata, kwa muda mrefu wakazi wa Tabata hatupati maji ya bomba. Tunategemea maji ya kununua kupitia malori yanayouza maji. Hivi tatizo la maji Tabata litamalizika lini? Wananchi wanateseka sana. Lori moja la maji ni shilingi 40,000/=, nani atakuwa na uwezo wa kununua maji kila wakati? Hebu tupate maelezo tatizo la maji Tabata ni lini litapatiwa ufumbuzi na tatizo kumalizika kabisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, tatizo na maji katika Wilaya ya Mpanda, Kata yote ya Ikola na vijiji vyake lina matatizo makubwa ya maji na hata Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara Wilayani humo hoja ya tatizo kubwa aliloelezwa ni tatizo la maji. Akinamama wanapata shida kubwa mno ya kutafuta maji wakati wa kiangazi. Tunaomba vijiji vya Wilaya hizo wafanyiwe utaratibu wa kuchimbiwa visima vya maji ili kupunguza kero kubwa ya wananchi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne ni kuhusu shule za sekondari, shule za Kata, Ulungu, Kasanga na kadhalika moja ya matatizo ambayo Waheshmiwa Wabunge tunakutana nayo mara kwa mara tutembeleapo shule hizo ni tatizo la maji na wanaomba wasaidiwe kuchimbiwa visima vya maji. Je, Serikali ina mpango wowote wa kumaliza tathmini la maji katika shule zetu za sekondari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namalizia kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla kwa kazi yake nzuri anayoifanya katika Wizara hii. Tunamtakia mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashukuru kupata majibu katika haya niliyoyauliza. Naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. ROBERT K. MASHALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa ushirikiano wao ambao umewezesha Wizara kuwasilisha hotuba nzuri yenye lengo la kuinua sekta ya maji na mifugo na hasa wananchi ambao ni wadau wa sekta hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba nzuri na mafanikio makubwa yaliyofikiwa na Wizara, bado kuna matatizo makubwa ambayo yakiachwa yaendelee wananchi wetu watapunguza imani kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo ni moja ya mazao ambayo yanachangia Pato la Taifa na kuinua hali ya uchumi kwa jamii, hivyo ni wajibu wa Serikali kutoa elimu kwa wafugaji hasa kuhusu zoezi la kinga ya mifugo kwa magonjwa ya kuambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la chanjo ya mifugo lina lengo la kutoa kinga kwa mifugo yetu ili isiathirike na magonjwa, lakini zoezi hili linapofanyika bila elimu kwa wafugaji matokeo yake yanakuwa mabaya na mfugaji analaumu Serikali.

Mheshimiwa Spika mfano hai ni chanjo iliyofanyika mwezi Februari hadi Machi, 2004 nchi nzima zoezi hili. Kwa Wilaya Bukombe na Kahama limeleta athari kubwa sana, baada ya chanjo ng’ombe wengi walikufa katika Kijiji kimoja cha Lubeho ng’ombe baada ya chanjo, ng’ombe wengi walikufa baada ya kupata vidonda kwenye sehemu ya chanjo na hawakujua wahudumiwe vipi kidonda kinachotokana na chanjo. Hivyo wananchi wanaihoji Serikali kwa nini ng’ombe wao baada ya chanjo walikufa na Serikali haijaenda kutoa ufafanuzi kuhusu matokeo ya vifo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine lililopo katika Wilaya ya Bukombe ni kutokuwa na Mganga wa Mifugo wa Wilaya ya Bukombe ina ng’ombe 350,000, mbuzi, kondoo na nguruwe lakini ina upungufu sana wa wataalam wa mifugo hivyo tunaomba Wizara iangalie uwezekano wa kutuletea mganga wa Mifugo wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kusikia kilio cha wananchi wa Mjini Ushirombo, Makao Makuu ya Wilaya Bukombe kwa kuwapatia mradi wa maji visima virefu sita, mradi ambao ukikamilika mji wa Ushirombo utakuwa na uhakika wa maji kuliko ilivyo sasa Ushirombo kuna shida ya maji naomba Mheshimiwa Waziri usaidie kuhimiza zoezi la kuchimba visima hivi liende haraka ili wananchi wa Ushirombo wajikomboe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. Pamoja na kuunga mkono hoja ya Wizara hii, nina mambo machache ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai, kwa ajili hii maji yana matumizi mengi. Miongoni mwa matumizi ya maji ni pamoja na kwanza, matumizi ya maji majumbani, pili, matumizi ya maji viwandani, tatu, matumizi ya maji ya uzalishaji wa umeme na nne, matumizi ya maji katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uzito na umuhimu wa matumizi hayo ya maji nashauri Serikali Kuu, Wizara hii ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ijenge utaratibu wa kuratibu matumizi ya maji na kuweka *cost recovery* ya matumizi ya maji.

Nashauri katika kuratibu matumizi ya maji ni muhimu sana kwa Serikali kuu iwezeshe Wizara hii ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kujua ni meta za ujazo kiasi gani kwa sekunde moja ya maji ya mito yetu zinaingia baharini. Najua kwa sasa Serikali imeweka utaratibu wa kujua kiasi cha maji yanayotumika kwa matumizi ya majumbani na viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika kama Serikali inajua ni meta za ujazo gani kwa sekunde moja zinazotumika katika kilimo cha umwagiliaji kwa ekari moja, ingawa naelewa kuwa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji inasimamiwa na Wizara ya kilimo na chakula, nashauri Serikali ifikirie kukubali *management* ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Vile vile sina hakika kama Serikali inajua ni meta za ujazo ngapi kwa sekunde moja zinazotumika katika mitambo inayozalisha umeme. Nashauri Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, iweke *cost recovery* ya maji yanayotumika katika mitambo inayozalisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maji ni uhai wa nchi yetu ni vizuri Serikali kuwa na mipango ya kujenga Mabwawa ambayo yatakuwa na *regulatory reservoir.* Haitoshi kujenga Mabwawa kutoa maji kwa wafugaji peke yake. *We have to build dams which will be used to enhance agricultural development as well as to generate power.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua ujengaji wa mabwawa na *regulatory reservoirs* inahitaji uwezo mkubwa wa mtaji. Nashauri Serikali yetu ijifunze kutoka nchi ya Misri katika ujengaji wa *Aswam dam.* Haikuwa rahisi kwa marehemu Rais Nasser, kupata wawekezaji, lakini kwa ujasiri mkubwa Marehemu Rais Nasser alitumia *Suez Canal* kama raslimali ya nchi ya Misri kupata wawekezaji. Alifanikiwa kupata wahisani, aliwapata Warusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja hii ya kupata mtaji au kupata wawekezaji, nashauri Serikali yetu ikishirikiana na nchi wanachama wa *Nile Basin Initiative* kutumia raslimali zetu kupata wawekezaji katika kujenga mabwawa na *regulatory reservoir systems.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maji ni uhai wa Taifa letu ni muhimu sana Serikali yetu kuu ihusike katika *Water Management Use.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mifugo nashauri hoja ya kuwezesha wamiliki wapya wa Ranchi za Taifa zilizogaiwa kwao, Waziri atamke tarehe ya kupatikana mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyomfahamu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa na ninavyomfahamu Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Anthony Diallo na ninavyomfahamu Katibu Mkuu wake Dr. Vicent Mrisho, hawa ni viongozi wenye kujali *timing.* Kwa ajili hii ni vizuri mikopo ya mwezeshaji wamiliki wapya wa mashamba ya Ranchi za Taifa, Waziri atoe *time frame* ya kupata hiyo mikopo.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbinga Magharibi na mimi mwenyewe binafsi nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa kutayarisha mpango mkubwa na mzuri wenye nia ya kutatua matatizo ya maji safi na salama pamoja na uendelezaji wa mifugo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefurahishwa mno na mpango mkubwa wa maji wenye thamani ya shilingi bilioni 102.7 itakayofanyika katika Wilaya mbalimbali pamoja na mpango wa kupambana na ugonjwa wa mdondo unaosumbua na kuangamiza kuku wa kienyeji. Mpango huu ukikamilika utawasaidia sana wanavijiji kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kukumbusha maombi yangu ya maji katika Jimbo langu la Mbinga Magharibi. Namwomba Mheshimiwa Waziri mwenye huruma na msikivu kwa wote wanaomwomba, nami nayafikisha maombi yangu tena kwake, maombi ya mradi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwanza, mradi wa maji kata ya Kingirikiti, usanifu umekamilika kwa msaada wa shilingi milioni mbili tulisaidiwa na Wizara yako pamoja na michango ya wananchi Kata ya Kingirikiti.

Pili, mradi wa maji Kata ya Ngumbo, Chiwanda na Mtipwili, miradi hii imekamilika nusu na nusu bado. Shirika la *DANIDA* lilikamilisha nusu ya miradi lakini hawakumalizia. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri ni vema miradi hii ikakamilika kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, mradi wa maji Kijiji cha Litumba, Kuhamba, usanifu umekamilika na gharama ya kukamilisha mradi ni shilingi milioni 80 na nne, mradi wa maji Kata ya Mbaha, *survey* bado lakini ni mradi muhimu sana kwa wananchi wa Kata hii ya Mbaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu sana Mheshimiwa Waziri ana mpango mzuri wa kupunguza matatizo ya maji hapa nchini lakini anakabiliwa na uhaba wa fedha. Hata hivyo, naomba katika fedha za maendeleo ya shilingi bilioni 104.7 zilizotengwa katika Bajeti hii ya mwaka 2004/2005 walau mradi mmoja kati ya hiyo niliyoitaja hapo juu ukatengewa fedha. Natumaini sana kwa hekima za Mheshimiwa Waziri hatanisahau hata kidogo kwa ombi langu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, mimi kwa niaba ya wananchi wa Mbinga Magharibi na mimi mwenyewe binafsi naunga mkono hotuba mia kwa mia. Asante sana.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kwa dhati kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Naibu Waziri Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wataalamu wote wa Wizara hii kwa kazi na juhudi kubwa wanayofanya. Wizara hii imeleta mapinduzi makubwa sana ya maendeleo katika kuhakikisha vijiji na miji mingi inapata maji na mifugo inazidi kuboreshwa. Naipongeza Wizara hii kwa ubunifu.

Pili, pongezi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Korogwe nakuomba upokee shukrani kwa juhudi kubwa ulizofanya pamoja na Wizara yako kwa kutembelea Korogwe na kujionea mwenyewe kero ya maji Korogwe. Katika miji ambayo inashida ya maji ni mji wa Korogwe na Vitongji vyake. Lakini kwa kuliona hilo, juhudi kubwa imefanyika kupata visima viwili vikubwa, kimoja *Old Korogwe* na kingine eneo la Mtonga Korogwe. Visima hivyo hasa cha Mtonga hakijamalizika ni imani yangu mwaka huu kitakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi na kero sugu, bado naendelea kumwomba Mheshimiwa Waziri kutusaidia kufanya yafuatayo:-

Kwanza kwa kuwa tayari tupo kwenye miradi ya Benki ya Dunia, naomba sana Mradi wa Mashindei ukamilishwe. Mradi huu ndiyo mkombozi wa Korogwe na vitongoji vyake. Mradi huu ni wa *gravity* na umekwishafanyiwa usanifu.

Pili, mradi wa pili ni wa *HTM,* toka niingie ndani ya Bunge hili nimekuwa nikiomba kupata maji ya *HTM* ambayo chanzo chake kinatoka Tabora kwenye Jimbo langu. Lakini sielewi ni kwa nini Serikali haitaki wananchi wanywe maji hayo yanayopita katikati ya Mji wa Korogwe. Kwa kweli watu wa Jimboni kwangu hawaelewi ni kwa nini maji hayo hatuyapati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi kwa kuwa tupo kwenye mradi wa *World Bank,* naomba maji hayo sasa tuyapate hasa kwa Kata ya Mgombezi kwa vijiji vya Mgambo, Kitifu na Mgombezi kwenye chanzo cha maji hayo na Korogwe Mjini. Huu ndio utakuwa ufumbuzi wa kuondokana na kero ya maji mjini Korogwe.

Tatu, mradi wa tatu ni maji katika mji wa Hale, Mheshimiwa Waziri atakumbuka mimi na yeye tuliwenda Hale, namshukuru sana. Nataka kumhakikishia hadi leo hii

wananchi wa Hale hawana maji, hali ni mbaya sana.  Hale sasa ni mji mdogo na kuna sekondari mpya.  Baada ya kuonekana kwamba hakuna maji chini ya kisima, iliamuliwa wapate maji ya Mto Ruvu na kuyachuja ili yaingie kwenye kisima na hatimaye kuyagawa kwa wananchi.  Jambo la kusikitisha ni kwamba hadi leo hii mradi huo hauna dalili za kupata maji.  Kero ya Hale sasa ni ya kisiasa.  Tatizo hili ni la kitaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri suala hili la Hale alipatie uzito wa kipekee kuhakikisha sasa wanapata maji.  Wapinzani wa Chama cha Mapinduzi maji Hale sasa ni *agenda* yao, naomba sana ufumbuzi wa kero hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa nne ni maji mji wa Magoma, Makao Makuu ya Tarafa ya Magoma. Mjii huu tumepata msaada mkubwa sana wa shilingi milioni 97 toka *World Vision.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mji wa Magoma wamejitolea kuchimba mtaro kilometa 10 toka katika milima ya Bumbuli kazi ambayo imeokoa zaidi ya shilingi milioni 20.  Bado kuna matatizo ya mabomba ya kusambaza maji mjini na hatimaye kufika hadi *Magoma Secondary School,* mabomba hayo hayapo.  Ili kuunga mkono juhudi za wananchi naomba sana Wizara ituunge mkono kwa kutusaidia mabomba hayo ya kusambaza maji katika mji wa Magoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano ni kuhusu machinjio ya kisasa.  Nashauri Wizara isambaze machinjio haya kwa Kanda badala ya kuwa na hii moja tu ya Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita ni kuhusu majosho.  Naomba kutoa ombi maalumu kwa josho langu la Kata ya Mnyuzi liliko katika Kijiji cha Lusanga kupatiwa fedha kiasi ili likamilike.  Zinahitajika shilingi milioni 1.6 tu kulikamilisha.  Kama utakumbuka nilikwisha kuomba mara nyingi.  Kwa bahati mbaya josho hilo linahudumia Kata zaidi ya kumi, lakini halijapata mgao wowote wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja hii muhimu sana.

**MHE. ESTHERINA KILASI:**  Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza kutoa rambirambi kwa Ndugu na wapigakura wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kwa kifo cha Ndugu yetu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi.  *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza, Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Anthony  Diallo, Naibu Waziri Maji na Maendeleo ya Mifugo, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambazo wamekuwa wakifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika mambo yafuatayo:-

Kwanza, wakala wa uchimbaji maji na Ujenzi wa mabwawa kumekuwa na matatizo makubwa katika utendaji wao wa kazi, aidha, ni kutokana na ukosefu wa vifaa au utalaamu kwani kazi inafanywa kwa kubahatisha.

Nashauri Mheshimiwa Edward Lowassa, aone ni vipi anaweza kusaidia kitengo hiki. Wananchi wamekuwa wakichangia gharama za uchimbaji visima katika Wilaya ya Mbarali na kuungwa mkono na Serikali Kuu lakini matokeo ni ya kusikitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua visima vya wananchi wa Kijiji cha Monovallo, Muhongole vilivyoko katika Kata ya Ubaruku na Kijiji cha Kongaya kilichopo Kata ya Mawindi ni lini vitakamilika ili kuwapa moyo wananchi hawa waendelee kuchangia na waone msaada waliyopewa na Serikali Kuu haupotei bure?

Pili, ni kuhusu uchimbaji wa malambo. Mheshimiwa Waziri amekuwa akihakikisha kuwa Wilaya zote zenye mifugo mingi zinapewa Malambo kwa kuungana na nguvu za wananchi. Wilaya ya Mbarali imepewa shilingi milioni 6.00 kwa ajili ya Malambo mawili, kiwango hiki ni kidogo sana kwani lambo moja dogo halipungui shilingi milioni 9.5, ningependekeza kiwango kiongezwe, vile vile ukizingatia wingi wa mifugo uliyopo Wilayani Mbarali naomba tathmini ifanywe upya ili kuongeza idadi ya Malambo na wananchi wako tayari kuchangia ili kupunguza kasi ya wafugaji kuhama hama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji vijijini. Wilaya ya Mbarali iko kwenye ukame mkubwa sana, naomba Mheshimiwa Waziri aone umuhimu wa kuipa kipaumbele Wilaya hii katika upanuzi wa mradi wa maji ya matumizi ya nyumbani (binadamu) muda mwingi tumekuwa tukitumia visima tu kitu ambacho kimekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi hawa hususan Kata ya Ubaruku, Mawindi, Utengule Usangu na Madibira. Kata hizi zina matatizo makubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu chanjo za mifugo, pamoja na Serikali kuachia baadhi ya magonjwa ya mifugo (chanjo) mikononi mwa sekta binafsi, tunaomba kabla ya kuruhusiwa kuanza kufanya shughuli za chanjo kwa wafugaji, wafanyiwe tathmini kwanza na Halmashauri zao zitoe taarifa mapema kwa wafugaji au elimu itolewe mapema na wajulishwe kuwa nani atawajibika iwapo kutatokea athari kwenye mifugo yao. Kwa kufanya hivyo kutaondoa migogoro mbalimbali ambayo imekuwa ikitokea katika Wilaya ya Mbarali. Ni vizuri kampuni husika ikatangazwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wanaomsaidia Mheshimiwa Waziri katika shughuli zake kwa maana ya Maji na Mifugo hawatoshi. Mbarali tuna Mhandisi wa Maji hana Msaidizi na anaitwa Mkuu wa Idara, shughuli mbalimbali zimekuwa zinakwamam kwa kukosa ufuatailiaji wa karibu. Tunaomba vitengo hivi katika Wilaya ya Mbarali viangaliwe upya ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezo wake na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri naomba aone ni vipi atasaidia tatizo hili la kutenga maeneo ya wafugaji na wakulima Mbarali, vifo vinaendelea siku hadi siku. Naunga mkono hoja.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii ili niweze kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa hotuba yake nzuri na yenye malengo ya matumaini mazuri. Nampongeza sana kwa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa kazi nzuri waliyoifanya katika mwaka wa 2003/2004 na mipango mizuri ya maendeleo wanayotarajia kuitekeleza katika mwaka 2004/2005. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi, sasa naunga hoja hii mkono 100%. Baada ya kuunga hoja mkono sasa nina machache ya kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tarehe 4 Oktoba, 2000 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin Mkapa, alitembelea Wilaya ya Serengeti. Katika hotuba yake Mheshimiwa Rais aliahidi wananchi wa Serengeti kuwa watachimbiwa bwawa la Manchira na kukamilika ifikapo mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Benjamin Mkapa, Rais wetu kwa ahadi yake aliyotoa kwani ahadi hii sasa inatekelezwa na wananchi wa Serengeti wana matumaini makubwa ya kupatiwa maji ya uhakika kutoka kwenye bwawa la Manchira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa na Naibu wake, Mheshimiwa Anthony Diallo, kwa juhudi kubwa walizofanya kufuatia ahadi ya Mheshimiwa Rais ya bwawa la Manchira na linachimbwa. Miaka yote minne nikiwa hapa Bungeni tumeshirikiana na Mheshimiwa Edward Lowassa kwa karibu sana na kuhakikisha kuwa Bwawa la Manchira linachimbwa, sasa kazi imeanza tangu mwezi Februari, 2004 na kazi hiyo inaendelea vizuri na watu wote wa Serengeti wanamshukuru sana Mheshimiwa Edward Lowassa kwa juhudi zake za kufuatilia bwawa hili kwa karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kuwapongeza wafanyakazi wote wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kufuatilia ahadi ya Rais. Wafanyakazi hawa wamefanya kazi nzuri na wanastahili pongezi nyingi sana. Naomba wawe wanajisikia nyumbani wakati wakiwa Wilayani Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa kazi ya ujenzi wa bwawa la Manchira inaenda vizuri sana namwomba Mheshimiwa Edward Lowassa, aendelee kufuatilia kwa karibu ili kazi hii iweze kukamilika kabla ya mwaka 2005 haujaisha ili ahadi ya Mheshimiwa Rais iweze kutimia kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Serengeti ni ya wafugaji, pamoja na msaada mkubwa Serikali imetupatia mashine ya kuchimba *Charcore dams* katika Wilaya ya Serengeti. Tunaomba Serikali isichoke kutusaidia kwani bado sehemu nyingi za Wilaya hazina maji kwa ajili ya mifugo na watu. Tunaomba tupatiwe fedha kwa ajili ya kuchimba Malambo madogo katika vijiji vya Rigicha, Rung'abare, Nyambureti, Muchuri, Nyamakendo, Nyamisingisi Kemogesi na Msati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuiweka Wilaya ya Serengeti katika mradi wa maji unaogharamiwa na Benki ya Dunia. Tunaloomba sasa ni kuwa mradi huo uanze mapema iwezekanavyo. Sisi wananchi wa Serengeti tumechanga fedha zinazohitajika kuchimba visima kupitia mradi huu na tutaendelea kuhamasisha wananchi wa vijiji vilivyobaki kuchanga fedha ili waweze kuchimbiwa visima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumaliza kwa kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii. Naunga mkono hoja 100%, asante sana.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampa *sobhai* Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kumpongeza yeye na Naibu wake kwa kazi nzuri sana katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msukumo wa Wizara hii umesaidia sana kupunguza kero ya maji nchini. Hasa kwanza, utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji toka Ziwa Victoria kwenda Miji ya Shinyanga na Kahama naamini baadaye itafuata Nzega na Igunga.

Pili, mradi mkubwa wa maji wa *World Bank* katika Wilaya 50, endeleza kusukuma watendaji hasa Wilayani kuhakikisha maji yamewafikia wananchi vijijini na tatu, uchimbaji wa Malambo kwa ajili ya mifugo, kitendo hiki kiendelee kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iangalie kwa makini juu ya sheria ya kuogesha mifugo. Je, haiwezekani kukawa na ruzuku kwa sekta ya mifugo kama ilivyo katika sekta ya kilimo? Sheria iongezewe nguvu ili wafugaji wote waogeshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mpango gani wa kuendeleza kiwanda cha nyama Shinyanga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza tena waendelee kwa kazi, uzi ule ule.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Bajeti 2004/2005 ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote natoa pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, Mbunge wa Ulanga Mashariki, aliyefariki ghafla Dodoma hivi karibuni. Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kubuni mipango mizuri ikiwemo mradi wa maji na usafi wa mazingira vijijini *(Rural Water Supply and Sanitation Project - RWSSP)* ikiwemo Wilaya ya Liwale inayofadhiliwa na mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia. Kwa niaba ya wananchi wa Liwale tunamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuiteua Wilaya ya Liwale ambayo ni Jimbo langu kuwa miongoni mwa Wilaya 50 zitakazonufaika na mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kueleza kwamba wananchi wa Liwale wameshaanza kuchangia juhudi hizi za Serikali kwa vitendo kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya ya Liwale. Mradi huu utasaidia upatikanaji wa maji kwa baadhi ya vijiji na pia Liwale Mjini ambayo mfumo wa maji ni wa zamani haitoshelezi mahitaji ya hivi sasa kwa vile wakazi wameongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya maji katika Jiji la Dar es Salaam bado ni mbaya, pamoja na kwamba mwendeshaji ni *City Water,* maeneo mengi ya mji wa Dar es Salaam ama hawapati maji kabisa au wanapata kwa mgao. Matokeo ni kwamba wananchi wengi wananunua maji ya boza au madumu ambayo hayana uhakika wa usalama wake. Nashauri Wizara ifuatilie kwa karibu zaidi kuona kama maji yanayouzwa kwenye maboza au madumu ni safi. Nani anayeyakagua maboza kama kweli yana usafi wa kutosha kuchukua maji kwa matumizi ya binadamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba Wizara inapofuatilia ubora wa maji, ijulishe wananchi mara kwa mara ili wachukue tahadhari. Nchi nyingi huwatangazia wananchi wake endapo maji yana kasoro yoyote, pia Wizara ivikague visima vinavyochimbwa kiholela mikoani na hasa mijini kama Dar es Salaam maeneo ya Sinza na kadhalika kama maji yanayopatikana kwenye visima hivyo ni salama. Wasiachiwe wachimbaji peke yao kuamua kuchimba kibiashara bila ya kuchukua tahadhari ya afya kwa watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kufuatilia kwa karibu mifugo hasa ng'ombe. Nashauri Serikali iongeze juhudi kwa mifugo mingine kama mbuzi, kondoo hata kuku, bata na kadhalika vinginevyo tutaagiza kuku kutoka nje.

Pia Serikali iandae utaratibu/mkakati wa kuboresha ufugaji wa kuku nchini hadi kufikia kiwango cha kuuza nje *(export).* Newzealand ilikuwa ina *export* kuku na mayai. Katika *supermarket* baadhi wanaagiza kuku au bata kutoka nchi za nje kama Afrika Kusini na kadhalika. Ni vyema Tanzania tukawa na utamaduni wa kuzalisha kuku au bata bora kwa lengo la matumizi ya nchini na kuuza nje *(export).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kutoa pongezi tena na kuunga mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri wanayoifanya kuiendeleza sekta hii. Hakuna kipofu ambaye haoni mabadiliko yanayofanyika katika kupunguza kero za wananchi hasa katika sekta ya maji. Wizara imekuwa makini sana katika kujenga mahusiano mazuri na nchi mbalimbali wahisani na mashirika ya nje ili kusaidia kuendeleza huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia machache ili kuboresha sekta hizi. Sote tunaelewa kuwa mifugo ni sekta muhimu sana katika kuondokana na umaskini hasa umaskini wa watu vijijini. Tukiweza kuiendeleza vizuri sekta hii, itatusaidia pia kuondokana na njaa, kumaliza vifo vya watoto, kuondokana na magonjwa ya kuambukiza na mengineyo, kupunguza tofauti za kiuchumi, kijinsia na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanikisha haya, ni muhimu wananchi vijijini waelimishwe sana kujiunga pamoja katika vikundi ili kuunda vikundi vya ufugaji hasa wa wanyama wadogo wadogo kama sungura, nguruwe, kuku, bata na wengineo. La muhimu ni kuhakikisha kuwa maafisa Ugani *(Extension Staff)* wanawatembelea na kuwapa maarifa ya ufugaji.

Pili, utafutwe utaratibu wa Serikali kutoa mikopo midogo midogo ili kuendeleza vikundi na tatu, suala la magonjwa ni kubwa, ndilo linalorudisha nyuma suala la ufugaji hasa vijijini. Hapa nchini kwa mfano, watu wengi wanakula nyama ya kuku wa kienyeji kuliko kuku wa kisasa. Kwa sababu hiyo, kuna haja kubwa sana kwa Serikali kushughulikia suala la madawa ya mifugo, la sivyo, ufugaji ni jambo gumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama Pakistan imepoteza umaarufu mkubwa katika sekta ya mifugo kutokana na magonjwa mpaka wanalazimika kuomba msaada kutoka Mashirika ya Kimataifa kusaidia kifedha na kiutaalamu. Tukinge kabla ya kutibu.

Tatu, ni suala la mafunzo ya ufugaji. Kama ilivyo kwa Kilimo wataalam wa Mifugo wapate mafunzo ya ufugaji ikiwa ni pamoja na wafugaji wenyewe vijijini kupitia vikundi au mmoja, mmoja. Kupitia mafunzo haya, wafugaji wanapata uelewa mwingi wa namna ya kuendeleza mifugo yao na elimu kuhusu utunzaji wa mahesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji, mradi wa hifadhi ya maji ya mvua kwa njia ya mabwawa ni muhimu sana kama Wizara inavyoelewa lakini pia ni gharama. Kwa kuwa maeneo kama ya Mbarali, Same, Chunya na Mwanga yana ukame mwingi, kuna umuhimu mkubwa kwa Wizara kutafuta ufadhili wa kugharamia miradi kama hii hata kama ni kwa awamu. Maji mengi ya mvua hasa yanayotiririka kutoka milima ya Upare yanapotea tu lakini ni muhimu kwa mifugo na Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na miradi mikubwa kama hiyo, kuna haja ya kutoa elimu ya uchimbaji wa mabwawa madogo madogo. Juhudi kama hizo pia zinaweza zikasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo, naunga mkono hoja ya Waziri asilimia mia moja.

**MHE. PROF. PHILLEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Rorya kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara kwa ushirikiano na wananchi wa Rorya kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maendeleo ya mifugo na huduma ya maji, utekelezaji wa Ilani ya CCM imejieleza bayana pale wananchi wa Kata za Goribe, Roche na baadhi ya Kata ya Kitembe kwa muda mrefu kabla na baada ya Uhuru walikuwa wanapata maji kwa ajili ya matumizi yao binafsi na mifugo yao kutoka nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuhamasishwa na maafisa wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na Mbunge wao, wameweza kuchimbiwa Malambo matatu na kumaliza kabisa kero kubwa ya miaka mingi ya kufuata maji nchi ya jirani. Wanaishukuru CCM na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri kuwa kero ya maji kwa wananchi (wafugaji) Jimbo la Rorya, wanaishi mbali kutoka Ziwa Victoria, bado ni kubwa. Nilitoa ombi maalum kutoka kwa wananchi (wafugaji) kuhusu kupatiwa Malambo matatu, barua kuhusu orodha ya Malambo kwa majina, Kata na Tarafa nilimpelekea Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri awafikirie kwa moyo wa huruma wananchi (wafugaji) wa Jimbo la Rorya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, wananchi wamemwomba Mheshimiwa Waziri awatembelee ili waweze kumshukuru. Naunga mkono hoja.

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuweka kwako utaratibu huu ambao umenipa fursa kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusikilizwa hotuba hii na kupitia kwa kina vipengele mbalimbali, napenda kuthibitisha kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kigoma Kusini na mimi binafsi nampongeza Waziri, Mheshimiwa Edward Lowassa pamoja na Naibu Waziri wake, kwa sababu Wilaya ya Kigoma Vijijini ni miongoni mwa Wilaya 38 ambapo programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini itatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru kwa namna ya pekee Naibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Diallo, kwa kunifafanulia matarajio hayo ya maji katika Jimbo langu na Wilaya ya Kigoma kwa ujumla mwaka 2003/2004 nilipofuatilia matatizo hayo

Ofisini kwake Dar es Salaam. Naishukuru Wizara nzima na ni vivyo hivyo kwa wananchi ninaowawakilisha wanavyobainisha tunapobadilishana mawazo ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi, shukrani na ushauri niliokwishatoa kupitia Kamati ya Kilimo na Ardhi, ambamo mimi ni mjumbe nina maoni na ushauri wa ziada kama ifuatavyo:-

Kwanza, mradi wa uvunaji wa maji ya mvua, ni vema upewe kipaumbele kwa sababu mvua nyingi imekuwa ikinyesha na maji yake ambayo ni raslimali kubwa na muhimu kupotea. Hatua hii iandamane na usimamizi wa kutengeneza vifaa vya kukinga na kuhifadhi maji nchi nzima kwa sababu hata sehemu zenye maji mengi, si safi na salama ukilinganisha na maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubora wa maji ni muhimu kama ulivyo wingi wa maji, kwa sababu inakadiriwa kiasi cha 80% ya magonjwa yote yanasababishwa na maji yasiyo safi na salama na 90% ya vifo milioni 15 kila mwaka katika nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mradi huo upewe msukumo unaostahili, ni vema kuangalia upya sera ya maji kwa sababu haiusisitizi ipasavyo uvunaji wa maji ya mvua au teknolojia kwa shabaha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vitakavyofanikisha utekelezaji wa mradi huo vitambuliwe na kupewa ruzuku na/au tuzo kufidia gharama za vifaa watakavyokuwa wametumia katika utekelezaji wa mradi huo. Nashauri motisha kama hizo zielekezwe kwa miradi ya vikundi na hata watu binafsi.

Nafurahi kuambatisha uzoefu wa sehemu nyingine, hata zilizoendelea katika suala la maji kupitia mawasiliano kati ya Dr. Kaitilla/Ndeka *(E-Mail)* (Mawasiliano katika utandawazi), ili kuimarisha ushauri katika mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa na umakini ulioonyeshwa na Wizara katika mtawanyiko na uwiano, idadi ya maeneo yaliyofanyiwa uchunguzi wa maji chini ya ardhi mwaka 2003/2004 , Kigoma Vijijini haikuwamo lakini mwaka 2004/2005 imo chini ya programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalopenda kufahamishwa ni je, mradi huu wa maji na usafi wa mazingira utafanya pia uchunguzi wa maji chini ya ardhi zoezi ambalo halikuhusisha Wilaya ya Kigoma Vijijini mwaka uliopita? Na je, mradi huo utajumuisha uchimbaji visima na ujenzi Mabwawa kwa kutumia wakala wa kuchimba visima *(DDCA)* kwani Mkoa mzima wa Kigoma haumo kabisa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango yangu Bungeni, iwe kwa kauli au maandishi, nimekuwa mara zote nikisisitiza umuhimu wa kutambua utajiri mkubwa wa raslimali za aina mbalimbali Mkoani Kigoma na Ukanda wa Magharibi kwa ujumla na kwamba ni muhimu majanga yanayotishia uharibifu wa raslimali hizo yakadhibitiwa

mapema. Nashauri sana Wizara ijielekeze kwa namna ya pekee katika eneo hilo kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza kwa muhimu wa viambatisho Na. 4 (a) na (b) hakuna kazi yoyote iliyotekelezwa kusimamia raslimali za maji kwenye bonde la Ziwa Tanganyika katika mwaka 2003/2004. Bonde la Ziwa Tanganyika linagusa Mikoa ya Shinyanga, Tabora, Rukwa na Kigoma kwa sehemu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bonde hili lilipofunguliwa mwaka 2003/2004 hakuna kilichotekelezwa na mwaka 2004/2005 utekelezaji unapoanza ni vyanzo 50 vitakavyokaguliwa, ikilinganishwa na vyanzo 1132 (Rufiji), 392 (Pangani), 169 (Ziwa Victoria), 127 (Nyasa), 117 (Kati) na 373 (Bonde la Ruvu) ikijumuishwa miaka 2003/2004 na 2004/2005, linaloshtua zaidi ni hotuba kubainisha kwamba hata vyanzo hivyo 50 vitakapokuwa vimekaguliwa hakuna hati yoyote itakayotolewa si ya muda mfupi wala ya kudumu na kwamba hakuna mgodi au kiwanda kitakachokaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Tanganyika, ambalo ni raslimali kubwa na ya kujivunia kwa nchi yetu, linatishiwa na uchafuzi wa mazingira kutokana na kushambuliwa uoto wa asili katika ukanda ambao ni vyanzo vya mito inayotiririka katika Ziwa hilo *(catchment area)* eneo ambalo linalipatia Ziwa hili 30% ya maji yake, Mto Malagarasi ukiongoza kwa kuchangia kiasi kikubwa zaidi cha maji katika hiyo asilimia 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchunguzi uliofanywa na watafiti wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dr. Hudon Nkotagu, Mtaalamu wa Haidrolojia) amegundua chembechembe za kemikali za *mercury* na za madawa ya kupulizia tumbaku katika Mabwawa ya Nyamagoma, Kata ya Nguruka Jimbo la Kigoma Kusini. Inadhaniwa zebaki na kemikali nyingine zinatoka katika migodi ya Bulyanhulu/Kahama maeneo ambayo ni vyanzo vya Mto Muyovosi na/au Nzega ambako ni chanzo cha Mto Igombe ambayo yote inaingia katika Mto Malagarasi na kuishia Ziwa Tanzanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kuenea makambi ya Wakimbizi Mkoani Kigoma (makambi kumi), Tabora moja, Mpanda matatu na wote hao wakitegemea kuni toka popote pale hata kama ni vyanzo vya maji ni sababu tosha na nzito kwa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kukagua vyanzo vingi zaidi. Lakini ukaguzi pekee haitoshi ni vema hati zitolewe za muda mfupi na wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukaguzi wa migodi ni muhimu na kwa kweli unatakiwa kwa haraka. Mfano, kwanza, Mgodi wa chumvi wa Uvinza ni tishio kubwa la vyanzo vingi vya maji kwa sababu ya matumizi ya kuni wanazokata kutoka kwenye misitu ya asili. Kwa karibu karne nzima sasa uvunaji misitu ya asili kama chanzo cha nishati kwa ajili ya kuzalisha chumvi umekuwa ukiendelea.

Pili, vipo viwanda vidogo vya Chokaa na Pemba ambavyo navyo vinatishia vyanzo vya maji na tatu, kilimo cha tumbaku, licha ya uchafuzi wa mazingira kupitia

mbolea za chumvi chumvi na madawa wanayopulizia mashambani, kinatishia vyanzo vya maji kwa ukataji miti kupata kuni za kukaushia tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni matarajio yangu na watu na Jimbo la Kigoma Kusini na Mkoa kwa ujumla kwamba pamoja na shughuli nyingi zinazomkabili Waziri, atamudu kutenga siku chache katika kipindi kilichobaki, kwa ajili ya ziara Mkoani Kigoma. Hilo likiwezekana nitapendekeza akague Mito ya Luiche na Lugufu na sehemu ya Mto Malagarasi, ambako katika jitihada za kutafuta maji wanayoona ndiyo pekee safi na salama, hasa wakati wa kiangazi wananchi kadhaa wameishia kukamatwa na mamba wakali, kuliwa au kupata vilema vya kudumu. Uvunaji wa maji ya mvua utawaepusha na madhala haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia utekelezaji mwema wa Bajeti hii ambayo naiunga mkono na naamini Bunge zima litafanya hivyo.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, natoa pole kwa familia na wananchi wa Ulanga Mashariki kwa kuondokewa na mpendwa wao Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira na namwomba Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Pili, natoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri Edward Lowassa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu na Naibu wake, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri na inayoonekana dhahiri katika kuendeleza mifugo na miundombinu ya maji nchini. Hongera sana.

Baada ya pongezi hizo kuna maeneo machache ambayo napenda kuyatilia mkazo na mengine yatahitaji ufafanuzi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa 27 wa hotuba nimefarijika sana kuona kwamba Wizara imedhamiria kufanya usanifu wa miradi ya maji hasa kwa miji ya Masasi na Nachingwea kwa kutumia Chemchem ya Mbinyi ambayo iko maeneo ya *Makonde Plateua.* Nafahamu tatizo la maji katika mji wa Masasi kwa vile mimi ni mzaliwa na mkulia wa sehemu hiyo. Mji wa Masasi umekuwa na matatizo ya maji kwa muda sasa hasa baada ya maji ya Bwawa la Mchema kukauka kabisa. Ingawa Serikali ilitoboa mlima ulioko pale mjini lakini maji yake ni ya chumvi sana kiasi kwamba wananchi wanayatumia kwa shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tegemeo la maji lilikuwa visima vya kienyeji ambavyo baadaye viliendelezwa na mradi uliofadhiliwa na Serikali ya Finland, lakini miundombinu yake iliharibiwa na wananchi ambao hawakujali kuitunza. Pia mji wa Nachingwea umekuwa na matatizo ya maji kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nina imani kwa kutumia chemchem ya Mbwinji kwa kuvuta maji toka huko basi tatizo la maji katika miji hii miwili litapungua kama siyo kwisha kabisa hasa ukienda sambamba na miradi ya uchimbaji wa visima virefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Serikali imeendelea kutoka miongozo mbalimbali kuhusu sekta ya maji na kadhalika kwa upande wa taratibu za kutambua wananchi ambao wanapaswa kusamehewa ulipiaji huduma za maji bado hazifuatwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wizara ikishirikiana na wadau wengine isisitize utekelezaji wa taratibu hizo lakini zaidi elimu itolewe kwa wananchi ili wafahamu cha kufanya endapo watakuwa kwenye kundi la jamii inayoshindwa kulipia huduma za maji mijini na vijijini. Elimu ya uvunaji wa maji kwa teknolojia ya kisasa itolewe kwa wananchi kwa kasi kubwa zaidi isibakie kwa watafiti tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa 77 wa hotuba umeeleza kuwa wananchi wamefundishwa jinsi ya kuua mbung’o kwa kutumia mionzo ambao ulifanikiwa huko Zanzibar. Hivyo nashauri endapo utaalamu huo unafaa uenezwe katika Wilaya zenye matatizo ya mbung’o kwa sababu itasaidia kukomesha mbung’o hao kuendelea kuzaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kushauri haya naomba ufafanuzi, je, wakala wa uchimbaji wa Visima na ujenzi wa Mabwawa *(DDCA)* unachimba visima vya Serikali tu au hata wadau binafsi wanaweza kutumia wakala huu kwa kutoa utaalamu huo wa uchimbaji visima? Je, kuna uhusiano gani kati ya Wakala *(DDCA)* na mamlaka za Maji Mijini kwa mfano *MOROWASA, DAWASA, DOWASA* na kadhalika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maswali haya naunga mkono hoja na kuwatakia kila la kheri Waziri na watendaji wote wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu waliyojipangia kwa mwaka 2004/2005.

**MHE. SUMRI A. S. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani za dhati kwa kuweza kunipa nafasi ya kuchangia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii pendwa. Aidha, napenda kutoa pole kwa msiba uliyotupata wa kufiwa na Ndugu yetu mpenzi Mheshimiwa Kepteni Mstaafu Theodos Kasapira, Mbunge wa Jimbo la Ulanga Mashariki, pole tele kwa familia na wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, Mola aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiunga mkono hotuba hiyo ya Mheshimiwa Waziri na kuiunga mkono asilimia mia kwa mia na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Diallo, Makatibu na Wahandisi wote Mikoani na Wilayani kwa kazi yao nzuri inayoonekana, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wapigakura wangu, wa Jimbo la Mpanda Magharibi, napenda kuwashukuru kwa uvumilivu wao wa kuwa na matumaini ya kupata maji safi na salama, ingawa katika sehemu nyingi bado hatuna maji safi na salama. Vijiji vingi vya Kata ya Wabungu, Kata ya Mpanda Ndogo na pia Kata ya Mwese na Katuma, vile vile Kata ya Karema, Kata ya Ikola, bado wana shida kubwa ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya Kakase yana wafugaji wengi ambao wana matatizo makubwa ya malisho ya mifugo na maji. Hali hiyo ipo katika Kata zote nilizozitaja.

Katika hotuba ya Waziri ya bajeti ya mwaka 2003/2004, niliomba tusaidiane kuwekewa Bwawa pale Kakese, Katuma na Kata ya Karema. Bado tena tunazidi kumwomba Mheshimiwa Waziri, atufikirie juu ya Mabwawa hayo na hasa Kakese, ambapo utafiti ulikwishafanywa. Bonde hilo ni kubwa kwa kilimo cha umwagiliaji na malisho kwa mifugo.

Katika vijiji vya Mwese, napo tunahitaji visima na pia kule Bujombe katika vijiji vya Karema na Ikola, Kasanga, Mtongwe, Isengule, Kafisha, Kalumbi, Tupondogoro na Ipako, wote hawa hawana visima virefu. Baadhi ya vijiji vina visima vifupi ambavyo ifikapo mwezi Septemba vinakuwa vimekauka maji na kuleta matatizo ya maji kwa wananchi. Jimboni kwangu kuna vijiji vya Mpanda Ndogo karibu vyote havina visima na vilivyopo vichache vinawahi pia kukauka wakati wa kiangazi. Hivyo tunaomba kwa Mheshimiwa Waziri, atupe kipaumbele walau hata visima viwili kwa kila Kijiji. Eneo letu lipo nyuma sana. Naomba nguvu kubwa kutoka kwake ili tutengewe fungu maalum kwa ajili ya Jimbo la Mpanda Magharibi ili tuweze kutekeleza Ilani yetu ya Uchaguzi. Hali ni ngumu sana kwa upande wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000, kuhusu kuendeleza sekta ya maji na mifugo inasisitiza juu ya ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji kufufua na kujenga Mabwawa ya maji, hivyo tunaiomba Wizara kwa hilo tuweze kupata majosho kule Karema, Mwese, Kakese, Ikola na Mpanda Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia na kule Mishamo, kuna visima vingi vilivyoharibika vilivyoachwa enzi ya *TCRS,* tunaomba Wizara iweze kutusaidia ukarabati wa visima hivyo kwa matengenezo ya *pump* zilizoharibika. Kwa kuwa ni visima vingi vilivyoharibika vijiji vya Isenga, Bulamata, Kamsanga, Mbogwe na maeneo ya Mwamkuri, Nkungwi, Kasekese, Kaseganyama, Kibo na Igalula, pia na Sijonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara na Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwa kuweza kufikiria swala la upatikanaji wa dawa za mifugo kwa bei nafuu kwa kutoa ruzuku kwa wafugaji, hilo litafurahiwa sana na wafugaji wetu na kuona kuwa sekta ya ufugaji inathaminiwa sana kwa mchango wao wa uchumo, hasa kwa uchumi tunaojenga sasa kwa mifugo. Katika maeneo yetu tunaiomba Wizara iweke maeneo ya Kakese, Sibwesa, Kasekese, Katuma, Nkuswe, Kafisha, Mpanda Ndogo, tuwekwe katika mpango wa udhibiti wa mbung'o chini ya mpango wa *Farming in Tsetse Controlled Areas.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema yote hayo nizidi kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa juhudi za kweli anazotuonyesha kwa maendeleo ya Ilani yetu ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, mia kwa mia.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi na kimsingi naiunga mkono hoja hii bila kigugumizi chochote kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba nichangie kwa ufupi kama ifuatavyo:-

Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri mnayofanya katika Wizara hii. Kazi yenu ni nzuri na imetambulika nchini kote. *Let me say keep it up.*

Pili, shughuli za mradi wa maji na mazingira chini ya Benki ya Dunia ambao umeanza vizuri kule Kondoa, ni sehemu ya juhudi nzuri za Mheshimiwa Edward Lowassa na Naibu wake, Mheshimiwa Anthony Diallo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zimeanza katika vijiji kumi na mji wa Kondoa wa kumi na moja. Nawashukuru na kuwapongeza sana.

Tatu, pamoja na ufanisi huo, naomba Waziri arejee barua yangu ya mwezi Juni ya kuomba baadhi ya Vijiji ambavyo mifugo yao ina shida sana ya maji, wachimbiwe Malambo yaani Mabwawa madogo madogo kama ilivyo kwenye barua yangu, ni muhimu sana. Najua Wizara yake ina mfuko wa shughuli hizo ambazo wananchi wa Halmashauri hutakiwa kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji hivyo ni Keikei, Bumbuta, Atta, Mwembeni, Kikilo-Kati, Mitati (Mihembeti), Isari na Hondomairo. Hivyo vingi vyao ni vipya na vinakaliwa na jamii ya Kibarabaig, Wambulu, Wamasai, Wasandawe na Warangi. Naomba wapewe umuhimu wa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kuna bonde kubwa sana la Mto Bubu linalopita katika sehemu ya Vijiji vilivyopo katika Wilaya ya Kondoa na Jimbo la Kondoa Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuanzishwa mradi mkubwa wa kujenga Bwawa kubwa eneo la Munguri ili kusimamisha maji ambayo yataleta faida zifuatazo:-

Vijiji zaidi ya kumi kuondokewa na matatizo ya maji ya watu na mifugo, vijiji zaidi 15 na wakazi wa Mji wa Kondoa watashiriki Kilimo cha Umwagiliaji, ufugaji wa samaki utaibuliwa na umaskini utapungua. Naunga mkono hoja.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia japo kwa maandishi. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Simanjiro na mimi binafsi natoa pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira na wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kwa kifo cha Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, Mungu aiweke roho yake mahala pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri wa Maji na Maendeleod ya Mifugo. Nampongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Anthony Diallo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watumishi wa Wizara hii kwa mengi ya mafanikio katika muda huu mfupi toka kuanzishwa Wizara hii. Pamoja na pongezi hizo nina yafuatayo:-

Kwanza, Maji, namshukuru Waziri, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa juhudi za kupunguza tatizo la maji katika Wilaya ya Simanjiro. Pia nashukuru kwa Wilaya ya Simanjiro kuingizwa kwenye mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki mbili zilizopita ilionyeshwa kwenye luninga hali ya maji Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro (Orkesumet). Njia pekee na ya kuaminika kuondoa tatizo la maji Makao Makuu ya Wilaya, Orkesumet ni kuvuta maji toka Mto Pangani. Namwomba sana Mheshimiwa Edward Lowassa, suala hili lishughulikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kwamba hili litawezekana kama ilivyowezekana mradi wa Chalinze na Mradi wa Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mgogoro wa Losokonoi, kwa vile kuna Kampuni yenye leseni ya uchimbaji wa Madini, izingatie eneo lake na iache kabisa maeneo ya maji na mifugo. Wahamishe kambi iliyo karibu na maji na kupekeka eneo lake la mita 300 x 300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Lesokonoi wameniomba rasmi nimwombe Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo na Mheshimiwa Daniel Yona, Waziri wa Nishati na Madini wafike eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kwamba popote ambapo wananchi wanamiliki maji kwa utaratibu wa mila, tafadhali wamilikishwe, vinginevyo wageni wajanja watakuja kumiliki hayo maji na patakuwa na matatizo au migogoro mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mifugo, ili kutibu bila kubahatisha, tunahitaji maabara zenye wataalam na vifaa vya kisasa. Kuna maabara mbili kwa kadri ninavyofahamu Arusha na Maabara Kuu ya Temeke, Dar es Salaam. Hivi kweli mfugaji wa Simanjiro, Maswa, Geita, Mbarali na kadhalika ana matumaini kwamba atapata huduma hii kwa usahihi na kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwanza, kila Mkoa wenye mifugo mingi pawepo na kituo cha kuchunguzia magonjwa ya mifugo. Ikiwa na watumishi wenye utaalam na uzoefu na yenye vifaa vya kisasa.

Pili, kila Wilaya yenye mifugo mingi pawepo na huduma walau ya huduma za mwanzo za kuchunguzia magonjwa ya mifugo. Kumbuka kuanzia Chuo cha Mifugo Simanjiro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuzuia magonjwa ya mifugo, kwa sasa kuna magonjwa mengi ambayo yana chanjo lakini mpaka sasa Serikali inachanja bure kwa ugonjwa wa Sotoka na *CBPP.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini wananchi na Taifa kwa ujumla ipoteze fedha nyingi kwa mifugo kufa kwa mgonjwa ambayo kuna chanjo? Je, kwa hali hiyo tutaweza kuuza mifugo/nyama nchi za nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwanza, Serikali ihusike katika upatikanaji kwa wakati na ubora wa dawa za chanjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali ipange ratiba ya chanjo kwa kila ugonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Serikali igharamie dawa za chanjo, kwa magonjwa yote yenye chanjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, wataalam hasa wa ugani wanolewe tena kwa kupewa mafunzo.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba nitumie nafasi hii kutoa pole na rambirambi zangu kwa familia, ndugu na jamaa wa aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, Marehemu Capt. Theodos James Kasapira. Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya Marehemu mahali pema poponi. *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo ya utangulizi, ninaomba nichangie machache katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza na kuishukuru Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kuamua kuiingiza Wilaya ya Kondoa katika mradi wa maji unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Kwa niaba ya Wapiga Kura wangu wa Jimbo la Kondoa Kusini, ninaishukuru sana Wizara na Serikali kwa ujumla kwa uamuzi huo. Pia kwa niaba ya Wapiga Kura wangu, ninaahidi kushirikiana na mfadhili kuondoa kero ya maji katika jimbo langu kupitia mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninaishukuru Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa utaratibu ulioibuni wa kutoa fedha kwa ajili ya kuchimba malambo ya maji katika jimbo langu. Hivi sasa tayari malambo manne yemechimbwa katika Vijiji vya Goima, Jenjeluse, Mapango na Ombiri. Ninataka kumwarifu Mheshimiwa Waziri kuwa, malambo haya yanasaidia tu kuweka maji wakati wa msimu wa mvua, lakini yanakauka mara mvua zinapokatika. Hivi sasa (mwezi Julai), malambo haya yamekwisha kauka. Kwa maneno mengine, hayasaidii kutatua matatizo ya maji, hususan wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hii ya kuendelea kuchimba malambo katika mikoa kame ya Dodoma, Singida, Arudha, Manyara, Shinyanga, Tabora na kadhalika, ni kupoteza pesa ya Serikali bure. Ushauri wangu ni kuwa katika mikoa kame, kama Wizara inataka kuondoa matatizo ya maji, inawajibika kuchimba mabwawa makubwa badala ya malambo. Hivyo, mimi kwa dhati kabisa, ninaiomba Wizara itoe pesa kwa ajili ya kuchimba mabwawa hata machache katika kila Wilaya kwa mwaka katika mikoa kame niliyoitaja hapo juu, badala ya kuchimba malambo mengi ambayo hayana faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, ninaomba niikumbushie Wizara kuhusu ombi langu la kuchimbiwa Bwawa la Farkwa Wilayani Kondoa, ili kutatua matatizo ya maji katika Tarafa za Farkwa na Kwamtoro. Bwawa hili pamoja na kutatua matatizo ya maji, litapunguza umaskini wa Wananchi wa maeneo hayo kupitia shughuli mbalimbali zitakazofanyikwa, ikiwa ni pamoja na kilimo cha umwagiliaji, uvuvi, na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaro wa Ntomoko ambao unategemewa na vijiji zaidi ya 18, umechakaa sana. Ninaiomba Wizara isaidie kukarabati na kuunda chombo cha kusimamia kwa niaba ya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, ninatamka kuwa, ninaunga mkono hotuba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. Ahsante.

**MHE. LEPHY B. GEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wapiga Kura wa Jimbo langu la Mpanda Kati, nianze kwa kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia, kutoa rambirambi zangu kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na Wapiga Kura wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kwa msiba huu mkubwa uliotufika wa Mbunge mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira. Naomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *(Amin)*

Vile vile nitoe pole nyingi kwa familia, ndugu, jamaa, mafariki na Wapiga Kura wa Jimbo la Mbeya Vijij, kwa msiba uliotupata wa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Marehemu Yete Sintemule Mwalyego. Naomba Mwenyezi Mungu, ampumzishe kwa amani. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya remabirambi zangu hizo, nichukue nafasi kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote wa Maji Mijini na Maji Vijijini na Wataalam wote, kwa maandalizi mazuri ya hotuba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi anayoifanya Mheshimiwa Edward Lowassa na timu yake, ni kubwa na anastahili kupongezwa. Pamoja na pongezi hizo, mchango wangu utalenga hasa Jimbo langu na Mpanda Kati. Mpanda ni Mji ambao upo miaka mingi toka 1947. Mpanda ni Mji wa zamani na una historia kubwa kwa kuchangia kwa kiwango kikubwa uchumi wa Taifa hili. Hivyo, ningependa nitoe maombi yangu kwa Mheshimiwa Waziri, naomba sana pamoja na juhudi anazoendelea nazo Mheshimiwa

Waziri kunisaidia, kwanza, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutusaidia kupata mashine ya kusukuma maji *KVA 75* ambayo tayari imeshanunuliwa. Lakini Mheshimiwa Waziri, Mji wa Mpanda umepanuka sana. Ni kwamba, mji huo kwa sasa wanaopata maji ya bomba ni walio katikati ya mji tu. Kwa sababu mtandao wa bomba upo katikati ya mji tu, sehemu nyingine kama Kata ya Ilembo, Mapinduzi, Misunkamilo, Milupwa, Kampuni, Shanwe, Kanajense, Kazima, Kashaulili, Mpanda Hoteli, Makanyagio, Nemulwa na kadhalika, hakuna mtandao wa bomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ningeomba Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, mji huu upewe kipaumbele cha kuwa na mradi mkubwa wa kutandika mabomba sehemu zote ambazo hazina. Kwa sababu uwezo wa mashine tulizonazo zinaweza kutosheleza kupampu maji ya kutosha mji mzima, ili mradi matangi mengine yaongezwe kwa ajili ya sehemu nyingine zote kupata maji ya bomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua Maji ni Uhai. Maendeleo ya haraka yanahitaji kuwa na maji ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote haya bila Wizara kuingilia kati, tutabaki katika hali ya matatizo ya maji kwa muda usiojulikana. Uwezo wa Halmashauri ni mdogo na Mamlaka ya Maji bado changa vilevile. Chanzo chao cha maji ni finyu, kwa sababu wateja ni wachache. Kwa sababu mtandao wa bomba umewafikia watu wachache kuliko ambavyo ingetakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa yote. Maombi haya ayafikirie. Akumbuke vilevile kila siku kuna ongezeko la wagonjwa wa UKIMWI ambao kwa mujibu wa utafiti wa *TGNP* kuwa mgonjwa mmoja anatumia ndoo 20 – 24, hivyo, maji ni muhimu sana kwa afya na mahitaji ya binadamu ya kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nitumie nafasi hii kutoa pole za Wananchi wa jimbo langu na mimi mwenyewe kutokana na kifo cha ghafla cha Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira. Namwomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Anthony Diallo na Katibu Mkuu, Ndugu Vicent Mrisho, ambao wameonyesha kwamba, wao wanafanya kazi kama timu inayoonyesha kuwa Wizara hii ni miongoni mwa Wizara bora nchini. Ninawaomba waendelee na moyo huo katika kuondoa kero mbalimbali za Wizara hii. Lakini pia pongezi za pekee zimwendee Mheshimiwa Edward Lowassa na Mheshimiwa Anthony Diallo, kutokana na ushirikiano wao na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitendo vya hujuma vinavyofanywa na baadhi ya wafanyakazi wa Wizara, ambao wanaamini kuwa kama miradi ya maji haitafanikiwa,

basi mwaka 2005 sitarudi Bungeni. Vitendo vya hujuma kwa maana kwamba, mwaka 1996, Serikali ya Uingereza ilitoa msaada wa *£. 8,000* za Kiingereza ili kuchimba visima viwili katika Kitongoji cha Tipo. Wachimbaji 10 walikaa kijijini siku 28 bila mafanikio. Fedha zilikwisha na maji sikupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 2000 nimeomba kama Mbunge ambaye napata wageni mbalimbali, lakini hadi leo Mhandisi wa Maji hajanipatia kisima hata kimoja. Maji nachota kilomita 27 kwa kutumia *Sim-tanks* lita 5,000 wakati ninapokuwa jimboni. Wananchi wanapata maji ya kungojea umbali wa kilomita sita tangu tupate uhuru. Kwa makusudi Mhandisi wa Maji wa Wilaya anahujumu hata ugawaji wa visima. Mfano hai ni Mradi wa *JICA* Kilwa Kusini, walipata visima tisa na jimboni kwangu visima vitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki ya jana tuliandaa matumizi ya Sh. 24,000,000/= zilizotolewa na *Regional Integrated Programme (RIP).* Kilichotokea, Mchimba Visima Mkuu wa Wizara na Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Kilwa, walimchukua mkandarasi ambaye ana mitambo mibovu ili ahakikishe kuwa maji hayatoki. Mradi unaohujumiwa ni Mradi wa Maji Kata ya Tingi. Mchimbaji na Mheshimiwa Diwani wa Tingi, wamethibitisha njama hizo. Hivyo, haitoshi Afisa huyo anahangaika kugawa vifaa vya michezo jimboni kwangu, amerejea wiki jana. Hivyo, huu ni ushahidi kuwa jitihada zangu zote tangu 1996, zimehujumiwa na huyu Afisa wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho namshukuru Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa jitihada zake za kuleta mifugo Kusini. Tunafaidika na maziwa pamoja na samadi. Mungu awasaidie wandelee na moyo huo wa kuchapa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa ya kuchangia hoja ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Kabla sijafanya hivyo, naomba uniruhusu kuchukua fursa hii kutoa rambirambi zangu kwa familia na Wapiga Kura wa Majimbo ya Uchaguzi ya Mbeya Vijijini na Ulanga Mashariki, kwa misiba mikubwa ya kufiwa na ndugu zetu wapendwa, Marehemu Mheshimiwa Yete S. Mwalyego na Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos J. Kasapira, waliokuwa Wabunge wa Majimbo hayo, kwa vifo vya ghafla na vya kusikitisha sana wakati wakiwa Bungeni kikazi. Mwenyezi Mungu, azilaze roho zao mahali pema peponi na awape ndugu na jamaa wa Marehemu mioyo ya subira. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirejea kwenye hoja, ningependa kumpongeza kwa dhati Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, Naibu wake, Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Vincent Mrisho, pamoja na wafanyakazi wa Wizara na Taasisi zake zote, waliochangia katika maandalizi ya hotuba hii nzuri sana na kazi nzuri zinazofanywa na Wizara hii, ambazo zinaleta matumaini makubwa kwa Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango na utekelezaji wa mipango ya Wizara hii, imezingatia ipasavyo Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000 na Dira ya Taifa ya 2025. Sera na mipango ya Wizara hii ina shabaha nzuri na ina mwelekeo mzuri wa kuifikisha Tanzania pale panapotarajiwa kwa muda mfupi. Hata hivyo, ipo haja kwa Wizara kuwa na tahadhari maalum hasa katika maeneo ya ubinafsishaji na uwekezaji katika sekta ya maji na mifugo. Mfano mmoja ni Kiwanda cha Maziwa Tanga, ambapo aliyekinunua amekigeuza kiwanda hicho kuwa sehemu ya kuhifadhia na kuuza matrekta badala ya kusindika maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uzuri wa sera ya binafsishaji kwa ujumla, kuna haja ya kuangalia kwa makini utekelezaji wake hasa katika vijiji vilivyo duni kiuchumi. Kwa mfano, uendeshaji wa miradi ya maji, malambo na majosho, kwa msingi wa ubinafsishaji na kuwatarajia Wananchi mmoja mmoja kulipia gharama husika, inakuwa vigumu sana. Katika sehemu nyingi bado ipo haja ya kuendesha miradi hiyo chini ya Uongozi wa Serikali za Vijiji au vikundi mahsusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama yalivyo maeneo mengi ya pembezoni hapa Tanzania, Jimbo la Mkinga lipo duni kiuchumi, wakati ambapo jimbo hilo lina raslimali nyingi pamoja na nguvukazi ya kutosha kuwatoa Wananchi wake kutoka kwenye lindi la umaskini walimo. Pamoja na rasilimali nyingi zilizopo, ni maeneo makubwa yenye rutuba na hali ya hewa ifaayo kwa maendeleo ya mifugo na miundombinu bora ya maji safi na salama kwa Wananchi na mifugo. Ningependa kuipongeza Serikali, Halmashauri ya Wilaya, Wahisani na Wananchi wenyewe, kwa jitihada kubwa za awali ambazo zimeanza kuonyesha mafanikio mema. Lakini bado kero ni kubwa na kuna nafasi kubwa ya kupambana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mifugo, hasa ng’ombe wa maziwa, hatua ya kuridhisha imepiga hasa kupitia Ushirika wa *TDCU* na *TADAT.* Miradi ya Ng’ombe wa Maziwa, ilipata msukumo mkubwa chini ya mradi wa *TDDP.* Tokea *TDDP* ikome, kazi ya maendeleo ya miradi ya ng’ombe wa maziwa imepungua. Iko haja kubwa kwa Serikali kusaidia kwa nguvu zaidi hasa kwa kuwasaidia wafugaji kupata mitaji nafuu kwa ajili ya ununuzi wa mitamba, madawa, majosho, malambo, mitambo ya usindikaji, uhifadhi na usafirishaji. Kadhalika, kuna mahitaji makubwa ya huduma bora za ugavi, mafunzo na utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni moja ya kero kubwa sana Jimboni Mkinga. Takriban Kata zote zina kero ya maji, ingawa kero hiyo ingeweza kuondolewa au kupunguzwa kwa kiasi kikubwa kwa gharama isiyo kubwa sana, ikizingatiwa kuwa Jimbo la Mkinga lina mito na vianzio vizuri vya maji vingi. Ni jambo la faraja kubwa kwamba, Wilaya ya Muheza ni miongoni mwa Wilaya zinazotazamiwa kufaidika na Mradi wa Maji chini ya mkopo wa Benki ya Dunia. Naomba Jimbo la Mkinga lipewe kipaumbele cha juu katika kuliondolea kero kubwa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuikumbusha Serikali kwamba, nafasi nzuri iliyopo kwa Jimbo la Mkinga kuchangia katika uchumi na ustawi wa Wananchi wa Jimbo hilo na Tanzania kwa ujumla, haiwezi ikatumika kwa vile katika sehemu kubwa ya

jimbo hilo, hakuna umeme, hakuna mawasiliano, hakuna miundombinu bora na hakuna hata maji. Uwekezaji na maendeleo endelevu katika Jimbo la Mkinga ni ndoto. Kwa kuanzia, tunaiomba Serikali ilikumbuke jimbo hili angalau kwa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba mkubwa wa maji Jimboni Mkinga, siyo tu kero na hatari kubwa kwa Wananchi, mifugo na shughuli nyingine za uchumi, bali ni aibu kubwa sana, hasa maeneo ya mipakani kama vile mpakani Horohoro, Mwakijembe na Jasini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya hizo Kata za Mpakani za Duga, Mwakijembe na Moa, takriban kata zote nyingine zikiwemo Kanza, Mkinga, Mtimbwani, Kwale, Combero, Maramba, Mhinduro, Kigongoi na Dahini, zina vijiji vingi vyenye kero kubwa ya maji. Kero hii ni kubwa kiasi kwamba, Wananchi na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, bila msaada wa Serikali Kuu na Wahisani, hawawezi kuondoa kero hii.

Hivyo, naiomba sana Serikali itoe kipaumbele cha juu kabisa katika kuondoa angalau kero hii kubwa ya maji kwa Jimbo la Mkinga ili hatimaye kero za umeme, mawasiliano, miundombinu, afya na elimu, ziweze kushughulikiwa mapema iwezekanavyo kwa awamu ili Jimbo la Mkinga nalo lianze kufaidi matunda ya uhuru na kuingia katika mkondo wa maendeleo kama sehemu nyingine za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurudia ombi langu kwa Serikali kutoa kipaumbele maalum kwa Jimbo la Mkinga, kama vile sehemu nyingine za nchi hii, zilizo katika hali duni kiuchumi na kimandeleo kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupatiwa nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, ambayo naiafiki asilimia mia kwa mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze sana Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu, rafiki yangu, Ndugu Vincent Mrisho, Naibu Katibu Mkuu, Dr. Charles Nyanda, pia Ndugu Mutalemwa, Mkurugenzi wa *DAWASA* na Kitengo cha kuchimba Visima Ubungo, kwa ushirikiano wa hali ya juu katika kunisaidia kuondoa kero mbalimbali kwenye Jimbo langu la Kinondoni na kwa ujumla Jili la Dar es Salaam. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina nyongeza juu ya matatizo ya maji safi na salama kwenye Jimbo langu kwa sasa, mbali na yale maombi ya kwenye swali langu la tarehe 22 Julai, 2004. Maeneo hayo, naomba Serikali iwasiliane na *City Water*, watusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo mchango wangu ni wa Kitaifa, kuhusu vianzio vya maji vinavyochafuliwa kwa makusudi kabisa na baadhi ya Wananchi wasiojali uhai wa Watanzania wenzao. Sasa wakati umefika kwa Serikali ambayo najua inajali

maisha/uhai wa Taifa hili na Wananchi wake, kwa sasa kudhibiti ki-dola maeneo yote ya nchi yetu yenye vianzio vya maji ili Taifa hili na Wananchi wake waendelee kufaidika na maji hayo aliyopewa Mtanzania na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi majuzi kulikuwa na taarifa ya maeneo ya misitu ya Mkoa wa Dar es Salaam (Temeke/Ilala) na pia maeneo ya vianzio vya mto huko Singida/Kondoa, yaliyovamiwa na Wananchi wasiojali uhai wa wenzao. Je, kweli Serikali inashindwa kuwatia hatiani hawa wahalifu? Naomba sana tena sana, Serikali idhibiti vianzio vyote vya maji ya nchi na ikilazimu kuajiri walinzi kwa maeneo yote ya vianzio vya maji ili kuhakikisha nchi hii haigeuki kuwa jangwa kwa kujitakia sisi wenyewe kwa uzembe tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili naliomba sana tena sana lizingatiwe na litekelezwe kwa maana ya kuwa *at the sight of every source of water* aliyotupa Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Lakini nina ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vingi vya maji nchini, vinaharibiwa na Wananchi. Hawa Wananchi wanapoharibu vyanzo kwa kulima au kukata miti, hawafanyi kwa makusudi, wengi upeo wao wa kuelewa ni mdogo. Lakini watendaji wa Serikali hawafuatilii wala hawatoi ushauri au maelekezo kwa Wananchi. Hali hii iliyoachwa na viongozi na watendaji wazembe, imeonyesha athari kubwa ya vyanzo vingi vya maji kukauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali sasa ilete Muswada na Sheria ambayo itakibana kila kijiji kutunza vyanzo vya maji. Aidha, Wizara hii ingeandaa mkakati wa kuhamasisha na kuelimisha Wananchi juu ya umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji. Huu uwe mradi kamambe nchi nzima, ama sivyo nchi yetu itageuka jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina mito mingi mikubwa ambayo ingeweza kuleta ukombozi kabisa kwa Wananchi katika suala la maji. Lakini maji haya yote yanaishia baharini. Nchi yetu haina mpango wowote wa kuyatunza au kuyakinga maji haya. Wizara ilishapeleka ujumbe Misri. Kama mlizinguka, mliona jinsi Misri inavyotumia vizuri maji ya Mto Nile, wametengeneza Bwawa la Aswan, ambalo linazalisha umeme na kivutio cha utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina mito mingi kama Rufiji, Mbwemkuru, Ruaha na kadhalika, mabwawa yaliyojengwa ni ya kutegea umeme tu. Maji ya Mto Ruvu yote yanaishia baharini. Ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuvuna maji haya? Ukitokea ukame kama wa mwaka 2003, tunahangaika. Nashauri Wizara iwe na mikakati inayoeleweka ya kuweka mabwawa kando ya mito mikubwa ili kuvuna maji. Wizara hii iliahidi kufuatilia hili katika kujibu hoja yangu, katika bajeti ya 2002/2003, lakini hadi

sasa hakuna mpango wowote. Nashauri tusichelewe, mipango ianze haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarafa ya Ng'apa, Lindi Vijijini, hawana maji ya uhakika. Wananchi wanategemea Mto Lapululu na visima vichache. Lakini kipo kisima ambacho kilichimbwa na watafuta mafuta, ambacho kilizibwa, nashauri Serikali ifukue kisima hiki ili Wananchi waweze kupata maji safi ya uhakika. Kama maji yatakuwa mengi, kisima hiki kinaweza pia kuwa jawabu kwa Wananchi wa Mji wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Hai katika Wilaya ya Hai, ni mojawapo ya Wilaya inayokabiliwa na ukame wa mara kwa mara, hususan kwenye ukanda wa tambarare, wenye Vijiji vya Mtakuja, Rundugai, Tindigani, *Sanya Station*, Kawaya, Shivi Mgungani, Mijongweni, Longoi, Cheki Maji, Cheuka, Kinashuku, Makuna na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukanda huu hukaliwa zaidi na jamii za wafugaji ambao ni wa jamii ya Kimasai, sambamba na makabila mengine, wakiwemo Wapare, Wachaga na hata Wameru. Mifugo huathirika sana na ukame, ambapo wafugaji hulazimika kuhama wakati wa kiangazi sababu ya uhaba wa maji na malisho ya mifugo. Kuhama huku huathiri sana Wananchi hawa na hasa watoto ambao hulazimika kukatisha masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukanda huu una hazina kubwa ya maji safi ardhini. Aidha, ukanda huu una upepo mkali wakati wote. Nishati hii ya upepo inaweza kutumika kwa kutumia *windmills* kwa ajili ya ku-*pump* maji toka ardhini. Maji ardhini ni mengi mno na upepo ni mkali mno kiasi kuwa maji ya kutosha kwa kilimo, mifugo na binadamu, yanaweza kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wananchi wengi wanatumia maji ya visima, ambayo si safi na salama. Aidha, wengine hutumia maji ya mito kutoka ukanda wa milimani (Meru na Kilimanjaro), ambayo pia si safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi hawa, naiomba sasa Serikali isaidie ili *windmills* ziweze kupatikana na zisaidie kuwaondolea Wananchi hawa adha kubwa. Ni imani yangu kuwa, gharama ya *windmills* ni nafuu kuliko umeme ambao hata hivyo hauko kwenye vijiji vingi nilivyovitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri. Naitakia kheri na naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na Wasaidizi wake, wakiongozwa na Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, pamoja na Wataalam wote, kwa kuandaa hotuba ya aina yake; kwani imejaa changamoto na kiwango cha hali ya juu ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi nimefurahishwa sana na upeo mkubwa na umahiri aliouonyesha Mheshimiwa Waziri tangu ashike Wizara hii. Nampongeza sana. Sambamba na mafanikio haya yote, napenda tu kuiomba Wizara ikumbuke sana kuwasaidia Wananchi wangu na hasa kuwawezesha kupata maji ya mabwawa, kwani ni tatizo sana jimboni kwangu. Naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kupata malambo katika vijiji vifuatavyo:-

(i) Kuzindua malambo yaliyoziba au kubaribika yafuatayo: Bwawa la Nyaluhande, Bwawa la Nyangili, Bwawa la Shigala Lwangwe, Bwawa la Dilanda Mkula na Bwawa la Mwangika.

(ii) Kuchimba mabwawa madogo madogo *(charcoal dams)* katika maeneo ya Ng'wang'wenge, Mwamigongwa na Jisesa Ngasano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watumishi wote, kwa kazi nzuri waifanyayo kwa mshikamano wa pamoja. Naunga mkono hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ninamshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa Mfuko wa maji kuanzishwa Kitaifa. Kuna umuhimu wa kuwa na mfuko wa Maendeleo ya Mifugo ili kuwa na maji yenye uhakika. Naelewa kuwa maandalizi yalikuwa yanaendelea, lakini kwa nini kasi yake ilikuwa ndogo kiasi hicho, wakati tunaelewa umuhimu wa Mfuko huo kwa uhai wa Taifa letu? Tuanze na fedha zetu wenyewe, nami nitatoa ushauri wa njia mbalimbali za kuchangia Mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 1998/99, kumekuwepo na ahadi za Serikali za kushughulikia mfumo mzima wa maji Mjini Sumbawanga kwa kutumia fedha toka *ADB*. Hata katika hotuba za Waziri kuanzia mwaka 2000 hadi 2003/2004, ziliwajulisha Wananchi kuwa kutokana na Makao Makuu ya *ADB* kuhama, mipango sasa itafanywa kwa msaada wa Benki ya Dunia. Je, Serikali ina mpango upi mbadala ili Wananchi waelewe nini kinafanyika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya maji katika Mji wa Sumbawanga kuanzia mwezi wa Oktoba, itakuwa mbaya. Tunategemea kupata kiasi tu cha mahitaji yetu 25% (robo) tu. Naomba msaada wa kuchimbiwa visima angalau vinne ili kutuwezesha kukidhi mahitaji yetu. Nashukuru kwa wataalam waliochimba kisima kimoja cha utafiti hivi karibuni. Bonde la Luiche limeonyesha kuwa na maji mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeomba nguvu hii itusaidie kutuwezesha hata kugharamia mishahara ya watumishi. Bila visima hivi, pato la mji litakuwa dogo sana na kuendelea kuiomba Serikali kulipa mishahara ya watumishi wote mpaka mpango kamambe wa visima na vianzio vingine vitakapopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe pia Wizara ione namna ya kuvisaidia vijiji 25 vinavyozunguka Halmashauri ya Mji wa Sumbawanga. Tangu Mamlaka ianzishwe, uwezo wake wa kushughulikia miradi ya vijiji, umepungua sana. Miradi iliyoanzishwa na *NORAD* miaka ya 70, imeharibika na inahitaji ukarabati mkubwa sana! Wananchi wanajitahidi kukarabati yale yaliyo ndani ya uwezo wao. Ningeomba apatikane Afisa wa Maji (Mhandisi wa Maji), kwa ajili ya vijiji ambavyo vina zaidi ya wakazi 60,000. Pia tuendelee kuomba tupatiwe na wahisani kwa ajili ya miradi yote hiyo. Hatuna wahisani, hivyo, Wizara ndiyo mhisani. Hii ndiyo sababu yangu ya kuomba kuanzishwa kwa Mfuko wa Maji Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kuanzisha Mradi Maalum kwa Bonde la Rukwa. Maana kutokana na mifugo mingi kukimbilia bonde hilo, kumejitokeza uharibifu mkubwa wa mazingira ambayo yana madhara makubwa kwenye Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukubaliana na Waziri kuwa Mikoa, Wilaya na Vijiji, bado hawajasimamia kwa nguvu zote hifadhi ya mazingira. Kazi hii pia siyo ya Wizara moja au mkoa mmoja. Kuna haja ya kuwa na kongamano lingine la Maji/Mifugo/Mazingira/Utawala Bora. Hii itasaidia kukwepesha mitafaruku mbalimbali kati ya wafugaji/wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa juhudi zake za kuiendesha na kuisimamia Wizara hii vizuri, akishirikiana na Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wote na Wafanyakazi wa Wizara hii, ambayo ni mhimili mkuu wa maisha na maendeleo ya watu pamoja na mifugo yao hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi kubwa ambazo zinafanywa na Mheshimiwa Waziri na wahusika wenzake, wanajitahidi sana sana katika kuwapatia Wananchi huduma hii muhimu kwa watu pamoja na kuwa nchi yetu ni kubwa sana na huku ikiwa katika juhudi za kujenga uchumi na maendeleo ya Taifa letu ambalo kwa miaka mingi tulikuwa nyuma kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, imetuonyesha juhudi zinazofanywa na Wizari hii pamoja na Serikali yetu Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuwaondolea Wananchi matatizo ya upatikanaji wa maji hapa nchini kwa matumizi ya watu, mifugo, pamoja na shughuli nyingine ambazo zinahitaji maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, imetuelezea juu ya mkakati wa kupunguza umaskini nchini, ambapo imeelezwa kuwa Sekta ya Maji na Mifugo, zinapewa kipaumbele katika Mkakati wa Taifa wa kupunguza umaskini nchini. Kwa kweli hapa ni lazima kwa dhati kabisa, naipongeza sana Wizara hii kwa kuliona hili na kulisimamia kwa muda wote, jambo ambalo linawapa matumaini Wananchi kuwa Mkakati huu wa Taifa wa kupunguza umaskini nchini, unaweza

kufanikiwa vizuri na pia kuwa na matumaini ya kufikia matarajio yao ya kuondokana na matatizo ya upatikanaji wa maji safi na salama hadi hapo itakapofikia mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii tumeelezwa kuwa upatikanaji wa maji ni kigezo na kichocheo muhimu katika kufanikisha jitihada za Serikali za kupambana na umaskini nchini. Kwa kweli dhana hii ni sahihi na ninaiomba sana sana Serikali yetu, iongeze juhudi zake binafsi pamoja na kutafuta misaada mbalimbali kutoka Mataifa na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ili kuweza kufanikisha lengo lake hili la kuwapatia huduma hii muhimu Wananchi wote wa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 14 unaeleza kuwa Sera ya Maji inalenga kujenga mazingira ya kuwezesha sekta hiyo kukua kwa haraka ili kuwawezesha Wananchi kuishi maisha bora zaidi na kuchangia zaidi katika kupunguza umaskini. Ni imani yangu kuwa, Wizara hii itafanikisha malengo haya mazuri yaliyolengwa na sera hii ya maji, ili kufanisha katika ujenzi wa mazingira yatakayowezesha Wananchi kuishi maisha bora zaidi katika kupunguza umaskini kwa Wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ya Mifugo, tunaelezwa kuwa mwelekeo wa Sera ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1977, inalenga kuiwezesha Sekta ya Mifugo kuwa kubwa zaidi, kuzalisha kibiashara na kuongeza pato la wafugaji na Taifa kwa ujumla. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kuielezea sera hii ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1977 katika hotuba yake hii, ambapo imeelezwa kuwa kuwezeshwa sekta hii ya mifugo kuwa kubwa zaidi. Kuzalisha kibiashara na kuongeza pato la wafugaji na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara hii pamoja na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwawezesha Wananchi kwa kuwapatia elimu na mipango mizuri itakayowawezesha kuamua kujenga nyumba za kuishi za kisasa kutokana na kuuza mifugo yao. Ninaiomba Wizara hii kuwaelimisha wale Wananchi ambao wanamiliki mifugo mingi sana, kuuza baadhi ya mifugo yao ili kujenga nyumba za kuishi za kisasa katika vijiji vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makazi bora ni msingi mzuri sana katika kumtoa mwananchi katika umaskini. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali Kuu, Wizara husika, pamoja na Watendaji wa Halmashauri na Vijiji, kuwajibika kwa Wananchi katika maeneo yao katika kuwaelimisha na kuwahamasisha Wananchi wajenge nyumba bora na za kisasa katika maeneo yao na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Wizara yake na Serikali yetu Kuu, kwa uamuzi wake wa kujenga mradi mkubwa wa maji utakaotoa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika Miji ya Shinyanga na Kahama, ambapo pia Vijiji 54 vitafaidika na mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ikiamua kufanya jambo, inafanya. Mfano ni mradi huu ambao ni mkubwa sana ndani ya nchi yetu, ambao utaleta maendeleo kwa Wananchi na nchi yetu kwa ujumla. Ni imani yangu kuwa, Wizara hii pamoja na

Serikali, itaongeza juhudi na ufanisi zaidi ili kuwapatia Wananchi wote nchini, huduma hii muhimu kwa maisha na maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamtakia kazi njema na ya mafanikio Mheshimiwa Waziri katika kusimamia majukumu yake. Ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa kazi nzuri anayofanya ndani ya Wizara, kwa kuzingatia maslahi na haki za watumishi na kuifanya Wizara kuwa shwari. Huduma za maji nchi nzima amejitahidi na hasa Kanda ya Ziwa kutuwezesha kupatiwa maji ya Ziwa Victoria. Mwenyezi Mungu, amjalie afya njema katika uongozi wake.

Hali kadhalika, pongezi natoa kwa Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo na Watendaji Wizarani kwa ushirikiano wao hadi Waziri ameweza kuwasilisha hotuba nzuri Bungeni leo tarehe 26 Julai, 2005. Kwa hiyo, naanza kwa kuunga mkono hotuba hii ya bajeti ya mwaka 2004/2005, kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni kuhusu kero za ulipishwaji wa *bills* za maji kwa makisio, unaofanywa na baadhi za Bodi za Maji Mikoani. Hakika mimi nawatetea Wananchi kwa vile najua hali zao za uchumi ni duni. Nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, utakapofanya majumuisho ya hotuba yako, unijibu mtindo huu wa *bills* za makisio utafutwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchimbaji wa visima binafsi, Wananchi wengi hupenda kuchimbiwa visima binafsi kwa matumizi yao na mifugo, lakini wanashindwa kwa sababu viwango vinavyotolewa na wataalam wako kwa maelekezo ya ofisi ni vikubwa (kwa mfano shilingi 2,000,000/=). Kwa nini Wizara yako isitofautishe gharama kwa taasisi na zile za Wananchi wa kawaida? Naomba maelezo juu ya suala hili ambalo ni nyeti kwa Wananchi na matumizi ya maji kijamii na mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema tena naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa shukrani na pongezi za dhati kwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Diallo na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa kazi nzuri inayoonekana. Mmetekeleza vizuri Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwa na jengo lenu Dodoma, ili kuepuka na upangaji kwa Wizara nzuri kama hii, je, juhudi zipi zinafanywa na Wizara hii ili muwe na jengo lenu hapa Dodoma, mnacho kiwanja au jengo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jedwali linaloonyesha idadi ya malambo, karika ukurasa 158 – 160. Kwa Morogoro Vijijini, imetaja Ngerengere, hakuna lambo hata moja. Ila Ngerengere Mji Mdogo, kuna mradi wa maji ya bomba wa *World Vision.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri afuatilie, amedanganywa. Vilevile alitoa Sh. 9,000,000/= kwa malambo matatu, lakini hadi leo, lambo moja tu lilifanyiwa ukarabati. Sh. 6,000,000/= za Ekenywa na Mkulazi, zimeliwa. Hawajui ziko wapi. Naomba Mheshimiwa Waziri, afuatilia, mimi nimeshindwa, achukue hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ya *TASAF* ya maji inaenda taratibu mno. Wananchi wana wasiwasi hasa mradi wa Kidugalo, kisima kirefu. Namwomba Mheshimiwa Waziri baada ya Bunge hili aje Kidugalo, Ekenywa, Mlilingwa na Ngerengere kuona miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wengi nchini, wangependa sana kuwa na malambo katika maeneo wanakoishi kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kuwe na Mfuko kama ule wa pembejeo ili kuwasaidia wafugaji wadogo wadogo na wakubwa ili kukuza sekta hii na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa nchi kama Tanzania yenye Waziri na Naibu Mahiri, kuendelea kuuza ngozi ghafi nje, badala ya kuzisindika. Mipango kamambe ya Wizara ifanywe kuonyesha juhudi hizo.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki. Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa Watanzania wote. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielezee suala la maji katika Wilaya ya Misungwi, hasa Misungwi Mjini (yaani Makao Makuu ya Wilaya). Tatizo la maji Misungwi ni jambo ambalo linahitaji ufumbuzi wa haraka ili Wananchi wa Misungwi waondokane na tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais katika ziara ya kampeni katika Uchaguzi wa 2000, alisema yeye kuwa tatizo la maji Misungwi atalimaliza. Hivyo, ilionyesha kuwa tatizo letu ni la Kitaifa. Wananchi wanasubiri kutimizwa kwa ahadi ya Rais. Mheshimiwa Naibu Waziri alitembelea eneo la Nyakiti, mahali mradi wa zamani ulipoanza kujengwa na kuishia njiani. Naibu Waziri anajua. Makamu wa Rais,

Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, alitembelea eneo hilo na kujionea kukwama kwa mradi huo ambao unaleta tatizo kwa Wananchi wa Misungwi na kuahidi atafuatilia. Makamu Mwenyekiti wa CCM Taifa, Mheshimiwa Dr. John Samwel Malecela, alieleza katika mkutano wake wa hadhara kuwa atalifikisha kwa Mheshimiwa Rais, ambaye pia ni Mwenyekiti wa CCM Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona mlolongo wa viongozi waliotembelea mradi huo. Lakini pia ninazo taarifa ya kuwa Serikali kupitia ufadhili wa Ufaransa, wamekubali kuleta maji katika miji mitatu, yaani Musoma, Bukoba na Misungwi. Upembuzi yakinifu umeanza. Naomba ufuatiliaji wa karibu ufanywe, kwani miradi kuna mingi iliyofanyiwa upembuzi na kuachwa bila kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kufanikisha ujenzi wa Mradi wa Maji toka Ziwa Victoria kwenda Kahama na Shinyanga. Mradi huu unaanzia katika Jimbo la Misungwi, Kata ya Ilujamate, Kijiji cha Nyang'homango, sehemu ya Ihelele. Mradi umeanza na ujenzi unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa tena shukrani kwa Serikali kusimamia fidia za watu ambao eneo lao limechukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa chujio la maji hayo na Kambi/Makazi ya mradi huo. Taarifa nilizonazo ni kwamba, watu waliotathminiwa sehemu zao, wameanza kulipwa kupitia Ofisi ya *DC* Misungwi. Sina shaka na Ofisi hiyo watatendewa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Misungwi wamefaidika na ujio wa mradi huo kwa ukarabati wa barabara ya Buhingo – Sekele – Nyamainza – Mbalama – Isesa hadi Ilujamate, zaidi ya km. 35, kwa sasa inapitika na umeme unachukuliwa toka Misasi hadi eneo la mradi. Utavinufaisha Vijiji vya Buhingo, Seeke, Nyamainza, Mbalama, Isesa, Nyang'homango hadi Iheleke. Mbali na faida hizo, Wananchi wa Misungwi wamepata ajira katika ujenzi. Napongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mchango wangu katika Sekta ya Mifugo. Ni hivi karibuni Waziri ametuonyesha ujenzi wa Machinjio. Hii ni kuifanya Sekta ya Mifugo iendelee kutoa mchango mkubwa kwa Taifa.

Faida za mifugo ni pamoja na kulima, kutoa maziwa na siagi, kutupatia mbolea, kusomba mizigo kwa kuvuta mikokoteni. Faida hizo ni kabla mnyama hajachinjwa, kwani baada ya kuchingwa, bado utauza ngozi, nyama utakula, utatengeneza viatu, vifungo, gundi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza machache ili kuonyesha umuhimu wa mifugo hapa Tanzania. Kwa hiyo naomba malambo yaongezwe sehemu ya wafugaji ili kuepusha kuhamahama kutafuta maji, pia Serikali iwasaidie wafugaji kupunguza ukali wa bei ya madawa ya mifugo, bei iliyopo ni kubwa mno na vilevile majosho ni sehemu muhimu katika suala la magonjwa. Majosho yaboreshwe na yajengwe mengine, ikifuatiwa na sheria ya kuyatumia (wafugaji waoshe mifugo).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizia kwa kutoa ombi kwa Serikali kutowanyanyasa wafugaji, kwani wamekuwa kama wakimbizi ndani ya nchi yao. Mfano ni Mahenge na Mbarali, wanafukuzwa eti warudi kwao. Huu ni unyanyasaji. Waziri walinde wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Ahsante.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa masikitiko yangu kwa msiba mkubwa uliotokea hapa Dodoka, kwa kufiwa na Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ulanga Mashariki. Mwenyezi Mungu amweke mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Anthony Diallo, Naibu Waziri na Bwana Vincent Mrisho, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa kuleta hotuba safi ya bajeti, yenye matumaini makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu kuhusu bajeti ya Wizara, yanakwenda moja kwa moja katika Mradi wa Mbwinji, wenye lengo la kupeleka maji ya uhakika Masasi na Nachingwea. Nampongeza Waziri kwa hatua hii. Naamini kwa hatua hii, Wizara itaondoa kabisa matatizo ya maji kwa Mji wa Masasi na vitongoji vyake. Lakini pamoja na juhudi hizi zote, bado tutakuwa na matatizo ya maji katika eneo la Masasi Magharibi, ambalo kwa sehemu kubwa lipo kwenye Jimbo langu la Masasi. Matatizo makubwa yapo katika Kata za Namajani, Namatutwe, Lukuledi na baadhi ya maeneo ya Kata ya Lisekese. Sehemu hizi hazina vyanzo vya uhakika vya maji na hivyo maeneo mengi yana shida kubwa ya maji. Ukame wa mwaka 2003 ndio uliongeza sana shida, kwani Wananchi walikuwa wanakwenda kutafuta maji zaidi ya umbali wa kilometa 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mradi wa maji ya Mbwinji, mto ambao upo Wilaya ya Masasi, Wananchi wengi wanaamini kuwa maji haya ya Mbwinji ndiyo yatakuwa mkombozi wa kutatua matatizo ya maji Masasi Magharibi kwa sababu yapo mengi. Wananchi hawataelewa endapo maji haya yatapelekwa Nachingwea kabla ya kutosheleza Masasi Magharibi, ambapo nafasi hii ingechukuliwa ili nao wapate maji. Bado Nachingwea wana bahati ya kuwa ma maji mengi ardhini na visima kadhaa, ambapo Masasi Magharibi hawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hatusemi kuwa Nachingwea wasipate maji haya, bali Wizara iangalie namna gani itakidhi maji Masasi Magharibi kabla ya kupeleka maji Nachingwea. Waziri asipofanya hivyo, huenda akazua mgogoro wa matumizi ya maji hayo. Nitashukuru kupata ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

**MHE. RAPHAEL N. MLOWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Naibu wake, Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu, Bwana Vincent Mrisho, Naibu Katibu Mkuu, Dr. Charles Nyamrunda, Viongozi na Wafanyakazi wote wa Wizara hii, kwa kazi wanayoifanya kuboresha maji na mifugo nchini mwetu. Kazi zimeonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ni moja ya vituo vya mafanikio *(a center of excellence),* katika kutekeleza majukumu ya Serikali kwa Wananchi wake. Ninaomba Mheshimiwa Waziri na wenzake waendelee kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu kuhusu hotuba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, utahusu mambo matatu; muda wa kukamilika kwa mradi wa Maji ya Ziwa Victoria kupelekwa Miji ya Kahama na Shinyanga, ombi la uchimbaji wa visima virefu vya Vijiji vya Lowa na Kakebe na hoja ya kuwa na msimamo thabiti wa *stock routes.*

Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi kwa niaba ya Wananchi wa Mji wa Kahama, napenda niungane na Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wetu, kwa kutoa msukumo wa utekelezaji wa mradi huu kwa kutumia fedha zetu. Mradi huu ndiyo jawabu pekee la kudumu la tatizo la muda mrefu la maji la Mji wa Kahama. Tunasubiri kwa hamu ukamilishaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo, ningependa nipate ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kuhusu muda halisi wa kukamilika kwa mradi huu. Japo katika aya ya 62 ya hotuba yake, ukurasa wa 44, Waziri amesema, pamoja na mambo mengine, nanukuu: "... kazi za ulazaji wa mabomba kutoka Solwa hadi Kahama na Shinyanga, zitafanyika mwaka ujao wa fedha". Hata hivyo, Waziri atapenda kufafanua kama kweli mradi huu utaweza kukamilika kabla ya Oktoba, 2005, hasa ukizingatia kwamba utachukua miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia kwa makini kiambatanisho Na. 5(1), ambacho ni Ramani yenye kuonyesha programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini hadi Juni, 2004. Kitu kinachoonekana sana katika ramani hiyo ni maeneo ya usaidizi wa wahisani. Kwa Mkoa wa Shinyanga, Mhisani Mkuu wa Maji ni Serikali ya Uholanzi. Kwa kweli Serikali ya Uholanzi imekuwa ikisaidia huduma ya maji Mkoa wa Shinyanga tangu mwanzoni mwa mwaka 1970. Hata hivyo, sisi wakazi wa Mkoa wa Shinyanga, tuna wasiwasi kuhusu taratibu za usambazaji wa maji vijijini, unaofanywa kwa msaada wa Serikali ya Uholanzi. Kazi ni ndogo, masharti ni mengi. Hofu yetu ni kuwa sisi wa Shinyanga tusije tukarudi nyuma na kupitwa na mikoa inayosaidiwa na wahisani wengine, hasa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hii, kwa kuwa Wanavijiji wa Lowa na Kakebe – Kata ya Nyandekwa, walichanga Sh. 400,000/= kufanyiwa utafiti wa kina wa maji kwa kutumia *vertical electronic sounding* mwaka 2000, lakini mpaka sasa upelekaji

wa maji katika maeneo yaliyobainishwa haujafanyika, namwomba Mheshimiwa Waziri, akubali kutenga fedha kama shilingi milioni kumi kwa ajili ya upelekaji wa visima hivyo. Kwamba, fedha hizo zipatikane ili mkandarasi ambaye tayari anapekecha visima vitano vya majaribio katika Mji wa Kahama, aweze kupekecha na visima hivyo vya Vijiji vya Lowa na Kakebe. Hii itadhihirisha usemi wa "kuua ndege wawili kwa jiwe moja". Mheshimiwa Waziri, chonde chonde kwa suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimalizie kwa kushauri kwamba, Wizara itoe mwongozo thabiti kuhusu kutenga na kutumia *stock routes*. Inasikitisha sana kuona jinsi barabara tunazohangaikia kuzitafutia fedha na kusimamia ujenzi wake, jinsi barabara hizo zinavyoharibiwa na mifugo inayopita juu ya barabara hizo hasa huko vijijini. Naomba Mheshimiwa Waziri, alione hili kama tatizo, wala tusilionee haya. Ni ukweli ulio dhahiri kwamba, hakuna *stock routes* katika sehemu nyingi za nchi yetu. Hata zile sheria ndogo ndogo kuhusiana na usimamizi wa barabara hizo, hazifuatwi. Katika hali kama hiyo, ni vyema Serikali ikaandaa utaratibu mahsusi kwa nchi nzima ili utumike kwa Wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo ya Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wa Makong'ondera, umekwama tangu siku nyingi. Mradi huo unaonekana umekwama na hakuna juhudi zozote zinazofanywa na Serikali ili kuuendeleza. Je, Serikali imeuacha mradi huo au bado? Mradi huo ni muhimu sana kwa kuwapatia maji Wananchi wa Kijiji cha Makong'ondera na majirani zake. Naiomba Serikali kuhakikisha kuwa, mradi huo unakamilika ili Wananchi ambao sasa wana shida sana ya kupata maji, waondokane na adha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine ambao umekwama ni Mradi wa Maji wa Ndwika – Mangaka, ambao umekwama kilometa chache kabla ya kufika Mangaka, kutokana na kuishiwa mabomba, kulikotokana na makadirio mabaya. Mradi huo unafadhiliwa na *TASAF* na mawasiliano na Makao Makuu ya *TASAF* bado kuzaa matunda. Hivyo, naomba Serikali ihakikishe mradi huo unakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ambayo imekwama ni ya uchimbaji wa mabwawa ya maji ndani ya Jimbo la Nanyumbu. Miradi ambayo tayari imeshafanyiwa *survey,* ni Mradi wa Bwawa la Maratani, Mradi wa Bwawa la Namasogo, Mradi wa Bwawa la Mpwahia, Mradi wa Bwawa la Maneme na Mradi wa Bwawa la Mpombe. Miradi yote hiyo, Wataalam wamefanya *survey,* lakini ujenzi wake haujaanza hadi sasa. Miradi yote hiyo imefadhiliwa na *TASAF.* Naomba Serikali ihakikishe miradi yote hiyo inakamilika kujengwa ili kuwaondolea adha ya maji Wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea naomba kuishukuru Wizara kwa Wilaya ya Manyoni kuwa miongoni mwa Wilaya 12 za kwanza kuingizwa katika Mpango wa upatikanaji wa Maji na Usafi wa *Mazingira (Rural Water Supply and Sanitation),* unaogharamiwa na Benki ya Dunia. Katika kutekeleza mradi huu, naomba kwa sisi tunaotoka katika maeneo ya ukame, pale inapobidi kuchimba visima, basi uwezekano wa kuchimba visima vyenye kina cha mita 150 – 200 uwepo. Nashauri hivyo kwa sababu sehemu nyingi zilizochimbwa visima visivyofikia kina hicho, maji hayakuweza kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kufanya uchunguzi *(survey),* naomba wataalam wawe makini katika kufanya kazi hii. Nalizungumzia hili kwa sababu katika Kijiji kimoja cha Mhanga, wachunguzi walionyesha kuwa katika maeneo mawili waliyopima, maji yangeweza kupatikana katika kina cha mita 60. Maeneo hayo yalichimbwa, moja katika kina cha mita 83 na kingine katika kina cha mita 120. Katika visima vyote hivi viwili, hayakupatikana maji wala tope. Hali kama hii iliwakatisha tamaa Wananchi na kutia wasiwasi juu ya utaalam wa wapimaji. Naomba hilo litazamwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Usafirishaji wa Mifugo, katika barabara ya Tabora – Itigi – Manyoni, bado makundi makubwa ya mifugo yanaswagwa kupitia barabara hiyo toka Mkoa wa Tabora.

Naomba Maafisa Mifugo wa Mkoa wa Tabora waache kutoa vibali vya kusafirisha mifugo kwa kuswaga kupitia barabara hiyo, kwa sababu wanaharibu barabara. Badala yake waitikie wito wa Mheshimiwa Rais wa kusafirisha kwa njia ya magari. Vilevile tunaomba Wizara iangalie uwezekano wa kututengenezea *stock route* toka Tabora – Itigi – Manyoni kwa ajili ya kupitisha mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tunaomba kufahamu Serikali ina mpango gani na Ranchi ya Kitaraka. Pale kuna *infrastructure* ambayo mpaka sasa haifanyi kazi. Wananchi wanaomba kufahamu.

Namalizia kwa kusema kuwa, naunga mkono hoja hii na kupongeza kazi nzuri sana inayofanywa na Wizara. Ahsante.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wasaidizi wote wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Nasema hongera sana. Hongereni sana kwa hotuba nzuri yenye kulenga na kuleta maendeleo ya maji na maendeleo ya mifugo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kutuletea maji Mkoa wa Shinyanga kutoka Ziwa Victoria. Huo ni ukombozi mkubwa wa kuleta maendeleo Kanda ya Ziwa. Namshukuru sana. Aidha, namshukuru sana kwa mpango mzima wa kujenga barabara toka Dodoma hadi Mwanza. Miradi miwili hii mizito aliyotupa sisi Kanda yetu ya Ziwa, hakika ameonyesha upendo kwa Wananchi wa kanda hii kwa dhati kabisa na huo ni moyo wa pekee na wa kishujaa. Hatuna cha kumpa, isipokuwa tu tunasema ahsante sana.

Napenda pia kumpongeza sana na kumshukuru Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kutupatia chanzo cha maji Wilaya ya Meatu. Kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Meatu na mimi Mbunge wao, tunamshukuru sana sana kwa kutujengea Bwawa la Mwanyahina. Bwawa ambalo hivi sasa limejaa maji na kilichobakia ni kusambazwa hayo maji kwa walengwa. Ahsante sana Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa jitihada zake pamoja na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu na Mkurugenzi wa Maji Vijijini, Ndugu Satu, nawapongeza sana kwa kuweka mpango madhubuti wa kusambaza maji ya Bwawa la Mwanyahina kwa watumiaji/walengwa. Nawapongeza sana. Naishauri Serikali ifanye jitihada kumpata mtaalam/fundi hasa wa kufanya kazi hii muhimu ya usambazaji maji ya bwawa hili la maji. Maji haya yafike Mjini Mwanhuzi, Meatu Sekondari, Mji Mpya, Kijiji cha Mwanyahina, Gereza la Meatu, Kimali Sekondari, Shule ya Msingi Bomani, Shule ya Msingi Mshikamano, Ofisi zote za Serikali na Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali vilevile kukamilisha miradi yake ya malambo ya maji kwa ajili ya kunyweshea mifugo katika Vijiji vya Mwanjoto, Chambala, Mwabuzo na Bukundi. Vijiji hivi vilikuwa vimepewa fungu na Serikali la Sh. 3,000,000/= kila kimoja. Hata hivyo, mpaka leo hii miradi hiyo haijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkoa wa Shinyanga una wingi wa mifugo hapa nchini, naishauri Serikali kuwa na minada ya Kitaifa kama ifuatavyo: Wilaya ya Meatu, minada ya Bukundi, Itenje na Malwilo iwe ya Kitaifa. Wilaya ya Kishapu, mnada wa Mhunze uwe wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafirishaji wa mifugo usiwe wa masafa marefu kama ilivyo sasa, kwani mifugo inayosafirishwa kwa njia ya reli, hupata madhara mengi njiani, hasa yale ya kutokuchunga wala kunywa maji kwa muda wa siku tatu hadi nne, kutoka Shinyanga hadi Dar es Salaam. Wanyama hao hukonda na wengine hupasuka hata kwato zao. Mifugo hiyo huwa inasafirishwa ikiwa imesimama wima na hufika safari yao hivyo hivyo ikiwa imechoka sana. Hivyo, huonekana wameteseka, kukonda na kuwa na bei ya chini na uzito wao huwa umepungua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara kuwa na vituo kama vile Shinyanga Mjini kuwa na Mnada wa Kitaifa, Tabora Mjini pawe na Mnada wa Kitaifa na mnada wa Dodoma wa Mailimbili uwe wa Kitaifa. Hii minada itaipunguzia mifugo hiyo usumbufu, na kutokondeana kama ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja iliyoko mbele yetu kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuna tatizo kubwa sana kwa Wananchi ambao mabomba yao hayatoi maji na bili bado wanadaiwa. Je, kuna utaratibu gani wa kudai utumiaji maji na wakati maji hakuna? Ni tatizo kubwa sana kwa Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo la Bukene, kuna vijiji ambavyo havina visima kabisa. Tunaomba sana kuangalia vijiji hivyo ambavyo pia wapo binadamu kama maeneo mengine. Kwa mfano, Bukene, Mwamala, Itobo, Mambali, Isagenhe na Mwangohe, ni vijiji ambavyo vinasumbuka sana kwa maji. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, aviangalie vijiji hivyo kwa moyo wa imani kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndala Nzega ni *centre,* lakini hakuna maji kabisa na kuna hospitali kubwa sana ambayo tunaitegemea hata kwa Wananchi wa Tabora Mjini, wanaotibiwa hapo. Lakini Wananchi wa Ndala hawana maji kabisa. Tunaomba sana huduma hiyo kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Sikonge ni mojawapo katika ya wilaya mpya ambayo ina tatizo kubwa la maji, ambapo Wananchi wa maeneo ya Sikonge wana tatizo hilo hilo kubwa. Tunaomba sana kuiangalia Wilaya hiyo, ingawa namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea mradi wa maji vijini na usafi wa mazingira, ambao utasambazwa vijijini. Ila bado Wilaya ya Sikonge Mjini, tunaomba hata tukipata visima virefu ambavyo vitapunguza sana matatizo ya maji Mjini Sikonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na juhudi za Mheshimiwa Waziri, nina imani visima hivyo virefu vitapatikana na Wananchi wa Sikonge watafaidika na juhudi zinazoonyeshwa kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Sikonge wameendelea sana na ufugaji wa kisasa, ila wana sikitiko la ng'ombe wao kupata chanjo mara moja tu, nao walielimishwa kuwa chanjo ni mara mbili. Hilo ni lalamiko la Wananchi wa Sikonge, Kata ya Chabutwa.

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii. Shughuli zao ni zenye mahitaji ya nchi nzima na kwa kila Wilaya mpaka katika Vijiji vyote. Lakini ninawapongeza kwa vile wameweza kuisambaza huduma ya maji katika maeneo mengi ya Tanzania. Naomba kuzungumzia matatizo ambayo yapo katika Jimbo langu la Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mashine ya Maji ya Mbawala Chini, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kukubali ombi langu la kutembelea Kijiji cha

Mbawala Chini, kwenda kuiona mashine ya maji wakati alipofanya ziara ya kutembelea Mkoa wa Mtwara. Mashine ya maji ya Mbawala Chini, imeharibika zaidi ya miaka 10 iliyopita. Mashine hii ilikuwa inahudumia Vijiji vya Mbawala Chini, Litumbo, Mkangala, Mbawala Juu, Naliendele na Nyengedi. Kutokana na kuharibika kwa mashine hiyo, baadhi ya vijiji hivyo vina matatizo makubwa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alifika na kuiona hali halisi ya kuharibika kwa mashine hiyo na pia akawapa matumaini Wananchi, naomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo juu ya kuifufua mashine hiyo ili kuwanusuru Wananchi kutokana na tatizo la maji. Tatizo la mgao wa maji Mtwara Mjini, liishe. Kuna wakati walikuwa wanasemea tatizo la umeme, lakini sasa umeme wa kutosha unapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu nipeleke salamu za rambirambi kwa familia, ndugu na wapiga kura wote wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kwa kufiwa na Mbunge wao, Marehemu Mheshimiwa Theodos J. Kasapira. Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Waziri wa Maji na Maendele ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, Naibu wake, Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu, Ndugu Vincent Mrisho, pamoja na Watumishi wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Maji ni muhimu sana kwa kila kiumbe, kama vile mimea, wadudu, wanyama na binadamu. Kwa binadamu, maji safi na salama ni muhimu sana.

Hongera tena wa Wizara kwa mambo mawili. Moja, ni kuanzishwa kwa Mfuko wa Maji wa Taifa pamoja na Dira ya Taifa ya kila mtu apate maji safi na salama ifikapo mwaka 2005. Hongera sana kwa Dira hiyo. Vyanzo vya maji vilindwe kwa hali yoyote ile. Kila njia na kila nafasi itumike ili kulinda vyanzo vya maji. Uchomaji moto ovyo, ni jambo hatari sana lenye mwelekeo wa kuvuruga hali ya hewa na kupotea kwa mvua na hata kuharibika kwa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba, Vyanzo vya Maji na Uchomaji Moto ovyo, ziundwe Kamati za kudumu za Serikali za Vijiji kudhibiti hali hiyo. Kama zikishindwa, Serikali za Vijiji ziwajibishwe. Jambo hili tusilifanyie mzaha. Ni lazima sheria kali zitumike na kama hazipo, zitungwe mpya au zilizopo zipitiwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya kutosha itolewe kwa Wananchi ili waweze kuelimishwa kuvuna maji ya mvua kwa njia rahisi. Lakini naomba Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Elimu na Utamaduni ili elimu hii isambazwe katika Shule zote za Sekondari, maeneo yaliyo na watoto wengi, hasa kule ambapo maji ya bomba au ya visima hayajafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba miradi ya maji ambayo imefadhiliwa na wahisani na ambao wameondoka, iorodheshwe na mara kwa mara ikaguliwe na Wizara. Najua wako Wahandisi wa Maji kule Wilayani, lakini tumeshuhudia mara nyingi maelekezo na maagizo kutoka Wizarani, hayafiki sawasawa kule chini. Katika hali kama hiyo, ni lazima Wizara iingilie kati. Nafahamu pia kwamba, suala kama hili siyo la Wizara hii peke yake, ni Wizara nyingi. Lakini kwa umuhimu wa maji, naomba ushauri huo uchukuliwe ili miradi hiyo isije ikafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wa *Manolo Group* pamoja na Mradi wa Maji wa *Mlalo – Mwangoi Water Project* wa Sh. 767,410,270/= na Sh. 273,926,360/=, tafadhali jitihada zifanyike ili miradi hiyo itekelezwe. Nashukuru kwa ahadi ya Wizara ya Sh. 12,000,000/= kwa visima katika Kata ya Shume. Ahsante sana, naomba pesa hizo zipelekwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ranchi za Taifa kubinafsishwa kwa wenyeji, hongera sana. Hawa wasaidiwe kwa mikopo, utaalam, miundombinu, madawa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri mnazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina masikitiko makubwa kwa kitendo ninachofanyiwa na Mkurugenzi wangu wa Kilosa, kutunyima mchanganuo. Kibaya zaidi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Kilosa tuna Miji Midogo mitatu, Miji midogo iliyopewa ni Gairo na Kilosa, Mji Mdogo wa Mikumi umeachwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Katibu Mkuu aongee na Mkurugenzi, ni kigezo gani ambacho ameingiza maji, miradi ya miji miwili, Kilosa na Gairo na kuiacha Kampuni ya Mikumi. Katika jimbo langu kuna makampuni mawili, Mikumi na Ruaha. Afadhali katika hizo, angenipa moja Kampuni ya Mikumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni haya mawili, Mikumi na Ruaha, naomba yaingie katika mpango. Mheshimiwa Waziri nashukuru unavyonisaidia. Nimerudi kwenye msiba, nitajitahidi kukuona nijue mbaya wa watu wa Mikumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kuigawa Ranchi ya Mkata. Naendelea kukumbusha, wafugaji wangu tumeomba kuondolewa kero iliyopo kati ya wakulima na wafugaji. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Wataalam wake, kwa hotuba nzuri. Hotuba hii imeandaliwa vizuri sana, haina tatizo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara ambazo zimefanya kazi yake vizuri, basi Wizara hii imefanya kazi nzuri sana. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa jinsi ambavyo wamekuwa karibu na Waheshimiwa Wabunge, wamekuwa wakitusikiliza vizuri na kutushauri vizuri, tofauti na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Wizara kwa kutoa fedha kwa ajili ya Ilula – Kilolo. Pale Ilula ni mji ambao unakua kwa haraka sana. Lakini bado ningeomba sana Mheshimiwa Waziri, endapo atakuwa na nafasi afike au atume wataalam wake waone uwezekano wa kutengeneza kitu cha uhakika pale Ilula na kutuongezea fedha kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya hii ya Kilolo, maji siyo tatizo, lakini tatizo ni jinsi ya kusambaza. Mfano, Kata ya Uhambingito, eneo hili lina shida sana ya maji, kwani ni eleo lenye udongo wa chokaa, hivyo maji yake hayafai kwa matumizi ya kawaida. Tungeomba Wizara hii ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, itusaidie mabomba ili Wananchi hawa waonje matunda ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilolo ni mpya, hivyo sijaona mipango yoyote ya maji Makao Makuu ya Wilaya. Lakini bahati ambayo tumeipata ni kwamba, Kanisa la Anglikana limeamua kuchangia karibu asilimia 70 ya maji katika Wilaya (Makao Makuu). Ningeomba sana tena sana, Mheshimiwa Waziri, atoe tamko la shukrani kwa Kanisa la Anglikana kwa msaada huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu majosho, bado bei ya madawa ni kubwa sana, ningeomba Wizara hii iliangalie upya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la utunzaji wa mazingira hasa katika vijiji vinavyopitiwa na barabara. Mifuko ya plastiki inatupwa ovyo na kusababisha vifo kwa mifugo. Ningependa kutoa ushauri kwamba, Wizara hii ndiyo ilifanyie kazi hili haraka, kwani ni kero.

Mwisho, ningeomba nilete ombi rasmi kwako ili Mheshimiwa Waziri, afanye ziara rasmi katika Wilaya ya Kilolo, kwani Wananchi wa Kilolo ndio walionituma hilo. Siyo mbaya kama utalisema leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Wizara hii pamoja na kazi nzuri iliyonayo, isiache kuongeza juhudi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa hotuba nzuri, bali pia kwa

yale mengi yaliyokwisha kutekelezwa katika sekta za Maji na Mifugo. Ni matumaini yetu kuwa mwelekeo wa baadaye wa sekta hizi mbili, utakuwa mzuri na wenye matumaini makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na mafanikio ya kuridhisha katika kusaidia mpango wa Taifa wa kupunguza umaskini. Tunaipongeza Serikali kwa kuanzisha na kukamilisha Ofisi katika mabonde yote tisa. Hata hivyo, ili mabonde hayo yaweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo, ni vyema tukaendelea kusisitiza yafuatayo:-

(a) Mabonde yapatiwe vitendea kazi vya kutosha, kwani bonde kama la Rufiji ni kubwa sana na majukumu yake ni mengi mno.

(b) Vikao vya Bodi lazima vikae kwa mujibu wa Sheria. Bodi nyingi hazikutani kwa kukosa fedha. Ni vyema Wizara ikatoa fedha (bajeti) mahsusi kwa ajili ya vikao vya Bodi, kwani makusanyo ya fedha yanayokusanywa na Bodi zenyewe ni madogo mno.

(c) Ni vyema Bodi za mabonde zikusanye mapato yote, yakiwemo yale ya *TANESCO,* kama ambavyo sheria inataka. Ila uwekwe utaratibu mzuri wa matumizi ya mapato ya mabonde.

(d) Wizara ihakikishe kama ilivyoahidi, mabonde yanapatiwa watumishi na wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Wizara kwa matumaini mapya waliyoahidiwa wafugaji. Sekta ya Mifugo ni muhimu sana katika kusaidia kuondoa umaskini vijijini. Sote tunafahamu bado sekta za Kilimo na Ushirika, ziko hoi na hazija-*deliver* vya kutosha. Hivyo, nadhani katika Sekta ya Mifugo yafuatayo yafanyike:-

(i) Kuendeleza juhudi za kutokomeza ugonjwa wa mdondo vijijini, kwani kuku wa kienyeji wana soko kubwa na la uhakika kuliko kuku wa kisasa ambao ni aghali na hivi sasa soko lake linapungua. Bado mdondo ni tishio vijijini.

(ii) Utaratibu ufanywe wa kusambaza majogoo bora ili kuboresha kuku wa kienyeji.

(iii) Mifugo ya mbuzi (hasa wa nyama) ni rahisi na wanahimili maeneo mengi nchini na wana soko kubwa hata vijijini. Ni vyema mikakati ifanywe ili ufugaji wa mbuzi uenezwe nchi nzima kwa kusambaza madume bora ya mbuzi wa nyama.

(iv) Mwaka 2001, Kituo cha Utafiti wa Mifugo cha Mpwapwa, walituhamasisha Wabunge kuhusu mifugo ya ng’ombe. Lakini pamoja na kuwaandikia kutaka kununua madume boraya ng’ombe na mbuzi, Mkurugenzi hata hakujibu. Je, nia ya maonyesho ya hapa Bungeni mwaka huo, yalikuwa nini? Ni vyema matokeo ya utafiti wa mifugo, yakapelekwa hadi vijijini.

(v) Tunaomba mpango wa kopa mbuzi lipa mbuzi, uenezwe Wilaya Rufiji kama ambavyo umeanza mradi wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe. Lakini ni dhana mbovu kuwakopesha maskini peke yao. Hata sisi wenye uwezo tukopeshwe ili tuwe mfano kwa wengine. Matokeo yake, mradi huu una-*fail* kwa vile hao maskini wenu hawana uwezo wa kuuendeleza mradi huo wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe. Tunaomba kusiwe na ubaguzi, kwani hata sisi tunaishi huko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga mkono hoja ya Waziri.

**MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa Mradi wa Maji Vijijini *(50 Districts Programme),* Nachingwea ipo kwenye programu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iharakishe kukamilisha mradi wa visima 10, fedha shilingi milioni 140 zipo. Nashauri zitumike kufunga mashine na kutandaza mabomba. Tuwe na *task force.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa *Mbwinji Project* kwa ajili ya Nachingwea na Masasi. Ninaahidi kuwa Wananchi watahamasishwa ili washiriki kwa njia ya ujenzi wa Taifa, kuchimba mitaro ya kutandaza mabomba. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, atembelee Nachingwea na Masasi ili atoe maelezo kuhusu habari hizi njema za Serikali kugharamia mradi huu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wote walengwa wa mradi huu, ninawashukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote, kwa ushirikiano mzuri.

**MHE. BUJIKU K. P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, wakiongozwa na Katibu Mkuu, kwanza kwa kazi kubwa wanaoifanya ya kuwapunguzia/kuwaondolea kabisa Wananchi, adha ya shida ya maji safi na salama, si kwa binadamu tu, bali pia kwa mifugo yao. Hotuba hii ni nzuri, wazi na ya kutia imani na matumaini kwa Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya Wapiga Kura wa Jimbo la Kwimba na Wilaya ya Kwimba kwa ujumla, kutoa shukrani kubwa kwa Wizara hii kutokana na malambo na majosho yaliyokarabatiwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2003/2004. Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa huduma ya maji Wilayani kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kwimba ni Wilaya pekee Mkoani Mwanza, ambayo haipakani na Ziwa Victoria hata kwa chembe. Hivyo, kwa ujumla Wilaya hii ni kame kuliko Wilaya zote Mkaoni Mwanza. Tarafa ya Mwanashimba ndiyo iliyo kame kuliko sehemu kubwa ya Kwimba. Hivyo, kilio kikubwa cha Tarafa hiyo na maeneo yanayozunguka Tarafa hii ni ukame. Juhudi za Serikali kupeleka maji toka Rurere katika Tarafa hiyo miaka ya 70, hazikuzaa matunda.

Aidha, juhudi za kuisaidia Tarafa hii kupitia Mradi wa *HESAWA,* haukuzaa matunda yaliyotarajiwa kutokana na ukame. Aina ya miamba chini na *water table* kuwa chini sana, hivyo visima vilivyotarajiwa au havikutoa maji kabisa au vilitoa maji ambayo hayangelifaa kwa matumizi ya binadamu na mifugo. Taarifa kuwa mradi wa kupeleka maji Shinyanga kutoka Ziwa Victoria, itaweza kufikisha maji Kwimba, hususan Tarafa ya Mwanashimba, si tu imepokelewa kwa shangwe kubwa na Wananchi wa Kwimba, hususan wakazi wa Tarafa ya Mwanashimba, bali pia wanapongeza sana uamuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado Wananchi wanachanganyikiwa kwa vile licha ya Tarafa ya Mwanashimba Wilayani Kwimba, kuna eneo la Mwanashimba vilevile Mkoani Shinyanga. Hivyo, hawajui ni Mwanashimba ipi inayotajwa katika mradi, vilevile kwa vile miradi miwili ya kupunguza tatizo la ukame katika Tarafa ya Mwanashimba. Wanazidi kumwomba Mungu awezeshe mradi huu kama umelenga Tarafa hii, ufanikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoelezea kuwa Kwimba ni kame sana, Makao Makuu yake, yaani Mji wa Ngudu nao una shida kubwa ya maji. Hivyo, kwa niaba ya wakazi wa mji huu wa Ngudu, ninaiomba Wizara kadri uwezo utakavyoruhusu, iangalie uwezekano wa kutoa msaada wa kuwezesha mji huu upate maji ya kutosha. Ikiwezekana mji huu uweze kuunganishwa na mradi wowote wa kutoka Ziwa Victoria, iwe huu huu wa Shinyanga au kupitia Wilayani Misungwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mji huu wa Ngudu, kuna mji wa Hungunalwa ambao uko katika *main road* ya Mwanza – Shinyanga. Huu ni mji mdogo unaokua haraka sana. Chanzo cha maji kwa mji huu ni vitongoji vyake. Kinaweza kuwa Runele, kwenye vyanzo vilivyotarajiwa kutoa maji kwa Tarafa ya Mwanashimba. Vyanzo hivi viko kama kilometa nane hivi toka Hungumalwa. Pesa zikipatikana inawezekana kufikisha maji katika mji huu mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zinazofanywa na Wizara hii ni nzuri sana. Wote tunaamini kuwa wakiendelea kupewa muda na uwezo, wataendelea kufanya maajabu. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kwimba, naunga miono hoja hii.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa pongezi zangu kwa Wizara kushughulikia kuondosha tatizo la maji katika Vijiji vya Chikonji na Kitomanga, ndani ya jimbo langu. Kwa bahati mbaya miradi yote miwili haijaanza na hivyo Wananchi kuhisi kuwa ahadi/azma ya Serikali ni maneno matupu. Mradi wa Chikonji upo chini ya Taifa na haifahamiki utaanza lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuniokoa na kadhia kutoka kwa Wapiga Kura wangu, ambao wananiona kiongozi mwongo, naomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anafanya majumuisho, awatamkie Wananchi wa Chikonji tarehe, mwezi na mwaka wa *JICA* kutekeleza mradi huu.

Aidha, upatikanaji wa fedha kwa mradi wa Kitomanga, ulikamilika kwa awamu ya kwanza na kwa niaba ya Wananchi wa Kitomanga, naipongeza sana Wizara. Mwaka huu wa fedha wa 2004/2005, tumetengewa shilingi milioni 20. Naomba fedha hizi tupatiwe mapema ili mradi huu ukamilike, kwa sababu hivi sasa tunaendelea na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, mradi unaohitaji maji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, awapeleke wataalam Milola, ndani ya Jimbo la Mchinga, ili kuona namna bora ya kuboresha mradi wa maji wa Chipwapwa, ambao unahudumia vijiji vya Milola Mashariki, Milola Magharibi, Legezamwendo na Kinyope.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ya Chipwapwa ambayo yanasambazwa katika vijiji hivi vinne, hutiririka kwa nguvu ya *gravity*. Hata hivyo, ni kiasi kidogo sana kinachotumiwa na wanadamu, kwani kiasi kikubwa cha maji hayo hutiririkia katika Mto Lupululu ambao huingia Ziwa Rutamba na kisha kutokea upande wa pili hadi Bahari ya Hindi. Maji haya yanaweza kuhudumia vijiji vingi zaidi badala ya kuachiwa kwenda baharini. Maji ya Chipwapwa hutokea kwenye pango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JOSEPH J. MUNGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri sana ya bajeti na kwa kuiwasilisha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ina uchambuzi mzuri wa hali halisi kwa *data* na mipango mizuri ya maendeleo ya Sekta za Maji na Mifugo. Kutokana na hotuba hii, tunaona tulipo na tunakokwenda. Napongeza sana mpango wa maji kwa Jiji la Dar es Salaam na ukodishwaji kwa *City Water*, ambao unaonesha matumaini makubwa wa hali ya maji kuboreka kuanzia miezi michache ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji Iringa Mjini, nashauri isiishie usanifu, kwa sababu huu ni mradi wa miaka mingi. Inafaa ujenzi wa mradi huu uanze mwaka huu wa fedha. Nachukua fursa hii kumwomba sana Mheshimiwa Waziri katika mpango wa Maji Mijini, uingizwe pia Mji wa Mafinga, ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Mufindi. Katika takwimu za kukua kwa miji, Mji wa Mafinga umetamkwa kuwa *the fastest growing town south of the central line.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Mafinga Mjini, ambao ni sehemu ya Jimbo langu la Mufindi Kaskazini, naomba Wizara isaidie kukamilisha mradi wa maji wa Mji wa Mafinga ambao awamu ya kwanza umehisaniwa na *Japan Food Aid Conterpart Fund,* kupanua *intake,* kujenga *raising main* na kujenga tangi la Changarawe.

Tunaomba Wizara isaidie ukamilishaji wa mradi huo kwa usambazaji wa maji mji wote na ujenzi wa tangi la Kinyanambo.

Aidha, tunaomba Wizara isaidie ujenzi wa chanzo kipya cha Mto Nyamalala, ili kuongeza wingi wa maji kwa ajili ya ongezeko kubwa la watu. Mhandisi wa Maji wa Mkoa anao mchoro kamili wa mradi huo wa maji wa Mji wa Mafinga, kwa sababu Ofisi yake ndiyo iliyoikagua na kuidhinisha michoro hiyo. Kwa hiyo, huu siyo mradi mpya, bali ni mradi unaoendelea na ulioandaliwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, mtafute namna ya kutusaidia. Nawapongeza sana kwa kazi nzuri mnazozifanya na tunatumaini mtapokea ombi letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii nzuri sana.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri ya utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Hivyo, naunga mkono hoja ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, ninayo maoni yafuatayo kuhusu uchimbaji wa malambo: Mwaka 2002/2003, Wizara ilituunga mkono kwa kuchangia gharama za uchimbaji malambo. Kwa kila lambo, Wizara ilituchangia shilingi milioni tatu, tunashukuru sana. Ombi la kwamba Wizara iendeleze utaratibu huu, mwaka huu tunao mpango wa kuchimba malambo matatu Wilayani Manyoni. Tunaomba na kuikaribisha Wizara ituchangie kama ilivyofanya 2002/2003. Malambo haya ni muhimu sana kwa mifugo na matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchimbaji wa mabwawa ya umwagiliaji. Wilayani Manyoni, tunao mradi wa kilimo cha umwagiliaji chini ya ufadhili wa *IFAD.* Tunashukuru kwamba, katika *scheme* tano, mifereji ya kupeleka maji mashambani pamoja na mabanio ya kuongoza maji*,* vimejengwa na vinafanya kazi. Tatizo ni kwamba, *IFAD* hawana fedha za kujenga mabwawa ili wakulima wahifadhi maji na wayatumie wakati wa kiangazi. Kwa hiyo, miradi hii inatumika wakati wa mvua tu. Ombi ni kwamba, Wizara izibe pengo hili kwa kusaidia ujenzi wa mabwawa hayo kwa awamu au ituunganishe na wahisani wengine wanaofadhili miradi ya mabwawa. Awamu ya kwanza, mabwawa tungependa yajengwe katika sehemu za Saranda na Msemembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kufufua mradi wa *Rift Valley* (Manyoni). Mradi huu ulijengwa miaka ya 1970 na ulihusisha Vijiji vya Chibumegwa, Mpendagani,Chiwingali na Majiri. Vyote vipo katika Bonde la Ufa. Chini ya mradi huu, kisima kilichimbwa na matengi yalijengwa katika vijiji vyote. Vilevile mabomba yalitandazwa kutoka chanzo cha maji hadi katika vijiji vyote. Muda mfupi baadaye, mradi huu mkubwa uliporomoka na mtandao wa mabomba ukavurugika kwa mabomba kuibiwa. Baada ya miaka mingi ya Wananchi hao kukosa huduma hii, upo umuhimu wa kushirikiana baina ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni na Wizara kufufua mradi huu.

Miundombinu muhimu bado ipo, kwa mfano, kisima na matangi. Kazi kubwa ni kurejesha mtandao wa mabomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kuunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. DR. IBRAHIM S.R. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kutamka kuwa naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri na kwa utendaji bora wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Naomba nimpongeze pia Naibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Diallo, Katibu Mkuu, Bwana Vincent Mrisho, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wakuu wa Mashirika na Taasisi zote zilizoko kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa na mpango wa kuboresha huduma ya maji katika Wilaya ya Kibaha, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake. Kwa muda mrefu sasa, hali ya upatikanaji maji Wilayani Kibaha, haijawa ya kuridhisha. Kwa wastani, anayepata maji sasa, hupata huduma hiyo kwa siku 10 kati ya 30 za mwezi. Hata hivyo, malipo ya huduma hiyo yanabaki kuwa zaidi ya Sh. 18,000/= kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kukamilisha Mradi wa Maji wa Wami – Chalinze. Mradi huu una umuhimu wa pekee kwa eneo lote lile la Jimbo la Chalinze na Kata moja ya Kibaha – Magindu. Nashauri Wizara iendelee na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya awamu ya pili ya mradi, ili Wapiga Kura wangu wa Kata ya Magindu ambako kuna ukame mkubwa, nao wanufaike na huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linalonikera zaidi kwa sasa ni hatua *ya City Water* kusitisha huduma ya maji kwenye *line* ya Kongowe – Vikuge – Soga, Wilayani Kibaha. Baada ya kulifuatilia suala hili kwa karibu, ikiwa ni pamoja na kwenda eneo husika na baada ya Mkuu wa Wilaya ya Kibaha kushughulikia suala hili, imebainika kuwa *line* ya maji ya Kongowe – Vikuge – Soga, imefungwa. Tarehe 22 Julai, 2004, Meneja wa *City Water* Kibaha, alimwandikia Mkuu wa Wilaya, barua Kumb. Na. *City Water/KIB/2/VOL.2/85,* kumwarifu kuwa maji ya *line* ya Soga na Vikuge, ilikatwa tangu tarehe 6 Julai, 2004, kwa sababu wateja wa vijiji hivyo hawalipi bili za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *line* ya maji ya Kongowe – Vikuge – Soga hairidhishi. Lakini pale maji yanapopatikana, *line* hii huhudumia watu wengi, wakiwemo Wananchi wa Kijiji cha Vikuge, Shamba la Serikali la Malisho Vikuge, Shule ya Sekondari ya Rafsanjani Soga, Zahanati na wakazi wa Kijiji cha Soga. Kati ya wateja wote hao, wapo wanaolipia ankara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ijumaa tarehe 23 Julai, 2004, Mkuu wa Wilaya ya Kibaha aliwatuma Afisa Usalama wa Wilaya *(DSO)* na Katibu Tarafa wa Kibaha, kwenda Vikuge na Soga kuhakiki orodha ya wateja iliyotolewa na *City Water* kwa Mkuu wa Wilaya na hali ya upatikanaji maji katika *line* hiyo. Uhakiki huo umebaini kuwa

orodha iliyotolewa na Meneja wa *City water* kwa Mkuu wa Wilaya ya Kibaha siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wa walioorodheshwa ni watu ambao hawajawahi hata kuwa na mtandao wa maji, hata wateja wanaolipa ankara zao wamejumuishwa kuwa hawalipi, Shule ya Sekondari ya Rafsanjani na wateja wengine kama wao, wanapewa ankara moja badala ya ankara nyingi kulingana na idadi ya nyumba zilizopo na hivyo kuikosesha kampuni mapato, pia ankara hizo zinaandaliwa mezani bila ya kujua kilichopo kwenye eneo husika *(field)* na taarifa za wateja, ankara na upatikanaji maji kwa ujumla si sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha *City Water* kufunga *line* nzima bila ya kujali anayelipia na asiyelipia maji, siyo tu cha kuwakosesha wateja wazuri huduma muhimu ya maji, bali pia ni cha kutoa adhabu ya jumla *(Collective Punishment),* kwa watu wengine wasiokuwa na hatia. Kitendo hiki kimewanyima wateja haki ya kusikilizwa na kimewakosesha fursa ya kuhudumiwa kwa haki *(Fair Treatment).* Kitendo hiki ni ukiukwaji wa haki za msingi na uvunjwaji wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *City Water* ni wawekezaji na wanastahili kuvumiliwa ili watimize mipango yao. Hata hivyo, usitishwaji wa huduma kwa ujumla mithili ya kutoa adhabu kwa aliyekuwemo na asiyekuwemo, si sera zetu za uwekezaji. Nashauri *City Water* wafanye yafuatayo:-

(a) Wafunge *line* ya maji ya Kongowe – Vikuge – Soga, ili wale wanaostahili wapate maji;

(b) Wahakiki wateja wao ili wawe na orodha sahihi;

(c) Waache kutoa adhabu za jumla na badala yake wawafungie maji wale tu wasiolipia ankara;

(d) Wafanyie matengenezo madogo madogo *line* za maji hadi hapo watakapokuwa na uwezo wa kuboresha miundombinu husika; na

(e) Waache kutoa taarifa zisizo na ukweli juu ya hali ya maji Kibaha/Soga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namwomba Mheshimiwa Waziri, atembelee Wilaya ya Kibaha na afike kwenye *line* ya maji ya Kongowe – Vikuge – Soga, ajionee mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani zangu kwa ushirikiano wako.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Jimbo la Uchaguzi la Kilombero, naomba kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa maandalizi ya hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, pamoja na tangulizi za rambirambi za awali, naomba kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Kilombero, kuwapa pole sana kwa msiba wa Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira, Wananchi wote wa Ulanga Mashariki. Mwenyezi Mungu, aiweke mahali pema peponi roho ya marehemu. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia machache kwenye bajeti ya Wizara hii. Baada ya kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, lilijitokeza kwa upande wa maendeleo ya sekta, hususan ya Maji, Wilaya ya Kilombero haijapewa mtazamo wa maendeleo, ulio wazi. Vyanzo vya maji Kilombero ni vingi na Jedwali Na. 2 limeonyesha kwamba maeneo yaliyofanyiwa uchunguzi wa maji chini ya ardhi, umefikia chunguzi 27. Lakini sijui katika idadi hii ya chunguzi 27, ni kiasi gani imebaini vyanzo vya maji safi na salama. Hilo jibu ni muhimu sana, hususan kwa Mji wa Ifakara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Wizara kupokea mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge na Wadau wengine juu ya uanzishaji wa Mfuko Maalum wa kuendeshea miradi ya maji, je, Wizara itajielekezaje na hili kwa Kilombero endapo *The Africa Water Facility* kwa mantiki ya ombi langu la maji safi na salama kwa Mji wa Ifakara? Kwenye bajeti ya mwaka wa fedha wa 2003/2004, nilizungumza hili kwa ufasaha, lakini sijapewa maelekezo au ufafanuzi wa tatizo la maji na kipindupindu kwa Mji wa Ifakara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia kwa mpito tu juu ya Nyanda za Malisho. Kilombero, kwa asili ni Wilaya ya Kilimo. Lakini kwa muda sasa, wafugaji kutoka kaskazini mwa nchi yetu, wameanza kuingia na kusababisha migogoro, lakini Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake, mwaka 2003 alizungumzia taratibu ya kuzuia wafugaji kutumia barabara kuu kwa kusafirisha mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiutekelezaji, hili halijatekelezwa kikamilifu na mifugo bado inazagaa na kusafirishwa kwenye barabara hizo kubwa na kusababisha uchafuzi wa mazingira na ajali za magari kugongana na mifugo na hatimaye kusababisha vifo kwa abiria. Nashauri sheria tekelezeka, iandaliwe kuzuia matatizo haya, ili hatimaye sera ya kuendeleza mifugo kisheria iweze kutekelezeka. *Nomadic Movement of Livestock ought to be controlled as intended so as to achieve MDGS by 2025 in this sector.*

Nimalizie kwa kumkumbushia Mheshimiwa Waziri ombi langu la mradi wa maji wa Kibulubulu kwa kutufadhili, akizingatia kuwa pato zima la Jimbo na Halmashauri ya Kilombero, ni takriban Sh. 485m./=. Hivyo, siyo rahisi kwa Kilombero kwa nguvu zake yenyewe, kukamilisha mradi wa shilingi bilioni moja. Kukamilika kwa mpango huu utaliokoa Jimbo la Kilombero na vifo vya milipuko vya magonjwa ya maji. Kwa sababu tu ya *high water table level* ya Mji wa Ifakara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya machache, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini, naungana na Wabunge wenzangu, kutoa salamu za rambirambi kufuatia msiba mkubwa uliotufika kwa kufiwa na Mbunge mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Capt. Mstaafu Theodos Kasapira, Mbunge wa Ulanga Mashariki. Naomba Mwenyezi Mungu, ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Hongera sana. Nimefurahishwa na mipango mizuri ya kuendeleza sekta ya Maji na Mifugo Wilayani Muleba, hususan Jimboni Muleba Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Muleba una tatizo kubwa sana la maji kama ilivyo kwa Tarafa zote za Kimwani, Nshamba na Muleba. Mito ipo na Ziwa Victoria lipo, lakini Wananchi hawana maji safi na salama vijijini. Kwa hiyo, Wananchi watafurahi iwapo utekelezaji wa miradi ya mwaka 2004/2005, itawaondolea au kupunguza kero hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii vilevile kuipongeza Wizara kwa jitihada zake za kuhamisha Kituo cha Mifugo Nshamba. Hongera Mheshimiwa Edward Lowassa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa kuboresha Wizara hii. Yeye na Naibu Waziri, pamoja na Wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya, hasa ukizingatia ukubwa na matatizo ya maji ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru wewe na pia kupitia kwako, nimshukuru Waziri kwa kutupatia Jimboni, kwa maana ya Jimbo la Songwe, tumechimbiwa visima vitano na viwili tumepata toka kwa wafadhili (*Safari Royal).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Waziri, lakini mara baada ya kuchimba visima hivi vitano, bado havijafungwa pampu na Watendaji wanadai hawakulipia pampu na jitihada ya kupata toka Halmashauri, imeshindikana. Naomba Waziri, visima vile vipate pampu na vifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vipo vijiji vifuatavyo ambavyo vimekwisha mwandikia barua na vina shida kubwa sana, tena sana. Vijiji hivyo ni Kapalala, Kininga, Saza, Patamela, Mbala, Namkukwe na Iseche. Lakini pia lipo tatizo kubwa sana la maji ya kutosha pale Mkwajuni, Makao Makuu ya Jimbo toka Mwambani chini. Tayari tumepeleka umeme mpaka kwenye kisima, lakini hakuna pampu ya kupeleka maji pale Mkwajuni, ambako kuna Hospitali ya Wilaya. Naomba Mheshimiwa Waziri, aangalie uwezekano wa kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitarajii kusimama ikiwa nitajibiwa haya machache, yaani visima kwa Vijiji vya Kapalala, Kininga, Patamela, Mbala, Iseche na Namkukwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa rambirambi kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Mtama, kwa Wananchi wa Ulanga Mashariki, kwa kifo cha Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira. Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa dhati kabisa, nimpongeze Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa hotuba nzuri ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2004/2005. Naiunga mkono hotuba hiyo kwa asilimia zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti ombi langu sasa ni moja tu. Nalo ni la kuwawezesha Wananchi wa Rondo, kuiendesha mitambo yao ya maji kwa kutumia umeme badala ya *diesel*, kwa sababu mitambo ya *Lister Peter* iliyopo inatumia mapipa sita ya *diesel* kwa nusu mwezi, yaani lita 1,200 x 900/= (*diesel* bei ya Lindi) = Sh. 1,080,000/= au Sh. 2,160,000/= kwa mwezi kamili na pia inatumia fedha nyingi za ukarabati na ununuzi wa vipuri kutokana na uchakavu wa baadhi ya viputi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya gharama za umeme iliyofanywa na Ofisi ya Mhandisi wa Maji, ambayo ilishirikisha *TANESCO* Lindi, ilikwishatolewa Wizarani mwaka 2003. Tathmini hiyo inaonyesha kwamba, kutoka kwenye *line* ya umeme (Nyengedi) hadi kwenye mashine/chemichemi ya maji ambayo Mheshimiwa Waziri, alipata nafasi ya kutembelea, ni kilomita 12. Kutoka chemichemi hadi Rondo ni kilomita saba. Jumla ni kilomita 19 ambazo zitakuwa na *transformers* tatu na gharama zake jumla zitafikia Sh. 450m./=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kuwa, kutokana na kazi kubwa na nzuri ambayo Mheshimiwa Waziri ameifanya Rondo na sasa Chiuwe na kutokana na uwezo wake wa kufuatilia miradi mbalimbali ya maji, mwaka ujao wa fedha, Wizara ilipe uzito suala la umeme Rondo ili kupunguza gharama ambazo Wananchi sasa wanazibeba kwa gharama ya ndoo moja Sh. 40/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutamka kuwa, naunga mkono hoja hii.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa na Wizara hii, kwa kutekeleza kwa dhati, ahadi alizowaahidi wakazi wa Manispaa ya Shinyanga mwaka 1995. Pia napenda kuwapongeza wafadhili

waliofadhili miradi ya maji katika Manispaa yetu. Hawa ni *OXFAM* England na *OXFAM* Ireland, fedha ambazo zilitolewa na *DFID* Uingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kuwa, kweli Wizara hii imenifagilia kabisa hasa kama nitapenda kugombea tena Ubunge. Matatizo ya maji kwa Kata za Mjini, Manispaa ya Shinyanga, zimeshughulikiwa kikamilifu na tatizo hili limepungua kwa zaidi ya asilimia 75. Tatizo kwenye Kata za Vijiji ni Nkola Ndoto, Ibadakuli, Chibe, Mwamahili, Kizumbi na Mwawaza, bado tatizo ni kubwa. Naamini usambazaji wa maji ya Ziwa Victoria yatazifikia Kata hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mifugo, naomba kupata maelezo yaliyokwamisha ubinafsishaji wa Kiwanda cha Nyama cha *Old Shinyanga*. Kuna tatizo gani la msingi, maana wawekezaji waliwahi kuomba, lakini kwa nini wawekezaji hawakupewa kiwanda hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *DDCA, p*ale Ibadakuli, walipewa kazi ya kusafisha kisima cha Ibadakuli. Badala yake wakachimba kisima na kushindwa kupata maji. Baadaye wakapewa tena fedha, wakachimba na wakakosa maji. Pale Ibadakuli kuna kisima kilichokuwa kinatumika miaka ya zamani, lakini hawataki kukisafisha. Hivi kuna sababu zipi za msingi za kushindwa kusafisha kisima hicho? Wanadai maji hayafai. Fedha nilizopewa Sh. 20m./= karibu zimeisha na maji bado kuyapata. Naomba Wizara ituongezee fedha ili tuweze kukamilisha kazi ya kuwapatia maji Kata ya Ibadakuli. Kuna *Rajani Secondary School, Dispensary, Primary School,* Wananchi, pamoja Kiwanja cha Ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitakia Wizara kila la kheri na mafanikio ya utekelezaji wa waliyojiwekea kwa mwaka wa fedha 2004/2005. Mola awabariki sana.

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa hotuba nzuri. Kwa kweli huyu ni Askari wa Mwamvuli, maana tunaona juhudi zake nzuri za kuendeleza Sekta ya Maji na Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia tu kwa kumwomba Waziri, azisaidie Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka, kupata fedha zao mapema, wanazodai Mashirika ya Serikali. Maana hii ni kero kubwa sana, hususan kwa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo na Naibu wake, Mheshimiwa Anthony Diallo, kwa kazi zao nzuri na mahusiano mazuri ya kikazi na Waheshimiwa Wabunge. Pia naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na nampongea kwa hotuba ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitaelekeza kwenye maeneo yafuatayo: Kuhusu Mtandao wa Maji katika Mji wa Babati. Mtandao wa sasa ulijengwa tangu miaka ya 1945 – 1950. Hivyo, ni dhahiri kuwa mabomba yamechoka, mabomba ni madogo sana, kwani ililenga wakazi 2,000 – 3,000 tu, mabomba yamechakaa na yanavujisha zaidi ya asilimia 60 na matangi ni madogo, yanakidhi asilimia 45 - 50 tu. Wakati wa kiangazi, uzalishaji unashuka hadi asilimia 50 au chini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuunda Mamlaka ya Maji Taka na Maji Safi kwa Mji wa Babati. Mamlaka ilianza kazi rasmi tarehe 1 Desemba, 2003. Mamlaka inahitaji iongeze visima kama vitatu ambapo kuna maeneo mazuri yenye maji kama vile Kijiji cha Singe, ambapo kisima kirefu kiliwahi kuchimbwa na kutoa maji mengi sana.

Kwa bahati mbaya mradi huo ulioanzishwa na Marehemu George Neema, aliyekuwa Katibu Mkuu katika Ofisi ya Waziri Mkuu, haukuweza kukamilishwa. Hivyo, naomba Mamlaka/Wizara ifanye utaratibu wa kufanya utafiti hapo Songe na kuchunguza kisima hicho ambacho kimezibwa hadi sasa. Eneo la pili ni sehemu ya Kitongoji cha Hangoni C karibu na Mji na eneo la tatu ni sehemu ya Kijiji cha Nabwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushauri huu, inaonyesha kuwa mamlaka inahitaji karibu shilingi milioni 400 katika kuweka mita elfu moja, kukarabati mtandao huo wa tangu mwaka 1945 – 1950, kuchimba visima na kujenga matangi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kuwa Wizara imeonyesha nia ya kusaidia Mamlaka hii mpya, kama inavyoonyesha kwenye Hotuba ya Waziri, ukurasa wa 45, *paragraph* ya 64.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya maji vijijini, Mradi wa Maji wa Minjingu, umefanyiwa upembuzi yakinifu mwaka 2000/2001 na kuonyesha kuwa ufufuaji wa kisima kirefu *(borehole)* iliyopo Kitongoji cha Kakoi Minjingu, itahitaji karibu Sh.110m./= na usambazaji utahitaji kiasi hicho.

Hivyo, mradi huu muhimu utagharimu karibu Sh. 200m./=. Mradi huu ni muhimu kwa sababu kijiji hiki kinahemea maji kutoka Wilaya ya Monduli (Mswakini) na vitongoji vingine wanachangia maji na wanyama na hivyo magonjwa kama *amoeba,* kichocho na *typhoid* ni tatizo kubwa. Hili ni eneo la wafugaji, hivyo, matatizo ni makubwa sana. Mradi huu unapaswa kupewa kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wa Magugu (km. 52), ni mradi mkubwa na unapaswa kuhudumia vijiji zaidi ya kumi (10). Ni kweli kuwa Wizara imeweka kwenye bajeti tangu mwaka 2003 na makisio ya awali yalikuwa Sh. 58m./=. Hata hivyo, taarifa nilizonazo ni kuwa, Wizara imetoa Sh. 10m./= tu hadi sasa. Nashukuru kuwa Wizara imeuweka tena mwaka huu (ukurasa 29 – 30) wa hotuba ya Waziri. Naomba sana tena sana, Wizara ijitahidi kutoa kipaumbele kwa ukarabati wa mradi huu kwa kiwango kikubwa, ikiwezekana niondokane na adha ninayoipata kwa mradi huu ambao ni mkubwa na unaathiri watu wengi na Wananchi wameanza kukosa

imani kutokana na utekelezaji mdogo wa mradi huu. Najua Wizara ikiamua inaweza kukamilisha mradi huu katika muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine mikubwa ipo katika Kata za Namine, Gallapo, Qash, Malangi, Sigino, Chemchem-Sarame na Sangaiwe. Hii ni miradi inayohitaji kujengwa na mingine kukarabatiwa. Naomba Wizara iangalie maeneo hayo pamoja na niliyoyataja, yanaweza kuwa chini ya Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira.

Napenda kutanguliza shukrani zangu kwa kuiingiza Wilaya ya Babati chini ya mradi huu. Nakuhakikishia ushirikiano wa kina na patakapotokea matatizo, nitakuarifu mara moja kwa hatua zako za haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakutakia kazi njema na naunga mkono hoja hii.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaongea nami naomba nitoe pole zangu kwa familia za wenzetu waliotutoka. Nina hakika Mwenyezi Mungu atawapa nguvu wafiwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu. Inaeleweka kabisa kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi wangependa tutoe majibu kwa kila hoja iliyotolewa aidha, kwa kupitia mchango wa maandishi au kwa kuongea. Lakini nina hakika muda hautoshi na nina hakika wanaelewa hilo. Kwa hiyo, tutajaribu kujibu yale ambayo muda wetu utaturuhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ambaye ni wewe, kwa kutoa ufafanuzi mzuri wa maeneo mengi na mmekuwa mkitusaidia sana tangu Kamati hii ianze kufanya kazi na sisi. Nina hakika yote ambayo mmetushauri tutaweza kuyashughulikia na kuboresha sehemu zote ambazo uwezekano upo. *(Makofi)*

Pia, napenda nimshukuru Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, kwa kuunga mkono hoja na kwa kutushukuru. Kwa kufika hapa kuleta bajeti hii, amekuwa ni mchango mzuri sana na amekuwa ni mtu mwenye uzoefu wa kuelewa mambo mengi. Kwa hiyo, tunapenda tumshukuru kwa hilo. *(Makofi)*

Napenda pia nimwarifu kwamba, tatizo alilolieleza ambalo Chuo cha Sokoine wanalifanyia kazi, la utafiti wa uvunaji wa maji ya mvua linaeleweka Wizarani na kama ilivyo kwenye taarifa tumeeleza kwamba, maeneo mengi kwa mwaka huu na mwaka uliopita tumekuwa tukifanya utafiti ili kujua chanzo cha maji chini ya ardhi na pia kama mlivyosikia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameeleza jinsi gani mwaka huu tutakwenda hata kutoa mafunzo kwa ajili ya uvunaji wa maji ya mvua kwenye baadhi ya maeneo. Lakini tatizo linabaki pale pale kwamba bajeti isingeweza kukidhi maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda tupokee shukrani kwa ziara ambayo tulimhusisha ya kwenda Misri, wameona mengi na kwa kweli uwezekano ungekuwepo

Waheshimiwa Wabunge wengi wangeweza kwenda kwenye maeneo kama hayo ili kuona wenzetu wanafanya nini na mambo ya kilimo, utunzaji wa maji na kadhalika. Kwa hiyo, napenda nimshukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda niende haraka haraka kwa maeneo ambayo ameyazungumzia Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha. Kuhusu *low consumption* ya nyama, suala hili limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. *Low consumption* ya nyama yaani hatuli nyama nyingi, hii inaeleweka. Makabila ya wafugaji hapa nchini ukweli ni kwamba huwa hatuli nyama, tunangoja mpaka afe ndiyo tunakula na ndiyo ilivyo. Hata baadhi ya familia zetu wanaoishi mijini nyama ni mboga, hata ukienda hotelini unaagiza naomba wali kwa nyama, tofauti na wenzetu ambao utakuta *consumption* ni kubwa. Chakula ni ile nyama, ni ile mboga na mara kwa mara huwa hawatumii mchuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi mchuzi ukiwepo na nyama kidogo unaweza kumaliza ugali kilo mbili. Ndiyo hali ilivyo na hasa ukiwa Msukuma kama mimi. Kwa hiyo, kuna tatizo hilo la asili na kuna matatizo mengine pia ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumza ya uwezo na kadhalika. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bei ya mitamba kuwa juu na kuomba ipunguzwe, suala hili kwenye hizi *livestock multiplication units* zetu bei zilizopo ukweli ni kwamba hazizingatii faida ya kuweza kusema ni ya kibiashara. Kwa hiyo, bei ziko chini ila wale ng'ombe wanakuwa na matunzo mazuri sana. Kwa hiyo, gharama za kutunza mifugo hao zinakuwa ni kubwa sana. Hiyo ndiyo sababu kubwa inayofanya bei kuonekana kuwa ghali, lakini tunasema ni ghali tunapolinganisha na ng'ombe ambao wako kwenye hali mbaya zaidi ambao Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, alikuwa anasema wanatembea kwenye treni siku tatu wanafika Dar es Salaam wakiwa kwenye hali ya udhoofu sana. Kwa hiyo, ukinunua ng'ombe wa mtamba kutoka kwenye maeneo hayo ni hakika kwamba bei tunayotoa haina faida kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kufufua majosho, ukweli ni kwamba Wizara yetu ikishirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa mwaka uliomalizika tumejitahidi sana kupeleka fedha kwa ajili ya majosho na kwa ajili ya kuchimba Malambo mengine kwa ajili ya kutumika kwa ajili ya umwagiliaji.

Waheshimiwa Wabunge, tatizo lililokuwepo huko nyuma wakati Halmashauri zetu za Wilaya zilikuwa zinaangalia haya majosho walikuwa wanatoza kodi, wanachukua fedha na hizo fedha zinatumika kwenye semina, hazirudishwi kwenye kujenga au kukarabati majosho.

Sasa ni Serikali Kuu tu imechangia muda wote huu kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majosho. Kama ilivyo kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri mtaona kwamba, mwaka 2003 tumekarabati majosho mengi sana, lakini inategemea ni maeneo yapi ambako tunaanzia. Kwa hiyo, tumeanzia sehemu ambazo kuna mifugo mingi na sasa hivi tunaendelea chini ya Reli ya Kati yaani Mikoa ya Kusini na kadhalika.

Hii inatokana na kwamba kwa miaka mingi sana tulikuwa hatuweki fedha kwa ajili ya ukarabati. Tulikuwa tunachukua tu fedha kutoka kwa wafugaji, lakini haturudishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vya nyama, hilo nakubaliana nalo kwamba sasa tumeanza na hilo tatizo lilikuwepo kwa sababu *investment* haikuwepo. Sasa hivi tumeanza na hizi *abattoir,* tuna matarajio makubwa kwamba hizi *abattoir* baada ya kuziweka kwenye mikono ya watu binafsi kwa sababu Serikali hatutakiwi kufanya biashara, tutazalisha fedha ambayo ita-*revolve* na tutaendelea na ujenzi na kukabidhi kwa *Private Sector* kama itakavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niende kwa yale ambayo Mheshimiwa Shellukindo ameyazungumza. Kwanza nakubaliana naye kwamba tunapozungumzia maji ni vizuri sana kuzungumzia juu ya mazingira kwa sababu kwa kipindi kirefu tumeona sasa hivi bila kuzingatia mazingira yetu hali ambayo ameielezea Mheshimiwa Njelu Kasaka, itaendelea kuwepo ya kupungua kwa maji mwaka hadi mwaka.

Kwa hiyo, ndiyo maana Wizara ikaliona hilo na tunachokifanya sasa hivi tunapoangalia kwamba tunapeleka mradi wa maji tunahakikisha kuwa mradi huo unaendana na usafi wa mazingira. Baada ya hapo nina hakika kwamba hali itabadilika baada ya kupitisha sheria, maana tuna mapendekezo ya sheria tunayoleta kwa Waheshimiwa Wabunge ya kubadilisha sheria ya maji. Kwa sasa hivi sheria haizungumzii juu ya vyanzo vya maji, lakini sheria tunayoileta itazungumzia juu ya vyanzo vya maji. Maeneo yatatangazwa kwamba ni maeneo ya vyanzo vya maji na hatutaruhusu *activities* za kibinadamu kwenye hayo maeneo. Kwa hiyo, nina hakika kwamba hii itatufikisha mahali pazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya maji ya Ziwa Victoria, napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliozungumzia suala hilo. Kwa kweli ni hatua moja ambayo tunatakiwa kuiandika kwamba wakati wa enzi zetu kama Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tuliwezesha kuchukua maji na kuanza kuyapeleka maeneo nje ya Kando ya Ziwa. Kwa hiyo, napenda niwashukuru sana kwa hilo na nina hakika kwamba mtaendelea kutupa nguvu. Sasa hivi tunaangalia uwezekano wa Miji mingine ambayo ina matatizo kama ilivyoelezwa Tarime na sehemu nyingine. Hatuoni sababu kwa nini tusifikie mahali matatizo ya maji ya kunywa yakapungua ili tuanze kuangalia matatizo mengine ambayo tunaweza kuya-*solve* kwa kutumia njia mbadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kwamba Bumbuli hakuna maji, lakini kuna chemchem, kwa bahati nzuri Bumbuli iko kwenye programu ya *World Bank.* Ni Wilaya zote na naomba nijibu hili kwa kujumuisha wote ambao wamezungumza kama Mheshimiwa Paul Kimiti amezungumza juu ya Wilaya yake kwamba ina matatizo ya maji.

Waheshimiwa Wabunge, naomba suala hili tulizingatie. Chini ya programu za *World Bank,* Wilaya ndiyo zinatakiwa kuibua miradi kwani wao ndiyo wanapanga miradi. Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tukae karibu na *DED* na

Wahandisi wa Wilaya wa Maji kwa sababu usipofuatilia watapendekeza sehemu ambazo huenda hazina matatizo na maji na usipoangalia mvutano wa kisiasa unaweza kukukumba.

Waheshimiwa Wabunge, nawaomba sana tukirudi kwenye maeneo yetu tuzingatie kwamba miradi yote itakayopendekezwa chini ya huo mpango wa Benki ya Dunia tumeiona kwa sababu mpango huo ukweli ni kwamba hauna *limit.*

Kama una miradi kumi na uwezo wa kuchangia ile *five percent* kutoka kwenye Kijiji na *five percent* kutoka kwenye Halmashauri upo, hatuna *limit* ya miradi, unaweza ku-*draw* mpaka *1 billion* au ukachukua zaidi, inategemea na idadi ya miradi na ukubwa wa miradi.

Kwa hiyo, ningependa sana niwaombe Waheshimiwa Wabunge ambao Wilaya zao ziko kwenye awamu ya kwanza na wale ambao wako kwenye awamu ya pili waanze sasa hivi kushughulika pamoja na Halmashauri ili miradi hii yote ambayo wameizungumzia iingizwe.Miradi ile kama ya Kwakidole kwa mtani wangu, Mwangifuta, *Mhalalu Wells,* Mumbuzi, Soni, Bumbuli Juu, yote hiyo mnaweza kuiingiza kwenye hiyo programu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo amelizungumzia Mheshimiwa ni kutushukuru. Ametushukuru kwa mipango mizuri, naomba tupokee shukrani zake.

Kuhusu alivyouliza Mheshimiwa Kisyeri Chambiri, naomba hilo Mheshimiwa Waziri atalielezea vizuri zaidi kwa sababu ilikuwa ni ahadi ya Rais, nina hakika kwamba ataridhika na ataturuhusu twende tukashughulikie huo mpango.

Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, tunashukuru sana kwa kutupongeza kwa shughuli ambayo tumeifanya hadi leo. Ni kweli Kisarawe ilikuwa na matatizo mengi sana, tumejitahidi kwa uwezo wetu wote kutatua matatizo yaliyokuwa ndani ya uwezo wetu na kwa bahati nzuri Kisarawe nayo iko chini ya mpango wa *World Bank.* Kwa hiyo, hizo Kata alizozisema, huo mradi wa Mzenga, yote hiyo sasa hivi wanaweza kuileta kama programu. Programu hiyo imeishaanza na nadhani mmeshaona kwenye vyombo vya habari wametangaza tayari kutafuta *consultant* kwa ajili ya kutengeneza hiyo miradi katika hali inayokubalika na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la kunywa maziwa, Wazaramo wameanza kunywa Maziwa. Nashukuru sana na nina hakika kwamba hiyo ni *credit* kwangu na kwa Mheshimiwa Waziri kwa kuwawezesha Wazaramo kunywa maziwa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Jumanne Nguli, ametupatia pongezi, tunazipokea. Kuhusu Kata 13 za Singida Vijijini, bahati nzuri Singida wako kwenye programu nyingi sana. Kuna *Water Aid,* wako pia kwenye *World Bank* na eneo la Mjini wako kwenye *project* ya *BADEA.* Mheshimiwa Jumanne Nguli, nadhani sioni kitu gani kingine ambacho tungeweza kufanya. Tumejitahidi sana kutatua matatizo katika Mji wa Singida na

maeneo yanayozunguka. Kwa ujumla, karibu katika Mkoa mzima wa Singida, tumejitahidi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sheria ya kuogesha mifugo, hilo nalo limo, tunajaribu kuli- *fine-tune* sasa hivi ili tuweze kuleta mapendekezo ya hiyo sheria.

Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, naomba Mheshimiwa Waziri atakupa maelezo kuhusiana na hoja kama mbili, tatu, ulizozielezea. Lakini kimoja ambacho labda nikizungumzie tu ni kwamba, Meatu au Mwanhuzi lile bwawa kubwa ni kweli limekamilika na ile *distribution* tumejaribu kuzungumza na Waholanzi na wamekubali. Hapo awali walikuwa hawakubali kuhudumia miradi ambayo ni ya malambo au mabwawa, lakini sasa hivi wamekubali. Sasa chini ya programu ya Waholanzi inakidhi mahitaji ya maji maeneo mengi sana ya vijijini, karibu shilingi bilioni 9 zinatumika kwa mradi huu. Kwa hiyo, ni ushirikiano tu unahitajika kati ya Wilaya, Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani, ili tuweze kutatua matatizo ya wananchi ambayo yapo mpaka wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mengine aliyouliza Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Waziri atajaribu kuyazingatia kama nilivyomweleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyomwelewa Mheshimiwa Benedict Losurutia, anajaribu kutueleza kwamba urasimu wa programu ya *World Bank* ni mkubwa. Lakini urasimu huo ni matakwa ya *procedure* za uwazi na ukweli kwenye *project* zote za *World Bank,* huwezi ukaruka. Tatizo letu pia ni pale tunapoomba takwimu inakuwa ni tatizo kuzipata kutoka kwa watendaji wetu. Lakini nina hakika kabisa miradi kama hii hata kama ungekuja kwenye eneo langu ningependa huu mradi ungetokea jana na siyo leo, kwa sababu tuna nia na tuna tatizo kubwa la maji. Kwa hiyo, tutajaribu kuboresha pale ambapo itawezekana.

Mheshimiwa Benedict Losurutia, suala lingine ambalo umelizungumzia ni kwamba Vijiji vilichimba Malambo, lakini maji yamekauka na bahati nzuri umeeleza kwamba ni kwa sababu ya ukame. Hatuwezi kuzuia tatizo la ukame kwa sababu kama unavyoelewa tunategemea mvua na kwa bahati mbaya sana hamko karibu na eneo ambalo lina maji mazuri ya kutosha, mko mbali na mito na mko mbali na maziwa. Kwa hiyo, ni tatizo ambalo tutajaribu kulitatua kwa kuwapatia malambo kila inapowezekana ili kupunguza matatizo angalau kwa kiwango fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matatizo ya fedha zinazotoka kwa ajili ya malambo, amesema shilingi milioni 3 hazitoshi. Ni kweli tumeliona hilo, wenzetu tunaoshirikiana nao sasa hivi Wizara ya Kilimo na Chakula tumekubaliana iwe ni shilingi milioni 5 kwa baadhi ya malambo na shilingi milioni 10 hadi 15 kwa baadhi ya malambo. Kwa hiyo, hilo linaeleweka na tunashukuru sana kwa kutukumbusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, ametupatia pongezi, tunazipokea. Kuhusu kwamba gharama za uzalishaji ni kubwa kwa sababu ya miundombinu iliyochakaa, chini ya programu hii ambayo Wafaransa wanafanya *study*

sasa hivi nina hakika mitambo itaboreshwa na matatizo hayo yatapungua. Gharama hazitapungua kwa sababu kama mnavyofahamu gharama za umeme bado ziko juu na kadhalika, ila ni sehemu ambazo wanatumia maji ya mtiririko au *gravity,* pale gharama zinakuwa chini kidogo. Kwanza kwa mashine zinazotumia umeme mara kwa mara zinalika haraka sana, hivyo vipuri vinahitajika mara kwa mara. Kwa hiyo, gharama hiyo ni vigumu sana kuikwepa.

Lakini pia tuna tatizo moja kwamba, huko nyuma tulizoea kwamba maji yalikuwa ni ya bure, sasa hiyo *hangover* ni lazima tujaribu kuiondoa. Pia, bado wakati mwingine unaondoka nyumbani huku unaacha bomba limeharibika na maji yanavuja, lakini hujali! Wanapokuwekea mita ndiyo unaanza kushtuka kwamba: "Alaa, kumbe bei ya maji ni kubwa!" Hiyo inatokana na mazoea ya huko nyuma na hatuwezi kumlaumu mtu yeyote. Haya mazoea yatakwisha *overtime* na nina hakika kwamba mambo yatabadilika na watu watakuwa na nia ya kutunza maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza mwaka 2003, leo watu wachache sana hapa ambao vyoo vyao vina *double flash,* ina maana ukijisaidia haja ndogo utatumia *flash* ndogo ya maji kidogo, lakini ukienda haja kubwa utatumia *flash* kubwa ambayo ni *five US gallons.* Kwa hiyo, kwa matumizi yote hayo baadaye tutabadilika kwa sababu ya gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *sharing* ya maji ya mifugo na wanyamapori, hiyo ni kweli. Lakini rafiki yangu Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, sasa hivi hakuna ujanja, kuna maeneo mengine wana maji ya malambo sasa utafanyaje? Tunachowashauri wananchi ni kuchemsha yale maji ya kunywa. Acha hivyo, kuna wengine tunaishi na wanyama, kuna wenzangu rafiki zangu wa Kichaga wanalala na wanyama ndani ya nyumba. Kwa hiyo, ni mila zetu. Unachotakiwa ni kuchemsha maji ya kunywa, lakini kwa kuwa maji haya mengine mradi yanaonekana ni masafi ni vizuri ukayatumia kwa matumizi mengine. Lakini tabia hizo huwezi ukazibadilisha siku moja, itachukua muda, ukitaka kuzibadilisha siku moja utapata matatizo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *metered customers* ni kweli alilolisema Mheshimiwa na maagizo ya Wizara ni kwamba, mahali ambapo kuna mita ni lazima mtu alipe kufuatana na mita ile. Lakini sasa kuna uhuni unafanyika wakati mwingine kuhusu hili ulilolieleza Mheshimiwa Ibrahimu Marwa. Unakuta kwamba mtu amewekewa mita, halafu anachimba shimo ana-*tap* maji kutoka sehemu nyingine, anachosahau ni kwamba ile *meter reading* ya mara ya kwanza ilipowekwa tulisha-*record* matumizi yake. Sasa unakuta *all over sudden* bili ilikuwa inakuja labda shilingi 3,000/= au shilingi 4,000/= unashtukia imeteremka shilingi 500/=, lakini ukiangalia ile kaya ukakuta kuna familia ya watu 10, unashindwa kuelewa kimetoeka nini! Pale inabidi wajaribu kukaridia kwa sababu siyo ukadiriaji ambao ni wa kimbumbumbu, ni ukadiriaji wa kisayansi kwa sababu *meter reading average* ya huko nyuma tunaifahamu.

Kwa hiyo, kwenye maeneo kama hayo ambayo siyo mengi mambo kama hayo yanatokea, lakini pia sheria zinavunjwa. Tunawaambia kila siku watu wetu wa Mamlaka za Maji kwamba watu wa namna hiyo wapelekeni Mahakamani, lakini tuna matatizo

kwamba mnajuana wewe ni mtoto wa fulani, kupelekana Mahakamani inakuwa tabu. Kwa hiyo, wanachofanya ni kwamba wanakupiga faini, mambo yanaendelea. Lakini tatizo kweli lipo na tunalikubali kwamba litapotea kadri siku zinavyoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la Mheshimiwa Martha Wejja, nina hakika Mheshimiwa Waziri atalijibu. Mheshimiwa Martha Wejja, amezungumza juu ya mambo ya *City Water.* Pia, kuhusu maji ya chupa ni kweli, leo Mheshimiwa Martha Wejja, ameeleza kitu nikakielewa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishazungumza na watengenezaji wa maji kama miezi sita, saba, iliyopita. Niliwaambia kwamba haya matatizo ya magonjwa tunayoyapata yanatokana na maji yao, yanakuwa *tempered* kama alivyokuwa anaelezea kiufundi kabisa Mheshimiwa Martha Wejja. Lakini sasa kila siku matatizo ya *tempering* ya bidhaa ni makubwa sana, siyo kwa maji tu, yako kwa vitu vingi sana. Nadhani labda wameshindwa vitu vingine ambavyo vinakuwa taabu sana kuviiga, lakini uigaji uko kwingi sana. Mfano hata redio, unaweza kukuta redio ambayo siyo *Phillips* wameandikwa *Phillibs,* badala ya *'p'* imewekwa *'b'.* Hiyo ni *tempering,* ni *counterpart.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa matatizo kama haya tunachowashauri watengenezaji ni kwamba, unapouza bidhaa yako, nenda ukakusanye baadhi ya *sample* uje ucheki kama zina ubora ambao ulitoka kiwandani. Ukiona kuna matatizo pale unatakiwa kuchukua hatua ambazo zinaweza kuzuia hilo tatizo kama kushtaki wanaohusika. Uzuri wa *Private Sector* wanajua sana kupeleleza, *information* zote wanazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulilozungumza pia ni kwamba, watengenezaji wa maji ya chupa leseni zao zinasema ni *bottled water,* siyo kwenye *plastic bags.* Tumezungumza nao waache, sasa nashangaa sana labda wanataka tutumie sheria, lakini nina hakika ni watu wanaoelewa. Leseni zinaruhusu maji kuwekwa kwenye chupa na siyo kuwekwa kwenye vile vipaketi, *as a result* wanachafua mazingira. Ukifika stendi ya basi ndiyo utashangaa sana, mifuko ya *plastic* iko kila sehemu! Kwa hiyo, nina hakika kwa kupitia Bunge lako Tukufu watengeneza maji watakuwa wametusikia na watatekeleza yale ambayo tulikubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Paul Makolo, anasema kwamba Jimbo lake ni kame, tunakubaliana naye. Lakini kwa bahati nzuri huu mradi hatua ya kwanza utapeleka maji Mjini Shinyanga na vile Vijiji vya upande wa juu wa Jimbo lake kwa sababu kuna Vijiji kwenye Jimbo lake ambavyo vitaguswa. Sasa tutaangalia hapo baadaye maeneo yapi pia tunaweza ku-*supply* nje ya Shinyanga kwa sababu lile bomba linatosheleza mahitaji ya maji kwa miaka 20 ijayo.

Kwa hiyo, tunaweza baadaye tukasema: *"Okay,* miaka 20 ni mingi sana, tuongeze *distribution* tuwe na uwezo wa kutimiza mahitaji ya miaka 10." Kwa hiyo, ina maana nusu ya maji yatakayokuwa yanapelekwa Shinyanga yanaweza kufika kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Paul Makolo, ni kweli kabisa Jimbo lako ni kame na linaeleweka kuwa ni kame, lakini siyo ukame tu, pia lina madini ambayo ni mabaya kwa afya ya binadamu. Kile kisima ulichokieleza cha Maganzo, wakati kinachimbwa baada ya kuvuta maji kulionekana kuna *chemical* mbaya na ni kweli walikataza maji yale yasitumike. Baada ya kukataza kutumika sasa sababu ya *destruction environment* maji yaliyopo sasa hivi hayawezi kutosha kuweka pampu ikayachukua na kuweza kuya-*distribute.* Sasa hiyo *technology* ya kusafisha maji imepatikana. Ukienda Kolandoto ambao ni jirani zako, sasa hivi wamefunga mashine pale kwenye kisima ambacho kina maji mengi na wanasafisha hayo maji na kutoa hiyo *chemical* kwenye hayo maji kwa ufanisi zaidi. Kwa hiyo, hiyo *technology* tuna hakika kwamba itatusaidia kupunguza haya matatizo ya maji kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Paul Makolo, kuhusu suala la kwamba madawa ya mifugo ni ghali, nadhani amesikia Mheshimiwa Waziri amesema tunatafuta uwezekano wa kupunguza makali kwa kuweka ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, nadhani ndiye aliyefuatia jioni hii na ameongelea kuhusu *rainwater harvest,* ndiyo tunakazania hilo. Mvua inanyesha, *runoff* ya haya maji yanakwenda kwenye Mito, baadaye yanakwenda baharini bila kutumika.

Kwa hiyo, tumeomba Halmashauri zetu za Wilaya, za Miji na kadhalika ili waweke masharti kwamba unapopeleka ramani zako za ujenzi wa nyumba ni lazima katika ujenzi wako wa nyumba uweke *gutter* kwa ajili ya kukusanya maji ya mvua. Kuna baadhi ya mapaa ni makubwa sana kiasi kwamba unaweza kukusanya maji yakakutosheleza miezi mitatu mpaka minne wakati wa ukame. Kwa hiyo, hilo tunakubaliana na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, kwamba Wizara inashughulikia tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ugani wa mifugo, suala hilo ni lazima tuelewe utaratibu uliopo sasa hivi. Zamani Maofisa wa Ugani walikuwa chini ya Wizara moja kwa moja, sasa hivi wako chini ya Halmashauri za Wilaya na Halmashauri za Miji. Katika maboresho maeneo yote haya sasa hivi yanatafutiwa wataalam, waajiriwe wataalam wanaoweza ili maeneo haya yote yaanze kupewa vifaa. nina hakika Ndugu zangu, kuvunja nyumba inachukua masaa tu, lakini kujenga nyumba inachukua muda mrefu. Mfumo ambao ulikuwepo huko nyuma ndiyo uliotufikisha hapa tulipo, sasa tunajaribu kuboresha maeneo mengi na nina hakika kwamba mtashirikiana na Serikali katika kutatua haya matatizo ili mfumo wetu uweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la wafugaji wa kuku, tumewasaidia sana katika maeneo mengi. Sasa hivi kuna chanjo ya mdondo ambayo inatengenezwa na Wizara na imesaidia sana kwani kuku anaonekana ndiyo mali ya maskini. Kuku ndiyo wanamfanya mama awe na uamuzi wa asilimia 100. Mama akiwa na matatizo ni rahisi kuuza kuku kuliko kuuza ng'ombe au mbuzi. Hayo yanahitaji ridhaa ya mzee. Kwa hiyo, nina hakika kwamba kwa hatua ambazo tumezichukua matatizo haya ya ufugaji wa kuku yatapungua na tutaendelea kuboresha zaidi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa John Mwakipesile, amezungumzia kuhusu maji Kyela. Kyela iko chini ya mradi wa *World Bank,* pia hiyo miradi yote uliyoisema, hata Kyela Mjini kwa sababu ni Wilaya. Vile vile, Kasumulu, *Kanga Group,* tena yako ma-*group* mengi tu, kuna *Sinyanga Group,* nadhani nakumbuka. Yote hayo mtayaingiza kwenye huo mradi na huu mradi kwa bahati nzuri unaanza ku-*takeoff* kuanzia mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, nina hakika Mheshimiwa John Mwakipesile, utatumia nafasi hiyo ili kuweza kutatua matatizo ya wananchi wa Wilaya ya Kyela.

Mheshimiwa Njelu Kasaka, suala la ulaji wa nyama nimelizungumzia. Kuhusu *Private Sector Involvement,* tumeanza kuihusisha hivi karibuni tu haina muda mrefu. Kwanza haya majosho yalikuwa chini ya Halmashauri kama nilivyoeleza. Tunaanza kuwakusanya wafugaji na tunawajengea majosho chini ya mradi wa *Tanzania Livestock Marketing Project.* Tunawajengea majosho halafu wanajikusanya wanafungua mifuko na wanaweka uongozi. Mambo hayo tumefanya sehemu nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti,*Private Sector* ambao ndiyo wafugaji wenyewe tumeanza kuwashughulikia hivi karibuni tu, hatuna muda mrefu sana. Kwa hiyo, tungoje kuona mafanikio yake. Lakini mafanikio mengi nina hakika yatakwenda kama tulivyotarajia kwa sababu *so far* tunaona wanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kwamba malambo yamebomoka, ni kweli. Usimamizi usipokuwa mzuri malambo yatabomoka. Hapa napenda nitoe mfano wa Wilaya ya Misungwi. Misungwi zile shilingi milioni 3 tulizowapa walichofanya ni kwamba waliajiri watu. Kwa kweli malambo haya ya namna hii na makubwa zaidi yalikuwa yanachimbwa na watu miaka ya nyuma, sasa wao waliajiri watu na Mhandisi wao akasimamia vizuri.

Baada ya hayo malambo kuchimbwa wakazungushia uzio wa miti fulani ambayo huwa inakua haraka sana halafu wakaweka geti, pia wakachimba mfereji unakwenda sehemu ya nje ambako wakajenga *trough* ya ng'ombe. Kwa hiyo, hilo tatizo la kuchanganya ng'ombe na binadamu halipo, halafu hilo eneo linakuwa liko *protected.*

Lakini kuna maeneo mengine ambayo inasikitisha sana, wahandisi wetu na wengine siyo wahandisi maana tumegundua wengine basi wanajiita wahandisi tu, unakuta *design* waliyoweka inabomoka mvua ya kwanza tu. Kwa hiyo, hilo tatizo linaweza kuwa limetokea Chunya na tunasikitika sana na tutaangalia katika hatua ya pili, tuone uwezekano wa kuweza kuyaboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ambayo umeeleza ya kata zenye matatizo, Mbugani, Chokaa, Makangorosi na maeneo mengine, tutajitahidi kuyaingiza kwenye programu ambazo zitakuja *through ministry.* Lakini wakati huo huo ni vizuri sana tuziombe Wilaya kwa sababu mpaka sasa hivi Wilaya nyingi sana haziweki *project* za maji kwenye bajeti zao. Ni Wilaya chache sana zinazoweka bajeti. Hata kuwaajiri waandisi hawaweki bajeti ya ajira ya wahandisi. Bado wana-*hangover,* wanategemea Serikali Kuu, itawaletea wahandisi. Kwa hiyo, nina hakika kwamba matatizo mengi

Mheshimiwa Njelu Kasaka, uliyoeleza ni kweli tuna matatizo nayo na tuna hakika tutayatatua jinsi tunavyokwenda kama tulivyokueleza tulikupa malambo mwaka 2003 na nina hakika yangetengenezwa vizuri kama tulivyotarajia yangesaidia sana. *(Makofi)*

Lakini tatizo lingine ambalo tumeliona baada ya kuongeza bajeti nina hakika sasa hivi katapila na vyombo vingine vikubwa vitatumika katika kuchimba. Maana ukiwa na shilingi milioni 10 au shilingi milioni 15 itakuwa ni *cost effective* kukodisha trekta au katapila kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hiyo, kazi inaweza kuwa nzuri zaidi.

Pia Mheshimiwa Paul Kimiti, amepongeza *TRA* sawa, matumizi ya vyombo vya habari nakubaliana naye ni vizuri sana. *Lake Victoria* tunakubali kwamba tumejitahidi pamoja na ninyi kwa ajili ya kufanikisha miradi yetu hiyo, mradi wa kwanza ukiwa ni huo ambao ni mkubwa sana. Mfuko wa bajeti ni kweli lilikuwa wazo ulilolitoa na tukalipokea na wakati huo huo hili wazo tulifufua kumbe Wizarani lilikuwepo miaka mingi. Tulichofanya sasa hivi ni kuboresha ili likidhi mahitaji haya ya leo ya *project* zetu za maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *pending project* ziko nyingi, tunajaribu kuzipunguza. Kama tulivyoeleza mwaka 2003 tumefanya kama 30, mwaka huu ziko kama 40 kwenye kitabu cha bajeti kama ulivyoona. Vyanzo vya maji kwa ajili ya Sumbawanga ni kweli, Sumbawanga ina matatizo. Lakini pia wananchi wa Sumbawanga watusaidie. Walichoma vyanzo vya maji vyetu mwaka 2003 ikaharibu sana upatikanaji wa maji kwa Mji wa Sumbawanga. Kwa bahati sana Sumbawanga ulivyoeleza inapata *supply* kwenye vijito vidogo vidogo sana na napenda nichukue fursa hii kumshukuru sana Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Sumbawanga kwa sababu amefanya yaani ile *pure engineering ingenuity.* Amefanya vitu vingine ambavyo hatukutegemea. Anahamisha maji kutoka Mto mmoja anapeleka Mto mwingine. Hiyo ni katika jitihada za fundi huyo na timu yake kutatua matatizo ya maji ya Mji wa Sumbawanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *ADB* bado tunashughulika nalo. Sasa hivi wame-*stabilize* na tunajaribu kuangalia upande wa *BADEA* sasa hivi. *BADEA* wamekuja juu sana kwa sababu wamekuwa wakilaumiwa kwamba walikuwa hawa-*support* sana miradi ya Afrika. Mradi wa kwanza kama mlivyoona ni huu ambao tumepata kwa ajili ya Mji wa Singida. Sasa wamekuja tunaongea nao kuhusu miradi mingine na Sumbawanga imo kwenye hiyo *project.* Lakini haina maana kwamba *ADB* tume-*withdraw application* yetu, bado ipo kule. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, tunashukuru sana kwa kutupa hongera. Matanki zaidi tunaangalia uwezekano kama ulivyosema *generation* ya umeme kwa Kigoma ina gharama sana. Utashangaa mteja mkubwa sana wa *TANESCO* Kigoma ni Mamlaka ya Maji Mjini Kigoma. *Generation* yao ya umeme karibu asilimia 40 inatumika kwa ajili ya pampu za maji. Kwa hiyo, kuna *limitation.* Lakini ulilolisema hili la kuongeza matanki nina hakika *Managing Director* ameshaliandikia *project* na kwa vile *part of the costs* bado tunawasaidia kulipa kwenye umeme nina hakika kwamba tutasaidiana kwa bahati nzuri na wewe unafahamu sana mamlaka hiyo kwa sababu kwa njia moja au nyingine unahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia juu ya uchafuzi wa mazingira, wanachafua *TANESCO* na wengine. Nina hakika kwamba kuna uongozi pale ukiutumia wanaweza kuwachukulia hatua. Kwa sababu uchafuzi wa mazingira haukubaliki, iwe inachafua Serikali au mtu binafsi au kikundi chochote kile haikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nadhani michango mingi ambayo ni ya maandishi na michango mingine atajaribu kuipitia Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukweli kama tulivyoahidi mwaka 2003/2004 wakati Mheshimiwa Waziri, akifunga mjadala tutakwenda kutengeneza vizuri inakuwa kama *working document* yetu na *the same time* tutawaeleza Waheshimiwa Wabunge, maeneo ambayo wameyauliza kwa ufanisi zaidi na kama walivyosema wenyewe ofisi zetu, Ofisi ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, maofisa, ziko wazi, lakini kwa ninyi Waheshimiwa Wabunge muishie kwetu, huwa hatuna *appointment.* Kwa hiyo, kwa matatizo mengi tutawaomba tukae na kuyajadili kama mnavyofanya mnapokuwa Dar es Salaam au hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina dakika 20 za kujibu hoja za Wabunge waliozungumza 16 kwa mdomo na 78 waliochangia kwa maandishi. Dhahiri sitaweza kumaliza zote, kwa hiyo, naomba radhi mapema mkubaliane kama alivyopendekeza Naibu Waziri kwamba, tutaandika majibu haya na kumpatia kila mmoja wenu aliyetuuliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwatambue wafuatao ambao walichangia kwa kuongea, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Kisyeri Chambiri, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Jumanne Nguli, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mheshimiwa Martha Wejja, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou na Mheshimiwa Anthony Diallo. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi ni kama ifuatavyo, kama nilivyosema wako 78 ambao ni Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Lephy Gembe, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Maria Watondoha na Mheshimiwa Freeman Mbowe naye aliunga mkono. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, Mheshimiwa Abdukalkarim Esmail Shah, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Omar

Mjaka Ali, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Ramadhani Hashim Khalfan, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Tembe Nyaburi, Mheshimiwa Kisyeri Chambiri, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo na Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi naye aliunga mkono. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Robert Buzuka, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mheshimiwa Margareth Bwana, Mheshimiwa Robert Mashalla, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Mpeme, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Joseph Mungai, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Shamim Parkar Khan, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mheshimiwa Sumri Mohamed, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mheshimiwa Wilson Masilingi na Mheshimiwa Ally Karavina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata faraja sana ya michango tuliyoipata. Tunawashukuru sana mmetuimarisha na kutupa *charge* upya. Nitajibu hoja chache sana. Naanza na Mheshimiwa Kisyeri Chambiri, kuhusu Tarime.

Nakubali Mheshimiwa Kisyeri Chambiri kwamba Rais wetu na Jemedari wetu Mkuu, alitoa maelekezo na ahadi wananchi wa Tarime kwamba maji yapatikane Tarime. Napenda kukuthibitishia na kuwathibitishia wananchi wa Tarime kwamba, umelifuatilia jambo hilo kwa makini sana Wizarani kwangu na hata siku moja hukuzembea. Umeifanya kazi hii kwa uaminifu sana na mimi ningependa kuwahakikishia wananchi wa Tarime kwamba Mheshimiwa Mbunge wenu amefanya kazi nzuri na mimi nitakuwa mtu wa ajabu sana nisipotekeleza maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo, tunawaomba wananchi wa Tarime watuamini tutatekeleza na tumeanza mwaka huu peke yake tumekupa shilingi milioni 20 kwa ajili ya kufanyia usanifu na tutakuchimbia visima vitatu haraka sana kuondoa tatizo liloko pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ambalo limesemewa sana ni vyanzo vya maji, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, mliozungumzia jambo hili na mimi ningependa kuongeza sauti yangu kwa yale mliyosema. Hali ya vyanzo vya maji nchi ni

mbaya. Ni mbaya kwa sababu watu wanaamua kukiuka kabisa taratibu zilizopo wanavamia maeneo ya vyanzo vya maji.

Nilikuwa Morogoro, Mindu. Mindu inavamiwa haijapata kutokea. Pale wanakwenda watu kutafuta dhahabu na dhahabu ile nyingine wanaoshea ndani ya bwawa. Wote tunajua kwamba jambo hilo ni hatari sana kwa watumiaji wa maji. Mzakwe hapa hapa Dodoma bado tuna matatizo. Tuna mgogoro kidogo bado kuna watu wamebaki katika eneo lile na wanatupa matatizo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba Waheshimiwa Wabunge, mkumbuke kwamba mwanzo tulikuwa tunaambiwa Dodoma kuna shida kubwa ya maji na mahitaji ya Dodoma ya maji tuliambiwa ni galoni milioni 30 kwa siku. Kupitia Mzakwe kwa msaada wa Wachina leo tunatoa galoni milioni 40 kwa siku na mahitaji ya Dodoma yamepungua kwa sababu ya mita yamepungua galoni milioni 25. Lakini chanzo kama hicho kiko hatarini kwa sababu ya kuvamiwa. Lushoto mliona katika *television* wamevamia, wameingia mpaka kwenye misitu mpaka chanzo ambacho zamani walikuwa wanaita Lushoto ndiyo Swaziland ya Tanzania. Mheshimiwa William Shellukindo, nina mashaka kama itaendelea kuwa Swaziland ya Tanzania tukiruhusu watu wale waendelee kuvamia vyanzo vile. *(Makofi)*

Kwa hiyo, la kwanza tunawaomba viongozi wote watuunge mkono kukemea jambo hili, watu waache vyanzo vya maji. *(Makofi)*

Pili, Serikali itakuja na mapendekezo kama alivyosema Naibu Waziri mapya ya kutunga sheria ya kusimamia vyanzo vya maji. Sheria ile inakusudia kwamba eneo la chanzo cha maji liwe *demarcated* na iwe hairuhusiwi binadamu yeyote wala mnyama yoyote kuingia sehemu hiyo. Naomba tutakapoleta Muswada huo mtusaidie kutuunga mkono ili tulinde vyanzo vya maji. *(Makofi)*

Lingine ambalo ningependa kulisemea ni suala la mradi wa maji vijijini unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Naibu Waziri ameeleza kidogo. Ningependa kusema hivi chukueni kitabu changu angalieni ukurasa wa 140 nasema ifikapo Julai, Tanzania nzima itakuwa tayari katika mradi huu wa Benki ya Dunia. Kwa hiyo hakuna Wilaya hata moja ambayo itakuwa imeachwa. Ila nawaomba Waheshimiwa Wabunge, niwaarifu mapema tuna matatizo na matatizo haya ndiyo wanatuambia wafadhili wetu na wanaotukopesha kwamba uwezo wetu wa kutumia fedha ni mdogo. Kwa nini unakuwa mdogo? Unakuwa mdogo kwa sababu ya matatizo ya ushirikishwaji. Jambo moja kubwa Waheshimiwa Wabunge wengi hawashiriki hawana habari na jambo hili. Tumeamua Wizarani kwamba kuanzia sasa taarifa yoyote kuhusu mradi huu tunayoipeleka Wilayani tutampa na Mbunge nakala yake, ili watusaidie kulisukuma jambo hili. Hizi fedha ziko pale sisi ndiyo tunashinda kuzitumia. Sasa kuna shida ya maji vijijini pesa zipo tunashindwa kuzitumia tunamlaumu nani? *(Makofi)*

Nitawapeni mifano michache, kwa mfano, katika zile Wilaya ambazo tumeanza nazo waniwie radhi sana Waheshimiwa Wabunge wanaohusika, kuna tatizo la wananchi kutotoa michango yao. Kwa mfano, Rufiji walitakiwa wachange shilingi milioni 16

wamechanga shilingi milioni 11. Kilosa, kuna Kilosa moja inafanya vizuri walitakiwa wachange shilingi milioni 30 wamechanga milioni 15.9. Mpwapwa walitakiwa wachange shilingi 47 milioni wamechanga milioni 24. Hiyo ndiyo hali inayojitokeza hata kwa Wilaya nyingine katika nzima. Jambo hili linatokea kwa sababu viongozi wa kuwasukuma wananchi wa kuwashawishi wananchi hawahusishwi. Kwa hiyo, tunatoa maelekezo na maagizo kwamba viongozi wa kisiasa wahusishwe kwenye jambo hili ili waweze kuwashawishi wananchi wachangie miradi na miradi iweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni juu ya *City Water.* Mheshimiwa Mama Martha Wejja, leo umezungumza vizuri hata mimi nakusifu kweli Mheshimiwa Martha Wejja, umelieleza vizuri sana nakubali. Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, ananiambia eti unaitwa *Miss Bunge,* mimi hilo sijui. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini Waheshimiwa Wabunge, *City Water* imechukua madaraka muda mfupi uliopita, ombi letu kwenu ni kwamba tunaomba tuwape muda wafanye kazi. Wanakumbana na matatizo makubwa sana. Matatizo haya tusiyapuuze. *Mozambique* walibinafsisha shughuli za maji pale Maputo, walipobinafsisha ile kampuni ilipochukua baada ya miezi sita walikimbia, wakaondoka, wakaacha mradi wakaenda zao, wakarudi Ufaransa. Wanakuta mambo ya ajabu, wanakuta bomba lile limekaa kiajabu ajabu hamna mfano duniani, halichoreki, lakini Dar es Salaam lipo.

Lakini la nne, kuna utaratibu na *(culture)* utamadumi wa watu tunataka kulipia maji, hili linasumbua sana, sasa hatusemi kwamba kwa matatizo haya tuwaachie wafanye visivyo. Napenda kuwaahidi kwamba tutawafuatilia kwa karibu sana kuhakikisha kwamba wanatekeleza wajibu wao. *(Makofi)*

Lakini naomba matatizo madogo madogo yanayotokea, tuwape ushirikiano na hasa mabalozi wa nyumba kumi kule Dar es Salaam wawasaidie watu hawa kufanya kazi, wawasaidie kuwaonyesha watu ambao wanaiba maji, kuna watu wamefunga pampu kubwa sana za maji, wanavuta maji wanawauzia majirani, ni kinyume cha sheria. Sasa tunasema watu kama hawa wasaidieni *City Water,* wawajue, wawachukulie hatua za kisheria vinginevyo tutakuja hapa tutawalaumu kwa sababu hali ya mambo wanafikiria ni kama Ulaya, Tanzania ni *Bongoland* mambo ya ajabu sana yanafanyika mle.

Sasa naomba tuwasaidie ili wafanye kazi yao. Lakini napenda kuwaahidi hatutawaachia wafanye kienyeji, makubaliano yote tuliyokubaliana yatazingatiwa na yatatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tano, ni la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, nakubaliana kwamba liko tatizo la kusafirisha mifugo kutoka Mwanza kupeleka Dar es Salaam, tulikarabati mabehewa 58 kwa fedha za *ADB* na pengine nimjibu Mheshimiwa Paul Makolo, hapo hapo kwamba hatuwezi kuziachia zile fedha kwa sababu mkataba wetu na *ADB* ni kwamba fedha zitakazopatikana kwenye minada tutazitumia kuendeleza minadi chini ya reli na tumeanza.

Kwa hiyo, tukikuachia wewe fedha hizo, tutakosa uwezo ambao ni mkataba na *ADB.* Lakini tumekarabati mabehewa hayo hayatoshi. Nakubaliana na wewe kwamba Shinyanga kule sasa kuna ng'ombe wakubwa sana na wanapokuja kwenye Soko la Pugu kwa kweli mnada unatikisika wanakubali ng'omba wazuri wa Usukumani wameingia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nakubaliana nawe kwamba tutafute utaratibu mzuri wa kuhakikisha mifugo inasafiri. Lakini jambo la uhakika katika jambo hili ni kufungua viwanda vingine vya nyama ndiyo dawa yake. Hata utamaduni wa kula nyama utaongezeka maana mtapata *customer* za Kimataifa kwa hiyo, mtakula nyama kwa wingi zaidi. *(Makofi)*

Sasa tumemaliza kiwanda cha Dodoma tunategemea kukibinafsisha na tunategemea vile vile tutakazopata pale ama zile ambazo Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, anatusaidia sana kuzipata kutoka *BADEA* tutaanzisha viwanda vingine Shinyanga na Mbeya. Ninamwomba sana Mheshimiwa Basil Mramba, aendelee kutuunga mkono, *BADEA* wameonyesha nia yao ya kutufadhili na mimi sina mashaka kabisa na Mheshimiwa Basil Mramba, kwa sababu ukimpelekea jambo ambalo linataka fedha na umeliweka vizuri mara nyingi sana hutusaidia. Kwa hiyo, napenda kumshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema ifuatavyo:-

Mmetupa pongezi nyingi sana, mmetupa shukrani nyingi sana, lakini nasimama hapa kwa unyenyekevu mkubwa sana kuwaambieni kwamba anayestahili pongezi hizo na shukrani ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. *(Makofi)*

Naomba radhi sana nimewasahau kuwataja kwamba waliochangia ni pamoja na Mwenyekiti wa Kamati, Msemaji Mkuu wa Upinzani na Mheshimiwa Parseko Kone, amechangia kwa maandishi. Naomba radhi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ya maji kwa mfano Mradi wa Ziwa Victoria ambaye amekuwa anafuatilia siku hadi siku na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, juzi ameniagiza, ameniambia karibu naacha magongo, nikiacha magongo mradi wa kwanza nitakaotembelea ni mradi wa *Lake Victoria. (Makofi)*

Najua kuna ahadi yake nyingine hatujatekeleza anayofuatilia kwa karibu sana rafiki yangu, Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, ya Mbwinji, Masasi, Nachingwe, lakini ningependa pia kuwaahidi wananchi wa Mbwinji, Masasi na Nachingwea kwamba tutaitekeleza ahadi hiyo ya Rais kwa njia yoyote inayowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ninayo timu ya vijana wa Kitanzania ambao wana sifa za kufanya kazi kama hizi Kimataifa lakini wanazifanya Tanzania, ni vijana wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo wanaostahili pongezi hizi na shukrani zenu. Wamefanya kazi nzuri sana kwa kweli pongezi na shukrani hizi naomba muwafikishie wao na wale pale wanawaona mkiwashangilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali hoja ni nyingi tutazijibu moja baada ya nyingine, lakini tunaweza kupata maji katika Wilaya zote za nchi zetu kama tutashirikiana kusuma utekelezaji na utendaji katika Wilaya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 49 - Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ... ... 1,842,711,300/=

**MWENYEKITI:** Haya tumewaona waandike wote haraka haraka. Mheshimiwa Esther Nyawazwa, uketi, Mheshimiwa Paul Ntwina, uketi, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Raynald Mrope na Mheshimiwa Job Ndugai.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi kutokana na kifungu 1001 kwenye mshahara wa Waziri naomba anisaidie kunieleza, tunapokuja hapa Bungeni maji ni tegemeo kubwa sana kwa Wabunge na wananchi ambao wanaishi eneo la Dodoma. Labda Mheshimiwa Waziri anisaidie tu ni kitu gani ambacho kimetokea mwezi huu Julai, kupandisha gharama za maji nikitolea mfano kwamba zamani *unit 0* mpaka *unit 18* walikuwa wanalipa shilingi 5,500/= lakini mwezi huu imekuwa kuanzia *unit 0* mpaka *unit 10,* shilingi 3,500/= na *unit 10* mpaka *unit 25* unalipia shilingi 5,250/= ambayo jumla unapata shilingi 8,750/=.

Ni kwa vipi sasa Mheshimiwa Waziri kama angetaka kuwasaidia wanaotumia maji wa maeneo ya Dodoma kwa nini basi asichukue kigezo cha kutumia ile ya kwamba ile *unit 0* mpaka *unit 18* basi akaweka *unit 0* mpaka *unit 10* ikawa shilingi 3,500/= halafu akachukua tena *unit 10* mpaka zile *unit 18* ambayo wananchi walielewa walizoea yaani kila *unit 8* zinazozidi walipe shilingi 2,800/= ambayo jumla itakuwa shilingi 6,500/= na litakuwa ongezeko la shilingi 800/= tu. Lakini ukichukua kwa bei ambayo wameongeza kwa sasa itakuwa ongezeko la shilingi 3,250/=.

Naomba Mheshimiwa Waziri, anieleze tu ni kigezo gani ambacho kimefikia kupandisha bei kiasi hicho? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba tuna mamlaka zetu za mijini, Tanzania zimepata sifa kutoka Benki ya Dunia, kwa kufanya kazi yao vizuri sana. Vigezo vinavyoangaliwa vinazingatia kwa mfano Mheshimiwa Esther Nyawazwa, anajua kwamba bei ya umeme imepanda ni dhahiri lazima watapandisha bei. Lakini Mheshimiwa Esther Nyawazwa,

ajue vile vile kwamba katika maeneo ya Mjini ambako kuna watu, maskini tuna utaratibu maalum wa kuwapa watu maskini maji bila kuyagharamia. Lakini inapokuja gharama za kawaida za umeme na vitu vingine ni shurti mamlaka ile itafute jinsi ya kupata fedha zake, vinginevyo haitaweza kukopesheka, haitaweza kukubalika na misaada itakuwa tabu kupatikana.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni katika kusaidia wananchi ambao hali zao ni za chini sana. Mheshimiwa Waziri, hawezi kuona basi angalau hii 800/= ikaongezeka kidogo hata kama gharama ya umeme imepanda maana wananchi hata gharama za umeme wanalalamika sana kwa nini basi hiyo shilingi 800/= isiongezwe Mheshimiwa Waziri tukasaidia wananchi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kurejea maelezo yangu wale wananchi maskini ambao hawana uwezo wa kulipia maji, tuna utaratibu wa kuhakikisha kwamba hawalipii maji, wanapewa maji bure.

Nasema kama Mheshimiwa Esther Nyawazwa, ana watu anaowajua wa namna hiyo, hawajatoa huduma hiyo, niko tayari kuisikiliza kuifuatilia. Lakini kwa suala la bei ya umeme umepanda niwazuie mamlaka hii kwamba bei ya umeme imepanda msipandishe bei, tutakuwa tunawafanya hawa washindwe kufanya kazi na nadhani tunakuwa na wajibu wa kuwaambia wananchi wafanye kazi. *(Makofi)*

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nina machache ambayo napenda nimhoji Waziri. Wachangiaji wa maandishi tumekuwa wengi sana 78 na ni dhahiri Waziri asingeweza kutujibu sote.

Lakini mimi niko *concern* na vijiji vitatu ambavyo vimechimbiwa visima lakini *hand pumps* havina katika kutekeleza kazi yangu, nimejaribu kufuatilia Wizarani, Halmashauri na penginepo sijapata msaada wowote. Katika maandishi nimemwomba Waziri, anisaidie kuweza kupata hivi visima *pumps* na ni maeneo ambayo yana matatizo sana kwa mfano Galula, Mbuyuni na Mbangala.

Pia nimemwomba vijiji saba kama ningeweza kupata kisima kimoja kimoja kama alivyosema mwenzangu miaka ya karibuni kumekuwa hakuna maji ya kutosha nalo ningependa kupata maelezo juu ya hilo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhahiri nisingeweza kumjibu Mheshimiwa Paul Ntwina, maelezo yake yaliyoandikwa kwa maandishi kwa sababu sikuweza kuyapitia yote na majibu yake sikuweza kuyapitia yote pia. Lakini ningependa kumwambia kwamba suala la *hand pumps* tunalifahamu zilikuwa zimeagizwa zitakapofika zitafungwa mara moja katika visima hivyo. Suala la visima hivi vingine saba nitaomba tulitazame sitaweza kutoa ahadi hapa sasa hivi. *(Makofi)*

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nimeshika fungu 1001, namwomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo yake na wananchi wamsikie yeye mwenyewe juu ya huu utaratibu wa kutoa *bills* za maji kwa makisio na nini faida ya kufunga mita kwa wateja kwa sababu Naibu Waziri hapa hakulijibu wazi, amelifumbafumba. Kwa hiyo, tunaomba yeye mwenyewe aeleze kwa vile tunajua ni uwezo wake na jinsi anavyowapenda wananchi katika masuala haya ya maji. Hilo ni moja.

La pili, niliuliza kwa maandishi kuhusu wananchi ambao wanaomba kuchimbiwa visima binafsi. Bei ya uchimbaji ni juu sana kiasi ambacho hata kama unahitaji kwa mtu wa kawaida anashindwa. Sasa nilikuwa naomba maelezo, utaratibu upo vipi labda tunakuwa hatuelewi vizuri kwa sababu wananchi wanatuuliza na kwa uwezo wangu nashindwa kutoa majibu, naomba yeye atusaidie na asikike kwenye redio wananchi wamsikie, wanampenda sana. Namshukuru. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotoa maelezo wakati nachangia, ukweli ni kwamba maelekezo na makubaliano yetu na Mamlaka za Maji ni kwamba pale wanapofunga mita wanatakiwa wasitumie *flat rate.* Sasa ukikuta wanatumia *flat rate* napenda nimwelezee Mheshimiwa Esha Stima kwamba, Mamlaka nyingi wamefunga *software* ya *computer* ambayo ina-*monitor trend* ya kila *account.* Wanapokuta hii *account* baada ya muda mfupi bili yake imeanguka ghafla, kinachotokea ni nini?

Kwanza wanapeleka watu kukagua. Mara nyingi ukikuta tatizo la namna hiyo utakuta kwamba mtu ame-*bypass,* ameweka bomba la wizi wa maji. Ikitokea namna hiyo, kinachofanyika ni kwamba watamkadiria kwa *average bill* ya zile bili ambazo zilipelekwa kwake, kwa hiyo atalipa. Hiyo ni kumsaidia kwa sababu *otherwise* angeshitakiwa, ni *criminal offence* hiyo, wizi! Ukikuta sehemu ambayo wanatumia *flat rate* kwa kiwango kikubwa ni mahali ambapo mita hazipo. Lakini ikifungwa mita, sasa itakuwa ni ajabu ufungiwe mita, gharama ile ya mita halafu wakati huo huo tena unalipa *flat rate* itakuwa haina maana na nadhani Mameneja na Bodi za Maji wana uwezo mkubwa wa kuweza kuelewa hilo.

Hili la gharama za uchimbaji wa maji, ukweli ni kwamba *DDCA, charge* zao mpaka sasa hivi ni chini sana na ndio maana utakuta kwamba wana kazi nyingi kiasi kwamba wanagombaniwa kila sehemu kwa sababu kuna *private companies* zinazofanya *drilling* lakini huwezi ukapata *company* ya *private* ambayo wataku-*charge* chini ya milioni tano. Lakini visima vya maji vinavyochimbwa na *DDCA* unaweza kukuta wana-*charge* kati ya shilingi milioni tatu na kuendelea. Inategemea kwanza na ugumu wa ardhi ya mahali pale, halafu umbali wa maji kuyafikia. Usitegemee kwamba kisima cha mita tuseme 100 itakuwa gharama ya shilingi milioni moja au mbili, hapana. Inaweza kufika mpaka milioni kumi! Tumeshaona wanachimba visima kwa milioni kumi kwa sababu zile *rigs* zake za kuchimbia maji zinalika sana mahali ambapo kuna mwamba mgumu. Kwa hiyo, inategemea na pia lazima ieleweke kwamba hiyo ni *agency* ya Serikali. Hawako pale *purely* kutengeneza faida, gharama zinatokana na matumizi halisi ya gharama zao za uchimbaji wa maji.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilimwomba Mheshimiwa Waziri atoe kauli yake hapa. Naibu Waziri hakuniridhisha na maelezo yake. Sasa nashangaa bado napata maelezo kutoka kwake. Hilo moja. *(Kicheko)*

La pili, suala la bili ya kukisia wala haitolewi kwa misingi kwamba kuna wananchi ambao wanaiba maji. Mimi mwenyewe hapa nyumbani kwangu nina kisima, navuna maji na nimefungiwa mita, lakini bili zinazokuja ni kubwa. Halikadhalika, wananchi wa Shinyanga, nazungumzia wananchi wa Shinyanga ambao hawana wizi wa maji na sio kawaida yao kuiba maji. Kwa misingi hiyo akisema hivyo kwa jumla tu, labda anazungumzia watu wa Mikoa mingine ambao ni wajanja wajanja. Lakini kwa wananchi wa Shinyanga hawana tabia hiyo na ndio sababu nimesema kwamba hilo halina ukweli Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi nilimwomba Waziri mwenyewe aseme na kama yeye amechukua nafasi hiyo angesema ule ukweli, sio kufunikafunika mambo ambayo yapo wazi. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Labda moja tuwekane sawa kwamba Serikali nzima inawajibika kujibu hoja za Wabunge. Kuna wakati fulani anajibu Waziri fulani kwa sababu suala linamhusu zaidi. Kwa hiyo, akijibu Naibu Waziri au Waziri Mkuu au *Attorney General* au nani, ni Serikali inajibu. Sasa labda nimwombe Mheshimiwa Waziri mwenyewe kama atasema tofauti na haya tumsikilize. Mheshimiwa Waziri labda naomba usimame kwa sababu Mheshimiwa ameomba rasmi kwamba anataka kusikia kauli yako wewe mwenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa dada yangu Mheshimiwa Esha Stima, sijui anataka aone hizi mvi au ni nini!!

Mheshimiwa Esha Stima, maelezo aliyetoa Naibu Waziri ni sahihi na amesema hivi, wale wote ambao wanatumia *flat rate* ni makosa na tutachukua hatua zinazopasa.

**MWENYEKITI:** Naona Mheshimiwa Esha Stima, amekubali. Hiyo ndiyo kauli aliyokuwa anaisubiri. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 49 Programme 10 Sub Vote 1001,* Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa niaba ya wananchi wangu kufikisha malalamiko yao. Nimechangia kwa maandishi, niliorodhesha miradi minne, lakini miradi hasa ninayoisimamia hapa ni miwili. Mradi wa Kijiji cha Litumbakuhamba na mradi wa Kata wa Kingirikiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hizi mbili zina matatizo makubwa sana. Akinamama hasa wakati wa kiangazi wanaondoka saa 9.00 usiku kufuata maji na mara zote nikiuliza maswali hapa niliambiwa kwamba tutakuwa katika mradi wa *KfW,* lakini nimeshangaa leo mambo yamebadilika, tunaambiwa tungoje awamu ya pili ya mradi wa

*World Bank.* Sasa ninavyoamini, hii miradi naona ni miradi ya muda mrefu, kwa hiyo nasimama kwa niaba ya wananchi wa Mbinga Magharibi kumwomba sana Mheshimiwa Waziri awafikirie wananchi hawa kati ya Kingirikiti na wananchi wa Kijiji cha Litumbakuhamba. Ni vyema Waziri akatumia hekima yake na ninaamini anayo hekima kubwa sana, akatumia upendo wake mkubwa alionao ili miradi hii miwili ikafikiriwa kwa upendekeo maalum ikaingizwa katika mradi wa awamu ya kwanza wa *World Bank* ama akatafuta fedha mahali popote ili miradi hii miwili ikafanikishwa. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, amewahi kuniona juu ya mradi huu wa Vijiji hivyo. Nimemsikiliza, ni tatizo la kweli, nimempa ahadi ya kumwambia mradi wa Benki ya Dunia unaanza mwakani mwezi Julai. Ningemwomba tu avute subira mwezi Julai tuanze kwa kishindo.

**MWENYEKITI:** Naona Mheshimiwa ameridhika, twende kwa Mheshimiwa Halimenshi Mayonga.

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niombe tu kwamba tangu Mheshimiwa Edward Lowassa, amekuwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwenye Jimbo langu amenisaidia sana na ninachosimama hapa naomba aendelee kunisaidia kwa sababu hapa ndipo nitakapoponea. Umeme umeshindikana na mambo mengine yameshindikana, kwa hiyo hii nguvu ya maji tu ndio na yeye mwenyewe Mheshimiwa Edward Lowassa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi niliandika hivi, kuna Kijiji jirani ambacho kinatoka Kidah, sasa tumejenga Sekondari Kata moja ya Simbo, ningeomba kwamba Kijiji kile cha Kidah, ni suala la mabomba tu na tanki. Mabomba ambayo ni kama kilometa tatu, si nyingi ni kilometa tatu tuweze kuunganisha kwenye hilo Jimbo langu na Vijiji vingine viwili ambavyo vinahitaji suala la mabomba na matanki tu ya kuongeza kwa sababu yatakuwa Vijiji vile vinapokezana.

Sasa kwa kuwa muda ule ulikuwa hautoshi na mchango wetu unakuwa ni mdogo, sasa je, hilo linawezekana? Kwa sababu ile Benki ya Dunia inasema mwakani, mwaka kesho kweli mimi nitakuwa si ndio kura za maoni tayari kwa mwaka kesho mwezi wa saba!? Sasa naomba tu hapo aweze kunisaidia hili. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, okoa jahazi. Maelezo! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kura za maoni zimekaribia na *television* zinatuona tuna kazi kweli kweli. Suala la Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, kama tulivyomsaidia wakati ule tunaweza kuangalia katika mradi. Mimi ninavyoona nadhani amesoma kitabu vibaya, yeye ni katika wale wa mwanzo mwanzo sio mwaka kesho, yeye yuko mwanzoni. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii. Nilimwandikia Mheshimiwa Waziri, lakini kwa sababu hoja ni nyingi asingeweza kujibu hili, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Serikali imebadili mwelekeo wake katika namna ya kuendesha Ranchi za Taifa kwa kuleta utaratibu mpya zaidi wa uendeshaji wa Ranchi hizo. Utaratibu huu umewezesha baadhi ya Ranchi kugawanywa katika vipande vidogo vidogo na wananchi wa Tanzania wakawezeshwa kupewa vipande hivyo ili waweze kufuga na Mheshimiwa Waziri ametuelezea hapa mipango mizuri iliyoko katika mazungumzo kati ya Wizara na Benki inayoitwa *BADEA* kuwezeshwa zoezi hilo kufanyika na haya ameyaelezea vizuri katika hotuba yake ukurasa wa 88 na 89.

Kwa jinsi hiyo, Ranchi za Mkata, Mzeri, Dakawa, Kalambo, Usangu, Kitengule mpaka kwa Mheshimiwa Aggrey Mwanri kule *West Kilimanjaro* na kadhalika sasa zinafanyiwa utaratibu huo wa kugawanywa vipande vidogo vidogo ili wananchi waweze kuwezeshwa. Lakini Ranchi ya Kongwa imekuwa ni *exception,* yenyewe inabakia hivyo. Sasa nilichotaka kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni maelezo tu kidogo akubaliane nasi kwamba sera hiyo inayoendelea sasa katika Wizara ni sera sahihi kabisa, Ranchi ya Kongwa isiwe *exceptional,* nayo iingie katika utaratibu huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, maelezo.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Job Ndugai, ni jirani mzuri wa Kongwa Ranchi, lakini naomba nimkumbushe kwamba tulipoleta maelezo hapa ya sera hiyo tulieleza kwamba Ranchi mbili, Ranchi ya Ruvu na Kongwa zitabaki bila kuguswa. Kwa nini? Kwa sababu hizi Ranchi kubwa sana, ni Ranchi za mfano. Kongwa sasa hivi kuna ng'ombe zaidi ya 13,000. Ukitaka kuona Morani wazuri Tanzania wako pale Kongwa. Hatuwezi kubinafsisha kila kitu, lazima Serikali iendelee kuwa na nafasi ya kuongoza vitu ili wananchi waweze kujifunza kutoka pale. Kwa hiyo kwa Kongwa na kwa Ruvu tumesema zinabaki kwamba ni mali ya *NARCO,* inaendelea kuwa ni ya mfano na inatusaidia tunapotaka kutenga maeneo ya kupambana na magonjwa, mnaweza kuwahi maeneo yale yakawa ni *Disease Free Zones. (Makofi)*

Kwa hiyo Mheshimiwa Job Ndugai, kama anatafuta ranchi anaweza kuipata Kalambo, Kifurula, tafadhali tuachie hii kama tulivyopanga, ni mipango ya uhakika zaidi. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu zote ambazo zimekuwa zikitolewa kwa kubakiza Ranchi ya Kongwa siku zote ni sababu ambazo ni za kutoka upande wa *NARCO,* Shirika linaloshughulika na masuala ya Ranchi. Lakini na sisi wananchi tuna sababu zetu. Sasa kwa kuwa kwingine kote utaratibu umebadilika lakini sisi tunalazimika kwa mazingira yaliyopo kubakia na utaratibu wa zamani. Sasa Mheshimiwa Waziri anawahakikishia wananchi wa Kongwa watafaidikaje kwa Ranchi ile kubakia vile ilivyo kwa siku zijazo?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niweke wazi kwamba Ranchi hizi wala haya maoni sio ya *NARCO* ni maoni ya Serikali. Lakini Ranchi hizi hatugawii wananchi eka moja moja,

nimesema tunatengeneza hekta 3000 Ranchi za kisasa na za Kibiashara, ndio tunachofanya, sio anakwenda kupewa mwananchi eka moja moja, kwa hiyo tukiamua hivyo maana yake wananchi wa pale Kongwa watapata eka moja moja, hapana. Tunataka kutengeneza ufugaji wa kisasa. Kwa hiyo, hakuna *double standards,* tumeamua tu kwamba hili ni eneo la mfano, tungetaka liendelee kubaki kuwa ni eneo la mfano. Ila kama Mheshimiwa Job Ndugai kuna tatizo kubwa la wananchi pengine wamekosa ardhi, pengine kuna shida maalum, njoo tuzungumze. Lakini hatuwezi kubadilisha sera hapa *simply* kwa sababu hiyo. Namkaribisha Mheshimiwa Mbunge, kama kuna jambo ambalo anafikiri wananchi wake wana tatizo kubwa sana la ardhi na hamna mahali pengine ni pale, basi namkaribisha tuzungumze. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naona ameridhika. Mheshimiwa Raynald Mrope, ndio wa mwisho.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuanzisha mradi wa maji wa Mbwinji. Chemchem ya Mbwinji iko mpakani kati ya Newala na Masasi lakini Mto wenyewe unatiririka katika Wilaya ya Masasi. Tunawashukuru pia Serikali kwa sababu toka awali walikuwa wameahidi kwamba mradi huu wa Mbwinji ndio utakaoondoa matatizo ya maji katika Wilaya ya Masasi na sisi wote, mimi pamoja na wananchi tuliamini hivyo. Tunaamini kwamba maji haya baada ya kutosheleza Masasi na baadhi ya sehemu za Masasi Magharibi, toka hapo ndio yatakwenda Nachingwea.

Sasa ikiwa taratibu zitabadilika kwamba maji yatatoka Mbwinji na katikati hapo, tugawane na Wilaya nyingine, naogopa mtaanzisha vita ya wenyewe kwa wenyewe. Kwa hiyo, ningeomba nieleweshwe pamoja na wananchi wa Masasi kwamba, je, azma ya Wizara ni kutosheleza maji haya Masasi kwanza na baada ya hapo yaende kokote kule yanapotaka kwenda? *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelewa *concern* ya Mheshimiwa Mbunge. Lakini kidogo cha kushangaza ni anavyolileta kwa sababu tumeeleza hivi, huo mradi tunauchukulia kama mradi mmoja. Ni kama tulivyoeleza Shinyanga, unahusisha na Vijiji vya jirani au Ruvu unapeleka maji katika Jiji la Dar es Salaam. Sasa tukianza kusema haya maji kwa sababu yako mpakani mwa Masasi na Newala, basi yasiende Nachingwea, nadhani hiyo ndiyo itatuletea vita kwa sababu *catchments* ya maji huwa inatoka sehemu nyingi sana na *in this case* yanatoka Newala wala sio Masasi. Ila Masasi inavyoonekana iko karibu kidogo. *(Makofi)*

Sasa tunachosema ni kwamba Mheshimiwa Mbunge, atafute, apate maji na tumeeleza kwamba Masasi na Nachingwea. La sivyo, atarudi kwenye methali ya Abraham Lincolin, alisema siku moja kwamba humtajirishi maskini kwa kumnyang'anya yule tajiri. Sasa ndio tunachotaka kufanya, hatutafika kokote. Naomba sana Mheshimiwa Mbunge akubaliane na sisi kwamba miradi hii miwili yote ya Miji hii miwili ni muhimu na Vijiji vya katikati ni muhimu. Maana hatuwezi kupitisha bomba tu

wananchi walioko njiani wakakosa maji na maji yatawatosheleza wote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Mimi nililotaka ni suala dogo sana.

Naomba Mheshimiwa Waziri anithibitishie maji haya yatatosheleza Masasi, Namatutwe, Lukuledi na Namajani? Kwa sababu hiyo ndiyo njia ya kwenda Nachingwea. Akinihakikishia hapo mimi sina maneno. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemshangaa kidogo kaka yangu Mheshimiwa Raynald Mrope, maana katika Wilaya ambazo zimepata bahati, yake ni mojawapo. Masasi inayo Mradi wa Benki ya Dunia, Masasi inao mradi wa *JICA,* Masasi inapata Mradi wa Mbwinji, Masasi na Nachingwea. Sasa rafiki yangu Mungu ampe nini? Ahsante sana. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* ... ... ... ... ... ... ... 465,220,400/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... ... 1,005,880,500/=
Kifungu 1004 - *Livestock Research and Training Institutes* ... 2,289,850,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 - *Water Resource Assessment and Exploration* ... ... 1,450,163,000/=

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kweli niliunga mkono hoja, lakini nataka ufafanuzi kidogo. Kuna hoja ya *Lower Moshi Irrigation* ambayo Mheshimiwa Rais aliwahi kutoa ahadi.

**MWENYEKITI:** Ni Kifungu namba ngapi Mheshimiwa Thomas Ngawaiya?

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** *Construction of Other Civil Works,* 310900, kifungu 2001.

**MWENYEKITI:** Haya endelea.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais alikuja pale akawaahidi wananchi wa pale kwamba angewaongezea idadi ya maji ambayo tayari walikwishakuwanayo ya mita *unit 3.71.* Lakini nilipouliza swali hapa Bungeni, nilijibiwa na Waziri wa Kilimo na Chakula kwamba ahadi ya Rais imeshatekelezwa. Sasa kwa sababu hiyo ahadi ilikuwa kweli haijatekelezwa, kwa kuwa Waziri mhusika wa Maji na Maendeleo ya Mifugo ndio mwenye dhamana Mheshimiwa Edward Lowassa, nilitaka nipate hayo kwa sababu nitakapokwenda kule wataniuliza. Walisikia kwenye

redio kwamba ahadi ya Rais imeshatekelezwa wakati bado hawajafanya yale yaliyokuwa yamekubalika pale. Ningeiomba ufafanuzi ili niweze kwenda kuwaeleza wananchi.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulijibu hapa Bungeni tukatoa maelezo marefu sana na Wizara ambayo inawasilisha makisio hapa, inashughulika na maji ya kunywa na ya viwandani sio ya umwagiliaji. *(Kicheko/Makofi)*

Hata hivyo, *water right* imeshatolewa kwa ajili ya kuongeza maji kwenye eneo la umwagiliaji la *Lower Moshi.* Mimi ningekuwa Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, ningejitahidi kuuliza sasa maswali ya kutafuta fedha za kutekeleza mradi ule, sio za kutafuta maji tena. Sasa namwomba aendelee kuunga mkono hoja ili tukishamaliza tupate fedha tukafanye kazi. *(Kicheko/Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *Central Stores* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 401,387,500/=
Kifungu 2003 - *Water Laboratory*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...560,325,800/=
Kifungu 3001 - *Urban Water Supply and Sewerage* ... ... 2,216,663,500/=
Kifungu 3002 - *Central Water Board* ... ... ... ... ... ... ... ... ... 712,305,600/=
Kifungu 4001 - *Rural Water Supply* ... ... ... ... ... ... ... ... 2,973,665,600/=
Kifungu 5001 - *Water Resources Institute*... ... ... ... ... ... ... 553,110,400/=
Kifungu 6001 - *Drilling* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ..111,320,700/=
Kifungu 7001 - *Veterinary Services*... ... ... ... ... ... ... ... ... 1,926,705,600/=
Kifungu 8001 - *Animal Production*... ... ... ... ... ... ... ... ... 3,127,240,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 49 - Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... ... 4,337,355,000/=
Kifungu 1004 - *Livestock Research and Training Institutes* ...215,600,000/=
Kifungu 2001 - *Water Resource Assessment and Exploration*... ... ... 120,000,000/=
Kifungu 2003 - *Water Laboratory* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...75,000,000/=
Kifungu 3001 - *Urban Water Supply and Sewerage* ... ... 72,385,946,430/=
Kifungu 3002 - *Central Water Board* ... ... ... ... ... ... ... ... ... 22,256,000/=
Kifungu 4001 - *Rural Water Supply* ... ... ... ... ... ... ... 24,076,461,770/=
Kifungu 5001 - *Water Resources Institute*... ... ... ... ... ... ... 100,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 6001 - *Drilling* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...310,000,000/=

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba tu nipate ufafanuzi kidogo kwenye upande wa Kifungu 6001, fedha zilizotengwa naomba nipate kujua zitakuwa ni kwa ajili ya kuboresha mitambo ya uchimbaji wa visima au kununua magari mapya kusudi kuondoa hali iliyopo sasa. Nasema hivyo kutokana na kwamba mashine ambazo zinatumika sasa kwa Wakala wa Uchimbaji wa Visima vya Maji na Mabwawa, kwa kweli viko katika hali mbaya sana. Hata Wilayani kwangu nilikuwa na visima vinne ambavyo wananchi wamechanga kwa kiasi kikubwa sana tukachimbiwa visima vinne na kuweka *pump* lakini havijatoa maji mpaka sasa na hii ni kutokana na kufanya kazi kwa njia ya kubahatisha. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie au anipe jibu kama kweli hizi pesa zitatosha kuhakikisha kwamba wanapata mitambo mipya ili kuweza kutia nguvu wananchi. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nasikitika kwamba mitambo yetu ilipokwenda kutafuta maji kule kwa Mheshimiwa Estherina Kilasi, kwa bahati mbaya visima havikupata maji na kwa bahati mbaya zaidi mitambo yetu ikaharibikia kule tukapata gharama mara tano ya gharama za awali. Lakini namshukuru kwa kutuonea huruma kwamba fedha hizo hazitoshi, lakini kwa kumhakikishia kwamba tumekwenda mbele zaidi, mitambo hii sasa kwa kibali cha Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, imeruhusiwa kukopa kutoka *CRDB,* fedha za kutosha za kuwawezesha kununua mitambo mipya na ya kisasa ya kuwawezesha kufanya kazi vizuri zaidi. *(Makofi)*

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 7001 - *Veterinary Services* ... ... ... ... ... ... ... ... 1,167,900,000/=
Kifungu 8001 - *Animal Production* ... ... ... ... ... ... ... ... 1,759,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka 2004/2005 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makisio hayo. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka 2004/2005 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, shughuli ambazo zilipangwa kwa siku ya leo, sasa zimeishia hapa na kwa hiyo, naliahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.32 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne tarehe 27 Julai, 2004 saa tatu asubuhi)*